# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Arobaini na Moja - Tarehe 3 Juni, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hiki ni Kikao cha Arobaini na Moja, katika Mkutano wetu wa Kumi na Moja. Katibu.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatayo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**:-

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBONI):-**

Taarifa ya Kamati ya Miundombonu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 323

### Kijiji cha Lamadi Kuwa Mji Mdogo

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. DKT. TITUS M. KAMANI)** aliuza:-

Kijiji cha Lamada chenye wakazi takribani arobaini elfu (40,000) kina shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii.

Je, ni lini Serikali itakipatia Kijiji hicho hadhi ya kuwa Mji mdogo na kurahisisha usimamizi na uendelezaji wake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Inawezekana hiki ni kijiji kikubwa kuliko vyote Tanzania maana kina wakazi elfu arobaini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI**) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengiya Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo haja ya Serikali ya kuanza kufikiria kupandisha hadhi ya kijiji cha Lamadi kuwa Mamlaka ya Mji mdogo kwani kijiji hiki kimeonekana kukua kwa kasi kwa maana ya ongezeko la watu na shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Lamadi kiko katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega na Makao Makuu ya Kata ya Lamadi. Kijiji hiki kina jumla ya wakazi 18,868 na kina shughuli nyingi za kibiashara kama benki ya *AZANIA, SACCOS,* soko la kisasa, nyumba za kulala wageni, maduka ya jumla na rejareja na stendi ya mabasi ya abiria na magari ya mizigo. Aidha kijiji hiki kina huduma muhimu za kijamii zikiwemo shule sita za msingi, sekondari mbili na huduma za maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007 kipengele cha tano cha jedwali la tano, kimetaja vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa katika kuanzisha Mamlaka ya Mji mdogo.

Aidha Sheria za Serikali za Mtaa Sura ya 287 na 288 toleo la 2002 imeeleza taratibu za kufuata katika mchakato wa kupandisha hadhi ya kijiji kuwa Mamlaka ya Mji mdogo ambapo imetamkwa wazi kuwa utaratibu utaanza katika ngazi za wananchi kupitia mkutano mkuu wa kijiji na kupata ridhaa ya Kamati ya Maendeleo ya Kata *(WDC),* Baraza la Madiwani, Kamati ya ushauri ya Wilaya *(DCC),* Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)* na hatimaye mapendekezo hayo huwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ya kupandisha hadhi Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kuingiza dhana ya Mipango Miji ili kuzuia ukuaji holela, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha huduma za jamii.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na wananchi wa Lamadi na uongozi wa Halmashauri na Mkoa ili kwa kuzingatia Sheria nilizozitaja hapo juu waweze kuharakisha mchakato wa kupandisha hadhi kijiji hicho kuwa Mamlaka ya Mji mdogo. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA**: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwa sababu katika majibu ya Naibu Waziri anasema kijiji cha Lamadi kina wakazai takribani watu elfu kumi na nane.

Lakini Mheshimiwa Mbunge mwenyewe wa Jimbo husika anasema idadi ya watu ni elfu arobaini. Sasa yupi tumwamini Mbunge au Naibu Waziri?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Kwa sababu shughuli zilizopo pale katika kijiji cha Lamadi ni nyingi na kubwa na kijiji kile kinajulikana Wilaya nzima ya Magu pamoja na Mara.

Je, Serikali kwanini isipeleke utaratibu mzuri ili kijiji hicho sasa kiwe Mji Mdogo?

**NAIBU SPIKA**: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Lamadi wanataka kuwa Mji mdogo kama Kibaigwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anazitaja takwimu hizi kwa sababu yeye yuko kule anajua ukuaji. Mimi ninazozitaja hapa, wala haziingii katika hii sensa ambayo tunazungumzia. Tunazungumzia takwimu tulizonazo kwa sasa. Inawezekana kabisa kwa *development* ya pale na ukuaji wao na *percentage* na nini inaweza ikawa imefika hapo.

Lakini sasa mimi nikiulizwa nimezitoa wapi mimi nitasemaje hapo? Ndiyo shida yangu hapa kwa sababu matokeo rasmi ya sensa yatatoka baadaye na tuliambiwa *figure* ya kitaifa; ndiyo maana sisi tumeona tuweke kwenye zile *quotation.*

Lakini hata hivyo ili kuwa na Mamlaka ya Mji mdogo unahitaji watu 10,000 tu hawa wapo 18,000. Kwa hiyo tayari hapa kwa kufuata taratibu tunazozisema hapa *already* hawa wameshakuwa na kigezo pale. Lakini nitakwenda ku-*verify* zaidi hizi Takwimu kama anavyoelekeza Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kujua kwamba ni nini hasa kinachosemwa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili na labda nieleze na kwa sababu najua kuna wengine wanataka kuuliza wakina Mheshimiwa Jenista Mhagama wote hawa ni watu wanaoshughulikia Mamlaka za Mji mdogo nafahamu.

Kwa kifupi kabisa tunachosema hapa na bahati nzuri umetamka, ukiuona mji unaanza kupandapanda kwa taratibu kama zile za Kibaigwa unachotaka pale ni kuuingiza huo mji katika mpango ili usije ukavurugika. Yaani usije ukafika mahali ukataka kuweka taa za umeme huna mahali za kuzipitisha, huna mahali pa kupitisha mtaro wa maji, huna mahali pa watoto kwenda kubembea na vitu vingine.

Kwa hiyo unaweza ukaweka viashiria vya mapema. Kwahiyo kitendo cha kuweka viashiria vya mapema na kitendo cha kuanzisha mamlaka ya mji mdogo ni kipindi cha mpito kuelekea mamlaka ya mji. Ndicho tunachotafuta hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Ndassa anachozungumza hapa kupeleka huduma hizo na nini, ndicho tunachokitafuta ili kuboresha huduma biashara ikue na maendeleo ya jamii yapatikane pale, hospitali zipatikane na maisha ya wananchi yaweze kuboreshwa zaidi. Sitaki kutaja miji ambayo imevurugika lakini wanafahamu kwamba miji imevurugika hapo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, hivi majibu ya namna hiyo ya mchakato, mpango, utaratibu, mkakati katika uanzishwaji wa miji midogo yanakwendaje? Kwa sababu katika maombi ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea, mji mdogo huo tunaouhitaji wa Madaba umetimiza vigezo vyote miaka takribani nane iliyopita mpaka idadi ya watu inazidi kuongezeka na vigezo vinazidi kuongezeka lakini mji ule hautangazwi. Hivi hiyo mikakati na utaratibu wa kutangaza na michakato inaishaje ili unitangazie mji mdogo wa Madaba sasa Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mhagama. Mimi nimekwenda mpaka Madaba yeye mwenyewe amenipeleka na amenionyesha Mji wa Madaba, nimeziona zahanati zilizoko kule ambazo zimekuwa vituo vya afya na kila kitu. Wala hapa haihitaji kutumia nguvu kubwa sana, nguvu kidogo tu ili kukumbusha. Kwa sababu moja ya sifa ya Serikali ni kukumbushwa na hiki tunachofanya hapa ni kukumbushwa kwa sababu ya majukumu yaliyomengi.

Nataka nikuthibitishie kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge ambaye niseme hapa mbele yako kwamba kwa kweli Mbunge huyu anapambana usiku na mchana kuwasaidia wananchi wake wote katika masuala haya. Tumekwenda Madaba pale sifa zipo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika sasa niseme kitu kimoja. Natamani ningekuwa na msamiati mwingine kuacha hiyo ya mchakato, jitihada sijui na nini; natamani ningekuwa nao ningesema hapa. Lakini niseme tu kwa kifupi hawa wote wanaoomba kuwa mamlaka ya mji mdogo na najua Mheshimiwa Ntukamazina ukimsimamisha hapa atauliza swali hilo, nawafahamu wote watasema maneno hayo. Wengi tu na kuna wengine Mawaziri ambao wako huku wanataka hivyo. Niseme kwa kifupi tu.

**NAIBU SPIKA**: Hata Paulina Gekul naye hivyohivyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, wote hao. Sasa ili tumalize wote wasije wakaendelea kuniuliza maswali hapa tukubaliane kwa kifupi tunachofanya kuanzisha Kata, kuanzisha vijiji, kuanzisha Wilaya, taratibu zote zipo.

Tunakusanya maombi yote ya nchi nzima na siku moja hivi tunafanya maamuzi yote kwa kupeleka mapendekezo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ndicho tunachofanya, hatuchomoki tukamtoa mmoja hapa. Wakisimama wa Mufindi wakija hapa Mafinga nao watakwambia hivyohivyo. Hatutoi moja tu hivi tukasema chukua, halafu kesho chukua na wewe na Rombo na wewe chukua ya kwako unakwenda. Tunazikusanya zote na nataka nikuthibitishie kwamba tunayo maelekezo kwamba tu-*compile* haya maombi yote ya vijiji, ya Wilaya yote tupeleke mapendekezo.

Kwa hiyo kazi hii inafanyika namwomba Mheshimiwa Jenista Mhagama asiwe na wasiwasi kwake na wataalam wameshatembelea na wamethibitisha kwamba mji ule unafaa kuwa mamlaka ya mji mdogo. *(Makofi)*

Na. 324

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Shinyanga**

**MHE. AZZA H. HAMAD (K.n.y. MHE. AHMED ALLY SALUM)** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliahidi kusaidia ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya iliyoko katika Jimbo la Solwa Kata ya Iselamagazi na Halmashauri ya Shinyanga imeomba maombi maalum Hazina mara mbili bila mafanikio:-

Je, katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 Serikali itatuhakikishia tutapata fedha za kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga haina Hospitali ya Wilaya na hivyo wakazi wake wamekuwa wakipatiwa huduma za rufaa katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Shinyanga ulianza katika mwaka wa fedha 2011/2012 ambapo hadi sasa Serikali imekwishatumia jumla ya shilingi milioni 270/- ikiwa ni Ruzuku ya Maendeleo.

Kwa mwaka 2012/2013, Serikali iliidhinishwa kiasi cha shilingi milioni mia mbili, kuendeleza ujenzi wa Hospitali hiyo. Serikali imeshatoa tangazo la Zabuni kukamilisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)*awamu ya tatu na kujenga wodi ya wanawake awamu ya kwanza.

Aidha nyumba moja ya mganga ipo hatua za mwisho za ukamilishaji, misingi ya nyumba mbili za watumishi imechimbwa na kumwagwa jamvi, wodi mbili, moja ya wanaume na nyingine ni ya wanawake zipo katika hatua za msingi iliyochimbwa na kujengwa. Pia nyumba ya kuhifadhia maiti msingi wake umeshachimbwa na kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha ujenzi wa hospitali hiyo unakamilika Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imepanga kutumia jumla ya shilingi 197,436,197/= kuendeleza ujenzi. Hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti na kuwepo kwa maombi maalum mengi katika Sekta ya Afya kuliko uwezo wa Serikali, Serikali imejiwekea mkakati wa kutenga fedha awamu kwa awamu katika kila mwaka wa fedha hadi kukamilisha ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Shinyanga kama ilivyoaanishwa hapo juu.

**MHE. AZZA H. HAMAD**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nimwulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa hospitali hii unaonekana kuwa na gharama kubwa sana na inavyoonekana itachukua muda mrefu sana ili hospitali ile iweze kukamilika.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kukubaliana na mimi sasa ili kupunguza msongamano mkubwa wa wagonjwa wanaokwenda katika hospitali ya Mkoa wa Shinyanga waweze kutoa kibali katika hospitali hii kwa sababu kuna majengo ambayo yamekamilika na kuna jengo la upasuaji ambalo liko tayari ili hospitali hii ianze kutoa huduma inayotakiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, wazo hili ni wazo zuri kwa sababu huwezi ukaacha watu wanasota wanapata matatizo na kama kuna alternative ambayo Mheshimiwa Mbunge ambayo iko pale. Lakini niseme tu kwamba wazo hili lazima tuliingize kwenye vikao vyetu. Lazima tuliingize kwenye Kamati ya Maendeleo na tuliingize kwenye Baraza la Madiwani, tuliingize katika *District Consultative Committee* na kama mmeshafanya hivyo mpitishe na kwenye *RCC* kwa sababu ina *financial implication* zake.

Kwa hiyo niombe tu kwamba sisi tutazingatia hayo maombi yakija kwetu sisi tutaangalia. Hatuwezi kuacha wananchi wanapata matatizo kule halafu unasema nendeni tu. Shinyanga penyewe pame-*bust* wanakwenda mpaka wa Geita na Wilaya nyingine zote wanakwenda kule. Kwa hiyo tunakubaliana na ushauri huu tutauangalia na tuufanyie kazi.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana name kwamba Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi inatatizo kubwa sana la *theatre* kwa ajili ya akinamama kiasi kwamba akinamama wengi wamekuwa wakifa kwa ajili ya

kupelekwa katika Hospitali ya *KCMC* na ile ya St. Joseph na tatizo hili ni la muda mrefu na Mheshimiwa Naibu Waziri analifahamu.

Sasa naomba kumwuliza ni lini ujenzi ule wa *theatre* utakamilika ili sasa Tanzania tuweze kuhakikisha kwamba tunakamilisha au tunafikia walau MDG-4 na 5?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri, utakuwa kwenye nafasi ya kulijibu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa kwenye nafasi ya kujibu kwa sababu kwanza naomba ni-*declare interest.* Hospitali hii ya Mkoa sisi watu wa Siha tunatibiwa huko huko. Kwa huyo mjue hilo; lakini niseme hapa kama alivyosema Mheshimiwa Susan Lyimo ni kweli sisi tumekwenda pale, yapo mambo mawili yanayofanyika katika ile hospitali kwa sasa hivi.

Kwanza ilikuwa ni kuweka vyumba vya upasuaji kwa ajili ya kusaidia zoezi la upasuaji ambalo limechukua muda mrefu sana na *concentration* ya fedha zilizopelekwa hata ukiangalia katika takwimu za Mkoa fedha zote zilizokwenda pale kwa ajili ya shughuli za maendeleo zote zimepelekwa pale. Milioni 700/- zimepelekwa kwa ajili ya kukamilisha hiki kitengo cha upasuaji kwa sababu ndicho kilionekana kwamba ni *priority.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pembeni tena pale kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge pameanzishwa wodi kwa ajili ya ya kinamama kubwa ya kisasa ambayo kwa hapa na Mheshimiwa Lyimo anafahamu zinatakiwa shulingi bilioni 14 kwa ajili ya kujenga hiyo wodi ya kinana. Tukasema nini? Tukasema moja tujaribu kuwa waangalifu. Tuangalie na watu wengine nje watusaidie na sisi Mkoa tuangalie kwenye *our own source* namna mbalimbali ambavyo tunaweza tukapa.

Lakini tukasema pia tuangalie uwezekano wa kufanya awamu kwa awamu, *though* tutazipata wapi hizo hela zote zinazozungumzwa? Kama nilivyosema fedha zote za mafungu yote tunaelekeza katika hiyo *theatre* ambayo tunazungumzia hapa.

Kwa hiyo ni pamoja na kutengeneza andiko tumezungumza na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Mkoa pamoja na *RAS* wanalifahamu jambo hili. Kwa hiyo, ni kweli kwamba pale pana hilo tatizo kwa sababu akina mama sasa msongamano ni mkubwa pale tutaona jinsi ya kuweza kusaidia kwa hayo maandiko na watu wengine kama wanaweza wakatusaidia *Development Partners* ili tuweze kuondoka katika katika hilo tatizo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Dkt. Kebwe Steven Kebwe.

Na. 325

**Mgogoro wa Mpaka Kata ya Wilaya ya Bunda na Serengeti**

*(Swali hilo liliondolewa na Mwuuliza swali)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuliondoa swali hili la Kijiji cha Rwemung'orori na Mekomariro, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali linaulizwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed Mbunge wa Ole.

Na. 326

**Mafanikio ya Mfuko wa Wajasiriamali**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED** aliuliza:-

Mwaka 1994 Bunge lilipitisha Azimio la kuanzishwa kwa Mfuko wa Wajasiriamali Wananchi (*NEDF*) ili uweze kutoa mikopo kwa wazalishaji na wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuondoa umaskini:-

(a) Je, malengo ya mfuko huo yamefanikiwaje?

(b) Je, ni mafanikio gani yamepatikana na mikakati gani iliyoandaliwa na *SIDO* ambao wamepewa jukumu la kuendesha mfuko huo?

(c) Je, mfuko huo una mtaji kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo wa Wajasiriamali *NEDF* ulianzishwa mwaka 1994 kwa Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa lengo kuu la kuwapa fursa wajasiariamali wadogo ya kupata mikopo yenye masharti nafuu ili kuweza kufanya biashara ya kupata mikopo yenye masharti nafuu ili kuweza kufanya biashara na kuondoa umaskini. *NEDF* imeweza kuchochea ongezeko na ukuaji wa wajasiriamali ndogo ambazo zimechangia kupanua wigo wa kukusanya kodi na mapato mengine ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, mafanikio ambayo *SIDO* imeyapata tangu kuanzishwa kwa mfuko huu ni pamoja na kutoa mikopo hadi vijijini. Kiasi cha shilingi bilioni 36.4 zilitolewa kwa njia ya mzunguko (*revolving*) kwa wajasiriamali wapatao 62,720 na ajira 126,418 zilipatikana kutokana na huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati uliopo kwa sasa ni kuendelea kuiongezea *SIDO* uwezo ili iweze kuwa na ofisi hadi katika ngazi ya Wilaya na kuwa na uwezo wa kuhudumia vijiji vingi. Aidha, Serikali itaendelea kuongezea fedha mfuko huu ili kuweza kupanua wigo wa kutoa huduma kwa wajasiriamali wengi zaidi kama ilivyokusudiwa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali kwa mtaji wa shilingi milioni 800 mwaka 1994 ambazo zimekuwa zikiongezwa na Serikali kila mwaka hadi kufikia shilingi bilioni 6.17 mwezi Machi 2013 kwa ajili ya kuendesha miradi ya uzalishaji na biashara kupitia mfuko huu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Bunge la Jamhuri ya Muungano ndiyo lilipitisha Azimio hili, na Mfuko huu ni wa Taifa, ninalotaka kujua, Je, kwa upande wa Zanzibar mfuko huu umepelekewa fedha kiasi gani?

Swali la pili, kama mfuko huu haukupelekwa upande wa pili wa Muungano. Nataka kujua ni lini Zanzibar itapata mgao wake kutoka fedha hizi? Kama hamtaki kutoa tunaomba leo Serikali itamke kwamba ninyi Wazanzibar hampewi?

**NAIBU SPIKA:** Maswali yanapaswa kuwa mawili tu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Ahsante nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mbunge angetaka kujua ni kiasi gani kimepelekwa Zanzibar na kama hakijapelekwa kitapelekwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ieleweke wazi kwamba Azimio hili lilipokuwa linaanzishwa mwaka 1994 halikuweza kuunganisha Zanzibar. Lilikuwa linahusu Tanzania Bara peke yake. Lakini kama Azimio linavyoonesha kwamba ni Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali. Kwa hiyo tafsiri ya Taifa ndiyo nafikiri Mbunge kwamba aanafikiri kwamba mfuko huu unaenda mpaka Zanzibar, lakini kwa utaratibu ulivyo mpaka sasa hivi haigusi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na sheria ambayo na ilianzishwa ya *SIDO* ambayo inasimamia mfuko huu sasa hivi *SIDO* inafanyiwa *review*.

*SIDO* imeanzishwa mwaka 1973 miaka 40 iliyopita sasa hivi inafanyiwa *review* na tutaangalia kuna uwezekano kama mfuko huu unaweza kufika hadi Zanzibar kwa sababu tunaamini kwmaba hata Zanzibar nako kuna Wajasiriamali kama Tanzania Bara, kwa hiyo hakuna kiasi chochote ambacho kimeshakwenda Zanzibar mpaka sasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanya, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Hivi mfuko huu ulipoandaliwa na fedha hizi zinatoka Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano, Benki Kuu ni chombo cha Sehemu mbili zote za Muungano, hawakuliona hili mwanzo kwamba na Zanzibar inahusika na mfuko huu na Zanzibar kunahitajika maendeleo kutokana na mfuko huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi, hawakuliona suala hili enzi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kweli busara inaonesha na haki inaonesha kwamba Azimio pale mwanzoni mwaka 1994 liliposema Taifa lilikuwa lina lengo labda mpaka Zanzibar lakini uendeshaji wa mfuko ulipokuwa umeanza na kusimamiwa na *SIDO* hili jambo kusema kweli halikuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunafanya *review* ya *SIDO* ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa mfuko huu, tuombe *Inshallah* kwamba sasa hivi itagusa Zanzibar. *(Makofi)*

Na. 327

**Kugundulika kwa Dhahabu - Kondoa Kaskazini**

**MHE. ZABEIN M. MHITA** aliuliza:-

Madini ya dhahabu yamegunduliwa katika Vijiji vya Tumbela, Changaa, Munguri na Maji ya Shamba katika Jimbo la Kondoa Kaskazini:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya utafiti ili kujua kiwango cha mashapo yaliyopo?

(b) Je, kwa nini wachimbaji wadogo wadogo walioanza uchimbaji mdogo mdogo wamesitishwa wakati walikuwa wakijitafutia kipato kwa njia ya kujiajiri wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa upo umuhimu wa kufanya utafiti wa kina wa madini katika maeneo ya vijiji vya Tumbela, Chang'aa, Munguri na Maji ya Shamba ili kujua wingi wa mashapo ya madini ya dhahabu katika maeneo hayo. Serikali kupitia wakala wa jiolojia Tanzania (*GST*), hufanya utafiti wa awali wa madini katika maeneo mbalimbali ili kujua madini yalipo.

Kwa sasa maeneo hayo yana leseni ya utafutaji mkubwa wa madini iliyotolewa tarehe 10 Desemba, 2012 inayomilikiwa na kampuni ya *Sterling Resources Ltd*. Aidha, kuna maombi ya leseni Nne ambayo yanaendelea kushughulikiwa. Hivyo, siyo rahisi kwa *GST* kufanya utafiti katika maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji unaoendeshwa katika maeneo ya Tumbelo, Chang'aa, Munguri na Maji ya Shamba ni uchimbaji usiofuata sheria, kwa kuwa wachimbaji wanaochimba katika maeneo hayo hawana leseni za kuwaruhusu kuendesha uchimbaji kwa mujibu wa sheria ya madini ya mwaka 2010. Kama nilivyoeleza katika kipengele cha kwanza hapo juu, maeneo haya yana leseni kubwa ya utafiti madini ya dhahabu na sheria hairuhusu kutoa leseni mahali penye leseni nyingine.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa, dhahabu ipo katika maeneo wanayoishi wananchi na maeneo mengine ni mashamba yao binafsi,

Je, kuna uhalali gani wa kumpa leseni ya uchimbaji mtu au kampuni ya kutoka nje na kumnyima mzawa aliyekwishaanza kazi hiyo ya uchimbaji?

Swali la pili, je, huku siyo kuwadhalilisha na kuwanyima haki wenye maeneo hayo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wanaomiliki maeneo ambako kunakuwa kuna madini wanayohaki kama walivyo watu wengine wowote, kwa sababu haki ya uchimbaji wa madini na haki ya kumiliki *surface right* na *mining right* zinatofautina ni haki mbili tofauti. Kwa hivyo, sheria ya madini haimkatazi mtu mwingine kuomba mahali ambako mtu mwingine ana shamba au ana nyumba ili mradi tu aweze kulipa fidia ya mtu aliyekuwa anaishi pale juu.

Kwa hiyo, kama wananchi wa maeneo hayo ya Tumbela, Munguri na maeneo mengine ya Maji ya Shamba kama wangeomba leseni kwa wakati wangeweza kupewa. Kama ni maeneo yao, huyo aliyeomba leseni hawezi akaendesha shughuli yeyote ya uchimbaji wa madini mpaka awalipe fidia zao, tena zile ambazo wataridhika nazo ndipo waendeshe uchimbaji.

**NAIBU SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa David Kafulila swali la nyongeza.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na tatizo kubwa katika Taifa hili ambapo baadhi ya Wawekezaji wanashika maeneo na wanakaa nayo kwa muda mrefu kama *speculators* na badala ya kuwekeza wanayafanyia udalali kwenye Mataifa mengine. Nakumbuka Waziri wa Nishati na Madini alipata kutoa kauli ya kwamba atafuta leseni za wawekezaji wote ambao wanakaa na maeneo kwa muda mrefu bila kuwekeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu Kata ya Buhingu kuna Mwekezaji yupo pale anasema anatafuta madini lakini anachukua mchanga kila kukicha hatujui anaupeleka wapi, tangu mwaka 1905 wakati wa Vita ya Majimaji mpaka leo bado anaendelea kutafuta na haondoki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupata kauli ya Serikali katika hili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sisi kwa mujibu wa sheria Wizara au Waziri anao uwezo wa kuzifuta baadhi ya leseni ambazo watu wamezishika kwa muda mrefu na hakuna wanachozifanyia chochote kile na utafiti unachukua muda mrefu, lakini sheria pia inawaruhusu walio na leseni hizo ku-*renew* hizo leseni. Wanapofanya hivyo ni kwa mujibu wa sheria siyo rahisi kuweza kumtoa.

Ingawa kusema toka mwaka 1905 vita ya Majimaji, sidhani kama ilikuwa mwaka 1905, lakini ninachotaka kusema ni kwamba hata kama wanamiliki maeneo hayo, wakawa wanafanya utafiti ambao haukamiliki tunao uwezo wa kuchukua hatua.

Baadhi ya hatua tumeshaanza na tumezifuta baadhi ya leseni nyingi tu hasa zile za maeneo ya uchimbaji wa *geothermo* na tunaendelea kuzifuta, tunapozifuta hizi ndiyo tunapochukua ile nafasi kuwapa wachimbaji wadogo maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Hii ya Kafulila ni mpya hii, utafiti wa zaidi ya miaka mia! Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba Mbunge wa Busanda, kwa niaba yake nimemuona Mheshimiwa Martha Mlata.

Na. 328

**Maeneo Maalum kwa Wachimbaji Wadogo Wadogo**

**MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA)** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alipotembelea kijiji cha Nyarugusu mwaka 2010 aliwaahidi wachimbaji madini wadogo wadogo kwamba watatengewa maeneo maalum kwa ajili ya kufanya shughuli zao za uchimbaji lakini mpaka sasa hawajatengewa maeneo hayo:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Raia kwa kuwatengea wachimbaji hao maeneo waliyoahidiwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Sheria ya Madini Na. 14 ya mwaka 2010 Kifungu Na. 16(a) na (b), Wizara yangu imekuwa ikitenga maeneo na kuwamilikisha wachimbaji wadogo wadogo wa maeneneo husika kadiri wamiliki wa leseni kubwa za utafutaji madini wanavyoachia maeneo yao wakati wa kuzihusisha.

Kwa upande wa Mkoa wa Geita, jumla ya viwanja 53 viligawiwa kwa wachimbaji wadogo wa Rwamgasa (viwanja 35) na Nyarugusu (viwanja 18) baada ya maeneo husika kuachwa wazi na Kampuni ya *IAMGOLD (T) LTD*. Mwaka 2007.

Aidha, kampuni ya *Shanta Mining (T) Ltd*. Imeamua kukabidhi Serikalini eneo la Mgusu Mkoani Geita ili ligawiwe kwa wachimbaji wadogo. Tayari viwanja 23 vimeshagawiwa kwenye vikundi vya wachimbaji wadogo ili viendeshe uchimbaji kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga maeneo kwa ajili wachimbaji wadogo wa Nyarugusu na maeneo mengine kadri hali itakavyoruhusu kwa kuhakikisha kuwa Sheria ya Madini haivunjwi. Sheria ya Madini inaruhusu kutenga maeneo maalum kwa wachimbaji wadogo kwenye maeneo yaliyo wazi na siyo kwenye maeneo yenye leseni zingine.

Napenda nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wachimbaji wa maeneo ya Nyarugusu kuwa na subira na kuunga mkono juhudi za Serikali katika kutafuta maeneo ya uchimbaji mdogo. Maeneo yakipatikana yatatengwa na kugawiwa kwao.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ambayo Naibu Waziri ameyatoa ya kuridhisha na kwamba hatua zilishaanza kuchukuliwa. Sasa ninaomba kumwuliza kwamba, kwa sababu ahadi ya Rais bado iko pale pale na wananchi wa Nyarugusu wanasubiri kwa sababu idadi yao ni kubwa, ninaomba awathibitishie zoezi hili litamalizika lini, maana sasa hivi tangu ile ahadi ni miaka mitatu?

Swali la pili; kwa kuwa, leseni kubwa zimekuwa zikiingilia wachimbaji wadogo, maana wachimbaji wadogo ndiyo wanakuwa wameanza kufanyakazi pale. Kwa mfano machimbo ya *Copper* ya Mkalama, Ibaga, ambako wachimbaji wadogo wamekuja wameondolewa amepewa mwenye leseni kubwa na wachimbaji wadogo tayari walishapimiwa yale maeneo na waliomba leseni, Serikali mliagiza kwamba watengewe yale maeneo.

Je, Waziri unawathibitishiaje wananchi wa Mkalama watapata haki yao kama mlivyowapimia awali kabla ya kumpa yule mwenye leseni kubwa? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Nyarugusu ipo ahadi ya Mheshimiwa Rais na jitihada kubwa inafanyika na Wizara kuweza kupata maeneo hayo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Utaona hata jibu langu la msingi nimeweza kutaja baadhi ya maeneo na idadi ya viwanja ambavyo tumewagawia wachimbaji wadogo.

Kwa hiyo, tutajitahidi kadri tunavyopata kuweza kuwapa wachimbaji wadogo zaidi kuliko kuhuisha hizo leseni ambazo kwa mujibu wa sheria kwa hakika yule anayemiliki leseni ana haki ya kuweza kuendelea lakini tunaendelea ku-*negotiate* nao kadiri tutakapopata maeneo tutawagawia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba kunakuwa kuna wachimbaji wadogo na wenye leseni kubwa wana wameza wale wadogo na wanachukua maeneo hayo makubwa na kuwaacha kama ilivyo kwa Mkalama, Ibaga kama alivyosema Mbunge. Niseme tu kwamba wananchi hawa wanapaswa kujua sheria inataka wafanye nini, wasianze uchimbaji mdogo bila kuwa na leseni.

Unaweza ukaanza uchimbaji pale huna leseni na baadaye akaja mwenzako akakukuta wewe unaendelea kuchimba anachofanya pale anaulizia tu wanazo leseni, kama hawana basi anachofanya anaenda kuanza mchakato wa kupata leseni. Anapopata leseni kule siyo rahisi mtoaji wa leseni akawa anaweza kujua nani alianza na nani alitangulia, au kuna wachimbaji wengine wadogo wako kule, wakati wengine wachimbaji hawa wakubwa huwa wanawaghilibu hawa wadogo kwamba tutashirikiana na ninyi, tutafanya pamoja na baadaye wanawageuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nichukue nafasi hii kuwaomba sana wananchi wote kwenye maeneo yote ya nchi hii ambako wanataka kufanya uchimbaji wa madini, wahakikishe kwamba wakishagundua kitu waende kuomba leseni, wakishapata leseni ndiyo waendelee na uchimbaji. Siyo waendelee kufukua fukua pale wakati leseni huna, atakapokuja mwingine akiomba atapewa leseni kwa hiyo atakumeza na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwaomba sana wananchi wawe wajanja sasa, sheria hii imetungwa toka mwaka 2010 lakini wananchi wetu wanapenda kazi ya madini lakini hawafanyi utafiti, hawataki kukubaliana na mawazo yanayotolewa kila siku na tumekuwa tukiwaeleza kila mara tunapokutana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwaomba na wale wananchi wa Mkalama waweze kufuata sheria, waombe leseni na sisi tutawafikiria.

**3FFRK3 MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa zaidi ya vijana 1,000,000 kutoka Mikoa mbalimbali wamejiri katika sekta hii ya uchimbaji mdogo mdogo na kwa vile sasa hivi wanahangaika hawana soko la uhakika na baada ya Benki Kuu kujiondoa katika shughuli hii ya kununua hasa dhahabu. Matokeo yake ni kwamba vijana hawa wanapunjwa. Serikali inakosa kodi ya mapato.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuandaa soko la uhakika kwa wachimbaji wadogo wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wako wachimbaji wengi wadogo na kwa hakika wanaweza wakawa wanapata madini mengi tu lakini tatizo kubwa pia limekuwa ni soko. Hili tumeliona na tumeanza jitihada za kutaka kuandaa soko na kwa sasa tunaandaa namna ya kuweza kuanzisha jengo moja kubwa ambalo litatusaidia ili kuweza kuwaweka kwenye *one stop centre* wanapokuwa wanapata madini yao.

Lakini nichukue changamoto hii na nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni jambo ambalo tunahitaji tuongeze kasi yake ili liweze kukamilika mapema kwa sababu kweli Serikali pia inapoteza mapato mengi sana kwa sababu uuzaji wake umekuwa wa kiholela wa madini mengi hususan dhahabu.

Na. 329

**Mapendekezo juu ya Muswada wa Sheria ya Vyombo vya Habari**

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI (K.n.y. MHE. MURTAZA A. MANGUNGU)** aliuliza:-

Mwaka 2006 Serikali ilitoa Muswada wa Sheria ya Vyombo vya Habari ambao ulionekana kuwa kandamizi na wadau wa vyombo vya habari walitoa mapendekezo mbalimbali ili kuuboresha:-

Je, mapendekezo yaliyotolewa na wadau wa habari yamezingatiwa kwa kiwango gani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijawahi kutoa Muswada wa Sheria kandamizi na haina nia ya kutunga sheria kandamizi kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuandaa Miswada ya Habari ulianza mwaka 2007 ambapo Serikali ilipokea maoni mbalimbali kutoka kwa wadau wa habari waliotaka kuwepo kwa sheria mbili za masuala ya habari; yaani Sheria ya Kusimamia vyombo vya Habari na nyingine ni Sheria ya Haki ya Kupata Habari.

Serikali baada ya kupokea mapendekezo ya utungwaji wa Sheria hizo, kwa sasa inaona ni muhimu kuwa na Sheria ya Kusimamia vyombo vya habari itakayounda vyombo muhimu vya kusimamia utendaji wa vyombo vya habari nchini na Sheria ya Habari ya kupata habari ikifanyiwa utafiti wa kutosha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kuona faida na umuhimu wa kuwa na Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari kwa wanahabari na wadau, tayari Baraza la Mawaziri limeridhia kutungwa kwa sheria hiyo na hivi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari ili uwasilishwe kwenye Bunge lako Tukufu kwa kujadiliwa na hatimaye kuwa sheria.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa ningeomba nimulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza utaratibu wa huu uwaandaaji wa Muswada umechukua muda mrefu sana na wadau mbalimbali wakiwemo Wabunge wamekuwa wakilalamika ucheleweshwaji wa Muswada huu na hata wakati wa hotuba ya Bajeti ya Wizara malalamiko yalikuwa ni mengi sana.

Je, ni lini hasa Serikali inaahidi kwamba Muswada huu utakamilishwa? Hilo la kwanza.

Swali la pili, nataka kujua kwamba Serikali imekuwa ikionekana vyombo vya habari vinakandamizwa. Je, Serikali inatoa kauli gani haswa kwa vile vyombo vimekuwa vikifungiwa kwa kutokana na kukiuka maadili ya uandishi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba ni kweli mchakato wa kutungwa kwa Sheria ya kusimamia vyombo vya habari imechukua muda mrefu kuanzia mwaka 2007. Lakini wakati wa majadiliano hapa ya Wizara ya Habari tulilihakikishia Bunge kwamba tayari MUswada huu sasa utawasilishwa Bungeni wakati wowote na katika majibu yangu ya msingi nimeeleza wazi kwamba Wizara yangu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inaandaa Muswada huu ili uwasilishwe Bungeni wakati wowote utakapohitajika. Hilo la kwanza.

La pili, ni kwamba Serikali haina nia ya kukandamiza vyombo vya habari, bali Serikali itahakikisha kwamba itasimamia Serikali zilizopo na zitakazotungwa kwa ajili ya vyombo vya habari ili vyombo hivyo viende na maadili na sheria ya vyombo habari inavyotaka. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi kuhusu jibu la lini kwenye Muswada huu wa Habari, watu wanauliza lini kila siku, hamna ratiba ya shughuli zenu? Ukisema kwamba

Muswada huu unahitajika, utakapohitajika. Huu ulishahitajika toka mwaka 2007. Kwa hiyo, tunataka jibu la lini ratiba yenu ya kuleta ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lini. Nimesema ni kwamba Serikali ni muhimili mmoja, Bunge ni muhimili mwingine. Tutakapopangiwa shughuli zozote sasa hivi ni shughuli za Bajeti. Ikiwezekana hata Bunge linalokuja tukapangiwa shughuli yoyote Serikali iko tayari kuwasilisha Muswada huo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Na. 330

**Kuzama kwa meli katika mkondo wa bahari – Nungwi**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Kumekuwa na hali ya kuzama kwa meli na vyombo vingine mara kwa mara katika mkondo wa bahari Nungwi. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa matukio hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2011 kumetokea ajali kadhaa katika eneo la mkondo wa bahari Nungwi. Matukio hayo ya kusikitisha yalisababisha vifo na upotevu wa mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia matukio ya namna hii na uchunguzi wa kina uliofanywa baada ya hapo kwa nyakati mbalimbali, kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wan chi Kavu na Majini *(SUMATRA)* imechukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha usalama wa usafiri baharini ili kuzuia ajali kama hizo zisitokee au zisijirudie. Hatua hizo ni pamoja na:-

Kufanya ukaguzi wa usalama wa vyombo vya baharini wa kawaida na kwa nyakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa vyombo hivyo vinakidhi viwango vya kutoa huduma kwa usalama kulingana na sheria, kanuni na taratibu.

Kuimarisha usimamizi wa meli na vyombo vingine vya baharini na taratibu za utoaji huduma kabla na baada ya safari kuanza ikiwemo ufuatiliaji na utunzaji wa taarifa na kumbukumbu muhimu za abiria na mizigo. Kusambaza taarifa za utabiri wa hali ya hewa hususani kuchafuka kwa bahari na kutoa tahadhari mapema kwa wadau wa usafiri majini ili kuzuia vyombo vya baharini visianze safari bila kuzingatia tahadhari zinazotolewa. Kupitia njia mbalimbali za habari na mawasiliano ikiwemo televisheni, redio, magazeti, na mikutano ya wadau kutoa elimu kwa umma na kwa waendeshaji na wamiliki wa vyombo vya usafiri wa majini kuhusu masuala mbalimbali ya usalama wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rai kwa wananchi kuwa wanapotumia vyombo vya usafiri wa majini wajali usalama wao. Pale wanapoona kuna uvunjifu wa Sheria za usafiri majini watoe taarifa kwa vyombo vya dola vilivyo karibu ili kuepukana na matukio ya ajali.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kati ya mwezi wa Juni na Julai upepo unakuwa mwingi baharini na bahari inachafuka sana. Je, Serikali iko tayari kuwepo ndege itakayofuatilia usafiri katika ukanda huu wa Bahari?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli miezi hii ya Juni, Julai na Agosti hali ya maziwa na bahari huchafuka sana. Tunacho Kituo Dar es Salaam *MRCC* ambacho kinajihusisha na utoaji wa habari za ajali zinavyotokea. Kwa sasa vyombo vya dola vinafahamishwa mara ajali inapokuwa imetokea. Kwa hiyo ni pamoja Polisi, Jeshi la Wananchi na Mamlaka zingine za dola.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Katika miaka ya awali ya 1980 na 1990 ukanda wa Pwani, Lindi, Mtwara na Tanga kulikuwa na meli ambazo zilikuwa zinasaidia kusafirisha mizigo na ikapelekea kupunguza mfumuko wa bei katika maeneo yale. Kwani meli husafirisha mzigo mkubwa na gharama zake za usafiri zinapungua. Je, sasa hivi Serikali ina mkakati gani katika kuleta tena meli badala ya zile meli za *MV Mtwara* na *MS Lindi* kupotoea? Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate taarifa hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli zamani zilikuwako meli zilizomilikiwa na Serikali zilizofanya kusafirisha watu na mizigo kuanzia bandari za Dar es Salaam-Zanzibar kuelekea Mtwara. Meli hizo zilizeeka, na Shirika la *TACOSHILI* lilifungwa. Sasa Serikali inawahamasisha wawekezaji wafanyabiashara wajenge meli kwa ajili ya kusafirisha abiria kwenda sehemu hiyo. Changamoto iliyopo ni kwamba barabara inakaribia kukamilika kwa hivyo wengi wanaona ni rahisi na mkato zaidi kutumia barabara kuliko usafiri wa majini. Lakini bado Wizara inawahamasisha wadau mbalimbali wenye uwezo wa kufanya hivyo wanunue vyombo hivi vya majijni kwa ajili kurahisisha usafiri wa mizigo kulekea maeneo ya kusini. *(Makofi)*

Na. 331

**Meli mpya – Ziwa Victoria**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Mwaka 2010 Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kutupatia meli mpya Ziwa Victoria itakayokuwa ikitoa huduma. Je, ni lini meli hiyo itapatikana na kuanza kazi?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa mwaka 2010, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria.

Katika kutekeleza ahadi hiyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya mazungumzo na Serikali ya Denmark kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa *(DANIDA)* kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa meli mpya tatu, moja katika kila ziwa yaani (Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa) na ukarabati wa meli za MV Victoria, MV Umoja na MV Serengeti, Serikali ya Denmark imekubali kufadhili mradi huu kwa kutoa mkopo nafuu yaani *(mixed credit funding)* ambao Serikali ya Tanzania itagharamia asilimia 50 na Serikali ya Denmark asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya uhifadhi wa mazingira wa mradi huu ilikamilika Aprili, 2013 na mradi huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwishoni mwa mwaka 2013 na kukamilika mwaka 2018. Mradi huu utagharimu dola za Kimarekani milioni 60.

Aidha, Serikali inawasiliana na Serikali ya Korea Kusini kupitia Benki ya Exim ili kupata mkopo wenye masharti nafuu wa kujenga meli 3 za abiria na mizigo katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kwamba, ifikapo mwaka 2015 meli hizo ziwe zimekamilika.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ambayo nimepokea lakini sikuridhika nayo. Ni dhahiri kwamba kwa ahadi ya 2010 tathmini imekamilika mwezi uliopita kwa kweli kazi haijafanyika.

Je, Serikali inasubiri na meli hii iliyopo, maana yake hii iliyopo sasa hivi ya Victoria ni ya zamani sana. Miaka ya 1950 au 1960 hivi. Imechokaa imechakaa. Kwa hiyo mnasubiri na yenyewe izame kama ilivyozama *MV Bukoba* watu wafe ndiyo wajenge nyingine?

Swali la pili, sasa hivi tuna barabara kutoka Mwanza na Kahama kwenda Bukoba, barabara nzuri ya lami, Serikali imejenga Serikali ya CCM. Lakini kutokuwepo na meli ya uhakika mizigo mikubwa mikubwa, mafuta *cement* vifaa vya ujenzi na vyakula vinapita barabara viharibu barabara hata miaka miwili haina ile barabara imeanza kuharibika.

Sasa mnataka na barabara hii iharibike tusiwe na barabara meli hakuna. Kwa nini jitihada za kutosha hazifanyiki kuleta meli hii ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tathmini ya athari ya mazingira imekamilika Aprili mwaka huu. Awali sharti hili kwa wenzetu wa DANIDA halikuwapo na mambo yote ya msingi yalikuwa yamekamilika. Sababu ya kwanza iliyokuwa imetolewa kucheleweshwa ujenzi wa meli hizo ilikuwa kwamba Mhandisi Mshauri ambaye alikubali kuja kufanya kazi Tanzania alikuwa na kazi nyingine Amerika ya Kusini na tulitoa taarifa hiyo hapa Bungeni. Wakati amepatikana ndiyo akaja na sharti jipya hili la athari za mazingira.

Tumeifanya kazi hiyo kwa haraka na tumekamilisha mwezi Aprili na tunamaini kwamba ujenzi utaanza kama nilivyosema. Sasa kwamba watu wazame ndiyo ijengwe nyingine tusiombe hilo litokee kwa sababu meli zipo zinafanya kazi na tunahakikisha kwamba usalama wa wasafiri na mizigo unazingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuharibika kwa barabara kutokana na mizigo kuongezeka. Naomba tu nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba ndani ya Ziwa Victoria mbali na meli za watu binafsi zinazosafirisha mizigo kutoka Mwanza na maeneo mbalimbali kwenda Bukoba, *Port Bell* Uganda na Kisumu ziko meli karibu ya nne za Serikali zinazomilikiwa na *Marine Services Company* ambazo zinafanya kazi ya usafirishaji wa mizigo kuelekea Bukoba na sehemu hizo zingine nilizozitaja.

Kwa hiyo hata hii meli ya abiria itakapojengwa hatutegemei kwamba itapunguza sana mzigo ambao unasafirishwa tofauti na hizi meli zilizopo sasa hivi.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kukataa kwamba meli ile iko vizuri. Lakini ningependa nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba MV Victoria siyo meli salama sasa hivi kwa kusafirisha abiria.

Lakini pia ningependa nijue kwa kuwa hapo zamani kulikuwa kuna meli ambayo ilikuwa ikipita Mesome mpaka Nyamirembe kwa ajili ya usafiri wa watu wanaoishi kando kando mwa Ziwa Victoria.

Je, lini sasa meli hii itaanza kazi ya kupita tena Mesome na maeneo jirani mpaka Nyamirembe na maeneo jirani mpaka Nyamirembe ili kuweza kuwarahisishia wananchi wanaoishi kando kando ya ziwa kupata usafiri ulio salama? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza labda ni-*declare* pia kwamba mimi jimbo langu liko huko huko ziwani ni mdau mkubwa wa vyombo hivi vya majini katika eneo hilo na kwa hivyo vinapoacha kufanya kazi mwathirika wa kwanza ni mimi.

Kwa hivyo Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba meli ya Victoria nimeitembelea mwenyewe na wataalam wa *SUMATRA* na watu wa DMI mara mbili kujiridhisha kwamba angalau viwango vyote vya usalama ambavyo *SUMATRA* wameviweka kwa ajili ya meli hiyo vimefuatwa. Liko suala la uchakavu wa meli. Hii hatukai, meli ni ya siku nyingi ya mwaka 1961, lakini habari ya usalama wake kwa maana ya *plates* na vifaa vya uokoaji vyote tumehakikisha kwamba viko vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu meli ambazo zilikuwa zinapita huko Ziwani katika visiwa vyetu mbalimbali, kwa sasa haziendi kwa sababu mbalimbali. Moja, ni ya kibiashara. *Marine Services* wameachiwa jukumu la kujiendesha kibiashara. Wao meli zao ni kubwa na hawawezi kutunga nauli kama vile wanavyofanya wafanyabiashara tofauti, wao wamedhibitiwa ili kutoa huduma nafuu kwa wananchi. Kwa hivyo, pale walipoona kwamba, wanakwenda kwa hasara, wameacha kwenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini maeneo mengine wameacha kwenda kwa sababu ya upungufu wa kina cha maji. Kina cha maji kimepungua katika Ziwa Viktoria na kwa hivyo, magati yale ambako walikuwa wanafikia mengi imekuwa haiwezekani kwenda huko, kwa hivyo, wamesitisha kwenda huko. Tuko katika programu ya kujenga magati mapya ndani ya Ziwa Viktoria na kurefusha yale ambayo yapo, ili kupata kina cha kutosha, kuweza kuzifanya meli hizi zifike maeneo hayo.

Na. 332

**Gharama za Simu**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kinyume na ahadi iliyotolewa na Serikali kuwa baada ya kuwekwa Mkongo wa Taifa gharama za simu zitashuka na mtandao wa *internet* utakuwa wa haraka, gharama za simu bado ziko juu na mtandao wa *internet* unakwenda taratibu sana na wakati mwingine haupatikanai kabisa:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa mchanganuo wa jinsi gharama za kupiga simu *(airtime)* zilivyoshuka kama ilivyoahidiwa?

(b) Je, Serikali imefikia hatua gani ya kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Serikali zinaunganishwa na Mkongo wa Taifa ili kuondokana na gharama za mawasiliano ya simu katika taasisi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za simu za muda wa maongezi zimekuwa zikishuka mwaka hadi mwaka ambapo miongoni mwa sababu zilizosababisha kushuka ni ushindani wa soko pamoja na kuanza kutumika kwa mkongo wa mawasiliano wa Taifa. Kwa huduma za simu za kiganjani, gharama zimeshuka kutoka Sh.147/= kwa mwaka 2009 hadi kufikia Sh.62/= kwa dakika kwa mwaka huu; hilo ni punguzo la 57%.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kupiga simu kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine, yaani *inter-connection fees,* zimeshuka kutoka Sh.115/= ilivyokuwa huko nyuma hadi Sh.34.92/= iliyoanza kutumika mwezi Machi mwaka huu. Aidha, gharama hizi zitaendelea kushuka mwaka hadi mwaka na dhamira yetu ni kwamba kusiwe na gharama kabisa za muunganisho wa kupiga simu kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki, gharama zilishuka kutoka Sh.599/= mwaka 2001 hadi Sh.326/= mwaka jana. Kwa upande wa gharama za simu za Kimataifa yaani nje ya Afrika Mashariki, zimeshuka kutoka Sh.2,305/= mwaka 2001 hadi kufikia Sh.492/= mwaka jana.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa zaidi ya taasisi 23 za Serikali, zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Mpaka sasa Ofisi za Wakuu wa Mikoa 24 na zenyewe zimeunganishwa na kuna mtambo pale unaitwa *Tele-Conferencing* ambapo Wakuu wa Mikoa wanaweza kuongea wenyewe kwa pamoja na kuongea na Makao Makuu ya nchi kupitia mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali, inaendelea na jitihada za kuhamasisha taasisi ambazo hazijaunganishwa katika Mkongo wa Taifa, ili ziweze kuunganishwa lakini pia inaandaa mpango wa kuweka mfumo madhubuti wa mawasiliano *(Tele-conferencing facilities)* kwenye kila Ofisi za Serikali.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni muungano wa nchi mbili; Tanzania Zanzibar bado hawajaunganishwa na Mkongo wa Taifa lakini vilevile baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara bado haijaunganishwa na Mkongo huu wa Taifa na hivyo kufanya mawasiliano kuwa magumu. Sasa hivi Halmashauri zetu zote katika Vitengo vyake vya Uhasibu, zinatakiwa vitumie mfumo wa *EPICO* lakini mara nyingi baadhi ya Mikoa ambayo haijaunganishwa na Mkongo wa Taifa, Halmashauri zao huwa zinapotea kwenye mtandao, kwa hiyo, mara nyingi kazi hazifanyiki katika Halmashauri kwa kuwa, *internet* inakuwa chini. Je, ni lini Serikali itakamilisha kuunganisha nchi nzima katika Mkongo huo wa Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kurahisisha somo la *TEHAMA,* kuna mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba shule zote zinakuwa na *internet,* nafikiri hata jana katika semina mlitwambia, lakini bado miundombinu ya shule zetu ni duni sana, hakuna umeme, lakini vilevile hakuna *Computer Labs,* shule zetu hazina madirisha, hazina sakafu, je, mpango huu utakamilishwaje? Nakushukuru.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza na tumepata fedha kwa ajili ya awamu ya tatu ya Mkongo wa Mawasiliano ya Taifa na kama mtakumbuka Rais wa China alikuja nchini miezi miwili iliyopita na tukasaini mkataba wa karibu dola milioni 403 kwa ajili ya awamu ya tatu ya Mkongo wa Taifa ambayo itatupeleka kwenye kila Wilaya pamoja na kutengeneza *Data Centres* katika sehemu mbalimbali za

nchi yetu. Kwa hiyo, tutakapokamilisha hiyo awamu ya tatu, basi swali lako litakuwa limejibiwa kwamba, kila Wilaya itakuwa imefikiwa na Mkongo wa Taifa. Kwa maana hiyo, kila Halmashauri na kila Ofisi ya Halmashauri na yenyewe itakuwa imefikiwa na huduma hiyo, kwa hiyo, itakuwa ni rahisi huduma za kiutawala na kiuhasibu kama *EPICO* kufanyika kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mhonga kwamba bado shule zetu zina changamoto mbalimbali za miundombinu na kwa hiyo, inakuwa ni vigumu kufikisha huduma za *internet* kwenye shule zote. Tumeanza mradi mkubwa sana unaitwa *TZ 21* na tumeanza *pilot* katika Mkoa mzima wa Mtwara ambapo tumeweka *internet* katika kila shule ya msingi na vilevile upande wa Zanzibar. Dhamira yetu ni kwamba, kwa kadiri tutakavyoendelea ku-*improve* miundombinu ya shule zetu, basi shule hizi zitapata huduma za *internet* na huduma nyinginezo za *TEHAMA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkongo wa Taifa, unaenda Zanzibar, kupitia waya wa umeme ambao utapelekwa kule na *TANESCO,* vilevile na Pemba. Kwa hiyo, nchi yetu yote itaunganishwa na Mkongo wa Taifa, haraka iwezekanavyo.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali imekuwa ikizungumzia faida zitokanazo na matumizi ya *new technology,* ikiwemo *internet,* lakini kwa bahati mbaya Watanzania walio wengi hawajafahamishwa madhara yatokanayo na matumizi ya *new technology,* ikiwemo madhara ya kiafya, madhara ya upungufu wa ajira na madhara ya uhalifu utokanao na matumizi ya *new technology,* kwa lugha nyingine *cyber crime.* Serikali, ni lini itaweka msisitizo katika kuwaelimisha Watanzania kuhusu madhara haya yanatokana na matumizi ya *new technology,* ili waweze kuchukua tahadhari?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia ni kama kisu, unaweza kukitumia kwa kufanya uhalifu, kwa

kumchoma mwingine na kufanya madhara na vilevile unaweza kukitumia kwa kukata nyama na kutengeneza mambo na kufanikiwa. Kwa hiyo, nadhani jukumu la kuwaelimisha wananchi kuhusu madhara ya teknolojia na ukituuliza sisi, teknolojia ina manufaa makubwa zaidi lakini ni kweli teknolojia yoyote hata *nuclear* inaweza kutumika kwa kuwasha umeme na vilevile inaweza kutumika kama silaha. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sote kuendelea kuwahimiza wananchi matumizi mazuri ya teknolojia kama ambavyo tunaendelea kuhimiza matumizi mazuri ya vitu vyovyote ambavyo vina manufaa kwa jamii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nimuulize swali dogo sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huduma ya simu ni huduma kama zilivyo huduma nyingine na huduma inatakiwa uilipie baada ya kuipata huduma ile, ni kwa nini, tunavyopiga simu kabla unayempigia hajapokea simu, tayari umeanza kukatwa hela kwenye simu na hata kama yule unayempigia hajapatikana, bado unakuwa umekatwa hela kwenye simu yako, huo sio wizi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunapokea malalmiko mengi kuhusu hoja aliyotoa Mbunge na moja ya mambo ambayo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inayashughulikia ni hilo. Tunaamini kwamba kwa kufunga mtambo wa kufuatilia mawasiliano, ambapo Serikali itaufunga mwaka huu, ambapo moja ya jukumu lake kubwa ni kuimarisha ubora wa huduma ya mawasiliano, ikiwemo simu kukatika mara kwa mara, ikiwemo kujaribu mara nyingi bila kupata na ikiwemo dhuluma inayotokana na kukatwa fedha bila kuongea. Kwa hiyo, ni jambo ambalo Serikali inalishughulikia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote mlioshiriki katika *session* ya asubuhi.

Sasa kwa haraka haraka nipitie matangazo ya wageni wetu na masuala ya kazi.

*Speaker's Gallery,* tunaye ndugu Rof Pash, Mkurugenzi Mkazi wa *Fredrick Ebenstitan Face,* ambaye ameambatana na Msaidizi wake ndugu Amon Petro. Karibuni sana, tunafurahi sana ujio wenu na tutakutana saa 7.00 kamili ofisini kwangu. *(Makofi)*

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wageni 74, ikiwa ni pamoja na Madiwani na baadhi ya Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Gairo; pale mlipo, wageni kutoka Gairo? Wageni wa Mheshimiwa Mbunge wa Gairo? Ahsante sana, karibuni sana. Niwahakikishie jirani zangu, ndugu zangu wa Gairo kwamba, Mbunge wenu Mheshimiwa Shabiby, anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni, kuwawakilisha. Pelekeni salamu kwa wingi kutoka Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 59, ambao ni Timu ya Mpira ya Machava kutoka Mkoa wa Kilimanjaro. Mnakaribishwa sana hapa Bungeni, tuna furaha kubwa sana kuwa pamoja nanyi. *(Makofi)*

Wanafunzi 28 kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari cha *DSJ,* Dar-es-Salaam. Karibuni sana wanafunzi, mjifunze namna ambavyo Bunge linafanya kazi. Baadhi yenu baadaye m-*specialize* kuwa Waandishi wa Habari za Bunge. Tutafurahi sana mkifikia huko. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Zungu, ndugu yetu Hassan Ndembela na Asha Digalu, pale mlipo tunawakaribisheni sana. Mheshimiwa Zungu, yuko hapa. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 7.00 mchana leo, ukumbi 227.

Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Zungu anawaomba wajumbe wote wakutane Ukumbi namba 231, saa 7.15 leo mchana.

Kamati ya Bunge la *LAAC,* Mwenyekiti wake Rajab Mohamed, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo kukutana ukumbi 219, saa 7.15 mchana.

Naomba Wageni wa Mheshimiwa Waziri kutoka Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia mliopo katika *gallery* ya Spika, msimame. Karibuni sana wote kutoka Wizara hiyo, tunawakaribisha, tunawatakia mawasilisho mema na mjadala mwema wa bajeti yenu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Iddi Azzan, anaomba niwatangazie matokeo ya mchezo wa Mpira wa Miguu na Mpira wa Pete kati ya *Bunge Sports Club* na *NSSF,* uliochezwa siku ya Jumamosi, tarehe 1 Juni, 2013. Mgeni rasmi akiwa ni mimi mwenyewe, Naibu Spika.

Kwenye Mpira wa Miguu, *Bunge Sports Club* ilifungwa na *NSSF* kwa bao moja kwa bila. Nyota kwa upande wa Mpira wa Miguu wa Timu ya *Bunge Sports Club,* alikuwa Mheshimiwa Ahmed Ngwali. Kwa hiyo, kombe likaenda *NSSF;* tulilikosa kwa almanusura na mpira huo ulioneshwa *live* na *television* ya *Star,* tunawashukuru sana kwa kufanya hivyo. Pamoja na Kamati ya Ufundi, iliyoongozwa na Mheshimiwa Nkumba lakini bado hatukuweza kurudisha goli hili. *(Makofi/ Kicheko)*

Mpira wa Pete, *Bunge Sports Club* walishinda, Mpira wa *Netball,* kwa mabao 31, *NSSF* wakiwa na mabao 11. Nyota katika mchezo huo kwa upande wa Mpira wa Pete alikuwa Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Ester Matiko. Pongezi nyingi ziende kwa Kamati za Ufundi ambapo kama nilivyoeleza kwa juzi ilikuwa chini ya Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kusaidia kuhakikisha kwamba timu zetu zinashinda. *(Kicheko/Makofi)*

Tangazo la mwisho, Waheshimiwa Wabunge linatoka kwa Mwenyekiti wa Wanachama na Washabiki na Wapenzi wote wa *Simba Sports Club* Bungeni, Mheshimiwa Azzan Zungu, anawaomba Wanachama hao na Mashabiki na Wapenzi, mkutane saa 7.00 mchana, Ukumbi wa Msekwa, kwa kikao kifupi sana cha mkakati wa kuchukua Kombe la Ubingwa wa nchi katika Ligi ijayo. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia

**NAIBU SPIKA:** Naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na bila karatasi yoyote anakuja kwa mawasiliano na teknolojia, Mheshimiwa Profesa, karibu sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge, kuhusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2012/2013 na malengo ya Wizara katika bajeti ya mwaka 2013/2014. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sisi sote kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge unaojadili bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niungane na Waheshimiwa Wabunge, ndugu na marafiki katika kuwafariji

na kuwapa salaam za rambirambi familia, ndugu na wapiga kura wa Marehemu Mheshimiwa Salum Hemed Khamis aliyekuwa Mbunge wa Chambani *(CUF)*. Daima tutamkumbuka kwa ucheshi wake, ukarimu, upole, busara, jitihada na moyo wake wa kujitolea katika kuwaletea familia yake na wananchi wa Jimboni kwake maendeleo na usawa. Mungu atupe moyo wa subira katika kipindi hiki cha msiba na aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hotuba za bajeti kwa mwaka 2013/2014. Aidha, hotuba hizo zimeelezea mafanikio, changamoto, matukio mbalimbali na hali ya uchumi wa taifa letu kwa mwaka 2012/2013 na mipango kwa mwaka 2013/2014. Pia, nawashukuru Mawaziri wote walionitangulia kwa kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo zinahusu Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Vilevile, ninawapongeza Waheshimiwa wabunge wote kwa michango yenu makini mliyoitoa kwa nia ya kuboresha mikakati ya utekelezaji wa mipango iliyowasilishwa na Serikali kwa maendeleo ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za pekee kwa wale wote walioniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kipindi kilichopita na ambao wameniwezesha kuandaa mpango wa mwaka wa fedha 2013/2014 na kuboresha hoja ambayo ninaiwasilisha katika hotuba hii. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa January Yusuph Makamba, Mbunge, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, Dokta Florens Martin Turuka, Katibu Mkuu, Profesa Patrick James Makungu, Naibu Katibu Mkuu, watendaji wote katika Wizara, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao katika kufanikisha uwasilishaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), kwa ushauri wao unaotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa tija na ufanisi zaidi. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mhe. Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki (CHADEMA) ambaye ni Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii ninayoiwasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inayo dhamana ya kusimamia, kuimarisha na kuendeleza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili viweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi. Vilevile, Wizara inayo dhamana ya kusimamia na kutoa miongozo ya kiutendaji kwa Taasisi, Mashirika, Tume na Kampuni ambazo zinafanya kazi chini yake. Taasisi hizo ni:-

(i) Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam.

(ii) Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.

(iii) Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha.

(iv) Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania.

(v) Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia.

(vi) Shirika la Posta Tanzania.

(vii) Kampuni ya Simu Tanzania.

(viii) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

(ix) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia katika kipindi cha mwaka wa fedha

2012/2013, imetekeleza majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/ 2013, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010–2015. Aidha, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imezingatia Sera, Mikakati, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayoongoza Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia ya mwaka 2010, Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo ya mwaka 2010, Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996, Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mipango na Bajeti ya mwaka 2012/2013. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilitengewa jumla ya Sh.70,107,712,000. Kati ya fedha hizo, Sh.30,275,286,914 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo za matumizi ya kawaida Sh.23,269,110,000 zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara na Sh.7,006,176,914 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa zilikuwa Sh.39,832,425,000 ambapo fedha za ndani zilikuwa Sh.38,706,547,000 na fedha za nje zilikuwa Sh.1,125,878,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu yaliyotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake katika kipindi cha mwaka 2012/2013 ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji katika sekta ya mawasiliano. Ujenzi na upanuzi wa matumizi ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, inaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchini. Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye awamu

tano (5) umekamilika katika Awamu ya kwanza na ya pili ukiwa na jumla ya kilomita 7,560 mkongo huo umeunganisha Makao Makuu ya Mikoa 24 ya Tanzania Bara. Pia, Mkongo umeiunganisha Pemba kupitia waya wa umeme uliopo kati ya Tanga na Pemba. Zanzibar itaunganishwa kupitia waya wa umeme unaowekwa kati ya Dar es Salaam na Zanzibar ambapo uwekaji wa waya huo unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2013, tayari makampuni saba ya mawasiliano *(Telecom Operators and Internet Service Providers -ISPs)* ya hapa nchini yameunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa ajili ya kutoa huduma za mawasiliano kwa wateja. Makampuni hayo ni *TTCL, Airtel, Tigo, ZANTEL, Iffinity Africa, Simbanet na Vodacom.* Aidha, mkataba wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano awamu ya tatu (3) itakayohusu ujenzi wa kuziba mapengo *(missing links)* na vituo mahiri vya kutunza kumbukumbu *(data centres)* katika jiji la Dar es Salaam umekamilika na kusainiwa tarehe 24 Machi 2013, kati ya Benki ya *EXIM* ya China na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa ziara ya Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu China nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikiwa kwa hatua hii ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa kumeijengea Tanzania uwezo mkubwa na kuleta manufaa makubwa ya kijamii na kiuchumi ikiwemo ajira, upatikanaji wa huduma bora zaidi na mawasiliano kufika kwenye eneo kubwa la nchi na kwa bei nafuu zaidi. Kwa mfano, huduma za intaneti 7 zimeshuka kutoka Sh. 36,000 kwa *Gigabyte (GB)* moja mwaka 2009 hadi Shilingi 9,000 kwa *Gigabyte (GB)* moja mwaka 2013, hii ikiwa ni punguzo la zaidi ya asilimia 75. Katika eneo la usafirishaji wa mawasiliano kwa masafa marefu, gharama za usafirishaji wa mawasiliano kwa umbali wa kilomita 1,000 kwa kasi ya *Megabits* mbili (2) kwa sekunde *(Mbps)* zimeshuka kutoka Dola za Kimarekani 20,000 kwa mwezi mwaka 2009 hadi kufikia Dola za Kimarekani 160 kwa mwezi mwaka 2013, ambalo ni punguzo la zaidi ya asilimia 99.2. Kwenye huduma ya simu za kiganjani, gharama zimeshuka kutoka shilingi 147

kwa dakika mwaka 2009 hadi shilingi 62 kwa dakika mwaka 2013, sawa na punguzo la asilimia 57.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa mengine ambayo ni muhimu sana kwenye uchumi wa nchi yetu na katika mahusiano ya kikanda, ni kutoa huduma za mawasiliano kwa nchi jirani kupitia Makampuni ya nje yaliyounganishwa kwenye Mkongo. Hadi hivi sasa, Kampuni ya Simu ya *MTL* ya Malawi, *UCOM* ya Burundi, *MTN* ya Rwanda na Kampuni ya Simu ya *MTN* na Airtel za Zambia zimeunganishwa kwenye Mkongo wa Mawasiliano wa Baharini wa *SEACOM* kupitia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Tume ya Taifa ya TEHAMA pendekezo lililowasilishwa Serikalini na wadau mbalimbali nchini la kuanzisha Tume ya TEHAMA liliridhiwa na Baraza la Mawaziri mwezi Juni 2012. Kikosi Kazi *(Task Force)* kilichoundwa kufuatia agizo la Serikali kusimamia jukumu hili kinachojumuisha wataalam kutoka Taasisi za Serikali na Kampuni kutoka sekta binafsi kimekwisha piga hatua kubwa katika utekelezaji wake. Hivi sasa, rasimu ya mapendekezo ya Muundo, Majukumu na Uwezo wa Kisheria imekamilika na inaendelea kujadiliwa katika vikao mbalimbali vya wadau. Kwa ratiba ya utekelezaji iliyopo, Tume hii inategemewa kuanza kazi zake katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa Mfumo wa Kuratibu Huduma za Mawasiliano Nchini *(Telecommunication Traffic Management System).* Serikali inaendelea kutekeleza uwekaji wa Mfumo wa Kuratibu Huduma za Mawasiliano nchini *(Telecommunication Traffic Management System)* ambao utahakikisha kuwa mawasiliano yote ya ndani na nje nchi yanapitia kwenye mlango mmoja na hivyo kuboresha udhibiti wa mawasiliano. Udhibiti huu utawezesha kuhakiki mapato yanayotokana na huduma za sekta ya mawasiliano husSo yale yanayotokana na mawasiliano ya nje ya nchi na hivyo kuwezesha Serikali kupata mapato sahihi yanayotokana na Sekta ya Mawasiliano nchini ikiwemo uwezekano wa mapato hayo kuongezeka kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, udhibiti huu utawezesha kuimarisha usalama na matumizi sahihi ya mtandao. Tayari Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imekamilisha mchakato wa kupata Mwendeshaji Mshiriki katika mradi huu baada ya mchakato wa zabuni kukamilika ambapo Mkataba umesainiwa na Mwendeshaji huyo tarehe 22 Machi, 2013. Aidha, kanuni za kusimamia mfumo huu zimejadiliwa na wadau na hivi sasa zinafanyiwa mapitio na Mwandishi Mkuu wa Sheria ili kuzikamilisha. Serikali, kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, inaendelea kukamilisha taratibu za mwisho katika kuendesha mfumo huu na unatarajiwa kuanza kutumika ifikapo Julai 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizi za kutumia chombo hiki cha kuratibu mawasiliano kwa lengo la kuongeza mchango wa sekta kupitia kodi na kuboresha usalama wa mtandao, zipo jitihada nyingine zinazoendelea katika maeneo yote mawili. Kwa upande wa usalama kwenye mawasiliano, juhudi zinazoendelea ni pamoja na uanzishwaji wa Kikosi Maalumu cha Ulinzi wa Kieletroniki na uandaaji wa Sheria ya Usalama wa Mtandao ambavyo vimeelezwa katika sehemu nyingine za kitabu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka kwa gharama za simu kati ya mitandao ya mawasiliano (*Interconnection Charges).* Bei za uunganishaji wa mawasiliano kutoka mtandao mmoja kwenda mtando mwingine *(offnet interconnection)* - mfano kutoka mtandao wa *TTCL* kwenda mtandao mwingine zimeendelea kushuka tangu utaratibu wa kusimamia bei hizo kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ulipoanza kutumika mwaka 2004. Bei mpya ya Shilingi 34.92 kwa dakika imeanza kutumika tarehe 1 Machi 2013 baada ya makubaliano na wadau mbalimbali kufikiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Notisi Na. 425 la tarehe 28 Desemba 2012. Bei hii mpya ni punguzo la takribani asilimia 65 kutoka kiwango cha mwisho cha Shilingi 115 kwa dakika kilichokuwa kikitozwa kabla ya hapo. Inatarajiwa kuwa gharama hizi zitaendelea kushuka hadi kufikia Shilingi 26.96 kwa dakika ifikapo mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya Teknolojia ya Utangazaji kutoka Analojia kwenda Dijitali. Nchi wanachama wa Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU) ikiwemo Tanzania, kwa pamoja, ziliridhia kusitisha mfumo wa utangazaji wa televisheni unaotumia teknolojia ya analojia na kuanza kutumia mfumo wa utangazaji unaotumia teknolojia ya dijitali ifikapo tarehe 17 Juni 2015. Sababu za uamuzi huo ni kutokana na faida zinazopatikana kwa kutumia mfumo wa utangazaji wa dijitali ambazo ni pamoja na:-

(i) Ubora wa picha na sauti;

(ii) Ubora wa matumizi ya masafa ya utangazaji utakaowezesha upatikanaji wa masafa yanayoweza kutumika katika kupanua na kuongeza huduma;

(iii) Matumizi bora ya nishati ya umeme;

(iv) Uwezekano wa kutoa huduma za ziada kama vile intaneti kwenye runinga; na

(v) Uwezekano wa kupanuka kwa matumizi ya teknolojia ya runinga za kiganjani na za kwenye magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia makubaliano hayo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kusitisha mfumo wa utangazaji wa runinga unaotumia teknolojia ya analojia ifikapo tarehe 31 Desemba, 2012 kwa lengo la:-

(i) Kutoa muda wa kutosha kwa nchi wanachama kufanya tathmini ya kiufundi ili kuweza kurekebisha kasoro zozote zitakazojitokeza kabla ya kufikiwa kwa tarehe iliyokubaliwa na *ITU*;

(ii) Kuwa na muda mfupi wa kuwa kwenye kipindi cha mpito ambapo mifumo yote miwili inayotumia teknolojia

za analojia na dijitali inatumika *(simulcast).* Hii ni kwa sababu gharama za uendeshaji katika kipindi hiki cha mpito ni kubwa kutokana na vituo kulazimika kuendesha mifumo yote miwili; na

(iii) Kutoruhusu nchi zetu kuwa soko la televisheni za analojia zilizopitwa na wakati zinazoweza kuingizwa nchini kutoka nchi zingine iwapo tutachelewa kuzima mitambo hiyo ya analojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua muhimu zilizochukuliwa. Kwa kuzingatia ukubwa na unyeti wa suala hili, hususan jinsi linavyogusa watu wengi, uhamaji huo ulibidi kufanywa kwa umakini mkubwa hatua kwa hatua. Kutekelezwa kwa hatua hizo kumeiwezesha nchi yetu kufikia hatua ya kuingia kwenye mfumo wa dijitali kwa mafanikio, ukilinganisha na nchi jirani ambazo bado zinahangaikia namna ya kutekeleza mabadiliko haya hivi sasa wakati ambapo ukomo wa kusitisha utangazaji wa analojia ukiendelea kukaribia. Hatua zilizotekelezwa ni pamoja na mambo yafuatayo:-

(i) Mwaka 2005: Waraka wa kwanza wa mashauriano *(consultative document)* kuhusu umuhimu na faida za kuhama kutoka mfumo wa utangazaji wa analojia kwenda dijitali ulitayarishwa na kufikishwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali nchini;

(ii) Mwaka 2006: Waraka wa pili wa mashauriano na mapendekezo ya muundo wa leseni kwenye mfumo wa utangazaji wa teknolojia ya dijitali ulitayarishwa na kusambazwa kwa wadau;

(iii) Mwaka 2007: Kamati ya kiufundi inayoshughulikia uhamaji kutoka mfumo wa utangazaji wa analojia kwenda dijitali iliundwa. Aidha, mkutano mkuu uliojumuisha vituo vyote vya utangazaji nchini ulifanyika Bagamoyo kupitia na kisha kuridhia mfumo wa leseni za utangazaji unaohitajika kwenye mfumo wa dijitali;

(iv) Mwaka 2010: Kampuni tatu (3) zilipewa leseni za kujenga miundombinu ya kusambaza matangazo kwa mfumo wa dijitali. Kampuni hizo ni pamoja na *Agape Associates Limited, Basic Transmission Limited* pamoja na *Star Media (T) Limited*. Sambamba na hili, Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Mabadiliko ya Utangazaji iliundwa. Kamati hii inajumuisha Makatibu Wakuu wa Wizara saba. Kamati imeendelea kufanya kazi kwa kukutana angalau mara moja kila baada ya miezi mitatu kufanya tathmini na kutoa maelekezo ya utekelezaji; na

(v) Mwaka 2011: Uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya kuelimisha umma kuhusu mabadiliko ya mfumo wa utangazaji uliohusisha nembo maalumu ulifanywa na Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 24 Agosti 2011. Kampeni hiyo ilihusisha pamoja na mambo mengine, wimbo mahsusi uliopigwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari wakati wote wa kampeni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa hatua hizi umefanyika kwa kipindi kirefu cha takriban miaka saba na kuhusisha majadiliano mapana na ya kina ambayo yasingefanyika kwa wakati Tanzania isingeliweza kufikia hatua ya kuhamia kwenye mfumo wa dijitali. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kuwa na mtazamo wa mbali uliotuwezesha kufanikisha zoezi hili. Vilevile, nawashukuru wadau wote, hususan kampuni za utangazaji ambazo zilitoa ushirikiano wa karibu uliowezesha kufikiwa kwa hatua hii. Kampuni hizo ni pamoja na *TBC, ITV, Channel Ten, Star TV, EATV, Tumaini TV,* Sibuka *TV, DTV, Clouds TV,* Mlimani *TV* na kampuni za kurusha matangazo ya digitali za *Agape Associates Limited, Basic Transmission Limited* na *Star Media (T) Limited.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi na uendeshaji wa mitambo ya kurusha matangazo ya dijitali. Hatua zilizofikiwa na kampuni tatu zilizopewa leseni ya kujenga mitambo ya kurusha matangazo ya dijitali ni kama ifuatavyo:-

(i) *Agape Associates Limited:* Kampuni hii imefunga mitambo ya dijitali kwenye miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha na Mbeya. Vile vile, inatarajiwa kuwa baada ya miezi mitatu (3) itakuwa imefunga mitambo mingine kwenye miji ya Kigoma, Tanga, Singida, Iringa, Tabora, Shinyanga na Musoma;

(ii) *Basic Transmission Limited:* Kampuni hii imefunga mitambo kwenye miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Mwanza. Kampuni hii imeshaanza kurusha matangazo ya dijitali katika Mkoa wa Dar es Salaam; na

(iii*) Star Media (T) Limited*: Kampuni hii imefunga mitambo ya dijitali kwenye miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha, Moshi, Tanga, Mbeya na Morogoro. Aidha, baada ya miezi minane, inatarajiwa kukamilisha ufungaji wa mitambo hiyo kwenye Mikoa mingine 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo ambavyo vimejiunga kwenye mfumo wa dijitali. Hadi hivi sasa, vituo vyote vya televisheni vyenye leseni ya kitaifa vimejiunga kwenye mfumo wa dijitali. Vituo hivyo ni *TBC, ITV, Channel Ten, Star TV* na *EATV* ambavyo matangazo yao yanarushwa na kampuni zote tatu zinazorusha matangazo ya dijitali. Vituo vingine ambavyo leseni zao si za kitaifa, vilivyojiunga kwenye mfumo wa digitali ni Tumaini *TV,* Sibuka *TV* na *DTV* kupitia mitambo ya *Star Media (T) Limited, Clouds TV* kupitia mitambo ya *Star Media (T) Limited* na mitambo ya *Basic Transmission Limited* na Mlimani *TV* kupitia mitambo ya *Basic Transmission Limited.*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya manufaa makubwa yanayotokana na kuhamia kwenye mfumo wa dijitali ni kuwezesha wananchi kupata matangazo ya televisheni zote za kitaifa katika maeneo yote ambapo mfumo huu unatumika. Hii ni pamoja na maeneo ambayo hapo awali yalifikiwa na baadhi tu ya televisheni hizi ikiwemo Jiji la Mbeya ambalo lilikuwa likipata matangazo ya *TBC1* tu, wakati Mji wa Moshi uliokuwa ukipokea matangazo ya *ITV* na *EATV* peke yake. Vilevile Mji wa Tanga ulikuwa ikipata matangazo ya *Channel Ten* na *TBC1* peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzimaji wa mitambo ya analojia katika miji mingine. Zoezi la uzimaji wa mitambo ya analojia tayari limefanyika katika miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Mwanza, Moshi, Arusha na Mbeya na hivyo kukamilisha awamu ya kwanza ya usitishaji wa urushaji wa matangazo kwa kutumia mitambo ya analojia. Kwenye miji yote mingine mitambo ya analojia bado ipo hewani na itakuwa hivyo mpaka pale mawimbi *(signal)* ya mitambo ya dijitali kwenye miji hiyo yatakapoanza kupatikana baada ya kukamilisha usimikaji wa mitambo na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya awali ya uzimaji wa mitambo ya analojia kwa Jiji la Dar es Salaam. Inakadiriwa kuwa zipo runinga zipatazo 600,000 kwenye kaya za Jiji la Dar es Salaam. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2012, zaidi ya runinga 250,000 kati ya 600,000 zilikuwa katika mfumo wa dijitali kupitia teknolojia za kupokea matangazo ya satelaiti na waya *(cable).* Idadi ya runinga zilizobaki 350,000 ndizo zilizohusika na mabadiliko ya teknolojia kutoka analojia kwenda dijitali. Runinga hizi 600,000 zilizokadiriwa katika Jiji la Dar es Salaam, hazijumuishi runinga zilizoko kwenye mahoteli, nyumba za starehe na maeneo mengine ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mabadiliko hayo, kati ya Januari 2012 na Januari 2013, zaidi ya visimbuzi 350,000 vilinunuliwa na wananchi katika Jiji la Dar es Salaam pekee. Kwa kutumia takwimu za mlinganisho kati ya runinga 350,000 zilizokadiriwa kuwa katika mfumo wa analojia na visimbuzi 350,000 vilivyokwisha kusambazwa, inaonyesha kuwa zoezi la mabadiliko katika jiji la Dar es Salaam kwa ujumla limetekelezwa kwa mafanikio makubwa. Aidha, visimbuzi zaidi vinaendelea kusambazwa Jijini Dar es Salaam kutokana na ukweli kuwa baadhi ya runinga ambazo zilikuwa zinapokea matangazo kwa mfumo wa dijitali kupitia teknolojia za Satelaiti na waya nazo pia zinaweza kutumia visimbuzi kupokea matangazo kupitia mitambo ya utangazaji ya ardhini *(telestrial broadcasting).* Tathmini halisi ya awamu ya kwanza ya utekelezaji imeanza ili kubaini

changamoto zilizojitokeza na kuzipatia ufumbuzi kabla ya kuanza awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekaji wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta katika Mkoa wa Dar es Salaam. Orodha ya Misimbo ya Posta kwa nchi nzima imekamilika na kuchapishwa kupitia Gazeti la Serikali Notisi Na. 220 ya tarehe 22 Juni, 2012. Wadau mbalimbali wameanza kutumia Misimbo ya Posta na Anuani hizo ikiwemo Taasisi ya Utambuzi na Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa *(NIDA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa programu hii ya Uwekaji wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta katika Mkoa wa Dar es Salaam umeanza. Hatua hii ya utekelezaji ilianza mara baada ya uzinduzi uliofanywa na Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Septemba 2012 ambapo pia alitoa agizo kwa Halmashauri zote tatu za Mkoa wa Dar es Salaam kuipa majina mitaa yote ya Dar es Salaam kama hatua ya kwanza ya utekelezaji wa programu hii. Kufuatia agizo hilo, Mkoa wa Dar es Salaam uliunda Kamati ya Utekelezaji, ambayo pamoja na mambo mengine, ilisimamia utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais na kusimamia utekelezaji wa mradi mzima katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa za Kinondoni, Temeke na Ilala zipo katika hatua za mwisho kukamilisha zoezi la utoaji wa majina ya mitaa na namba za nyumba. Sambamba na uwekaji wa majina ya mitaa, Kamati hii pia imeendelea na zoezi la ukusanyaji wa michango kutoka kwa wadau mbalimbali ikizingatiwa kuwa programu hii inatekelezwa kwa kushirikisha wadau wote ikiwa ni pamoja na sekta binafsi. Hadi hivi sasa fedha taslimu kiasi cha Sh. 239,300,000 zimekusanywa kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imejipanga kuendelea kukusanya fedha kutoka kwa wadau kupitia michango na kutumia aina mbalimbali za ubia na wadau

walio tayari kufadhili hatua mbalimbali za utekelezaji wa programu hii kwa mkoa wa Dar es Salaam. Hii ni pamoja na uwekaji wa vibao vya majina ya mitaa na namba za nyumba ambazo wanaweza kupata fursa ya kutangaza shughuli zao na hivyo pande zote kunufaika *(win-win)* sawia na malengo ya Sera ya Ubia Kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(P-P-P Policy).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii, kutoa wito kwa wadau mbalimbali kuendelea kuunga mkono jitihada hizi, ambazo kufanikiwa kwake kutaliwezesha Taifa letu kuwa na miundombinu madhubuti na sahihi ya mawasiliano ya posta ambayo pamoja na mambo mengine itawezesha kuwatambua wananchi wake na kutambua sehemu za makazi na sehemu za biashara na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Kikosi Maalum cha Ulinzi wa Kieletroniki *(Computer Emergency Response Team–CERT).* Kutokana na kupanuka kwa matumizi ya mtandao katika nyanja mbalimbali za maisha, Serikali imeunda Kikosi kitakachoratibu na kufuatilia matumizi ya mitandao ya kompyuta *(Computer Emergency Response Team–CERT).* Tayari Kikosi hicho kimeanzishwa na kinafanya kazi ndani ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Aidha, Kikosi hicho kimepewa jukumu la kufuatilia na kudhibiti uhalifu wa kimtandao nchini kikishirikiana na wadau wengine ulimwenguni. Kufuatia kukamilika kwa uundwaji wa Kikosi hicho, mafunzo ya kujenga uwezo wa rasilimali watu kwa ajili ya Kikosi hiki cha *CERT* yameanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utungaji wa Sheria ya Usalama wa Mtandao *(Cyber Security Law).* Katika kukabiliana na uhalifu wa mtandao, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao ni Shirika la Mawasiliano Duniani *(ITU),* Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na *SADC* inaandaa Sheria ya Usalama wa Mtandao *(Cyber Security Law).* Rasimu ya awali ya sheria imeandaliwa, hatua inayofuata ni kuwasilishwa kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni. Kwa kuanzia sheria hii itahusisha masuala ya uhifadhi wa taarifa *(Data Protection),* biashara mtandao

*(Electronic Transaction)* na matumizi salama ya mtandao *(Cyber Crime).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza kwa Utekelezaji wa Kupeleka Mawasiliano Vijijini Kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)*. Hivi sasa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote unatekeleza Awamu ya Kwanza ya mpango wake wa kupeleka mawasiliano katika Kata 152 zilizoainishwa kwenye awamu hiyo. Tarehe 11 Novemba 2012, Mfuko ulitangaza zabuni ya kupeleka mawasiliano katika Kata hizo 152 zilizoko Tanzania Bara ambapo baada ya kufanyiwa uchambuzi yakinifu, Kata 52 zilikidhi masharti ya zabuni na kupitishwa kwa ajili ya kupata ruzuku na kuanza utekelezaji. Kata hizo zipo katika Mikoa 14 na Wilaya 31 na zinahusisha jumla ya vijiji 316.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Machi 2013, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na kampuni za *Airtel (T) Limited, Tigo MIC (T) Limited, TTCL* na *Vodacom (T) Limited* zilitia saini kwenye mkataba wa ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano kwenye Kata hizo 52 ambapo Mfuko utatumia kiasi cha dola za Marekani 5,827,978 sawa na shilingi 9,441,324,360.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji katika eneo la sayansi, teknolojia na ubunifu. Ukamilishwaji wa Mikakati ya Utekelezaji wa Sera ya Utafiti na Maendeleo na Sera ya Bayoteknolojia. Kwa kutambua umuhimu wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika maendeleo nchini, Serikali imeandaa Sera kadhaa zikiwemo Sera ya Utafiti na Maendeleo na Sera ya Bayoteknolojia. Baada ya kuandaa Sera hizi, Serikali imekamilisha uandaaji wa mikakati ya utekelezaji kwa Sera zote mbili na kuisambaza kwa wadau na jamii kwa ujumla. Kuwepo kwa mikakati hii kumerahisisha utekelezaji wa malengo ya sera hizi kupitia mipango ya mwaka ya utekelezaji ambayo imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mikakati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandaaji wa Programu ya Mageuzi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Sambamba na

juhudi hizi za kisekta, Serikali inaendelea na programu ya kulifanyia mapitio eneo lote la ubunifu nchini *(National Innovation System – NIS)* kwa lengo la kuandaa Programu ya Mageuzi ya Sayansi na Teknolojia na Ubunifu nchini *(Science, Technology and Innovation (STI) Reform).* Hadi hivi sasa, Andiko Dhana *(Background Report)* la utekelezaji wa Programu hii limekamilika kwa kushirikisha wadau mbalimbali nchini. Hatua hii imefuatiwa na kupata mchango wa mawazo ya wataalam wa nje ambao pamoja na kulipitia Andiko Dhana wametoa uzoefu wa nchi zingine zilizofanya mageuzi ya namna hii kupitia Taarifa ya Uchambuzi ya Wataalam wa Nje *(External Review Report)* iliyowasilishwa Serikalini mwezi Machi 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa hatua hizi mbili kumewezesha hatua ya mwisho ya kuiandaa Programu yenyewe ya Mageuzi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kuanza. Programu hii inaandaliwa kupitia Andiko Jumuishi *(Synthesis Report)* linalochukua mawazo kutoka kwenye Andiko Dhana lililoandaliwa na wataalam wa ndani na Taarifa ya Uchambuzi ya Wataalam wa Nje. Uaandaaji wa Andiko Jumuishi unaendelea na unahusisha michango kutoka kwa wadau mbalimbali nchini na inatarajiwa kukamilika kabla ya Desemba 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu hii ya mageuzi katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu inatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa nchini kwa kuibua mikakati na miongozo mbalimbali ya kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu ikiwemo kutungwa kwa Sheria ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, na kuongeza vivutio kwa sekta binafsi kuchangia na kushiriki katika kuendeleza tafiti na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Kwa ujumla wake, kutelezwa kwa programu hii kutaongeza kwa kiasi kikubwa mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu kwenye kasi na ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuishukuru Serikali ya Afrika Kusini, ambayo kupitia Makubaliano ya Ushirikiano Katika Sayansi na Teknolojia baina

nchi yetu na nchi hiyo yaliyoanza tangu mwaka 2011, ilitoa Timu ya Wataalam watatu (3) ambao walifanya uchambuzi na mapitio ya mfumo wa sayansi, teknolojia na ubunifu kwa muda mfupi sana na bila gharama yoyote. Kwa kawaida, zoezi la namna hii kama lingefanywa na wataalam wengine wa nje kupitia zabuni lingegharimu fedha zisizopungua Sh. milioni 150. Aidha, kupitia ushirikiano huo, watafiti wa pande zote mbili wamenufaika kwa kuandika na kufanya tafiti za pamoja katika maeneo mbalimbali ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, imeandaa Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia ambao tayari imeridhiwa na Serikali (Baraza la Mawaziri). Mchakato wa kuandaa Sheria ya Kuendeleza Sayansi Nchini upo katika ngazi ya wadau kutoa maoni. Vilevile, Wizara yangu ilisimamia uandaaji wa Mwongozo wa Wabunifu. Mwongozo huo utawasaidia Wagunduzi namna ya kufikisha ugunduzi wanaoufanya katika ngazi mbalimbali na kwa mahitaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Programu ya Kuwahamasisha Wanafunzi Kupenda na Kuchukua Masomo ya Sayansi, Teknolojia na Uhandisi. Kwa lengo la kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa sayansi na teknolojia katika maisha ya kila siku na umuhimu wa kujenga uwezo wa rasilimali watu wenye ubora katika fani na ngazi mbali mbali na umuhimu wake katika kuongeza tija kwenye maeneo yote ya uchumi nchini, Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi ijulikanayo kama *Young Scientists* Tanzania mwezi Novemba 2012, ilifanya maonesho ya Kisayansi katika ukumbi wa *Diamond Jubilee,* Dar es Salaam. Maonyesho hayo yalihusisha wanafunzi kutoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar na kufadhiliwa na wadau mbalimbali, wengi wao kutoka sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *Young Scientists* Tanzania inaendesha programu ya kuwezesha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari hapa nchini kubuni na kufanya ugunduzi wa kisayansi kwenye maeneo yote ya taaluma ikiwemo sayansi jamii ambapo ugunduzi huo unaonyeshwa

na kushindanishwa kwenye maonyesho ya kitaifa. Programu hii inafadhiliwa kwa kushirikiana na Serikali ya *Ireland.* Programu ya namna hii imekuwepo nchini Ireland kwa miaka mingi na imeiwezesha nchi hiyo kujenga rasilimali watu madhubuti ambayo imeifanya nchi hiyo kuvutia uwekezaji wa kampuni nyingi katika masuala ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali zikiwemo taasisi zisizo za kiserikali katika kuhamasisha na kuchochea maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa makundi mbalimbali. Miongoni mwa taasisi hizi ni Chama cha Wanawake Wanasayansi Tanzania *(Science, Technology and Innovation for Women in Tanzania -STI4WT)* chenye Makao yake Makuu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Tanzania *Academy of Science (TAAS)* ambayo imepewa ofisi katika Tume ya Sayansi na Teknolojia. Tume na *TAAS* zimeshirikiana katika juhudi za kuwaunganisha watalaam na hatimaye kuwezesha kutoa mchango wa mawazo na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kisayansi na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu wa Shughuli za Utafiti Kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH).* Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeendelea kuratibu utafiti nchini. Ili kufanikisha shughuli hizi na kuleta tija, Tume ya Taifa Sayansi na Teknolojia imeendelea kukusanya taarifa zote za utafiti unaofanyika hapa nchini. Taarifa hizi zimewekwa kwenye benki ya takwimu za sayansi, teknolojia na ubunifu na pia kuwekwa kwenye tovuti ya Tume *www.costech.or.tz* ili kuwafikia wananchi wote na kuweza kutumia katika mipango ya maendeleo. Vile vile, Tume imeweza kusajili tafiti 430 za watafiti kutoka nje ya nchi kwa mwaka 2012/2013 na kufanya jumla ya tafiti zilizosajiliwa kufikia 1,911 kwa kipindi cha mwaka 2002 hadi 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kupeleka huduma za Tume ya Taifa Sayansi na Teknolojia kuwa karibu zaidi na wananchi wa Zanzibar, Tume imefungua Ofisi iliyopo katika jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika eneo la Tunguu Zanzibar. Ofisi

hii inashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo inajukumu la kuratibu shughuli za utafiti kwa upande wa Zanzibar. Ofisi ya *COSTECH* Zanzibar, kwa kushirikiana na wadau wa utafiti kutoka visiwa vya Unguja na Pemba, imeweza kukusanya taarifa ya tafiti mbalimbali zilizowahi kufanyika Zanzibar ili ziweze kuhifadhiwa na matokeo yaweze kutumika kwa tija na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha kwa ajili ya Utafiti na Maendeleo *(R&D).* Serikali imeendelea na jitihada za kuongeza tengeo la fedha kwa ajili ya Utafiti na Maendeleo kwa lengo la kufikiwa kwa dhamira yake ya kufikia asilimia 1.0 ya Pato Ghafi la Taifa. Kama ilivyo kwa nchi zote duniani, fedha za utafiti huchangiwa kupitia taratibu mbalimbali ikiwemo tengeo la Serikali moja kwa moja kwenye Mfuko wa Utafiti, tengeo kupitia sekta mbalimbali na michango kutoka kwa wafadhili na sekta binafsi. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, fedha zilizotengwa moja kwa moja kwenye Mfuko wa Utafiti na Maendeleo kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilikuwa Sh.21,479,961,000. Pia, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya Utafiti na Maendeleo kupitia sekta mbalimbali na kufanya fedha zote zilizoelekezwa kwenye Utafiti na Maendeleo kufikia takriban asilimia 0.29 ya Pato Ghafi la Taifa ikilinganishwa na asilimia 0.08 ya Pato Ghafi la Taifa katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika; Serikali itaendelea na juhudi za kuongeza kiwango cha fedha za utafiti na maendeleo kwa kuweka mikakati itakayoongeza uchangiwaji wa fedha za utafiti na maendeleo kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi, washirika wa maendeleo, ushirikiano wa kikanda na wawekezaji kutoka nje ya nchi. Juhudi hizi ni pamoja na utekelezaji wa mageuzi katika sayansi, teknolojia na ubunifu na uandaaji wa Sheria ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nilizozieleza hapo awali ambazo kwa namna moja au nyingine zimetoa kipaumbele katika suala la upatikanaji wa fedha za utafiti na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kupitia *COSTECH* inaendelea na utafiti wa Viashiria vya Sayansi,

Teknolojia na Ubunifu Barani Afrika unaotekelezwa kwa kushirikiana na *NEPAD* na ambao unaotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2013. Kukamilika kwa utafiti huu kutaziwezesha nchi za Afrika, ikiwemo Tanzania kuweza kubaini kwa uhakika zaidi kiwango cha fedha zinazoelekezwa kwenye masuala ya utafiti na maendeleo ikiwa ni pamoja na kuhuisha taarifa kuhusu mchango wa Pato Ghafi la Taifa katika shughuli za utafiti na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kulifahamisha Taifa kupitia Bunge hili kuwa Serikali kupitia Tume inafadhili miradi 59 ya utafiti kuanzia mwaka 2011/2012 na baadhi ya tafiti hizo zimeanza kuonesha mafanikio. Tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa chanjo ya ugonjwa wa kuku (*Newcastle vaccine*) na ule wa mbegu mpya ya mtama unaostahimili ukame unaofanywa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Mikocheni. Tafiti nyingine zilizopata mafanikio ni pamoja na utafiti wa kuongeza upatikanaji wa madini ya fosfori (*phosphorus*) katika kilimo hai (*organic farming*), utafiti wa kuboresha upatikanaji wa malisho ya mifugo kwenye bonde la Ugalla (*Ugalla ecosystem*), utafiti wa kudhibiti ugonjwa wa virusi kwenye zao la alizeti na utafiti wa dawa za mitishamba katika tiba ya 29 UKIMWI na maradhi yanayoambatana na ugonjwa huo. Matokeo haya ya utafiti yanaonyesha jinsi utafiti unavyoweza kuleta matokeo yenye manufaa makubwa kwa wakulima, wafugaji na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya utafiti hapa nchini, Serikali kupitia *COSTECH* imeendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya utafiti ambapo ujenzi wa maabara mpya za utafiti umekamilika katika taasisi za utafiti wa kilimo ikiwemo Makutupora - Dodoma, Kizimbani – Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Afya na Tiba (*NIMR* - Tabora) na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Naliendele (Mtwara). Kwa ujumla, ukarabati wa miundombinu ya maabara (majengo na vifaa) unaendelea kukamilishwa katika taasisi 19 za utafiti hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za Serikali kuendeleza rasilimali watu kwa ajili ya utafiti, wataalam 13 wamemaliza mafunzo ya Shahada ya Uzamili *(MSc)* katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (5) na Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili (8) na walitunukiwa vyeti vyao mwezi Novemba 2012. Aidha, wataalam wengine wapatao 90 watamaliza mafunzo ya shahada ya uzamili katika vyuo mbalimbali hapa nchini mwishoni mwa mwezi Juni, 2013. Wataalam hawa ni waajiriwa kwenye taasisi mbalimbali za utafiti na vyuo vikuu hapa nchini na wamepatiwa ufadhili wa Serikali kwa asilimia 100. Hivyo, Serikali inaamini kuwa wataalam hawa wataanza kupunguza makali ya uhaba 30 wa wataalam katika taasisi za utafiti hapa nchini. Vile vile, Serikali inaendelea kusomesha wataalam wapatao 84 katika Shahada ya Uzamivu katika vyuo vikuu vya Sokoine (30), Muhimbili (1), Ardhi (4), Dar es Salaam (18) na Nelson Mandela Arusha (31) ambao watahitimu katika miaka mbalimbali ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo katika Kutekeleza Miradi ya Utafiti na Maendeleo chini ya Ushirikiano Baina ya Tanzania na Jamhuri ya Afrika Kusini. Serikali ya Tanzania na Serikali ya Afrika Kusini zilifikia makubaliano ya ushirikiano katika nyanja za sayansi, teknolojia na ubunifu mwaka 2011 kama nilivyoeleza hapo awali. Katika kutekeleza Mpango Mkakati wa makubaliano hayo, miradi ya utafiti imeandikwa kwa ushirikiano wa watafiti wa nchi hizi mbili (*collaborative research projects*) kwa njia ya ushindani. Tayari maombi 36 yamepokelewa na Tume za Sayansi na Teknolojia za nchi hizi mbili kwa ufadhili wa pamoja. Maombi haya yapo katika maeneo ya tafiti za afya ya binadamu, mambo ya kale, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo, nanoteknolojia, TEHAMA na uzalishaji wa mifugo. Mchakato wa mapitio (*peer reviewing*) pamoja na uteuzi wa miradi itakayofadhiliwa umeanza. Matarajio ya juhudi hizi ni nchi yetu kunufaika na ufadhili wa miradi hiyo, kupata uzoefu katika nyanja hizo za utafiti na kupata fursa za kutumia maabara za kisasa za Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubiasharishaji wa Teknolojia. Katika kukabiliana na changamoto ya kuhamasisha ubiasharishaji (*commercialization*) wa teknolojia zilizokamilisha hatua ya utafiti (*prototype stage*) zilizo kwenye taasisi mbalimbali za Utafiti na Maendeleo hapa nchini, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ilitoa mwega katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kwa taasisi hizo ili kuziwezesha kuzalisha na kuzipeleka kwenye soko teknolojia hizo. Matokeo ya juhudi hizo yameanza kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwega wa Sh.200,004,058 kwa Taasisi ya TEMDO ya Arusha, Taasisi hiyo imeweza kutengeneza na kuuza mitambo ya kuunguza na kuharibu taka (*incinerators*) mahsusi zinazotokana na shughuli za hospitalini. Tayari mitambo saba imeshauzwa kwenye hospitali 7 kama ifuatavyo:- Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo, Hospitali ya Jeshi Lugalo, Hospitali ya Mzinga Corporation, Hospitali ya Mount Meru, Hospitali ya Bugando na Hospitali ya Wilaya Nzega na Hospitali ya Wilaya ya Mafia. Vile vile, *TEMDO* imefuatilia utendaji wa mitambo hiyo na kuiboresha ili isitoe moshi kabisa na hivyo kupunguza uwepo wa hewa ukaa inayokwenda angani. Maboresho haya pia yameifanya mitambo hiyo kutohitaji kutumia maji ya kupoozesha hewa inayozalishwa, jambo ambalo limeongeza ubora wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAMARTEC* ya Arusha ilipatiwa Sh.255,004,058 kwa ajili kuzalisha trekta dogo na zana zake kwa lengo la kulipeleka sokoni. Trekta hili limebuniwa kukidhi mahitaji ya mkulima mdogo wa Tanzania na lina bei nafuu ikilinganishwa na trekta za kawaida zinazoingizwa kutoka nje. Hadi hivi sasa, *CAMARTEC* imekamilisha utengenezaji wa trekta 11 kati ya 14 ambazo wanunuzi wamekwishawasilisha maombi ya kuzinunua. Sambamba na trekta hili, Kituo kimezalisha zana mbalimbali za kilimo zinazoweza kuendeshwa na trekta hilo ikiwemo plau, jembe la kulainisha udongo (harrow), jembe la palizi, jembe la kutengeneza matuta (*ridger*), pampu ya kusukuma maji kwa ajili ya umwagiliaji, mashine ya kusaga nafaka, na tela la

kubebea mizigo. Vifaa hivi vinauzwa pamoja na trekta kulingana na mahitaji ya mnunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Tanzania *Automotive Technology Centre* (*TATC*) iliyopo Kibaha ilipatiwa Sh. 193,490,000 kwa ajili ya kutengeneza vipuli vya treni na reli na kutengeneza trekta dogo la mkono (*power tiller*) lenye uwezo wa kulima, kupanda na kuweka mbolea. Moja ya lengo la utafiti huo ilikuwa kuliwezesha trekta hilo kuwa jepesi ili kuwezesha watumiaji wa jinsia zote kuiendesha kwa urahisi. Taasisi imekamilisha utengenezaji wa trekta hilo. Wakati huo huo, Taasisi imetengeneza vipuli vya reli na kuviuza kwa Kampuni ya Reli Tanzania na hivyo kupunguza hitaji la kuagiza vipuli hivyo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Mzinga lilipewa Sh. 181,143,212 kwa ajili ya kutengeneza mashine mbili za kusaga na kuchanganya vyakula vya mifugo; Kutengeneza ndoo ndogo 35 na ndoo kubwa 7 za taka kwa ajili ya manispaa na kutengeneza breki za treni. Kufuatia kupewa fedha hizo, Shirika limekwishatengeneza breki 5,966 za treni ambazo ni asilimia 54 ya mahitaji ya Kampuni ya Reli Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya mahitaji iliyosalia itakamilishwa ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013. Aidha, Shirika hilo limeshauza mashine za kuchanganyia vyakula vya mifugo kwa wanunuzi wa ndani na nje ya nchi na kufanikiwa kupata kiasi cha Sh. 49,939,200. Vile vile, Shirika limeuza ndoo kubwa na ndogo za taka kwa Manispaa ya Morogoro kwa kiasi cha Sh. 48 milioni. Katika mauzo ya vitu hivi, Shirika limeweza kupata faida ya Sh. milioni 32 ambazo zitatumika kuongeza uzalishaji wa vifaa na mashine.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ufadhili wa ubiashirishaji wa teknolojia zilizo kwenye taasisi hizi za utafiti na maendeleo zinaonyesha uwezo wa taasisi hizi katika kuzalisha bidhaa zenye ushindani sokoni na zinazoweza kuliingizia taifa mapato na kuokoa fedha za kigeni katika uagizaji wa bidhaa kutoka nje, pamoja na kuzalisha ajira

kwa wananchi na kuongeza ujuzi na kutumia rasilimali watu na mali ghafi iliyoko nchini kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujasiriamali na ubunifu katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Kupitia Atamizi ya Dar Teknohama *Business Incubator – DTBi.* Pamoja na TEHAMA kuwa na mchango mkubwa katika kurahisisha shughuli za uchumi na za kijamii, eneo jingine ambalo TEHAMA ina uwezo wa kuchangia kupitia ubunifu na ujasiriamali ni lile la kubuni na kuweka sokoni bidhaa mpya, kuanzishwa kwa Kampuni za TEHAMA na kuongeza fursa za ajira hususan kwa vijana wa Kitanzania. Hivi karibuni Taasisi ya REPOA ilifanya utafiti na kubaini kuwa tatizo la ajira kwa vijana limeongezeka kutoka asilimia 5.3 hadi kufikia asilimia 7.8. Kwa kutambua changamoto hii ya ajira, Serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) kwa kushirikiana na *infoDev (World Bank*) imeanzisha atamizi inayojulikana kama Dar Teknohama *Business Incubator* (DTBi) kwa nia ya kujenga uwezo wa kubuni bidhaa na huduma za TEHAMA na kuanzisha Kampuni za TEHAMA hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa atamizi hizi una lengo la kupunguza mzigo wa gharama za awali za kibiashara kwa kampuni changa za TEHAMA, hususan katika upatikanaji wa ofisi, umeme, intaneti na ushauri wa kitaalam katika kuanzisha biashara. Aidha, mafunzo ya kisasa wanayopata wajasiriamali wa TEHAMA yanawawezesha kuwa na uwezo katika usimamizi wa 35 biashara, masoko, ubora wa huduma na bidhaa pamoja na mitaji kwa lengo la kujiajiri na kuajiri watu wengine, mambo ambayo yanaisaidia jamii kupambana na umaskini na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwake Oktoba mwaka 2011, DTBi ina ngazi tatu za ushiriki wa waatamizi kama ifuatavyo:- *Pre-Incubation* ambapo wako waatamizi 23; *Start-up* ambapo wako waatamizi 12; na Makampuni ya waatamizi ambapo yako makampuni 11. Hadi hivi sasa ajira za moja kwa moja (*direct employment*) zilizozalishwa kupitia atamizi hii zinafikia 84 wakati huo huo

ajira ambazo si za moja kwa moja (*indirect employment*) zinakafikia 5,100. *DTBi* inashirikiana na mradi wa TEHAMA kwa jamii (*TANZICT*) unaofadhiliwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Finland, ambapo fedha zilizotengwa kwa ajili ya kusaidia waatamizi ni kiasi cha *Euro* 100,000 kwa sasa. Aidha, waatamizi wamefanya maonyesho katika viwanja vya Bunge (Dodoma) mara mbili na kwenye maonyesho mbalimbali katika nchi za Uingereza, Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*), Kenya na Sudan ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi wa *TANZICT*, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia pia imeweza kutoa fedha takriban kiasi cha Dola za Marekani 60,000 kwa vijana sita, kila mmoja takriban Dola za Marekani 10,000 na ili waweze kuendeleza ubunifu wao katika Sekta ya TEHAMA kwa kushirikiana na uongozi wa atamizi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmoja wa wajasiriamali Bwana Arnold Minde ambaye kampuni yake ya Safari Yetu iliatamiwa na DTBi ameshinda mashindano ya ubunifu yanayofadhiliwa na Shirika la *Start-up World.* Katika shindano hili, kampuni hiyo iliwasilisha mfumo wa kusaidia wananchi kununua tiketi za mabasi kwa kutumia simu za mkononi na kwa kupitia intaneti. Pamoja na kupunguza hitaji la kwenda katika ofisi za mabasi husika kununua tiketi, utaratibu unawaepusha wasafiri kutoka kwenye usumbufu wa wapiga debe kwenye vituo vya mabasi. Mfumo huu ulionekana kuwa bora na unaoweza kushindanishwa na mifumo mingine duniani. Kampuni ya *Google* ikishirikiana na *Start-up World*, imelipia gharama zote za kampuni hiyo kwenda Marekani mwezi Juni 2013 kwenye mashindano ya TEHAMA yatakayofanyika huko Silicon Valley, Califonia nchini Marekani. Aidha, Kimataifa, ufanisi wa atamizi ya *DTBi* umejitokeza tena kwa kampuni mbili zilizoatamiwa na atamizi hii kuchukua nafasi ya kwanza na ya pili katika ubunifu katika TEHAMA kwenye mashindano yaliyofanyika mwezi Mei 2013 nchini Tanzania yaliyoendeshwa na Shirika la Marekani liitwalo *GIST* na kushirikisha wawakilishi kutoka nchi 7 za Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ya *DTBi* ni ubunifu wa programu ya kukusanya mapato kwenye halmashauri uliyofanywa na kampuni ya atamizi ya *Day One Softcom*. Tayari programu hii inatumiwa na Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam na ambayo imeziwezesha kukusanya mapato vyema zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali ambapo zimeweza kuongeza makusanyo ya mapato yao kwa zaidi ya asilimia 300 katika mwaka mmoja. Kwa sasa kampuni hii imeshinda zabuni ya kusambaza mfumo huu katika Jiji la Mwanza, Arusha na Tanga. Progamu hii pia inatumika katika Manispaa za Morogoro, Mtwara, Kigoma na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *MAXCOM* iliyobuni teknolojia ya kukusanya mapato kwa kutumia vifaa vijulikanavyo kama Maxmalipo na ambavyo umaarufu wake umejitokeza ndani na nje ya nchi ilipitia katika atamizi ya *DTBi* katika hatua zake za kukua. Licha ya teknolojia hii kutumiwa na taasisi na kampuni nyingi hapa nchini ikiwemo *TRA* na kampuni za mawasiliano, teknolojia hii kwa sasa inatumika kwenye nchi za Rwanda na Burundi. Mazungumzo yanaendelea kwa teknolojia kutumika pia katika nchi ya Sudan ya Kusini. Aidha, *DTBi* imeatamia kampuni iliyobuni programu inayojulikana kwa jina la Popote *Media* inayotumia mtandao wa intaneti kumuwezesha mtumiaji kuonyeshwa “chochote”, “popote” na “wakati wowote” ambayo kwa sasa inatumiwa na Kampuni ya Ndege ya *Precision Air.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *Digital Brain* ambayo iliatamiwa na *DTBi* imetengeneza mfumo wa kisasa wa kudahili wanafunzi katika vyuo vikuu. Kwa kutumia mfumo huu, udahili unaweza kufanyika kupitia mtandao wa intaneti au simu ya mkononi na hivyo kuwapunguzia usumbufu wanafunzi katika kufanya udahili hususan wanafunzi walio vijijini ambao sasa hawalazimiki kusafiri. Hivi sasa, mfumo huu unatumiwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (*TCU*). Teknolojia hii imeshinda tuzo ya kwanza Barani Afrika na mazungumzo yanaendelea ili teknolojia hii iweze kutumika katika nchi za Afrika Kusini, Sudan ya Kusini na nchi za Afrika

Magharibi. Aidha, Kampuni ya *BlackMark Corporation* ilipitia kwenye Atamizi ya DTBi ambayo imefanikiwa kulisaidia Jeshi la Polisi nchini katika utoaji wa elimu kwa kutumia teknolojia mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni nyingine iliyopitia DTBi ni Magilatech iliyoanzishwa na mwanafunzi mbunifu wa Kitanzania ambaye amekuwa wa kwanza kuwekwa kwenye jarida la Bara la Afrika liitwalo *IT Africa*. Mbunifu huyu anatengeneza programu ya *eBunge* inayolenga kufanya uendeshaji wa shughuli za Bunge kuwa za kisasa zaidi. Kupitia teknolojia hii, wananchi wataweza kusikiliza shughuli za Bunge kwa kutumia simu za kiganjani na inapolazimu wataweza kupiga kura moja kwa moja kupitia simu zao na matokeo kuonekana Bungeni na hivyo kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi kwenye mambo muhimu ambayo Bunge litahitaji kupata maoni ya wananchi na kuliwezesha kufanya maamuzi yenye mchango mpana wa wananchi. Pia, *First Access* ni kampuni nyingine iliyoatamiwa na DTBi, ambayo inasaidia wajasiriamali mbalimbali kutunza kumbukumbu za biashara zao na hivyo kurahisisha upatikanaji wa mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uanzishwaji wa Atamizi ya Biashara ya Bidhaa za Kilimo *(Agri business Incubator).* Kutokana na mafanikio makubwa yaliyojitokeza kupitia *DTBi* kwenye ubunifu katika eneo la TEHAMA, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imekusudia kupanua wigo wa atamizi kwenye eneo jingine la kipaumbele la biashara ya bidhaa za kilimo kwa kuanzisha atamizi ya Biashara ya Bidhaa za Kilimo (*Agri-business Incubator*). Mchakato huu unafanywa kwa kushirikiana na wataalam kutoka programu ya Benki ya Dunia ya *InfoDEV* na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (*SUA*). Vilevile, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko katika hatua za mwisho za kuanzisha atamizi za aina hii Zanzibar zenye lengo la kukuza ubunifu katika TEHAMA na Biashara ya Bidhaa za Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeweza kuratibu na kufadhili mafunzo ya namna ya kusimamia na kuendeleza atamizi (*Incubator Management*) yaliyofanyika mwezi Mei 2013. Mafunzo hayo yaliendeshwa na wataalam waliobobea na ambao walipatikana kupitia programu ya kuendeleza atamizi ya *InfoDEV* ya Benki ya Dunia. Lengo kubwa la mafunzo haya ilikuwa ni kujenga uwezo wa kuelewa, kusimamia na kuratibu masuala ya atamizi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchakato wa Kuanzisha Mfuko wa Ubunifu. Katika kukuza ubunifu nchini, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la *DfID* ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha Mfuko wa Ubunifu. *Human Development Innovation Fund* ambao madhumuni yake makuu ni kukuza ubunifu katika sekta ya afya, elimu na maji-safi. Wajasiriamali na wabunifu watakaonufaika na fedha hizi ni wale ambao watafanya ubunifu wenye matokeo mapana katika jamii kwenye maeneo yaliyolengwa kama ubunifu wa M-Pesa ulivyoleta matokeo yanayogusa jamii kubwa kwenye huduma za kifedha. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli hizi wakati Mfuko huu utakapoanza ni Euro milioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa Katika Kuanzisha Mji Mahiri wa TEHAMA yaani *Smart ICT Village.* Katika mwaka wa fedha 2012/13 Serikali ilitenga jumla ya Sh.bilioni 5 kwa ajili ya kulipa fidia ya ardhi katika eneo litakalopatikana na kuanza ujenzi wa Mji Mahiri wa TEHAMA. Pamoja na mambo mengine, mji huu mahiri utakuwa na miundombinu muhimu ya majengo na ya TEHAMA yatakayovutia kampuni za mawasiliano na wajasiriamali kuwekeza na kufanya shughuli zao katika mji huo. Juhudi zinaendelea kufanywa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni kupata eneo la Mji huo Kigamboni au kwenye Eneo la Uwekezaji (*EPZ*) la Bagamoyo. Sambamba na juhudi hizi, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imekwisha andaa Mpango Kazi unaobainisha shughuli

zitakazotekelezwa katika Mji Mahiri huo, ikiwa ni pamoja na mpango wa mafunzo kwa watakaoshiriki katika kutafuta wabia wengine watakaowekeza katika mji huo zinaendelea. Hadi sasa wabia waliojitokeza ni pamoja na Kampuni ya *SEACOM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuendeleza Ubunifu na Ujasiriamali Kupitia Kongano Bunifu yaani *Innovative Clusters.* Serikali kupitia mradi wa *Pan- African Competitiveness Forum* unaoendeshwa na *COSTECH* kwa kushirikiana na Shirika la Sweden la SIDA, Taasisi ya Kuendeleza Sekta Binafsi ya *TPSF* na Baraza la Uwezeshaji Kiuchumi (*NEEC*) imeanzisha Kongano Bunifu nyingine mpya 28 katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji na biashara. Miongoni mwa kongano hizo ni kongano za Asali (Manyara, Manyoni, Singida); Mbegu (Arusha); Uyoga (Kibaha); Usindikaji wa mafuta ya alizeti (Singida na Dodoma); Uhandisi (Shinyanga); Viungo (Pemba, Unguja); Utalii (Unguja); ufugaji wa samaki, Useremala na Utalii (Bagamoyo na Tanga); Mkonge (Shinyanga); na Ufugaji wa kuku, Uchongaji wa sanaa na Kilimo cha mboga mboga (Morogoro). Kongano hizi ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inapenda kumshukuru Mheshimiwa Peter Kayanza Pinda, Waziri Mkuu kwa kuzindua na kuhamasisha matumizi ya mizinga ya kisasa kwenye Kongano ya Asali ya Manyoni Singida. Vile vile, nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi wa Mikoa ya Manyara, Singida, Morogoro, Songea, Ruvuma, Rukwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushiriki kimamilifu na kuahidi kutoa ushirikiano wa dhati katika kuendeleza kongano hizi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo itakayobuniwa kwenye Mikoa hiyo inalenga katika kuziendeleza kongano hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kongano Bunifu ni mojawapo ya nyenzo inayotumiwa ulimwenguni kote kuendeleza uzalishaji na ubunifu kwa wajasiriamali walio kwenye eneo moja la kijiografia, *cluster* na wanaojishughulisha na uzalishaji katika eneo moja la

uzalishaji *industry*, ambao kwa kuwa katika hali hiyo wanaweza kupata na kufikiwa na huduma za kitaalam za uzalishaji na kupeana hamasa ya ushindani miongoni mwao. Kongano Bunifu ambazo mafanikio yake yanajulikana ulimwenguni kote ni pamoja na kongano za Marekani za *Silicon Valley* kwenye TEHAMA na *Hollywood* kwenye picha za filamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha vikundi na wananchi kwenye maeneo yao kuanzisha kongano katika maeneo mbalimbali ya teknolojia na uzalishaji ambazo Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kupitia *COSTECH* itaweza kuzisaidia kukuza ubunifu, uzalishaji na ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi. Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, imetoa jumla ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya kuendeleza kongano 18 ambazo zilipata mafunzo na kutengeneza Mpango Mkakati kama ilivyoelezwa katika Hotuba yangu ya mwaka 2012. Fedha hizo zinalenga kuwezesha kongano hizo kuanza kutekeleza mpangokazi ambao umeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kongano 10 ambazo zimewezeshwa kifedha ni pamoja na Kongano ya Uhandisi - Morogoro; Kongano ya Mwani –Zanzibar; Kongano ya Asali-Manyoni; Kongano ya Mafuta - Singida; Kongano ya Uhandisi - Shinyanga; Kongano ya Katani - Kishapu; Kongano ya Uyoga- Songea; Kongano ya Mpunga - Magugu, Babati; Kongano ya Asali - Babati; na Kongano ya Mafuta- Babati. Aidha, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na *TPSF* kupitia mradi wao wa “Fanikiwa Kibiashara” na NEEC imeweza kutoa mafunzo katika mambo ya ubunifu na ushindani kwa Washauri wa Biashara kutoka taasisi mbalimbali nchini ikiwemo Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *SIDO*, Baraza la Uwezeshaji Kiuchumi la Taifa *NEEC*, na kampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutambua juhudi za Serikali za kuongeza mchango wa sayansi na teknolojia katika

kukuza uchumi na maendeleo ya wananchi nchini, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushawishi Jumuiya ya Kimataifa kuendesha Mdahalo Mahiri wa Ushirikiano yaani *Smart Partnership Dialogue*, utakaofanyika nchini kwetu tarehe 28 mwezi Juni hadi tarehe 2 Julai 2013 ambapo mada ya mdahalo huo itakuwa ni "Matumizi ya Teknolojia na Ubunifu kwa Ajili ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi Afrika". Pamoja na kulipa eneo la sayansi na teknolojia umuhimu mkubwa katika mchango wake katika uchumi na maendeleo ya wananchi, tukio hili litatoa fursa ya kuutangaza utayari wa nchi yetu kushirikiana na jamii ya kimataifa katika uwekezaji na ukuzaji wa uzalishaji na utoaji wa huduma unaotokana na ubunifu na matumizi ya teknolojia sahihi na za kisasa. Kupitia Bunge hili, ninazialika taasisi na kampuni mbalimbali za umma na binafsi kushiriki kikamilifu katika mdahalo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kukuza na Kuendeleza Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Kwenye Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti. Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia na Mradi wa Benki ya Dunia imeanza kutengeneza mtandao wa kuunganisha vyuo vikuu na taasisi za utafiti. Mtandao huu wenye uwezo mkubwa wa kusafirisha *data* umeviwezesha vyuo vikuu na taasisi za utafiti nchini kubadilishana taarifa za kisayansi na kitaaluma kwa kasi na haraka zaidi baina yao na baina ya nchi yetu na Mtandao wa Ulaya (*GEANT2*) ambao umeunganishwa kwenye mtandao huu. Kupitia mtandao huu, vyuo na taasisi za utafiti zimeweza kupata huduma mbalimbali ikijumuisha mtandao wa maktaba wa kielektroniki yaani *digital library* na kutolewa kwa elimu kwa njia ya masafa. Vyuo vilivyoko nje ya Mkoa wa Dar es Salaam vimeanza kuunganishwa kwenye mtandao huu kupitia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi huu, Tume imeweza kununua masafa yaani *bandwith* ya kiwango cha STM-1 (*155Mbps*) ambayo yameweza kutumiwa kwa kuunganisha taasisi 16 za utafiti na Elimu ya Juu. Pia, Tume kupitia mradi huu imekamilisha upembuzi yakinifu juu ya

uanzishwaji wa mfumo wa kutoa huduma ya vitabu na majarida ya kielektroniki yaani *digital library* na mfumo wa kutunza taarifa za masuala ya elimu - *Education Management Information System- EMIS*. Tume iko katika hatua za mwisho za kupata Mshauri Mwelekezi wa kufanya majaribio *pilot* ya mfumo huo wa elimu ya kielektroniki e-*Learning* kwa vyuo vikuu sita ambavyo ni Mkwawa *University College of Education,* Morogoro *Muslim University, Open University of Tanzania, CUHAS* - Bugando, *State University of Zanzibar* na Ardhi *University*. Kwa sasa Tume inakamilisha taratibu za kuanzisha programu ya mafunzo kwa ajili ya kuwawezesha vijana kujiajiri na kuajiriwa katika uchumi wa kisasa yaani *Information Technology/ Business Process Outsourcing - IT/BPO.* Kupitia mpango huu, Tume kwa kushirikiana na vyuo vikuu vya Tanzania pamoja na vyuo vikuu vya Marekani itatoa mafunzo ya kitaalam katika fani mbalimbali zikiwemo TEHAMA, fedha, uchumi, elimu ya biashara na bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuendeleza na Kudhibiti Matumizi Salama ya Nguvu za Atomiki. Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania - *TAEC* imeendelea kusimamia matumizi salama ya mionzi katika hospitali na vituo vya afya, viwandani na kwenye migodi na kuendelea kufanya tafiti mbalimbali zinazohusu matumizi ya nguvu za atomiki. Juhudi hizi zimeleta matokeo mazuri ikiwemo moja, kuboreshwa na kupanuliwa kwa huduma za tiba ya saratani, mbili, kuboresha mazao ya kilimo na mifugo, na tatu, kusimamia na kukagua uwepo wa mionzi kwenye vyakula na kwenye pembejeo za kilimo. Aidha, Tume imeendelea na maandalizi ya usimamizi wa migodi ya Urani ili kulinda wafanyakazi, kulinda mazingira na jamii kwa ujumla na kuendana na matakwa ya mikataba na makubaliano ya kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kutolewa kwa leseni ya awali ya uchimbaji wa madini ya Urani, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania itakuwa na majukumu makubwa ya kutoa elimu kwa jamii, kusimamia usalama wa mionzi kwa wafanyakazi, mazingira na jamii kwa ujumla, kushauri

na kuhakikisha uzingatiwaji wa taratibu za uchimbaji, usindikaji na usafirishaji salama wa madini ya Urani. Aidha, taratibu na kanuni za kusimamia eneo hili zimekamilishwa. Vile vile, Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanza kufanya tafiti mbalimbali zitakazowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za hali ilivyo sasa na kuzuia aina yoyote ya uharibifu kutokea. Sambamba na juhudi hizi, Serikali itaendelea kuiwezesha Tume kukamilisha ujenzi wa maabara zake ili kuiwezesha kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa ikipata misaada mbalimbali kutoka Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki IAEA. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Shirika hilo kwa kushirikiana na Serikali lilinunua mashine za kutambua kwa uhakika zaidi na kutibu saratani - *Gamma Camera na Simulator* kwa ajili ya Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, Dar es Salaam. Shirika hili pia limekuwa likisaidia jitihada za Serikali kuanzisha huduma za tiba ya saratani katika hospitali nyingine hapa nchini zikiwemo hospitali za Bugando, Mwanza; Mnazi Mmoja, Zanzibar; *KCMC*, Kilimanjaro na Hospitali ya Rufaa Mbeya ili kupanua na kuisogeza huduma hii karibu na wananchi walio kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu badala ya kutegemea huduma hii kutolewa na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha vifaa na miundombinu ya kubaini vyanzo vya mionzi na kudhibiti madhara ya vyanzo hivyo kwa kuwa na jengo la kisasa la kutunza mabaki ya mionzi na vifaa vya kukusanya vyanzo hivyo kwa kuvihamisha na kuvifadhi kwenye jengo mahsusi lililoandaliwa ili visilete madhara kwa afya ya wananchi na mazingira. Katika Mpango Mkakati wa kuanzia Januari 2014 hadi Desemba 2015, miradi katika nyanja za afya, maji, kilimo, maendeleo ya mifugo na uhakiki wa uchimbaji wa madini ya urani imepangwa kutekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imepata mafanikio makubwa kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya

matumizi salama ya nguvu za atomiki ambapo *TAEC* na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* zipo kwenye hatua ya kupata hadhi ya kuwa vituo vya mfano kikanda *Centre of Excellence*, katika udhibiti na uendelezaji wa matumizi salama ya nguvu za atomiki na matibabu ya saratani. Kwa kutambua mafanikio haya, Mkurugenzi Mkuu wa Tume za Nguvu za Atomiki Duniani, Balozi Yukiya Amano, alifanya ziara hapa nchini kuanzia tarehe 10 hadi 12 Februari, 2013. Katika ziara hiyo alizindua mashine ya kutambua na kutibu saratani katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* iliyofadhiliwa kwa pamoja na Shirika lake na Serikali ya Tanzania. Pia, alifanya majadiliano na viongozi wa Serikali wakiwemo mawaziri kuhusu mipango ya nchi yetu katika kupanua matumizi ya teknolojia za nyuklia ikiwemo matumizi ya mionzi katika kuhifadhi matunda na mazao ya nafaka na pia uwezekano wa kuzalisha nishati ya umeme kwa kutumia nguvu za atomiki. Aidha, kupitia Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, Balozi Amano aliahidi kuendelea kushirikiana na nchi yetu katika masuala mbalimbali hususan yanayohusu uchimbaji wa madini ya Urani, uendelezaji wa rasilimali watu, na maeneo mengine niliyoyataja awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Masuala ya ujumla katika Wizara. Uendelezaji wa Rasilimali Watu. Kwa upande wa kusimamia sheria, kanuni na taratibu na kuendeleza rasilimali watu, watumishi 15 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo baada ya kukidhi Vigezo vya Miundo ya Maendeleo ya Utumishi wa Umma vya mwaka 2002 pamoja na Tathmini ya Utendajikazi kwa Uwazi yaani, *Open Performance Review and Appraisal System - OPRAS*. Watumishi 127 wamejaza fomu za Mikataba ya Utendaji kazi kwa Uwazi na wanatarajiwa kufanya tathmini mwishoni mwa mwezi Juni 2013. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuwapatia nafasi ya mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya watumishi 23 wamepata mafunzo katika mwaka wa fedha 2012/13. Vile vile, Wizara imeweza kujaza nafasi 7 za Wakurugenzi Wasaidizi zilizokuwa wazi katika Idara kwa kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia maadili ya kiutendaji katika utumishi wa umma kwa kuwaelimisha watumishi kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002; Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.18 ya mwaka 2007; Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003; Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Toleo la mwaka 2009; na Nyaraka za Serikali na taratibu mbalimbali za utendaji kazi mbalimbali kupitia mikutano mbalimbali ya watumishi, mikutano ya Chama cha Wafanyakazi (TUGHE) na mkutano wa Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kujikinga na Maambukizi ya UKIMWI. Wizara katika mwaka wa fedha 2012/13 imeteua wajumbe wapya wa Kamati ya UKIMWI baada ya wajumbe wengi wa kamati ya awali kuhamishwa. Pamoja na mambo mengine, Kamati hii imeelimisha watumishi kuhusu kujikinga na kuepuka maambukizi mapya ya UKIMWI, upimaji wa UKIMWI kwa hiari, matumizi ya dawa za kurefusha maisha kwa waishio na virusi vya UKIMWI na njia za kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI na maambukizi ya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Elimu hii imetolewa katika mkutano wa watumishi wote mwezi Desemba 2012 pia katika mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika mwezi Mei 2013. Aidha, Wizara imeendelea kuelimisha watumishi kujitokeza ili wale waliopata maambukizi waweze kupatiwa huduma kwa mujibu wa Waraka Na. 2 wa mwaka 2006 kuhusu Kuhudumia Watumishi wa Umma wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uandaaji wa Sera na Miongozo Mbalimbali katika Sekta. Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma, Sheria na Mikataba.Ukaguzi wa matumizi ya fedha kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake umeendelea kufanywa kwa lengo la kuongeza nidhamu na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma na kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi ili kupata matokeo mazuri na yenye tija kwa Taifa. Taarifa za ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, CAG na ule uliofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi katika Sekta ya Umma, PPRA zimethibitisha mwenendo mzuri katika eneo hili. Aidha,

Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika masuala yote yanayohitaji ushauri wa kisheria ikijumuisha masuala ya mikataba, miswada, sheria ndogo ndogo, kuridhia itifaki za kikanda na kimataifa, na pale ilipojitokeza kurejea sheria zilizopo ili kuongeza tija na kuleta ufanisi katika sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iko katika hatua za mwisho za kurejea Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA ya mwaka 2003 ambapo Sera Mpya ya TEHAMA inategemewa kuwa tayari mwezi Agosti 2013. Pia, uandaaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo, *Implementation Strategy* unafanywa sambamba na uhuishaji wa sera hiyo. Vile vile, Wizara inafanya marejeo ya Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996. Kazi hii inafanyika sambamba na Programu ya Mageuzi ya Mfumo wa Ubunifu nchini *National Innovation System Reform* ambayo pia inatarajiwa kukamilishwa kabla ya mwezi Desemba 2013. Aidha, Wizara imekamilisha uandaaji wa mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya mawasiliano *Telecentres* ambao utaanza kutumika rasmi mwezi Julai 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuzingatiwa Taratibu za Ununuzi wa Umma. Wizara imeendelea kusimamia michakato mbalimbali ya kuwapata wazabuni wa kutoa huduma mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi Na. 21 ya mwaka 2004. Kupitia utaratibu huu, shughuli zote za Ununuzi na Ugavi zimesimamiwa kwa kushirikiana na Wakala wa Ununuzi na Ugavi wa Serikali GPSA ambapo ununuzi wa bidhaa na huduma zote Wizarani na kwenye taasisi zake umezingatia taratibu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwenye Taasisi za Mawasiliano. Shirika la Posta Tanzania *(TPC).* Shirika la Posta Tanzania katika jitihada zake za kuongeza na kuimarisha matumizi ya TEHAMA limeunganisha ofisi za Posta 88 katika mtandao. Pamoja na kufikiwa kwa hatua hii, Shirika limepokea vifaa vingine kutoka Umoja wa Posta Duniani *(UPU)* vitakavyoliwezesha kuendelea kuunganisha ofisi zake zingine 100 ifikapo mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta limeendelea kuboresha mazingira ya kazi na utoaji wa huduma kwa kuyafanyia matengenezo majengo ya Ofisi za Posta Kuu za Morogoro, Dodoma, Tabora, Sokoine *Drive* Dar es Salaam na Shangani Zanzibar na hivyo kupatikana nafasi za kukodisha. Vilevile, mchakato wa kuendeleza viwanja vya Shirika la Posta kwa ubia unaendelea kwa viwanja Na. 6 na Na. 7 vilivyopo mtaa wa Ohio/ Ghana Avenue na kwenye Kiwanja Na. 416/G kilichoko Ubungo Dar es Salaam. Pia, upanuzi wa Ofisi ya Posta ya Makao Makuu Dodoma umekamilika. Aidha, mkataba unakamilishwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi mpya za Posta ya Kibondo ambapo Mkandarasi ataanza ujenzi mwezi Julai, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za kujiimarisha, Shirika limeanzisha huduma mpya ikiwemo *City Urgent Mail, Bureau de Change* Dar es Salaam, na *EMS Cargo* ambazo zimeliwezesha Shirika kufanikiwa kupata zabuni kubwa za usafirishaji wa vifaa vya Tume ya Uchaguzi, vifaa vya Sensa ya Watu na Makazi na vifaa vya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA)*. Kwa upande wa mapato, Shirika limeanza kupata faida kwa mujibu wa hesabu zillizokaguliwa kwa mwaka 2010 na 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL).* Mapato ya *TTCL* kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2012 yamefikia shilingi bilioni 91.445, ikilinganishwa na shilingi bilioni 84.496 katika kipindi kama hicho mwaka 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili kwa kiasi kikubwa limetokana na *TTCL* kupanua utoaji wa huduma za mtandao wa mawasiliano *Backbone Network Services* wenye ubora wa hali ya juu unaotumia teknolojia ya kisasa ya *Next Generation Network- NGN.* Huduma muhimu zinazotolewa na *TTCL* ni pamoja na mawasiliano ya simu, *data* na *video*. Huduma hizi kwa ujumla wake hivi sasa zimefikishwa kwenye Makao Makuu ya Mikoa yote ya Tanzania na juhudi zinaendelea kuzisambaza zaidi katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* iliendelea kudhibiti matumizi ambapo matumizi ya mwaka 2012 yalikuwa chini ya kadirio kwa Sh.bilioni 8.556. Hii ni kutokana na kwamba matumizi yote ya mwaka yalikuwa Sh. bilioni 90.206 ikilinganishwa na kadirio la jumla ya Sh.bilioni 98.762. Aidha, matumizi ya Sh. bilioni 90.206 kwa mwaka 2012 ni chini ya yale ya mwaka 2011 yaliyokuwa Sh. bilioni 91.588. Kampuni inaendelea kuangalia njia za kupunguza zaidi matumizi yake ambayo itazichukua bila kuathiri tija na ufanisi wa shughuli za Kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa mapato kutokana na huduma zilizotolewa na Kampuni uliendelea kuimarishwa ambapo kwa mwaka 2012, ukusanyaji wa mapato hayo ulifikia wastani wa Sh. bilioni 7.667 kwa mwezi sawa na asilimia 94 ya thamani ya huduma zinazotolewa na Kampuni kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* imeendelea kujenga na kupanua njia za mawasiliano za mkongo katika mikoa yote na baadhi ya Wilaya nchini. Mtandao huu pia umeunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na baadae kuunganishwa na mikongo ya baharini ya *SEACOM* na *EASSy*. Hatua hii itaifanya *TTCL* kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa kampuni zingine zinazotaka kujiunga na mkongo huo wa baharini kupitia mtandao wake. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2012, *TTCL* imefanikiwa kutekeleza miradi mikubwa ya kutoa huduma za data kwa wateja wakubwa *corporate customers* zikiwemo benki, taasisi za fedha, ofisi na taasisi za Serikali, vyuo vikuu na taasisi nyingine za elimu ya juu, balozi na taasisi za dini kampuni mbalimbali na wateja wa nje ya nchi ikiwemo *Rwanda Development Board.* Aidha, kutokana na upana wa mtandao wa TTCL, kampuni nyingine za simu za hapa nchini ikiwemo *Tigo*, *Airtel*, *Vodacom* na *Zantel* zinatumia mtandao wa *TTCL* kuweza kuunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko kubwa la matumizi ya data pamoja na ongezeko la wateja ikiwa ni pamoja na kampuni nyingine za mawasiliano kutumia

mtandao wa *TTCL*, Kampuni imepanua uwezo wa mkongo wake katika Jiji la Dar es Salaam yaani *Dar es Salaam Metro Fiber* kutoka 10 *Gbps* na kuwa 20 *Gpbs* ili kuweza kukidhi mahitaji ya huduma. Aidha, *TTCL* pia imejenga njia za mawasiliano za *microwave* za Mikumi – Kidatu – Ifakara mkoani Morogoro pamoja na Karatu kwenda Geikurum, Arusha ili kuweza kutoa huduma kwa Ofisi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii - *National Social Security Fund - NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi na hujuma za mara kwa mara kwenye miundombinu ya mawasiliano inayomilikiwa na *TTCL* (ukataji wa nyaya za simu za shaba *copper cables* na mikongo ya vigae *optic fibre cables* umeendelea kuathiri biashara ya *TTCL* kwa kupunguza ubora wa huduma na kuongeza gharama za uendeshaji. Kampuni imeendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi, Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi na Serikali za Vijiji kukabiliana na tatizo hili. Aidha, *TTCL* imeanza kubadilisha mitandao ya nyaya za shaba kwa kuweka nyaya za vigae na pia kutumia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika maeneo ambako mkongo huo umepita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA).* Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania pamoja na mambo mengine, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwemo:-

(i) Kusimamia na kukuza ushindani katika sekta ya mawasiliano na utangazaji kwa ajili ya kuboresha tija ya sekta ya mawasiliano kiuchumi na huduma bora kwa mtumiaji;

(ii) Kutoa masafa na leseni za mawasiliano;

(iii) Kusimamia ubora wa uingizaji na matumizi ya vifaa mbalimbali vya TEHAMA nchini;

(iv) Kusimamia na kudhibiti gharama za matumizi ya teknolojia mbalimbali za mawasiliano; na

(v) Kuhakikisha ubora wa huduma za mawasiliano kwa mtumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kati ya Julai 2012 hadi Aprili 2013, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeweza kusimamia kwa ufanisi ushindani wa gharama za matumizi ya simu nchini ambapo kiwango cha kupiga simu ndani ya mtandao mmoja wa simu kwa kampuni zote nchini ilikuwa kati ya Sh.75 hadi Sh. 89 kwa dakika. Kiwango hiki kuendelea kutumika kwa muda mrefu kunaashiria kuwepo kwa ushindani ndani ya sekta ya mawasiliano uliosababisha bei zisipande na watoa huduma kujikita zaidi katika kushindana kupitia utoaji wa huduma bora ya ushindani kwa kupungaza gharama kama walivyokuwa wakifanya hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania pia imesimamia kuanza kutumika kwa gharama mpya za upigaji simu baina ya mitandao ambapo kuanzia tarehe 1 mwezi Machi 2013, gharama hizo zilishuka na kufikia Sh. 34.92 kwa dakika. Kwa mtiririko huu, inatarajiwa kuwa ifikapo tarehe 1 Januari 2017 gharama hizi zitashuka kufikia Sh. 26.96 kwa dakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi Julai 2012 hadi Mei 2013, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano ambapo zaidi ya asilimia 50 ya malalamiko hayo yalitokana na huduma za mawasiliano ya simu. Malalamiko mengi yalihusu zaidi matumizi ya lugha mbaya katika mawasiliano ya simu, kusitishwa kwa matumizi ya laini za simu yaani, *simcard blocking*, utolewaji wa huduma kwa wateja, *customer service* na matatizo ya usajili wa laini za simu. Aidha, malalamiko yaliyobaki yalihusu matumizi ya teknolojia mpya ya utangazaji ya dijitali. Mamlaka iliweza kushughulikia malalamiko hayo kwa mujibu wa sheria na taratibu ambapo adhabu zilitolewa kwa watumiaji na kampuni zilizokiuka sheria za Mawasiliano. Vile vile, Mamlaka ilitoa elimu kwa umma ili kutolea ufafanuzi

kwa malalamiko yaliyohusu uelewa mdogo wa matumizi ya vifaa vya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inakamilisha hatua za mwisho kuwezesha matumizi ya namba za dharura, yaani Namba 111 au 112. Namba hizi tayari zimeunganishwa na mitandao yote ya simu nchini na mwananchi yeyote ataweza kupiga namba hizi bure ili kuweza kupata msaada kutoka Jeshi la Polisi. Hivi sasa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iko katika hatua za mwisho za kufanya majadiliano na Jeshi la Polisi nchini ili kuona namna ya kusimamia uendeshaji wa matumizi ya huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, wananchi wote wameshuhudia mabadiliko makubwa yaliyotokea kwenye sekta ya utangazaji nchini ambapo matumizi ya teknolojia mpya ya dijitali yalianza rasmi tarehe 1 Januari 2013. Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imewezesha mabadiliko haya kufanyika kwa ufanisi mkubwa na wananchi wanaendelea kunufaika na mabadiliko hayo. Kupitia Bunge hili ninaomba wananchi walio katika maeneo ambayo mabadiliko haya bado hayajatekelezwa watoe ushirikiano wa kutosha pindi utekelezaji utakapoanza katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF).* Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)* umeajiri wafanyakazi saba ikimjumulisha Meneja wa Mfuko jambo ambalo limeongeza ufanisi wa utendaji wa Mfuko huo. Hii ni pamoja na utekelezaji wa programu ya kupeleka mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara ambao umeanza katika Kata 52 kama nilivyoeleza hapo awali. Aidha, Mfuko umeendelea na juhudi za upatikanaji wa fedha za kutekeleza programu hii ikiwemo fedha za ruzuku kutoka kwa Watoa Huduma za Mawasiliano na mkopo kutoka Benki ya Dunia. Sambamba na haya, Mfuko umeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kupitia Mpango Kazi wake, ikiwemo uendelezaji wa vituo vya mawasiliano vijijini *telecentres*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za maendeleo kwenye Taasisi za Sayansi Na Teknolojia. Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *DIT* imeendelea kufanya upanuzi wa udahili na uanzishaji wa programu mpya za Stashahada kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika mwaka wa masomo wa 2012/2013, Taasisi imedahili wanafunzi 1,371 na kufikisha jumla ya wanafunzi 2,721 ikilinganishwa na wanafunzi 2,583 katika mwaka wa masomo wa 2011/2012 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 28.62.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, pia imeendelea na ukarabati wa upakaji rangi majengo yote ya ofisi, karakana, maabara na bweni moja la wanafunzi wa kike na bweni moja kati ya manne ya wanafunzi wa kiume lililokuwa katika hali mbaya zaidi katika Kampasi ya Dar es Salaam. Vilevile, *DIT* imeendelea kufanya ukarabati kwenye jengo la utawala, jengo la uzalishaji na jengo la maabara katika Kampasi ya Mwanza iliyokuwa ikijulikana kama Tanzania *Institute of Leather Technology TILT*. Ukarabati huu umeiwezesha Kampasi hii kuwa tayari kuanza kutoa mafunzo mbalimbali. Aidha, ujenzi wa awamu ya pili wa jengo la kufundishia *DIT Teaching Tower* lililoko kwenye Kampasi ya Dar es Salaam unaendelea. Kazi zilizobaki kwenye jengo hilo ni pamoja na uwekaji wa milango; madirisha; kutenganisha kuta za ndani; usimikaji wa mabomba ya majisafi na majitaka; uwekaji wa waya za umeme, viyoyozi, na waya za mawasiliano simu na intaneti, na uwekaji wa lifti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utafiti na maendeleo, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imeendelea kutoa huduma za kitaalam kwenye nyanja mbalimbali ikiwemo upimaji na ushauri kuhusu udongo kwa ajili ya ujenzi. Baadhi ya kazi hizi ni utafiti wa udongo kwenye Msikiti ulioko Zanzibar na kwenye mradi wa *Inland Container Terminal Construction Mwanza*. Vile vile, Taasisi imeingia kwenye mkataba na Shirika la Nyumba la Taifa wa kufanya utafiti wa udongo kwenye eneo la Kibada Kigamboni. Aidha, Taasisi imeingia mkataba na Mamlaka ya Bandari Tanzania wa

kufanya utafiti wa udongo katika Makao Makuu yake Dar es Salaam. Mambo mengine ambayo Taasisi imeyafaya ni pamoja na kuweka jenereta *Power Generator installation* katika taasisi ya Baraza la Mitihani Tanzania na kufanya ukaguzi wa umeme *Electrical inspection* katika Jengo la Posta - Posta *House* Dar es Salaam. Hivi sasa, Taasisi inafanya upembuzi yakinifu wa mradi wa kuzalisha umeme wa maji *Mini Hydro Power* Ijangala huko Makete, Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), kimeendelea na upanuzi wa udahili na uanzishaji wa programu mpya. Katika mwaka wa masomo 2012/2013, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa imeongezeka kutoka wanafunzi 2,591 kwa mwaka 2011/2012 hadi kufikia wanafunzi 3,156 katika mwaka 2012/2013, ikiwa ni ongezeko la asilimia 22. Aidha, katika jitihada za kuongeza udahili wa wanafunzi katika Chuo hicho, msisitizo umewekwa katika kuongeza wataalam wa ngazi ya kati wakiwemo mafundi sanifu (*technicians)* na mafundi sadifu (*artisans)*, kwani kati ya wanafunzi 3,156, wanafunzi 2,310 ni wanafunzi wa ngazi ya stashahada (*technicians)* ikilinganishwa na wanafunzi 846 wa ngazi ya shahada. Pia, Chuo kilitoa mafunzo ya awali (*pre entry course)* kwa jumla ya wanafunzi 530, wasichana wakiwa 214 na wavulana wakiwa 316. Kupitia utaratibu huu, jumla ya wasichana 154 walifanikiwa kudahiliwa baada ya kufanya mitihani na kufaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la maktaba litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja, ulianza rasmi tarehe 6 Septemba 2012 na unatarajiwa kukamilika baada ya miezi 12. Hatua iliyofikia kwa sasa ni kukamilishwa kwa ujenzi wa ghorofa ya chini *basement floor*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa taaluma, Chuo kimekamilisha uandaaji wa mitaala mipya ya Teknolojia ya Maabara; Sayansi na Teknolojia ya Vyakula; Mekatroniki; Uhandisi Madini na Uhandisi Usalama na kuwasilisha mitaala hiyo kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* kwa

ajili ya kupata ithibati. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika nyanja mbalimbali ikiwepo ujenzi wa majengo, upimaji wa udongo na miradi midogo ya uzalishaji umeme kwa kutumia maji (mini *hydroelectric projects* katika maeneo ya nyanda za juu kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 2 Novemba, 2012. Aidha, Taasisi imeweza kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 83 mwaka wa masomo wa 2011/2012 hadi kufikia wanafunzi 135 katika mwaka wa masomo 2012/2013. Kati ya wanafunzi hao, 89 ni wa shahada ya uzamili na 46 ni wa shahada ya uzamivu. Pia, Taasisi imeajiri wafanyakazi 150, ambapo wanataaluma ni 49, waendeshaji ni 48, na mafundi sanifu ni 53.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi hii ni ya kipekee kwenye ukanda huu wa Afrika ya Mashariki ikiwa imelenga kuzalisha watafiti na wanataaluma watakaotumika kwenye vyuo vikuu vingine na kwenye utafiti katika taasisi na kampuni binafsi kuziba pengo kubwa lililojitokeza la upungufu wa wanataaluma hao kutokana na wengi wao kufikia umri wa kustaafu na nyanja nyingi mpya kujitokeza zinazohitaji utaalam mahiri. Wakati huo huo, Taasisi hii itaziba pengo katika miundombinu ya kimaabara kwa kuwa na maabara mahiri kwenye maeneo mbalimbali ya sayansi na teknolojia ikiwemo eneo la TEHAMA zitakazoweza kutumiwa na vyuo na taasisi nyingine za utafiti hapa nchini na kwenye ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Katika kusimamia utekelezaji wa sheria za kudhibiti viwango vya mionzi, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania iliendelea kupima sampuli za vyakula vyote vinavyoingia na vinavyotoka nchini. Aidha, Tume ilikagua na kutathmini usalama wa mionzi katika vituo 22 kati ya vituo 50 vilivyotarajiwa kukaguliwa. Kati ya vituo hivyo, vituo 11

vilikidhi viwango vya usalama. Kupitia ukaguzi huo, Tume imevifungia vituo 40 baada ya kuvibaini kutokidhi vigezo muhimu vya matumizi salama ya mionzi. Wakati huo huo, Tume imesajili vyanzo vya mionzi vipatavyo 1,029 na vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi vipatavyo 582 hadi ilipofikia tarehe 31 Machi, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Tume ilitathmini maombi ya leseni za vyanzo vya mionzi kutoka kwenye vituo 213 na ambapo ilivipatia vibali vituo 200 vilivyokidhi vigezo. Tume ilipima mionzi kwa wafanyakazi 841 kati ya wafanyakazi wanaokadiriwa kuwa 1,300 kwenye vituo 176. Vilevile, Tume ilipima mionzi kwenye sampuli za vyakula 1,286 kati ya 1,237 zilizotarajiwa kupimwa na kuzitolea vibali (leseni). Hali kadhalika, Tume iliweza kufanya matengenezo katika vifaa vya elektroniki vilivyo na vyanzo vya mionzi vipatavyo 25 na mashine za *X-ray* zipatazo tano (5) na kuhakiki vifaa vipatavyo 56 kati ya vifaa 75 vilivyotarajiwa kuhakikiwa mwaka, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Sayansi na Teknolojia. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Tume ya Sayansi na Teknolojia imeendelea kugharimia mafunzo ya wataalam 279 katika ngazi ya Shahada ya Uzamili (*MSc*) na Uzamivu (*Ph.D.*) ambayo yanagharimu jumla ya shilingi bilioni 6.17 kwenye vyuo vikuu sita (6) vya umma ambavyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Tiba na Afya cha Muhimbili, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Mzumbe na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha. Kipaumbele kiliwekwa katika kutoa nafasi nyingi za mafunzo kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzipatia jumla ya asilimia 37 ya ufadhili, ambapo asilimia 28 zilitolewa kwa watafiti wa sekta ya kilimo na asilimia tisa (9%) kwa sekta ya mifugo na uvuvi. Aidha, wataalam nane (8) kutoka Zanzibar wamepatiwa mafunzo kwenye ngazi ya shahada za uzamivu kupitia ufadhili huu. Sambamba na hili, Tume iliendelea na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ya utafiti ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.635 kililipwa kwenye taasisi mbalimbali za utafiti kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu.

Aidha, Tume imeendelea kuimarisha mahusiano yake na mashirika na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika masuala mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa fedha za utafiti na maendeleo na za kuendeleza sayansi na teknolojia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imeendelea kuratibu shughuli za maendeleo ya sayansi ikiwa ni pamoja na kuipatia ofisi Taasisi isiyo ya kiserikali ya *Tanzania Academy of Sciences* katika jengo la Tume. Sambamba na haya, Tume imeendelea kuratibu programu mbalimbali za sayansi na teknolojia kiwemo kufanya semina ya Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Wakuu wa Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyofanyika tarehe 17 Januari 2013 ambayo ililenga kuhamasisha matumizi ya ushahidi wa tafiti (*evidence based decision making*) katika kufanya maamuzi ya kisera na mipango na pia kutambulisha shughuli na kazi za Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utafiti hapa nchini, Tume imeendelea na juhudi za majadiliano na mashirika ya kimataifa ili kupata ufadhili wa miradi ya pamoja yenye manufaa kwa pande zote. Nchi za Sweden, Uholanzi, Canada na Marekani ni miongoni mwa nchi zilizoonyesha nia ya kushirikiana na nchi yetu katika kufadhili kwa pamoja utafiti na uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizopo katika Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu na malengo ya sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia zipo pia changamoto zinazopunguza kasi ya kufikiwa kwa malengo ya sekta. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi zinazoendesha programu za mafunzo katika ngazi za Diploma kutokuwa na stahili ya mkopo na kutegemea fedha za matumizi mengineyo. *MUST* na *DIT* zinaendesha programu za mafunzo

katika ngazi za Cheti na *Diploma* ambazo wanafunzi wake hawana stahili ya kupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kama ilivyo kwa wanafunzi wanaosoma katika ngazi ya Shahada. Pamoja na kwamba wanafunzi hao hulipa ada katika taasisi hizo, kiasi wanacholipa cha Sh.130,000 kwa mwaka ni kidogo sana ikilinganishwa na gharama halisi za kumsomesha mwanafunzi. Gharama za moja kwa moja *(student direct cost)* za wanafunzi hao hulipwa na Serikali. Gharama ambazo zinatakiwa kulipwa moja kwa moja na Serikali ni Sh.1,680,000 kwa mwanafunzi ambapo gharama za chakula kwa mwanafunzi mmoja kwa mwaka ni Sh. 1,190,000, na gharama ya mafunzo kwa vitendo viwandani ni Sh.490,000 kwa mwanafunzi mmoja kwa mwaka. Katika miaka ya hivi karibuni, kiasi cha fedha ambazo zinapatikana kutokana na fedha za matumizi mengine ni chini ya Sh.350,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka ikilinganishwa na mahitaji ya Sh.1,680,000 kwa mwaka ambazo zinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukubwa wa gharama hizi hufanya fedha zinazotengwa katika matumizi mengineyo (*OC*) kwa taasisi hizi kutototosheleza na hivyo kulazimu kuomba fedha kutoka Hazina, hali ambayo huyaacha maeneo mengine yanayohitaji kutumia fedha hizo za matumizi mengineyo kutokuwa na fedha za kuyatekeleza. Hali hii mbali na kuzifanya taasisi hizi kuwa duni katika maeneo yanayokosa fedha, huziweka katika hali ya wasiwasi ya migomo ya watoa huduma mbalimbali za msingi zikiwemo huduma za chakula kutaka kusitisha utoaji wa huduma hizo kwa kucheleweshewa malipo yao. Kwa upande wa masomo, kutopatikana kwa fedha kwa ajili ya matumizi mengine kunasababisha wanafunzi kuchelewa kwenda kwenye mafunzo kwa vitendo viwandani (*industrial pratical training)* wakingoja fedha kutoka Hazina ili kuziba pengo la fedha kutokana na matumizi ya wanafunzi kuwa ya juu kulinganisha na fedha inayotolewa. Matokeo ya uhaba huu wa fedha, ni kuwa Taasisi za mafunzo zimeendelea kuwa na malimbikizo ya madeni kwa watoa huduma za chakula na pia vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Hali hiyo imekuwa ikileta wasiwasi mkubwa katika uendeshaji wa taasisi hizo na pia

kuchelewesha kufikiwa kwa azma ya Serikali ya kuandaa rasilimali watu ya kutosha katika kutumia sayansi na teknolojia katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya utekelezaji wa mabadiliko ya mfumo wa utangazaji kutoka teknolojia ya analojia kwenda teknolojia ya dijitali. Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma na kujadiliana na wadau katika kutekeleza uhamaji kutoka mfumo wa utangazaji wa analojia kwenda mfumo wa utangazaji wa dijitali bila kurudisha nyuma juhudi za Serikali zilizofikiwa. Tathmini ya ufanisi katika utekelezaji wa awamu ya kwanza imeanza ili kubaini njia za kutekeleza awamu zinazofuata kwa ufanisi zaidi. Aidha, kwenye miji yote mingine mitambo ya analojia bado ipo hewani na itaendelea kuwa hewani mpaka pale mitambo ya dijitali kwenye miji hiyo itakaposimikwa na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama katika mitandao ya mawasiliano. Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na matumizi ya TEHAMA ulimwenguni kote ikiwemo nchini mwetu, kasi kubwa ya mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano ikiwemo simu za kiganjani, imeleta pia hofu ya usalama wa mitandao na mali za watumiaji na uvunjifu wa maadili katika jamii. Kama nilivyoeleza hapo awali, zipo jitihada za kitaifa na kikanda za kukabiliana na matishio haya kwa jamii. Juhudi zinazoendelea ni pamoja na kuanzishwa kwa Kikosi Maalum cha Kukabiliana na changamoto hizi na uandaaji wa Sheria ya Usalama katika Mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa kampuni za mawasiliano katika kupeleka mawasiliano kwenye maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara. Kasi ndogo na kukosekana kwa utayari wa watoa huduma za mawasiliano kupeleka mawasiliano katika baadhi ya maeneo ya vijijini na yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara vimeendelea kurudisha nyuma azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi wote mawasiliano. Katika kukabiliana na hali hii, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umeandaa namna muafaka ya kutoa

vivutio kwa watoa huduma hao na kuwashawishi kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo kupitia ruzuku. Juhudi zilizofanywa na Mfuko, ikiwemo utafiti uliofanywa kupitia Mshauri Mwelekezi zimeanza kuzaa matunda ambapo tayari kampuni nne (4) za mawasiliano ya simu zimejitokeza na kushinda zabuni za kujenga miundombinu katika maeneo yaliyochaguliwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango ulioandaliwa na Mfuko kama nilivyoeleza hapo awali. Aidha, Serikali kupitia Mfuko huu inaendelea na juhudi za kuongeza fedha kwenye Mfuko huo ili kuharakisha upelekaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo ambayo hayana mvuto wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchache wa mitaji ya kuwaendeleza ujasiriamali na ubunifu katika sekta ya TEHAMA nchini. Uwezeshaji wa wajasiriamali kwa mitaji umekuwa ni changamoto kutokana na taasisi za fedha zikiwemo benki kutozitambua fursa zilizopo kwenye biashara mpya hususan katika eneo la TEHAMA. Jambo hili limewaathiri kwa kiasi kikubwa wajasiriamali wachanga kwa kukosa mikopo ili kuanzisha biashara zao na kuendeleza ubunifu wao. Aidha, fikra za vijana wetu walio wengi kutaka kuajiriwa badala ya kujiajiri zinadhoofisha dhana ya ubunifu na kujiajiri. Wizara inatekeleza programu mbalimbali kuikabili hali hii ikiwa ni pamoja na uanzishwaji na uendelezwaji wa atamizi kupitia *COSTECH*. Ufadhili wa miradi kwa lengo la kuibiasharisha kupitia Mfuko wa Utafiti na Maendeleo na Ujenzi wa Mji Mahiri wa TEHAMA ambao utafungua milango kwa wajasiriamali kuwekeza na kuanzisha bidhaa mpya na kampuni chipukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ndogo ya utekelezaji wa programu ya uanzishaji wa anuani za makazi na misimbo ya posta nchini. Ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta unafanywa kwa kasi stahiki, suala la ushirikishwaji wa wadau muhimu katika utendaji na ufadhili limepewa kipaumbele kikubwa. Hadi sasa utekelezaji wa mradi huu unafanywa kwa ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI; Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar; Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano (SMZ);

Wizara ya Mambo ya Ndani; Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi (SMZ); Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; Ofisi ya Takwimu ya Taifa; Shirika la Posta Tanzania. Wadau wengine huhusishwa kwa misingi ya kuhitajika kwao kwa wakati husika. Aidha, kwa kuzingatia gharama za kutekeleza mradi huu kwa nchi nzima zinazokadiriwa kuwa shilingi bilioni 158, mradi umepanga kuzipata fedha hizi kupitia vyanzo mbalimbali ikiwemo kuchangiwa na wadau mbalimbali kama vile Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya; Taasisi mbalimbali; sekta binafsi na wananchi. Kwa upande wake, Wizara imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1 katika Bajeti ya mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za utafiti na maendeleo kutotengewa fedha za kutosha. Upungufu wa fedha umeendelea kuathiri utekelezaji wa malengo na ufanisi wa shughuli za utafiti na maendeleo. Azma ya Serikali ni kutumia asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa katika shughuli za utafiti na maendeleo katika siku za usoni. Kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali itaendelea kuongeza kiwango cha fedha za utafiti na maendeleo na kuweka vivutio kwa sekta binafsi na wadau wengine kuchangia fedha za Utafiti na Maendeleo. Juhudi hizi ni pamoja na mikakati inayoendelea kubuniwa kupitia programu ya mageuzi ya sayansi na teknolojia na sheria ya sayansi na teknolojia zinazokamilishwa. Pamoja na mambo mengine, mikakati hii itaweka vivutio kwa sekta binafsi na wadau wengine kuchangia mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ndogo ya wataalam katika nyanja za sayansi na teknolojia. Kuna uhaba wa wataalam katika nyanja mbalimbali za sayansi, teknolojia na ubunifu. Hali hii inajitokeza kwa kuwepo idadi ndogo ya wataalam; wataalam wengi kuwa wa umri mkubwa; wataalam kutokuwa na uelewa wa teknolojia mpya zinazohitajika sokoni hivi sasa; uchache wa mafunzo ya kazini unaotokana na uhaba wa fedha; na kutokuwepo kwa uwiano unaohitajika baina ya kada mbalimbali ndani ya taaluma kama vile uwiano wa kada ya Wahandisi na Mafundi Mchundo wa ngazi ya Cheti na Diploma; na Wauguzi na Madaktari. Baadhi ya sababu za upungufu wa wataalam

kwenye baadhi ya taaluma ni kujitokeza kwa maeneo mapya ya uzalishaji ikiwemo uvumbuzi wa madini ya urani huko Bahi (Dodoma) na Namtumbo (Ruvuma); uvumbuzi wa gesi Mtwara na uvumbuzi wa madini ya chuma huko Mchuchuma na Liganga kunakoongeza uhitaji wa wataalam katika kada zote ikiwemo za uhandisi wa madini na gesi. Wizara kupitia Sera ya Utafiti na Maendeleo inaandaa mikakati ya muda mfupi na mrefu ili kupata ufumbuzi wa kudumu kukabiliana na changamoto hii kwa kushirikiana na wadau wa sekta hii. Aidha, vyuo na taasisi za sayansi na teknolojia za *MUST*, *NM-AIST* na *DIT* zimeanzisha kozi mpya katika baadhi ya maeneo haya na kuanza udahili wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto nilizozieleza, Wizara itajitahidi kutekeleza majukumu yake ili kuzipatia ufumbuzi changamoto hizi na kuongeza mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014, mawasiliano. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuratibu zoezi la uhamaji wa mfumo wa utangazaji kutoka analojia kwenda dijitali baada ya kufanya tathmini ya kina ya utekelezaji katika awamu ya kwanza;

(ii) Kuendelea kutekeleza uwekaji na matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta (Physical Addressing and Post Code Systems) katika maeneo mbalimbali ya nchi;

(iii) Kuendelea kupanua mtandao na kuboresha huduma za mawasiliano ya simu na intaneti nchini ikiwemo kuimarisha vituo vya mawasiliano vijijini;

(iv) Kukamilisha zoezi la uhuishaji wa Sera ya TEHAMA, kuratibu utekelezaji wake na kuanza uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta;

(v) Kukamilisha uanzishaji wa Tume ya TEHAMA na kusimamia utendaji wa taasisi za mawasiliano hususan *TTCL*, *UCAF*, *TPC* na *TCRA*;

(vi) Kuendelea kupanua mtandao wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kuufikisha katika maeneo mbalimbali nchini na kupanua matumizi yake katika nyanja mbalimbali za kijamii, utawala bora na uchumi nchini na kutoa huduma kwenye nchi jirani;

(vii) Kuendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazoikabili sekta binafsi hapa nchini na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya mawasiliano ili iendelee kuchangia ipasavyo maendeleo nchini;

(viii) Kuendelea kuratibu ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA nchini ikiwa ni pamoja na ushiriki, utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kusambaza huduma zake nchi nzima;

(ix) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa kuunganisha vituo (*sites*) vipatavyo 200 kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano zikiwemo shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya afya, vituo vya posta pamoja na taasisi zilizoainishwa kwenye mradi wa *e-Schools* unaojulikana kama Tanzania *Beyond Tomorrow;*

(x) Kuratibu ushiriki wa nchi kwenye mikutano ya sekta kikanda na kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sayansi, Teknolojia na ubunifu. Kwa upande wa sayansi, teknolojia na ubunifu, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea na uimarishaji wa mifumo, taasisi na rasilimali watu ili kukuza utafiti na matumizi ya sayansi na teknolojia nchini;

(ii) Kukamilisha Programu ya Mageuzi ya Mfumo wa Ubunifu nchini *(National Innovation System Reform);*

(iii) Kuimarisha na kuboresha taasisi za utafiti, sayansi na teknolojia nchini;

(iv) Kubuni, kuandaa na kusimamia sera, mipango ya utekelezaji, miongozo, mikataba, itifaki, sheria na kanuni zinazolenga kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini;

(v) Kukamilisha andiko la programu ya matumizi ya nyuklia;

(vi) Kuimarisha uhusiano wenye tija na wadau mbalimbali katika sayansi, teknolojia na ubunifu ndani ya nchi, kikanda na kimataifa;

(vii) Kuhamasisha jamii kuhusu sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ujumla kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na

(viii) Kuratibu uendelezaji wa miundombinu na rasilimali watu katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya ujumla. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuajiri na kuwapandisha vyeo watumishi wenye sifa na wanaokidhi vigezo mbalimbali vilivyo kwenye Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi wa Umma za mwaka 2002 pamoja na Tathmini ya Utendaji Kazi kwa Uwazi (*OPRAS*);

(ii) Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa uadilifu kwa kutekeleza kanuni za maadili ya kiutendaji katika utumishi wa umma, kwa kuwaelimisha watumishi kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, kanuni na taratibu za uendeshaji katika utumishi wa umma na Sheria

ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007 ili utumishi wa umma uwe wenye ufanisi na wa kuheshimika;

(iii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Waraka Na. 2 wa Mwaka 2006 kwa kuhamasisha watumishi kupima afya zao ili wale watakaoonekana kuwa na upungufu katika afya zao waweze kupatiwa huduma;

(iv) Kuendelea kutoa huduma bora kwa kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi na stahili za watumishi kwa mujibu wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja;

(v) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18 ya Mwaka 2007 kuhusu Mfumo wa kupima Tathmini ya Utendaji Kazi kwa Uwazi (*OPRAS*) kwa kuwawezesha watumishi 157 kujaza mikataba ya kazi;

(vi) Kuendela kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa kuwapeleka kwenye mafunzo watumishi katika maeneo ya sayansi, teknolojia na mawasiliano ili kuwaongezea ujuzi, maarifa na ufanisi katika utendaji wao wa kazi;

(vii) Kuendelea kuimarisha sekta ya TEHAMA, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia utekelezaji wa mifumo ya kimenejimenti mathalani Miundo ya TEHAMA, mgawanyo wa majukumu pamoja na mpango wa kurithishana madaraka;

(viii) Kuendelea na usimamizi wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 (*PFA*) na marekebisho yake;

(ix) Kuendelea na utayarishaji na usimamiaji wa Hesabu na Taarifa za Fedha za Wizara kwa wakati;

(x) Kuendelea na usimamiaji wa miongozo ya Serikali inayohusu matumizi sahihi ya fedha na mali zote za Serikali. Aidha, itasimamia Sheria ya Ununuzi wa Umma (*PPRA*) ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005;

(xi) Kuendelea kuandaa nyaraka mbalimbali kwa ajili ya malipo ya pensheni;

(xii) Kuratibu uandaaji na uhuishaji wa sera na sheria mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara;

(xiii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2012/2013- 2016/2017);

(xv) Kuratibu uandaaji wa Taarifa ya Kusimamia, Kudhibiti na Kuratibu Mapato na Matumizi ya Serikali;

(xv) Kuratibu uandaaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010-2015;

(xvi) Kuratibu utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara na Taasisi zilizo chini yake;

(xvii) Kufanya tathmini ya matumizi ya fedha katika Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia *(Public Expenditure Tracking);*

(xviii) Kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika masuala ya madai, usuluhishi au jinai yanayohusu Wizara na Taasisi; na

(xix) Kushirikiana na vyombo vya habari kuelimisha umma kupitia redio, runinga, magazeti, machapisho na tovuti ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya TEHAMA, sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kudahili wanafunzi 1,500 katika programu za Diploma 860, B.Eng 610, M.Eng. 30 na hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 3,500; Kuanza kufundisha kozi mpya zifuatazo:-

(a) Shahada ya Uzamili ya Uhandisi *(Master of Engineering in Maintenance Management);*

(b) Shahada ya Kwanza ya Teknolojia katika Sayansi ya *Maabara (Bachelor of Technology in Laboratory Sciences);*

(c) Stashahada ya *Multimedia and Film Technology*; na

(d) Stashahada ya *Food Science and Technology.*

(ii) Kukamilisha taratibu za kuanza kufundisha kozi mpya za:

(a) Stashahada ya *Communication Systems Engineering;* na

(b) Stashahada ya *Renewable Energy Technology.*

(iii) Kuendelea kuhudumia wafanyakazi 43 walioko masomoni, wakufunzi 25 na waendeshaji 18; wengi kati ya hao wakiwa wanajilipia ada za masomo na wengine kufadhiliwa na wafadhili mbalimbali;

(iv) Kuendesha mafunzo ya *Pre-entry* ili kuwawezesha wanafunzi wengi wa kike kujiunga na kozi za Ufundi Sanifu. Katika mafunzo hayo taasisi inategemea kupata wanafunzi wa kike 80 wa kujiunga na kozi hizo; *(Makofi)*

(v) Kukamilisha andiko la matumizi bora ya ardhi yake iliyopo Mbezi Kilongawima, Dar es Salaam;

(vi) Kuendelea kuhudumia mradi wa majaribio wa Matibabu Mtandao (*Telemedicine)* utakaounganisha *DIT*, Hospitali za Muhimbili, Amana, Temeke, Mwananyamala, Mbeya, Tumbi na Bagamoyo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine;

(vii) Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la madarasa, maabara na ofisi za wafanyakazi lijulikanalo kama *DIT Teaching Tower* ili liweze kukamilika;

(viii) Kuendelea kujitangaza ili kupata zabuni za kufanya miradi mbalimbali kama vile kutengeneza na kuweka taa za kuongoza magari barabarani, kupima udongo na kazi zingine za kitaalam;

(ix) Kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu ya Kampasi ya Mwanza ya kilichokuwa Chuo cha Ngozi Mwanza ili iweze kuwa katika hali inayokidhi kutoa mafunzo bora ya muda mfupi yanayoendelea na mafunzo ya Stashahada ya Teknolojia ya Ngozi na bidhaa za ngozi yanayotegemewa kuanzishwa; na

(x) Kuendelea kuhudumia Kituo Mahiri cha TEHAMA *(DIT Centre of Excellence in Information, Communication and Technology)* kwa kutoa mafunzo ya TEHAMA, kuhamasisha matumizi ya *Super Computer* na kutoa huduma za *Telemedicine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MUST*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kitatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kudahili jumla ya wanafunzi 3,156 katika ngazi ya Stashahada na Shahada;

(ii) Kuendelea kutoa mafunzo ya awali (*pre-entry*) kwa wanafunzi wa kike kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kufikia 100;

(iii) Kuanzisha kozi mpya za fani za mekatroniki, sayansi na teknolojia ya vyakula, uhandisi usalama, uhandisi mawasiliano na uhandisi madini;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa jengo la maktaba katika awamu ya kwanza litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja;

(v) Kuendelea kujipanua kwa kuanzisha *College of Engineering and Technology; College of Science and Education;* na *School of Business Studies;*

(vi) Kuanzisha na kuendeleza uhusiano na taasisi na vyuo vikuu mbalimbali vya sayansi na teknolojia kitaifa, kikanda na kimataifa;

(vii) Kuajiri watumishi wapya 286, ili kuendana na uhitaji wa rasilimali watu unaotokana na kupanuka kwa Chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela-Arusha. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi ya Nelson Mandela itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha Sera na Miongozo *(Operational Policies and Procedures)* mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Taasisi;

(ii) Kununua vifaa, kujenga na kuweka miundombinu mbalimbali ikiwemo:-

(a) Kununua vifaa vya ofisi;

(b) Kununua vifaa vya kisayansi *(scientific equipment)* kwa ajili ya maabara;

(c) Kuchimba kisima cha maji;

(d) Kununua vitendea kazi na kompyuta *(tools and office equipment – e.g computers, printers and scanners);*

(e) Kujenga Kituo cha TEHAMA *(ICT Resource Centre);*

(f) Kununua samani;

(g) Kujenga mfumo wa kuvuna maji ya mvua;

(h) Kununua magari mawili (2) - gari moja la wagonjwa na basi la kuchukua wanafunzi;

(iii) Kuimarisha uhusiano na ushirikiano na vyuo pamoja na asasi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la Taasisi kujijenga kitaifa, kikanda na kimataifa;

(iv) Kuendeleza mawasiliano na washirika mbalimbali wa kimataifa walio na nia ya kushirikiana na kuendeleza Taasisi;

(v) Kuajiri wafanyakazi wapya 58;

(vi) Kudahili wanafunzi wapatao 150 katika ngazi za Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa mwaka 2013/2014;

(vii) Kukamilisha uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi *(Land use Plan)* wa eneo la Taasisi lililopo Karangai;

(viii) Kuandaa Mkakati na Mpango Mkuu kwa ajili ya kuanzisha *Technology Park na Eco park;*

(ix) Kufuatilia upatikanaji wa Hati Idhini *(Charter)* ya Taasisi; na

(x) Kuratibu ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Nelson Mandela kutoka Moshono hadi Usa River kupitia NM – *AIST* (Kampasi ya Tengeru).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuendelea na juhudi za kuimarisha matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa ili zitumike katika kuandaa sera, sheria, mikakati na mipango itakayoboresha huduma za sekta mbalimbali hapa nchini na katika uzalishaji wa bidhaa kibiashara;

(ii) Kuendelea kuratibu shughuli za utafiti nchini, ikiwa ni pamoja na zile zinazofadhiliwa na mfuko wa MTUSATE na TASENE *(Tanzania, Sweden and the Netherlands);*

(iii) Kuendelea na jitihada za uendelezaji na uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali nchini;

(iv) Kuendelea kugharamia ukuzaji wa matumizi ya sayansi nchini kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Uendelezaji wa rasilimali watu;

(b) Kuboresha mazingira ya utafiti, miundombinu na vitendea kazi;

(c) Kushiriki katika kugharamia miradi mipya ya utafiti na ile inayoendelea kulingana na vipaumbele vya taifa;

(v) Kuanzisha atamizi mpya ya biashara na kilimo (*Agri-Business Incubator)* ili kukuza ujasiliamali na uwekezaji katika sekta ya kilimo, hususan katika usindikaji wa mazao;

(vi) Kuendeleza kuboresha utendaji wa Kongano *(Clusters)* 45 ili ziweze kufanya vizuri zaidi katika soko la ushindani kwa kutengeneza bidha zenye ubunifu na ubora zaidi;

(vii) Kuanzisha mfuko utakaoongeza kasi katika kubuni na kuendeleza teknolojia *(Fund for Technology Development)* mbalimbali kwa njia ya ushindani;

(viii) Kuendelea kubaini vipaji mbalimbali kupitia wagunduzi na wabunifu ikiwemo wabunifu ngazi za vijiji (*grassroots innovators);*

(ix) Kuendelea kurusha vipindi 30 vya runinga, vipindi 20 vya redio kwa kushirikiana na *TBC*; kuchapisha makala 30 katika magazeti, jarida la kielektroniki la kila mwezi na kushiriki kwenye maonyesho 15 yanayohusu sayansi, teknolojia na ubunifu;

(x) Kuandaa maonyesho na makongamano ya wiki ya taifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu;

(xi) Kuboresha shughuli za kuratibu tafiti katika ofisi ya Zanzibar kwa kushirikiana na SMZ;

(xii) Kuendeleza jitihada za kutafuta wadau katika ujenzi wa Kijiji Mahiri cha TEHAMA (*Smart ICT Village)* ambacho kitachangia sana kuleta kampuni kubwa za kimataifa na hatimaye kuweza kukuza uchumi wenye kutumia zaidi maarifa katika uzalishaji (*knowledge economy);* na

(xiii) Kuendeleza jitihada za kutumia Mfuko wa MTUSATE kama kichocheo cha kuwavutia wafadhili wengine ili waweze kuchangia mfuko wa Utafiti na Maendeleo ikiwa ni pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (*TAEC*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki Tanzania itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kupokea na kutathmini maombi 350 ya leseni mbalimbali ili kuona kama yanakidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Usalama na Kinga ya Mionzi ya mwaka 2004;

(ii) Kuendelea na upimaji wa viwango vya mionzi *(personnel dosimetry service)* kwa Wafanyakazi 1,300;

(iii) Kutafuta na kukusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi na kuyahifadhi katika maabara maalum *(Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF)* iliyoko Arusha;

(iv) Kutoa elimu kwa wananchi waishio maeneo yenye madini ya Urani kwa kupitia makongamano manane (8) ili kuongeza uelewa na kuweka tahadhari pale inapostahili;

(v) Kuendelea na upimaji wa vyanzo vya mionzi katika sampuli angalao 5,000 za vyakula vinavyoagizwa kutoka nje;

(vi) Kuimarisha upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 26 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyingine;

(vii) Kuendelea na ukaguzi wa migodi 19 mikubwa inayofanya kazi ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo;

(viii) Kuratibu miradi ya Kitaifa na Kikanda (*AFRA*) inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani *(International Atomic Energy Agency-IAEA)* na kusimamia mchakato wa kuandaa miradi mipya kwa kipindi cha mwaka 2013/2014;

(ix) Kuendelea kutoa mapendekezo ya tafiti mbalimbali kwa wadau kwa ajili ya kutafuta ufadhili;

(x) Kuendelea kuimarisha uendeshaji wa shughuli na majukumu ya *TAEC*, kwa kuendelea na juhudi za kuanzisha ofisi ya kanda katika mkoa wa Ruvuma (Namtumbo) ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume;

(xi) Kuandaa kanuni, taratibu na viwango ili kuhakikisha usimamizi wa mionzi isiyoayonisha katika nyanja na sekta mbalimbali humu nchini;

(xii) Kufanya ukaguzi kwenye vituo 100 vinavyotoa mionzi isiyoayonisha *(non ionizing radiation)* kwenye minara ya simu, redio, runinga, na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika; na

(xiii) Kuanza mradi wa ujenzi wa maabara za kisasa ili kukidhi majukumu na mahitaji ya sasa na baadae. Pamoja na ujenzi huu, mkakati wa kupeleka huduma karibu na wananchi utaanza kwa kuweka maabara ndogo ndogo katika vituo vya Dar es Salaam na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta Tanzania (*TPC*). Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Shirika la Posta Tanzania litatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuendeleza, kuongeza na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika huduma zitolewazo na Shirika ikiwa ni pamoja na kuunganisha ofisi za Posta za Mikoa na Wilaya katika Mtandao wa Kielekitroniki wa Posta kutoka ofisi 85 za sasa hadi 120;

(ii) Kuendesha mafunzo katika maeneo ya uendeshaji pamoja na TEHAMA kama ifuatavyo:-

(a) Huduma ya uendeshaji - Kozi 40;

(b) Huduma kwa wateja na masoko - Kozi 80;

(c) Usimamizi na utawala bora - Kozi 50;

(d) Mafunzo katika nyanja ya TEHAMA - Kozi 75;

(iii) Kuanzisha miradi ya ujenzi mpya wa Posta za Kibondo, Sumbawanga, Babati, Mombo na kujenga Uzio katika posta ya Mahonda na kuendeleza upanuzi wa Posta House (Makao Makuu) Dar es Salaam, Posta Kuu ya Dar es Salaam, Jengo la Posta ya Zamani (*Sokoine Drive),* Posta ya Singida na Ofisi ya *EMS* Posta Kuu Moshi; na

(iv) Kusimamia shughuli zote za ununuzi na ugavi za idara na mikoa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005. Aidha, Shirika litafanya ununuzi wa vifaa vya uendeshaji ikiwa ni pamoja na mitambo, magari na kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Kampuni ya Simu Tanzania itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuongeza ufanisi katika biashara kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuongeza mapato kutoka Sh. bilioni 92.3 mwaka 2012 hadi Sh. bilioni 124.4 mwaka 2014 (ongezeko la 35%);

(b) Kuondokana na uendeshaji wa hasara kutoka hasara ya Sh. bilioni 11.4 mwaka 2012 hadi faida ya Sh.12.7 bilioni mwaka 2014;

(c) Kuongeza idadi ya wateja wake wa huduma mbalimbali za simu (voice na data) kutoka 268,563 mwaka 2012 hadi 386,379 mwaka 2014 (ongezeko la 44%);

(d) Uboreshaji wa Huduma kwa Wateja kwa:-

- Kuboresha na kuimarisha Mtandao Muhimili *(Core Network*) wa simu za mezani na kiganjani;

- Kuboresha na kubadilisha njia kuu ya mawasiliano kuwa ya teknolojia ya kisasa (*Modernisation of Transport Network);*

- Kuboresha Mtandao Muhimili wa data (*Data Core Network);*

- Kuboresha uwezo wa mtandao wa kasi ya Intaneti kwa simu za mezani *(fixed existing broadband capacity);*

- Kuimarisha usambazaji wa Mkongo mijini (*Metro Fibre Coverage);*

- Kuimarisha huduma ya Mkongo kwa Wateja Wakubwa;

- Kuboresha mitambo ya mawasiliano *(Upgrade of existing equipment);*

- Kuimarisha Uendeshaji wa Biashara (*Business Continuity);* na

- Kuboresha Vitendea Kazi (*Network Tools).*

(ii) Kupanua Mtandao wa simu za kiganjani inayotumia teknolojia ya *Code Division Multiple Access (CDMA)* ili kutoa huduma ya mtandao wenye kasi kubwa *(wireless broadband services*) kwenye miji mikubwa minane (8) Tanzania bara (Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Morogoro, Moshi) na Zanzibar kwa:-

(a) Kuboresha mitambo ya *CDMA* 41 iliyopo ili kuipa uwezo wa kutoa huduma bora ya data *(broadband wireless);*

(b) Kupanua mtandao wa *CDMA* kwa kujenga vituo vipya vya mtambo (*BTS*) vipatavyo 38 ili kutoa huduma katika maeneo mapya ya kibiashara;

(c) Kuboresha mitambo mikubwa ya *CDMA (upgrade of core mobile network)* kwa kuondoa software ya zamani na kuweka *software* mpya ili kuboresha huduma kwa wateja;

(iii) Kuongeza masafa (700 MHz au 2.6 GHz) kwa ajili ya kujenga mtandao wa *Long Term Evolution (LTE);*

(iv) Kuendelea kuboresha makusanyo yanayotokana na huduma za simu zinazotolewa kwa wateja

wake, ikiwemo Serikali Kuu na taasisi zake, lengo likiwa kukusanya angalau asilimia 96 ya mauzo ya kila mwezi husika;

(v) Kuendelea kushiriki kusimamia ujenzi wa Awamu ya Tatu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, pamoja na kuendelea, kuendesha na kuendeleza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; na

(vi) Kuendelea na mikakati ya kuwaunganisha watumiaji zaidi kwa kuongeza njia za kuwafikia wateja walipo *(Metro rings)* katika miji yote Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa uhamaji katika mfumo mpya wa utangazaji wa dijitali *(Digital Broadcasting)* kwa kuendelea kutoa elimu kwa umma na watoa huduma za mawasiliano kulingana na kanuni na sheria husika;

(ii) Kuboresha mifumo itokanayo na utangazaji katika mfumo wa teknolojia ya dijitali kama ifuatavyo:-

(a) Kuweka viwango vya gharama za kurusha vipindi (*transmission fees)* wanavyotozwa watengeneza vipindi (*content services providers)* na wasimika miundombinu ya utangazaji (*multiplex operators);*

(b) Kusimamia mchakato wa utekelezaji wa muingiliano wa visimbuzi *(interoperability of set-top-boxes);*

(c) Kusimamia ubora wa visimbuzi na kuweka mpango wa kusitisha uagizaji wa runinga za analojia;

(d) Kuwezesha uboreshaji wa mifumo ya utengenezaji wa maudhui ili kukidhi ongezeko la wigo wa masafa unaotokana na kuhamia kwenye teknolojia ya utangazaji wa dijitali;

(e) Kuweka mifumo na kanuni za utoaji wa huduma mbadala za dijitali kama vile matangazo ya runinga kwenye simu, huduma za kibenki, afya na nyinginezo.

(iii) Kuendelea kuratibu watoa huduma za mawasiliano ili washiriki katika ujenzi wa mitambo ya intaneti *(internet exchange points–IXPs)* na kuunganisha mitandao yao kwenye mitambo hiyo. Pia, itanunua mtambo na kuunganisha mkoa wa Mbeya na Zanzibar;

(iv) Kuendelea kushirikiana na Umoja wa Wadhibiti na Watoa Huduma za Mawasiliano wa Afrika Mashariki kufanikisha uunganishwaji wa *Internet Exchange Points* za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania kama ilivyoazimiwa na Umoja huo;

(v) Kuendelea kupokea na kutathmini maombi ya leseni za huduma za mawasiliano;

(vi) Kuendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa huduma za mawasiliano kwa kufanyia ukaguzi kampuni zilizosajiliwa ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vilivyowekwa kwenye leseni zao;

(vii) Kuendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu taratibu za kuwasilisha malalamiko yao kwa mamlaka pale ambapo hawakuridhika na huduma walizopewa na mtoa huduma;

(viii) Kuendelea kushirikiana na wadau wengine katika utekelezaji na utoaji wa elimu kwa wadau wa mradi wa kitaifa wa Mfumo Mpya wa Anuani za Makazi na Misimbo za Posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*) utatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutathmini mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara;

(ii) Kuendelea na awamu zinazofuata kupeleka mawasiliano katika kata zilizobaki katika awamu za utekelezaji za mwaka wa fedha 2012/13 na kuongeza kata nyingine kutokana na mahitaji ya mawasiliano katika soko;

(iii) Kuanzisha vituo vya mawasiliano vya kijamii na kupeleka huduma za intaneti kwenye shule kwa ushirikiano na jamii kupitia miundombinu iliyopo;

(iv) Kutathmini mahitaji ya mawasiliano kwenye vituo vya afya vijijini na maktaba za umma ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya-mtandao na elimu-mtandao;

(v) Kuendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya Posta kuhakiki mahitaji ya huduma za posta na kuangalia mahitaji mapya kwa kuzingatia kuwepo kwa Mfumo wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta; na

(vi) Kuendeleza ushirikiano na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, katika uunganishwaji wa mtandao wa mawasiliano kwa hospitali zote za Serikali ili kuleta ushirikiano wa kitabibu kwa njia ya mtandao na kuondoa tatizo sugu la uhaba wa madaktari bingwa katika hospitali zisizo na madaktari bingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2013/2014. Malengo katika Mpango wa Muda wa Kati na Mrefu. Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inaazimia kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano. Wizara yangu katika kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu imeazimia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu zoezi la uhamaji wa mfumo wa utangazaji kutoka analojia kwenda dijitali;

(ii) Kuratibu zoezi la uwekaji na matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta *(Physical Addressing and Post Code Systems)* katika maeneo mbalimbali ya nchi;

(iii) Kuendelea kupanua mtandao na kuboresha huduma za mawasiliano ya simu na intaneti nchini na kuratibu utekelezaji wa Sera ya TEHAMA kuhusu ujenzi wa vituo vya kijamii vya mawasiliano nchini;

(iv) Kukamilisha zoezi la uhuishaji wa Sera ya TEHAMA na kuanza uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta;

(v) Kukamilisha uanzishaji wa Tume ya TEHAMA na kufuatilia utendaji wa taasisi za mawasiliano hususan *TTCL*, *UCAF*, *TPC* na *TCRA*;

(vi) Kuendelea kueneza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupanua matumizi yake katika maeneo mbalimbali nchini na katika nchi jirani;

(vii) Kuendelea kuratibu miundombinu ya TEHAMA nchini ikiwa ni pamoja na ushiriki, utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikisha huduma zake hadi Makao Makuu ya Wilaya zote nchini (Awamu ya III – V);

(viii) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa kuunganisha katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano vituo 200 zikiwemo shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya afya, vituo vya Posta pamoja na taasisi zilizoainishwa kwenye mradi wa e-*Schools* unaojulikana kama Tanzania *Beyond Tomorrow-TBT.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Kwa upande wa Sayansi Teknolojia na Ubunifu, Wizara imeazimia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuimarisha mifumo, taasisi na rasilimali watu katika nyanja za utafiti, sayansi na teknolojia nchini;

(ii) Kukamilisha Programu ya Mageuzi ya Mfumo wa Ubunifu Nchini *(National Innovation System Reform);*

(iii) Kuimarisha na kuboresha Taasisi za Utafiti, Sayansi na Teknolojia nchini;

(iv) Kubuni, kuandaa na kusimamia sera, mipango ya utekelezaji, miongozo, mikataba, itifaki, sheria na kanuni zinazolenga kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini;

(v) Kukamilisha Andiko la Programu ya Matumizi ya Nyuklia;

(vi) Kuimarisha uhusiano wenye tija na wadau mbalimbali katika sayansi, teknolojia na ubunifu ndani ya nchi, kikanda na kimataifa;

(vii) Kuhamasisha jamii kuhusu sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ujumla kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(viii) Kuratibu uendelezaji wa miundombinu na rasilimali watu katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Napenda sasa kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia na kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Ni ukweli usiopingika kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2012/2013 yametokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa kampuni za simu za kiganjani kwa utayari wao katika kushughulikia changamoto za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mawasiliano hapa nchini. Ninazishukuru kwa jinsi zinavyoshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile uchangiaji wa damu salama, ujenzi wa vituo vya afya, ununuzi wa vitabu vya ziada na kiada vinavyotumika mashuleni na vyuoni, ununuzi wa madawati na ujenzi wa madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha, ninaishukuru Tanzania *Private Sector Foundation* kwa kukipatia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya vifaa vya kufundishia fani za Teknolojia ya Maabara, Sayansi na Teknolojia ya Vyakula, Mekatroniki, Uhandisi Madini, Uhandisi Usalama na baadhi ya vifaa vya Uhandisi Mawasiliano. Vile vile, naishukuru sana sekta binafsi kwa mchango wake katika kuendeleza sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia na hivyo kuongeza mchango wa sekta hii katika maendeleo ya nchi yetu. Ninatoa wito kwa kampuni na taasisi nyingine za ndani kuona umuhimu wa kuchangia maendeleo ya jamii kupitia sekta ya mawasiliano sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilinufaika na itaendelea kupokea misaada, mikopo na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo kwa kipindi chamwaka wa fedha 2013/2014. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukrani kwa Serikali za Marekani, Sweden, Norway, Finland, Uholanzi, Japan, Italia, Afrika Kusini, Jamhuri ya Korea, Jamhuri ya Watu wa China na India. Vilevile, natoa shukrani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Exim ya Jamhuri ya Watu wa China, pamoja na taasisi na mashirika wahisani ya Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, *KOICA*, *UNESCO*, *UNCTAD*, *UPU* na *ITU, Tanzania Private Foundation*. Pia sitapenda kuyasahau makampuni ya mawasiliano hasa makampuni ya simu ya hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia katika mwaka wa fedha 2013/2014 yamekadiriwa kuwa Sh. 63,147,599,460. Kiasi hicho cha fedha kimepangwa kutumika kama mchanganuo unavyooneshwa hapa chini:-

(1) Matumizi ya Kawaida Sh.27,218,364,000
(2) Matumizi ya Maendeleo Sh.35,929,235,460/=

**Jumla Sh.63,147,599,460/=**

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kutekeleza mipango yake iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2013/14, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 63,147,599,460 kwa mchanganuo ulioelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi, Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu, pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunisikiliza wakati wa kuwasilisha hotuba yangu. Hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara, ambayo ni www.mst.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunashukuru sana Mheshimiwa Profesa kwa hotuba yako nzuri.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea, niwatangazie tangazo moja muhimu, nalo ni kwamba ndugu zetu wa *NSSF* wametuletea watalam wa Hospitali ya macho ya Mvumi na Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, kwa pamoja wako hapa kwa ajili ya zoezi la upimaji wa macho, *blood pressure*, sukari na utoaji wa miwani kati ya leo na kesho tu. Kwa hiyo, huduma zote ziko hapo na zinatolewa bure, mnaombwa kwa wakati wenu muweze kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kuweka afya zenu sawasawa.

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, kwa niaba yake Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, karibu sana.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa Mujibu wa kifungu namba 99(9) cha Kanuni za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hii mbele ya Kamati kuhusu utekelezaji  na ushauri wa Kamati kwa kazi zilizopangwa kufanyika  katika mwaka wa Fedha wa 2012/ 2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2012/2013. Kamati ilitoa ushauri kuhusu utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Kamati inasikitika kutoa taarifa kwamba Wizara haikuweza kutekeleza ushauri huo kikamilifu kutokana na ufinyu wa Bajeti na ucheleweshwaji wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2012/2013 katika ukusanyaji mapato; katika mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Sh. 8,011,000/= kama Mapato ya Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013, Wizara ilikusanya jumla ya Sh. 21,083, 900/=, ikiwa ni ongezeko la asilimia 263.2 ya makisio yote. Sehemu kubwa ya fedha hizo zilitokana na mauzo ya nyaraka za zabuni mbalimbali na mishahara isiyolipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo; katika

mwaka wa fedha wa 2012/2013 ziliidhinishwa jumla ya Sh. 71,607,712,000/=. Kati ya hizo Sh. 23,269,110,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 7,006,176,914/= kwa ajili ya matumizi mengine. Aidha, fedha za maendeleo za ndani zilikuwa Sh. 38,706,547,000/= na fedha kutoka nchi wahisani zilikuwa Sh. 2,625,878,000/=. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2013 jumla ya Sh. 32,807,075,724.67 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo zilikuwa zimetolewa ambayo ni sawa na asilimia 45.81 ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii. Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo umeshindwa kukamilika kutokana na kutokutolewa fedha za miradi hiyo kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwelekeo na mpango wa bajeti kwa mwaka 2013/2014, kwa makadirio ya matumizi; katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inakadiriwa kuwa na matumizi ya jumla ya Sh. 63,147,599,460/= ambapo Sh. 27,218,364,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 35,929,235,460/= ni kwa ajili ya maendeleo kati ya hizo Sh. 30,295,482,000/= ni fedha za ndani na Sh. 5,633,753,460/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa bajeti kwa Wizara hii hauridhishi kwani ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2012/2013 na mwaka 2013/2014 inaonekana kuwa bajeti hii imeshuka kwa takribani Sh. 8,460,112,540/= sawa na asilimia 11.8. Vilevile, katika mwaka 2013/2014 Bajeti kwa ajili ya utafiti imeshuka kwa kiasi kikubwa kwani ikilinganishwa na mwaka 2012/2013 bajeti iliyotengwa ilikuwa Shilingi bilioni 21.4, mwaka huu 2013/2014 bajeti ya utafiti ni Shilingi bilioni 14.0. Kamati inajiuliza, kama kweli Serikali ina nia thabiti ya kutenga asilimia moja ya pato ghafi la Taifa kwa ajili ya utafiti kama ilivyokubaliwa katika Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni na ushauri wa Kamati, kuhusu Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Tekinolojia, Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuwa

japokuwa bajeti iliyotengwa ni ndogo, lakini ikitolewa kwa wakati itasaidia kuanza kutekelezwa kwa malengo mbalimbali ya Wizara.

Katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo imeshindwa kukamilika kutokana na kutotolewa kwa fedha za maendeleo kwa wakati na kama ilivyotarajiwa. Hadi kufika mwezi Machi, 2013 kati ya Sh. 38,706,540,000/= zilizoidhinishwa ni Sh. 13,150,390,631/= tu zilizotolewa sawa na asilimia 39.9 ya fedha zilizokasimiwa kwa ajili ya miradi. Vilevile Fedha za Utafiti kati ya Sh. 21,479,961,000/= zilizoidhinishwa, ni Sh. 6,979,961,000/= tu zilizotolewa sawa na asilimia 32.4 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza ushauri wake kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zitolewe kwa wakati ili kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iwe kubwa na maendeleo kuonekana kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* kwa juhudi mbalimbali inazozifanya katika kuhakikisha mawasiliano yanaboreshwa zaidi kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali ya teknolojia. Katika jitihada za kuwafikia wananchi kwa urahisi mamlaka imefungua Ofisi sita za kanda ambazo zipo Zanzibar, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam.

Aidha, kwa sasa Ofisi za Kanda za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania zina mitambo *(mobile frequency monitoring station)* sita ya kisasa, pamoja na minne iliyonunuliwa mwaka 2006 ambayo imesaidia kupunguza muda wa kumpangia mwombaji masafa, kutambua kwa urahisi watumiaji haramu wa masafa na kuelewa mahali walipo, na kuzuia mwingiliano *(harmful interference)* baina ya watumiaji wa masafa, hivyo kuongeza ubora wa mawasiliano nchini. Vilevile Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanikiwa katika kuboresha maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mfumo wa Utoaji Leseni *(Licensing Framework),* Mamlaka ya Mawasiliano ina mfumo wa utoaji leseni unaozingatia mwingiliano wa teknolojia unaojulikana kama *"Converged Licensing Framework (CLF)".* Mfumo huu wa leseni umekuwa chachu ya maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano kwani umeleta maendeleo katika mitandao ya simu za mkononi.

Vilevile kwa mara ya kwanza mitandao ya mkongo baharini (*Submarine cables*) ikifika Pwani, kwa mfano *Seacom* ambao ulizinduliwa mwaka 2009, na "*EASSy cable"* ambao ilizinduliwa mwaka 2010.

Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mawasiliano, kwani hivi sasa imerahisisha huduma mbalimbali kwa wananchi ikiwemo huduma ya matumizi ya internet, kutuma pesa kwa simu (M-Pesa ya *Vodacom, Airtel Money* ya *Airtel*, *Tigo-Pesa* ya *Tigo, Z-Pesa* ya *Zantel*, Mobipawa ya E-fulusi) pamoja na huduma za kulipia bili za maji, umeme, *DSTV, Star-Times*, huduma za benki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama za mwingiliano kati ya Makampuni ya simu nchini *(Interconnection Rates);* Kamati inaipongeza Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kupunguza bei unganishi ya mawasiliano kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine ambapo sasa bei mpya ni Shilingi 34.92 kwa dakika ambayo imeanza kutumika tangu mwezi Machi, 2013.

Jedwali lifuatalo linaonyesha mtiririko wa gharama za mwingiliano kati ya Makampuni yaSimu kuanzia mwaka 2004 hadi 2013.

| **Mwaka** | **Gharama** |
|---|---|
| 2004 | 10 cent USD |
| 2008 | 7.83 cent USD |
| 2012 | Shilingi 115 |
| 2013 | Shilingi 34.92 |

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huu ni wa kizalendo na unaozingatia mazingira halisi ya soko na uchumi wa Watanzania wengi kwani kwa sasa ambapo ndani ya nchi yetu kuna mitandao ya simu takribani saba, hivyo ni bugudha kwa mwananchi kubeba simu zaidi ya moja na wakati mwingine kumlazimu kubadilisha laini *(sim card)* ili kukwepa gharama za kupiga simu kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine. Kamati inashauri, pamoja na kushuka kwa gharama za mtandao, ni vyema ubora wa mitandao ukazingatiwa kwani usikivu hafifu unakera watumiaji wengi wa simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kusajili laini za simu lilianza kusimamiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuanzia tarehe 1Julai, 2009 kwa lengo la kuwalinda wateja, kuhakikisha huduma za ziada katika huduma za simu za mkononi zinakuwa salama, kwa mfano huduma za kibenki kwa kutumia simu na huduma za kulipia Ankara za huduma mbalimbali na kurahisisha Makampuni ya Simu kuwafahamu wateja wake. Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 80% ya laini za simu zimesajiliwa. Changamoto kubwa katika usajili, ni watu ambao wanatoa taarifa za uongo wakati wa usajili. Kwa mujibu wa sheria, ni kosa la jinai kuwa na laini ambayo haijasajiliwa. Kamati inashauri zoezi la usajili wa laini za simu litiliwe mkazo na kuhakikisha kila anayemiliki simu awe na laini iliyosajiliwa kwani hili likitekelezwa litasaidia kupunguza uhalifu wa kwenye mitandao ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nielezee kuhusu Shirika la Posta na Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta *(Postal Code).* Anuani za makazi na simbo za Posta ni muhimu katika maendeleo ya nchi kiuchumi, kibiashara, kisiasa na utoaji huduma mbalimbali za jamii. Faida za kuwa na anuani hizo zinamgusa kila mtu kuanzia Serikali na Taasisi zake, Makampuni, wafanyabiashara, watoa huduma mbalimbali za jamii (umeme, maji, gesi, huduma za kifedha kama benki, wasambazaji wa barua na vifurushi, ulinzi na usalama wa raia, watoa huduma za dharura kama vile zimamoto, magari ya wagonjwa na jamii kwa ujumla). Pia kutoa vitambulisho vya Kitaifa kwa Watanzania ambapo utaongeza ufanisi katika

usimamizi wa makazi ya watu, kutambua mali na kaya katika eneo husika na kuongeza tija katika huduma za uokoaji na maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, pamoja na faida lukuki zinazotegemewa kupatikana mfumo huu utakapokamilika, kasi ya utekelezaji imekuwa siyo ya kuridhisha kutokana na kutengwa kwa bajeti ndogo ambayo pia haitolewi kwa wakati. Kwa mfano, mwaka wa fedha wa 2012/2013 ilitengewa Sh. 709,518,000/= ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Fedha zilizokuwa zimetolewa ni Sh. 13,750,000/= sawa na asilimia 1.93 ya bajeti iliyotengwa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mapema mradi huu muhimu kwani utarahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa urahisi.

Aidha, Kamati inashauri, kwa kuwa mfumo huu ni mtambuka, Wizara zishirikiane kwa karibu kwa vile mradi huu ukikamilika utasaidia kufanikisha utoaji wa huduma mbalimbali za kibiashara, kijamii pamoja na utekelezaji wa mradi wa vitambulisho vya uraia. Vilevile, Kamati inaendelea kuishauri Serikali iendelee kuimarisha Shirika la Posta nchini, na kulipatia mtaji utakaowezesha kuweka mitandao ya kompyuta *(internet)* katika utoaji wa huduma zake ili kuhimili ushindani unaotokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa mabadiliko ya mfumo wa utangazaji kutoka analojia kwenda digitali ulianza mwaka 2001.

Chimbuko hasa la mabadiliko haya ni makubaliano ya nchi wanachama wa Umoja wa Mawasiliano Duniani *(ITU)* kusitisha mfumo wa utangazaji wa teknolojia ya analojia ifikapo tarehe 17 Juni, 2015 na kuanza kutumia rasmi mfumo wa digitali. Hii ni kutokana na umuhimu wa matumizi bora ya masafa *(radio frequency)* ya utangazaji, ubora wa picha na sauti, matumizi bora ya nishati *na* umeme, huduma za ziada kama *internet* na matumizi ya runinga za mkononi na kwenye magari.

Katika kutimiza azma hiyo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kusitisha mfumo wa urushaji matangazo kwa njia ya analojia tarehe 31 Desemba, 2012 ili kutoa muda wa kutosha kwa nchi wanachama kufanya tathmini ya kiufundi na kurekebisha kasoro zitakazojitokeza, kufupisha kipindi cha mpito *(simulcast)* ambacho kina gharama kubwa za uendeshaji na kutoruhusu nchi zetu kuwa soko la vifaa vya analojia vilivyopitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanza awamu ya kwanza ya mfumo wa urushaji matangazo kwa njia ya *digital*, changamoto mbalimbali zilijitokeza zikiwemo bei za ving'amuzi kuwa ghali, chaneli tano za kitaifa kutoonekana zote, picha kukwamakwama, rangi kubadilika na hata biashara ya matangazo katika televisheni kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo**,** Kamati iliitisha kikao na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na wadau wengine wa mawasiliano ili kuona namna bora ya utekelezaji wa mabadiliko haya. Kamati inashauri yafuatayo:-

Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano iunde kikosi kazi ambacho kitafanya utafiti ili kujua mafanikio na athari mbalimbali zilizoipata jamii kufuatia utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mfumo wa kurushia matangazo wa *digital*. Kikosi kazi hicho kiwahusishe wadau wote muhimu wa mawasiliano. Mamlaka ya Mawasiliano imalizie maeneo yaliokuwa yamelengwa katika awamu ya kwanza, na kusimamisha zoezi la kuzima matangazo ya analojia, ili kuweza kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika awamu ya kwanza ya matumizi ya mfumo huu zikiwemo ubora wa ving'amuzi, picha kukwamakwama, rangi kubadilika, bei za vingamuzi na kadhalika.

Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano itoe matangazo na elimu ya kutosha ili kupunguza malalamiko na hofu kubwa iliyopo kwa wananchi kuhusu mfumo huu mpya, kwani wananchi wengi wamekuwa hawafahamu kuwa kuna

chaneli tano za Kitaifa ambazo zinapaswa zionekane bure ambazo ni Tanzania *Broadcasting Coorporation - TBC, Independent Television-ITV, CHANELI 10, STAR TV* na *East Africa Television - EATV*. Hata hivyo, ipo haja ya kusimamia wasambazaji wa ving'amuzi, kwani kwa kiasi kikubwa chaneli zote tano ambazo zinapaswa zionekane bure huwa hazionekani zote.

Vilevile, kuhakikisha televisheni za kitaifa zinaonekana kote na changamoto zote zinadhibitiwa. Kamati inashauri mamlaka kushirikiana na wadau wote kwa kutoa namba maalum ambayo wateja wanaweza kupiga bure kwa ajili ya kupata na kutoa taarifa mbalimbali kuhusu ubora, matumizi sahihi ya ving'amuzi na kuondoa malalamiko mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa kuratibu huduma za mawasiliano nchini *(Telecommunications Traffic Monitoring System (TTMS)* unalenga kuhakikisha mapato yatokanayo na huduma za Sekta za mawasiliano yanajulikana vyema na yanachangia kikamilifu katika pato la Taifa. Kamati imefahamishwa kwamba tayari Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imekamilisha mchakato wa kupata mwendeshaji mshiriki baada ya mchakato wa zabuni kukamilika ambapo Mkataba umesainiwa tarehe 22 Machi, 2013.

Ujenzi wa mtambo umeanza na utakamilika mwisho wa mwezi Julai, 2013. Mtambo huu utakuwa na uwezo wa kufuatilia mapato ya Makampuni ya Simu *(Revenue Assurance),* kufuatilia jinsi *traffic* za simu za Kimataifa na Kitaifa na kufuatilia njia halali za simu pamoja na kufuta mianya ya njia zisizo halali. Kamati inashauri kasi ya utekelezaji wa uendeshaji wa mfumo wa kuratibu huduma za mawasiliano nchini iongezwe kwa kuwa kwa kukamilika kwa mfumo huu Serikali itaweza kujua mapato halisi yanayotokana na huduma za Sekta ya Mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano –*TEHAMA*. Ni dhahiri kuwa sasa Serikali inajiandaa kuingia kwenye Serikali mtandao *(e-Government).*

Hii ina maana kuwa shughuli zote, maamuzi na maelekezo katika ngazi mbalimbali za uongozi serikalini yatatolewa kupitia mtandao. Aidha, katika jamii ya sasa matumizi ya mtandao katika shughuli mbalimbali za kijamii na uchumi yamepanuka ikiwemo kufanya biashara, kupata elimu, kulipia Ankara mbalimbali na mengineyo kufanyika kwa njia ya mtandao. Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mtandao, wananchi wasio waaminifu nao wamekuwa wakiutumia katika masuala yasiyo na tija ikiwemo kutapeli mali na fedha. Vilevile maadili ya watoto na vijana yamekuwa yakiporomoka siku hadi siku mtandao ukiwa ni miongoni mwa sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta *(The Electronic and Postal Communications Act, 2010 - EPOCA)* inataka kuanzishwa kwa kitengo cha Taifa cha *Computer Emergence Response Team - CERT* chenye jukumu la kufuatilia na kudhibiti uhalifu wa kimtandao nchini. Kamati inashauri kitengo hiki kiimarishwe kwa kupatiwa rasilimali watu wa kutosha ili kudhibiti uhalifu mwingi unaofanywa kwa kutumia mtandao *(cyber crime).*

Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kuleta Sheria ya Usalama katika Mitandao *(Cyber Security Law)*. Aidha, elimu kwa wananchi iendelee kutolewa ili waweze kujua namna nzuri ya kutumia mtandao ili kuepuka kutapeliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yaliyoainishwa na Serikali kuwa ni ya kimkakati ambayo pia ni kipaumbele kwa mwaka 2013/2014 ni ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Kamati inatoa pongezi kwa kukamilika kwa awamu ya kwanza na ya pili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa ambapo kwa sasa una kilomita 7,560 ambayo inajumuisha Makao Makuu ya Mikoa 24 ya Tanzania Bara. Vilevile kwa upande wa Unguja na Pemba Mkongo umeunganisha Pemba kupitia waya wa umeme unaowekwa kati ya Dar es Salaam na Unguja ambapo unatarajia kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ujenzi wa Mkongo wa Taifa uliidhinishiwa Shilingi bilioni 2.0 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Wizara ilipokutana na Kamati ni Shilingi milioni 677.62 tu zilizokuwa zimeshatolewa sawa na asilimia 33.8 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mkongo wa Taifa. Kamati hairidhishwi na utoaji wa fedha hasa katika miradi ambayo ni ya kipaumbele cha Taifa.

Kamati inajiuliza, ikiwa sasa umebaki mwezi mmoja tu ili kumalizika kwa mwaka wa fedha 2012/2013: Je, Serikali bado ina nia ya dhati ya kuendelea kuuweka ujenzi wa Mkongo wa Taifa kuwa katika vipaumbele vyake ilihali bajeti bado haitolewi kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu?

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(Universal Communication Access Fund(UCAF)* ilikuwa ni kwa ajili ya kuzifikia sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijijini na kuhakikisha zinakuwa na mawasiliano. Changamoto kubwa ya utekelezaji wa Mfuko wa huu ni kukosekana kwa utayari kwa watoa huduma katika kupeleka mawasiliano sehemu zilizoainishwa ambapo ni takribani mwaka wa nane sasa tangu Sheria ya Mfuko huu itungwe.

Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umeainisha jumla ya Kata 152 zenye jumla ya Vijiji 869 na wakazi 1,617,310 zenye uhitaji mkubwa wa mawasiliano ambapo kwa kuanzia Vijiji 316 katika Kata 52 vimeshakabidhiwa kwa watoa huduma za mawasiliano. Hata hivyo, Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji ya Mfuko huu. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kushirikisha na kushawishi Makampuni ya Simu ili yapeleke mawasiliano katika maeneo yaliyoidhishwa. Aidha, Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu hatua zilizofikiwa na mikakati madhubuti iliyowekwa ili kuhakikisha Mfuko huu unaimarika kwani kwa sasa kasi ya utekelezaji wake bado hairidhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yetu yote itokee kwenye *Hansard* kama ilivyo kwa kuwa ni ndefu na muda ni mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL).* Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuwa Serikali iwekeze mtaji na kusimamia ipasavyo *TTCL* badala ya kuendelea na mawazo ya kuibinafsisha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiwezesha *TTCL* kwa kuiteua kuwa Meneja wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo imeweza kutoa huduma kwa kampuni mbalimbali ndani na nje ya nchi zikiwemo Rwanda, Zambia na Malawi. Vilevile kampuni ya *TTCL* imeshinda zabuni ya kutoa huduma ya Intaneti za Kimataifa kupitia mikongo ya baharini ya *SEACOM* na *EASSy cable*. Miradi hii kwa kiasi kikubwa itasaidia *TTCL* kupata fedha ambazo zitaweza kutekeleza miradi muhimu ya kampuni.

Aidha, Kamati ilipewa taarifa kuwa katika juhudi za kuliwezesha Shirika, kwa mwaka 2013/2014 Wizara ya Fedha kupitia Msajili wa Hazina imeagizwa kutenga fedha kwa ajili ya kununua hisa ili kumiliki *TTCL* kwa asilimia 100. Kamati inaendelea kushauri Serikali iwekeze mtaji *TTCL* na kuisimamia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtiririko wa bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida kwa Wizara pamoja na Taasisi zake tano zinazopata ruzuku ya Serikali ambazo ni Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam *(DIT),* Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, Tume ya Sayansi na Teknolojia na Tume ya Nguvu za Atomiki katika kipindi cha miaka mitano iliyopita imekuwa na sura inayoonekana katika jedwali lifuatalo:-

| **Mwaka** | **2008/2009** | **2009/2010** | **2010/2011** | **2011/2012** | **2012/2013** |
|---|---|---|---|---|---|
| Bajeti ya Matumizi Mengine | 3,755,329,000 | 13,755,329,900 | 11,300,308,000 | 9,290,101,000 | 7,006,176,914 |

Kama ambavyo jedwali limeonesha hapo juu, bajeti ya Wizara katika Taasisi hizi imekuwa ikiendelea kushuka mwaka hadi mwaka japokuwa majukumu ya Wizara na Taasisi hizi yamekuwa yakiongezeka. Kiasi kilichoidhinishwa na Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa mwaka

2012/2013 yaani Sh. 7,006,176,000/= ilikuwa chini ya bajeti ya Wizara hii iliyoidhinishwa miaka minne iliyopita (2008 - 2012), kama ambavyo jedwali hapo juu linavyoonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi hizi zimekuwa zikiongeza wanafunzi kulingana na matakwa ya Kitaifa katika fani mbalimbali huku bajeti za Taasisi husika zikiendelea kushuka. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya *(MUST),* pamoja na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, ni Taasisi ambazo huongeza wanafunzi kila mwaka. Mathalan, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya *(MUST)* idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 957 mwaka, 2008/2009 hadi 3,156 mwaka 20012/2013, wakati katika kipindi kilichotajwa bajeti imepungua kutoka Sh. 2,951,953,923/= mwaka 2008/2009 hadi Sh. 1,197,512,250/= mwaka 20012/2013. Kupungua kwa bajeti ni moja ya sababu ya kuongezeka kwa madeni ya chakula na vifaa vya kufundishia kwa Taasisi za Teknolojia Dar es Salaam *(DIT)* na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya *(MUST).*

Aidha, Taasisi ya Ngozi ya Mwanza imehamishiwa chini wa Wizara hii mwezi Januari, mwaka 2012. Tafsiri ya hali hii ni kuwa Wizara imekuwa ikikabiliwa na hali ngumu ya uendeshaji ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya madeni. Kamati inashauri uwekwe mkakati maalum wa kuboresha huduma za Vyuo na Taasisi hizi ikiwa ni pamoja na kulipa madeni yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha ni kuwa Taasisi bora ya elimu ya juu duniani inayolenga kukuza na kuhamasisha ubora katika sayansi na uhandisi na matumizi yake katika kukuza uchumi na maendeleo endelevu Afrika.

Maendeleo ya kiuchumi duniani yanapatikana kwa kutumia sayansi na teknolojia inayoibuliwa baada ya kufanya tafiti mbalimbali. Taasisi ya Nelson Mandela imeanzishwa kwa ajili kutoa mafunzo ya aina hiyo siyo kwa Tanzania tu, bali kwa Afrika kwa ujumla. Hata hivyo, inaelekea kuwa dira ya Taasisi hii haiwezi kufikiwa kutokana na bajeti ndogo

inayotengwa. Kwa mfano, mwaka wa fedha wa 2012/2013 Taasisi ilipangiwa jumla ya Sh. 2,800,000,000/= kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 4 Aprili, 2013 fedha iliyokuwa imetolewa ni Sh. 50,000,000/= tu ambayo ni asilimia1.8 ya bajeti ya maendeleo. Aidha, mwaka 2013/ 2014 bajeti ya maendeleo iliyopangwa kwa ajili ya Taasisi hii Sh. 2,500,000,000/= ambayo ni pungufu kwa asilimia 10.7 ya bajeti ya maendeleo ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inajiuliza: Je, Serikali bado ina nia ya kuifanya Taasisi hii kutimiza dira yake ya kuwa miongoni mwa Taasisi bora ya elimu ya juu duniani? Kama ndivyo, Kamati inaishauri Serikali iazimie kwa makusudi kuiboreshea kasma ya maendeleo ya Taasisi hiii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo ya mwaka 2010 inatoa mwongozo wa namna ya kuhamasisha na kulinda masuala mbalimbali yanayohusu Wagunduzi. Katika kuhamasisha na kuwapa moyo wagunduzi, Kamati inasisitiza ushauri wake kuwa Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuhamasisha ugunduzi hasa kwa wanafunzi na vijana kwa kuhakikisha bidhaa zinazogunduliwa *(prototypes)* zinatengenezwa kwa wingi na wananchi, wanashawishiwa kuzitumia ili kukuza ajira kwa Watanzania wengi na pia kuhamasisha watu wengi zaidi. Hili litatimia ikiwa Serikali itahakikisha kunakuwepo waalimu wa kutosha wanaofundisha masomo ya sayansi, maabara za kutosha katika shule na vivutio vingine vingi vitakavyoshawishi wazazi kuwahamasisha wanafunzi kupenda kusoma masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* kwa kutambua vipaji vya wagunduzi na kuwapa moyo kwa kutoa tuzo mbalimbali ikiwemo Tuzo ya Taifa ya Sayansi na Tekinolojia *(TASTA Award)* ambayo hutolewa kila mwaka baada ya kuthibitishwa na jopo la wataalam. Hata hivyo, kuwapa tuzo tu haitoshi, Serikali inatakiwa kuwaongezea ujuzi kwa kuwawezesha kupata elimu zaidi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imeomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 63,147,599,460/= ambapo Sh. 27,218,364,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 35,929,235,460/= ni kwa ajili ya maendeleo. Kati ya Fedha za miradi ya maendeleo Sh. 30,295,482,000/= ni fedha za ndani na Sh. 5,633,753,460/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kifungu kwa kifungu na sasa inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha maombi hayo yenye jumla ya Sh. 63,147,599,460/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa kuhitimisha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Aidha, nawashukuru pia Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa - Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa January Yusufu Makamba - Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Dkt. Florens M. Turuka - Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano wao ambao umeiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa. Ushirikiano wao na kujituma bila kuchoka wakati wa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha taarifa hii ambayo kwa niaba yao naiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kwa heshima kubwa, niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba – Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya – Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe ni Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Said Ramadhani Bwanamdogo, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana W. Kikwembe, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, MheshimiwaAbdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Suleman Masoud Nchambi, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Horoub Mohamed Shamis na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, katibu wa Kamati Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Ndugu Hosiana John kwa kuihudumia Kamati na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii.

Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtutura kwa kusoma maoni ya Kamati. Sasa moja kwa moja naomba nimwite Msemaji wa Kambi Upinzani kuhusu Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia – Mheshimiwa Susan Lyimo. Karibu sana.

**MHE. SUSAN J. A. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 99, kanuni ndogo ya 9 ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la 2013, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha, katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ina wajibu wa kusimamia utafiti, utungaji na utekelezaji wa Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA). Wizara hii pia ina jukumu la kusimamia mawasiliano ya posta, na ya njia ya simu. Vilevile ina jukumu la kupata na kutumia teknolojia, kuendeleza wataalamu wa ndani katika fani za sayansi na teknolojia; kufanya utafiti wa mawasiliano, sayansi na teknolojia, kusaidia uvumbuzi, na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, *dira ya Wizara hii ni kuwa na jamii ya Watanzania wenye maarifa na uwezo wa kisayansi, kiteknolojia na wa ki-uvumbuzi, kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na hivyo kuweza kukabiliana na ushindani wa Kimatifa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya tamko zuri la dira ya Wizara hii, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba Serikali hii haitekelezi kwa vitendo tamko hili jambo ambalo limeifanya nchi yetu kuendelea kuwa nyuma katika medani za sayansi na teknolojia na hivyo kuendelea kuwa soko la mawazo ya kisayansi na bidhaa zinazotokana na uvumbuzi wa kisayansi na technolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa Taifa kwamba wakati elimu ya Mataifa yaliyoendelea inalenga kuwawezesha watu wao kuvumbua vitu mbalimbali vya kumpunguzia binadamu ugumu wa maisha kupitia sayansi na teknolojia, sisi elimu yetu inalenga kumfundisha Mtanzania namna ya kutumia vifaa vinavyotokana uvumbuzi kisayansi

na teknolojia ya nchi zilizoendelea. Jambo hili linamfanya Mtanzania aendelee kuwa tegemezi kifikra kwa kuwa elimu yake ni katika kutumia tu na siyo katika kugundua vitu vipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa uchungu mkubwa kwa kuwa sioni jitihada za makusudi zikichuliwa ili kubadili Taifa letu kutoka hali duni tuliyonayo sasa, na kulipeleka katika hali nzuri zaidi kwa njia ya sayansi na teknolojia. Sina hakika pia kama teknolojia ya mawasiliano tuliyonayo sasa, na iliyoenea sehemu kubwa ya nchi yetu, inatumika katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi ili kulinusuru Taifa na umasikini uliokithiri. Hii ni kwa sababu, katika hotuba ya Bajeti ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya mwaka wa fedha 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani ilibaini upungufu katika Wizara hii muhimu na kuitaka Serikali kuchukua hatua ili mawasiliano, sayansi na teknolojia viweze kutumika katika kuleta mabadiliko ya kimaendeleo hapa nchini, lakini mwitikio wa Serikali umeendelea kuwa ni ule ule wa kusuasua. Miongoni mwa masuala muhimu ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani illitaka Serikali kufanya kwa mwaka wa fedha unaomalizika ni pamoja na yafuatayo:-

(1) Kuibua vipaji vya ubunifu na uvumbuzi wa ki-teknolojia miongoni mwa wanafunzi na wananchi wenye vipaji maalumu, na kuweka mkakati wa kuviendeleza vipaji hivyo ili kuondokana na utegemezi wa teknolojia za kigeni;

(2) Tuliitaka Serikali kutoa taarifa *(progressive report)* juu ya utekelezaji wa Mtandao wa Taifa wa Elimu na Utafiti *(National Education and Research Network-NERN);*

(3) Tuliitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* kuongeza wigo wa mapato yanayotokana na Makampuni ya Simu nchini, na kuitaka Serikali ufute misamaha ya kodi kwa Makampuni ya Simu nchini;

(4) Tuliitaka *TCRA* itoe bei elekezi kwa Makampuni ya Simu, ili wananchi wasiendelee kunyonywa gharama kubwa za matumizi ya simu;

(5) Tuliitaka Serikali kuthibitisha kama ni kweli Jeshi la Polisi lilinunua mtambo *Gi2* unaotumika kufanya *"sms spoofing"* kwa madhumuni ya kufanya manunuzi hayo. Aidha, tuliitaka Serikali pia kuweka Sheria ya Kuthibiti Matumizi ya Taarifa za *"sms spoofing*" hapa nchini, kama zilivyofanya nchi ya Australia na Uingereza;

(6) Tuliitaka Serikali iandae utaratibu wa kisheria wa kupata mapato kutoka katika mifumo ya malipo ya kieletroniki kwa mfano, *Mobile Money Transfer* kama vile *M-PESA* kwa Kampuni ya Simu ya *Vodacom, Tigo Pesa* kwa Kampuni ya Simu ya *Tigo, Air Tel Money* kwa Kampuni ya Simu ya *Air Tel;* na

(7) Tuliitaka Serikali kuiongezea pesa Tume ya Sayansi na Teknolojia ili iweze kufanya kazi zake kwa ukamilifu na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujielekeza katika masuala mahususi ya mwaka mpya wa bajeti wa 2013/2014 unaotarajiwa kuanza mapema tarehe 1 Julai, 2013, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, inaitaka Serikali kutoa taarifa *(progressive report)* ya utekelezaji wa hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani (zilizoorodheshwa hapo juu), ilizoitaka Serikali itekeleze tangu mwaka uliopita wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupata habari na mawasiliano ni moja ya haki za binadamu. Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu inatoa haki ya kupata habari na mawasiliano. Kwa mujibu wa Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa *(The International Covenant on Civil and Political Rights)* 1966 "wananchi wanahaki ya kupata habari na mawasiliano".

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo mikataba ya Kimataifa peke yake inayotambua haki hii, bali pia Ibara ya 18(b)(c) na (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, inatamka wazi kwamba, "kila mtu anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila kujali mipaka ya nchi.

Mwananchi ana haki ya kuwasiliana bila kuingiliwa, na ana haki ya kupewa taarifa kuhusu matukio yanayogusa maisha yake na shughuli muhimu za maisha yake."

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haki hii kutamkwa wazi na Katiba ya nchi yetu na Mikataba ya Kimataifa, Serikali imekuwa ikiwanyima wananchi haki hii kwa makusudi kupitia hila mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kuhama Kutoka kwenye Mfumo wa Analojia kwenda kwenye Mfumo wa Dijiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Uthibiti wa Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* iliamuru vituo vyote vya Televisheni nchini kuzima mitambo ya analojia na kuvilazimisha kuingia kwenye mfumo mpya na wa kisasa wa Digitali ambao unatumia ving'amuzi kupata mawimbi ya Televisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huo uliwaathiri sana wananchi na Taifa kwa ujumla kwani kulikuwa hakuna maandalizi ya kutosha, na pia wananchi wengi hasa wa vijijini wameshindwa kununua ving'amuzi hivyo na kwa jinsi hiyo kukosa haki yao ya kikatiba ya kupata habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCRA* imechangia sana tatizo hili kwa kuwa mpaka sasa haijaweka udhibiti wa bei wala usambazaji wa ving'amuzi na hivyo kuacha hali ya ushindani usio na afya kwa watumiaji wa huduma za ving'amuzi. Ving'amuzi hivi vimekuwa vikiuzwa kwa bei ya juu ambayo inafanya Watanzania masikini kushindwa kununua na hivyo kuwakosesha haki yao ya Kikatiba ya kupata mawasiliano. Aidha, *TCRA* haidhibiti usambazaji wa ving'amuzi jambo ambalo limesababisha kutokupatikana kwa ving'amuzi katika baadhi ya maeneo, na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaotaka kununu ving'amuzi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi, baadhi ya ving'amuzi kwa muda mrefu tangu kuzimwa kwa mitambo

ya analojia vimekuwa havirushi matangazo ya vituo vya televisheni vya ndani ya nchi, na cha ajabu katika taarifa ya Wizara kwa umma, Wizara iliwataka wananchi ambao hawapati matangazo ya vituo vya *television* vya ndani ya nchi wawasiliane na wauza ving'amuzi hili wapate suluhisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msisitizo, naomba kuinukuu sehemu ya taarifa hiyo kama ifuatavyo:-

"Serikali inapenda kuwakumbusha wananchi kuwa katika maeneo ambayo tayari kuna matangazo ya televisheni katika mfumo wa dijitali, watumiaji wa televisheni wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanapata matangazo ya televisheni zote zenye leseni za Kitaifa bila gharama yoyote ile ya ziada mbali na gharama ya kununua king'amuzi (kisimbuzi) ambacho kinawezesha kuona matangazo katika mfumo mpya wa utangazaji wa dijitali. Stesheni hizo ni *TBC1, ITV, Star TV, Channel 10*, na *East African TV*. Endapo matangazo ya televisheni ya vituo hivyo hayapatikani, wananchi wawasiliane mara moja na watoa huduma za ving'amuzi ili kuwasaidia kupatia ufumbuzi."

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii ilitolewa na kutiwa saini na Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa - Waziri Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia tarehe 2 Aprili, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa sana na tangazo la Wizara kwamba wananchi ambao hawaoni matangazo ya vituo vya televisheni za ndani wawasiliane na wasambazaji wa ving'amuzi. Hii ni kwa sababu Serikali ndiyo iliyotoa leseni kwa wasambazaji wa ving'amuzi, na ndiyo inayojua masharti ya leseni hizo. Hivi Mwananchi masikini wa kijijini kwa mfano wa Kijiji cha Mwamng'ong'o, kule Kigoma au yule wa Liwale kule Lindi atapata wapi nguvu na mamlaka ya kuyaambia Makampuni ya Usambaziji kwamba king'amuzi chake hakioneshi matangazo ya kituo cha televisheni cha ndani ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali kupitia

Wizara hii kuacha mara moja kufanya mzaha na haki ya wananchi ya kupata habari. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa agizo leo hii kwa Makampuni ya usambazaji wa ving'amuzi kuhakisha kwamba vituo *vya TBC1, ITV, Star TV, Channel 10, na East African TV* ambavyo vina leseni ya Kitaifa, vinaendelea kurusha matangazo yake bure kupitia ving'amuzi kama ilivyokuwa katika makubaliano ya wasambazaji wa ving'amuzi, wamiliki wa vituo tajwa vya televisheni na *TCRA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na *TCRA* kuzitaka Kampuni za utoaji huduma za simu Tanzania kupunguza gharama za kupiga simu na kutuma ujumbe mfupi wa maneno, Makampuni hayo bado yana bei ya juu, hasa kupiga simu toka mtandao mmoja kwenda mwingine *(interconnection charges)* hali inayosababisha wananchi kumiliki simu au *line* zaidi ya moja. Mbaya zaidi Makampuni ya Simu yamekuwa yakiwatoza wateja pale wanapopiga simu kwenda huduma kwa mteja *(customer care service)* na hakuna viwango vyenye mlingano kati ya Kampuni moja na nyingine.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Mdhibiti wa Mawasiliano ya Simu *(TCRA)* kukataza mara moja Makampuni ya Simu kuwatoza wateja pale wanapopiga simu ili kupata huduma kwa wateja *(customer care services)* kwa kuwa wateja wanapofanya hivyo huwa wana jambo aidha la kiufundi au la kiutaratibu wanalotaka kusaidiwa na Kampuni husika, na hakuna faida yoyote ya kifedha mpiga simu anayopata kwa kuomba msaada wa maelezo kutoka kwa *customer care*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye suala la utangazaji redioni na kwenye luninga. Kwa mujibu wa Sheria ya Utangazaji *'the Broadcasting Services Act', TCRA* ina wajibu wa kusimamia pamoja na mambo mengine maudhui ya matangazo kama ilivyoainishwa na kanuni za udhibiti wa maudhui ya utangazaji za mwaka 2005 yaani *the Broadcasting Services (Content) Regulations 2005].*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni hizo, vituo vya redio na *television* vinakatwazwa kurusha matangazo yenye maudhui ya kibaguzi kama vile ya rangi, kabila, dini na aina zote za ubaguzi. Aidha, kanuni hizo zinakataza vyombo vya utangazaji kuibua chuki baina ya makundi tofauti katika jamii, na wakati wote kulinda umoja, uhuru na maslahi ya Taifa, na kudumisha maadili ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni hizo pia zinavitaka vyombo vya utangazaji kuwalinda watoto katika matangazo yao dhidi ya lugha za matusi, na picha zisizofaa. Adhabu inayotolewa na Kanuni ya 28 ya kanuni hizi kwa kituo kitakachokiuka kanuni hizi ni faini kiasi cha milioni tano tu.

Mheshimi Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa kanuni hizi tangu mwaka 2005, vyombo vya utangazaji, redio na luninga vimekuwa vikivunja kanuni hizo kwa kuonesha picha na kurusha matangazo yenye lugha ya matusi, zenye kuchochea chuki za kidini, na kisiasa, zinazozorotesha maadili na kutishia umoja wa Kitaifa. Kwa mfano, hivi karibuni Kituo cha Redio cha *Clouds FM* kilipigwa faini kwa kosa la kushabikia mambo ya ushoga, jambo ambalo ni kinyume na maadili ya Taifa letu. Vituo vingine viwili vya redio Imani *FM* na Kwa Neema *FM* navyo vimefungiwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji; ni lini Serikali 'sikivu' ya CCM itaanza kuona kwamba vituo vingi vya televisheni na redio nchini vinaonesha picha na kurusha matangazo yaliyojaa maudhui yaliyopotoka kimaadili ili kuchukua hatua stahiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo sasa kwenye vituo vyetu vya redio na televisheni ni ushahidi mwingine unaodhihirisha ni namna gani Serikali ya CCM ilivyoshindwa kusimamia maadili ya Taifa letu, imeshindwa kusimamia maadili ya kisiasa, na sasa inaacha watoto wetu waharibiwe kimaadili kwa kuviachia Vituo vya redio na *television* kurusha picha na matangazo ambayo yanachochea mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu malipo ya tozo za minara ya simu kwa Halmashauri. Katika taarifa ya

utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Miundombinu kwa mwaka wa fedha unaomalizika, ni kwamba Wizara ilitakiwa kuwasiliana kwa TAMISEMI kuhusu kutofautiana kwa tozo mbalimbali za minara ya simu yaani *land levy* zinazotozwa na Halmashauri hapa nchini kwa lengo la kuwianisha tozo hizo ili zifanane.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara kuandaa mwongozo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ambao utaweka viwango vya kufanana vya tozo, Wizara imekwenda mbele zaidi kuweka utaratibu wa kuwa na Taasisi moja itakayokusanya tozo kwa niaba ya Halmashauri zote kisha kuzigawa kwa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huu ni wazi kwamba Taasisi *(agency)* itakayokusanya tozo kwa niaba ya Halmashauri itahitaji gharama za uendeshaji na hivyo ni dhahiri itafanya makato toka kwa tozo zinazokusanywa na matokeo yake ni kupunguza kiasi cha mapato ambacho Halmashauri ingekusanya moja kwa moja. Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali, kurekebisha Mwongozo uliotolewa na TAMISEMI kwa kuwa na kiwango kimoja cha tozo, na kuondoa Taasisi moja ya ukusanyaji mapato kwani, kwa utaratibu wa kisheria uliopo Halmashauri inaweza kukusanya mapato yake yenyewe; na Makampuni ya Simu yanazo Ofisi Mikoani na hivyo wanaweza kulipa tozo hizo bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu michezo ya bahati nasibu kwenye mitandao ya Simu. Makampuni ya Simu yamekuwa na utaratibu wa kufanya promosheni zinazohusisha kuwakata pesa wateja wanaoshiriki promosheni hizo.

Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko toka kwa watumiaji wa simu za mkononi kwamba mara kadhaa wameingizwa kwenye promosheni hizo bila ridhaa zao na hivyo kukatwa pesa hali inayopelekea kupata hasara na usumbufu mkubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kupitia *TCRA* na Bodi ya Kusimamia Michezo ya Kubahatisha

ya Taifa kuyataka Makampuni ya Simu kuweka utaratibu mzuri wa kucheza michezo hiyo ili kuondoa usumbufu kwa wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Makampuni ya Simu yamekuwa yakitoa huduma duni sana, na hivyo kuleta usumbufu kwa wateja. Mathalan kuna wakati kampuni fulani inaweza kupoteza kabisa *network* katika Mkoa, au Mji fulani na hivyo kukwamisha kabisa mawasiliano, bila kutoa taarifa wala kuomba radhi wateja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zama hizi ambazo mawasiliano ya simu yanawezesha shughuli karibu zote za kiuchumi, kijamii na kiusalama hali ya kukatika kwa network inahatarisha usalama wa maisha ya Watanzania, ukizingatia mtandao wa simu unawezesha siyo tu mawasiliano bali pia huduma za kibenki za watumiaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya sayansi na teknolojia yametufikisha mahali simu za kiganjani zimekuwa benki na Makampuni ya Simu yamekuwa Taasisi za kifedha hapa nchini. Malipo mengi yanafanywa kupitia huduma za *M-pesa, Tigo-pesa, Airtel-Money, Z-pesa* na kadhalika.

Pamoja na mamillion ya pesa yanayotumwa kila siku kupitia njia hii, na makato ambayo Makampuni ya Simu na mawakala wao wanayapata na kujichumia faida isiyo na kifani kupitia miamala hiyo, Serikali haipati hata senti tano *(5 Cent)* kama kodi kutokana na biashara hii. Lakini wakati huo huo Serikali hii imekuwa ikitoza Taasisi nyingine za kifedha kama Benki kodi chungu mzima.

Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaishangaa Serikali hii ya CCM inayojiita makini, kwa kushindwa kuandaa utaratibu utakaoiwezesha Serikali kupata faida kutoka na miamala ya pesa kwa njia ya simu ili kuchangia ongezeko la pato la Taifa. Katika hili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza Sheria ya Tozo itakapotungwa isilenge kuwapa mzigo watumiaji/wateja wa miamala hii, badala yake Makampuni ya Simu ndiyo walipe kodi na ushuru kwa Serikali, bila kuathiri wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, izingatiwe kwamba leseni za utoaji huduma za mawasiliano ya simu hutolewa kwa Makampuni na *TCRA*, lakini leseni za utoaji huduma za pesa kwa njia ya simu hutolewa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006 *(Banking and Financial Institutions Act 2006).* Hivyo, Serikali lazima ielewe kwamba biashara hizi mbili ni biashara tofauti, watoaji leseni wake ni tofauti; hivyo Serikali lazima ipate mapato tofauti kutoka Makampuni haya, katika biashara ya mawasiliano, na biashara ya pesa kwa njia ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumeibuka wimbi kubwa la wizi kwa njia ya mtandao *(Cyber Crime)*. Mamilioni ya pesa yameibwa kwenye Taasisi mbalimbali, hasa mabenki, machine za kutolea pesa *(ATM)* na miamala mingine inayofanyika kwa njia ya kompyuta vimeendelea kuzitia hasara Taasisi za kifedha nchini. Kwa mfano, tarehe 14 mwezi Febuari, 2013 watuhumiwa wa wizi wa fedha kiasi cha Shilingi milioni 500 kupitia kwenye *ATM*, walikamatwa Mkoani Mwanza. Huu ni mfano mmoja tu, lakini kesi za wizi kwa njia ya *ATM* zimekuwa zikiripotiwa kila mara katika maeneo tofauti nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wizi, kuna uhalifu mwingine unaofanyika kwa njia ya mtando kwa mfano, ubadhirifu kwa njia ya kompyuta *(computer fraud),* kuingilia mawasiliano *(hacking)* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, waathirika wa uhalifu huu ni pamoja na Taasisi za Kiserikali, mabenki, biashara binafsi, Vyuo vya Elimu, Wanasiasa wanaofanyiwa ushushushu, na jamii kwa ujumla. Pamoja na hali hii, Tanzania haina Sheria mahususi inayodhibiti uhalifu kwa njia ya mtandao. Mabadiliko madogo yalifanywa kwenye Sheria ya Ushahidi, yaani *the Law of Evidence Act* na Sheria ya Kanuni za Adhabu, yaani *the Penal Code* hazitoshi kudhibiti aina zote za uhalifu kwa njia ya mtando. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilete Muswada wa Sheria mahususi kwa madhumuni ya kudhibiti uhalifu huu wa kimtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani tulihoji juu ya kuwepo kwa taarifa za Jeshi la Polisi kuhusika na ununuzi wa mtambo wa kijasusi wa *Gi2* unaotumika kufanya "*sms spoofing*" yaani kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwa kutumia namba ambayo kiuhalisia mwenye namba hiyo hajatuma ujumbe huo, isipokuwa ni kuingilia kihalifu mawasiliano *(cyber trespass)* ambapo mtumaji anafanya *impersonation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni lini Serikali itaweka sheria ya kudhibiti matumizi ya taarifa za "*sms spoofing*" hapa nchini ama kukubaliana na matumizi yake au kupiga marufuku kama walivyofanya nchi ya Australia na Uingereza?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu suala la kuongeza pato la Taifa kupitia Mawasiliano. Katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2012/2013 Wizara iliahidi kuanza kutumia mtambo wa kuhakiki mawasiliano *(Tarrif Monitoring System-TMS)* ili kuhakiki mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu. Wizara ilijinadi kwamba imeanza mchakoto huo mwezi Juni, 2012. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni hatua gani mchakato huo umefikia kwa sasa hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kiambatanisho Na. 2 cha hotuba ya bajeti ya mwaka 2012 ya Wizara hii chenye kichwa: "Uwekezaji na Mchango wa Watoa Huduma za Simu za Mikononi Kupitia Teknolojia ya *GSM* Tanzania." Wizara ilishindwa kutoa taarifa za kikodi za Kampuni za Simu za *TIGO, AIRTEL, ZANTEL* kwenye baadhi ya aina ya kodi.

Taarifa ya kodi ya Makampuni *(Corporate tax)* iliyolipwa na Kampuni ya *TIGO* hazikupatikana, taarifa ya malipo kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (2009-2011) za Kampuni ya *Zantel* nazo hazikupatikana, taarifa za kiasi cha fedha zilizotumwa *(Mobile money transaction)* cha Kampuni ya *AIRTEL*, na *Zantel* hazikupatikina, Taarifa za mchango wa kijamii *(Corporate Social Responsibility)* wa kampuni ya Zantel hazikupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali hii ya CCM kushindwa kupata takwimu ambazo nyingine zinatakiwa kutolewa na Makampuni kisheria ni mwendelezo wa uthibitisho wa kushindwa kwa Serikali hii kutawala Taifa hili. Kitendo cha Serikali kushindwa kupata taarifa hizi kunaashiria uzembe na rushwa iliyokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza mchakato wa kumiliki Shirika la Mawasiliano ya Simu la Taifa *(TTCL)* kwa asilimia mia moja kwa kununua asilimia 35% ya hisa za M-bia mwenza Kampuni ya *AIRTEL*. Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na hatua hii kwa kuzingatia umuhimu wa wananchi kupitia Serikali kumiliki Sekta ya Mawasiliano ya Simu kwa umuhimu na unyeti wake. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuweka wazi tathmini ya bei ya hisa za *AIRTEL* kabla ya ununuzi wa hisa hizo na mkataba wa mauziano hayo uwekwe wazi na uridhiwe na Bunge lako Tukufu, ili kuziba mianya ya ufisadi, na kulipa Bunge haki yake ya kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uvumbuzi wa Kisayansi. Naomba kunukuu sehemu ya hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani iliyowasilishwa ndani ya Bunge hili Tukufu katika mwaka wa fedha 2012/2013 kuhusu rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuibua na kuendeleza vipaji maalumu vya kisayansi na teknolojia miongoni mwa wanafunzi wetu na wananchi wengine wenye vipaji hivyo.

Sehemu ya hotuba hiyo inasema hivi: "Mheshimiwa Spika, hakuna mkakati wa kuibua na kuendeleza wabunifu katika kuibua na kuendeleza teknolojia hapa nchini. Pamoja na nchi yetu kuonekana kuwa na vijana wenye uwezo wa hali ya juu katika kubuni na kuendeleza teknolojia itakayoweza kuinua uchumi wa nchi yetu, Serikali imeshindwa kutambua fursa hiyo na kuwaendeleza wabunifu hao. Mfano, ni kijana Frank Waya kupitia kipindi cha *Jenerali on Monday* kinachorushwa na Televisheni ya *Channel Ten,* ameonesha uwezo mkubwa katika kubuni teknolojia ambayo ikiendelezwa itasaidia sana Taifa katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kipaji alichonacho, ameweza kuonyesha jinsi teknolojia ya simu inavyoweza kutumika katika kutengeneza mfumo wa kuzuia vyombo vya moto kutoungua kutokana na shoti ya umeme na hata kutumia simu kwa ajili ya umwagiliaji wa bustani na shamba kwa kutumia pampu ya maji hata mtu akiwa mbali na shamba lake au bustani. Pia ameonesha uwezo wa kutengeneza *inventor* inayoweza kukaa na umeme kwa siku saba baada ya umeme wa *TANESCO* kukatika. Hiki ni kipaji cha hali ya juu ambacho kikitumiwa vizuri na kuendelezwa, kitasaidia Taifa hili kupiga hatua ya kimaendeleo.

Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu, kuna mkakati gani wa Serikali wa kuhakikisha kuwa vipaji kama hivi vinaendelezwa katika nchi yetu, na: Je, wenye vipaji kama hivi ni nani mwenye wajibu na jukumu la kuviendeleza na kuvikuza?"

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwaka mmoja umepita sasa tangu Kambi Rasmi ya Upinzani itoe rai hii kwa Serikali kuibua na kendeleza vipaji vya namna hii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua, Serikali kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita, imeibua na kuendeleza vipaji vingapi ili kutimiza dira na dhima ya Wizara hii ya kuwajengea uwezo wananchi wa kisayansi, kiteknolojia na ki-uvumbuzi ili kukabiliana na ushindani wa Kimataifa na hivyo kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muhtasari wa taarifa ya utekelezaji, yaani *Perfomance Review 2012/2013*, Wizara ilieleza kuwa Serikali inatumia Tume ya Sayansi na Teknolojia kufanya tathmini ya ugunduzi ili kuweza kurasimisha ugunduzi huo, na kwamba inaandaa Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, na kwamba kuna sheria inaandaliwa ili kuwahamasisha, kuwasimamia na kuwalinda wagunduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutumia sheria ambayo tayari ipo, Sheria ya Usajili wa Uvumbuzi ya mwaka 1994, Sura ya 217 ya sheria zetu, yaani *the Patents (Registration) Act, 1994 Cap 217*

ambayo kwa mujibu wa jina refu *(long title)* ya sheria hiyo, madhumuni ya sheria hiyo ni: Sheria ya kusajili uvumbuzi, kuweka mazingira bora ya kuhamasisha uvumbuzi na ugunduzi ili kuwezesha kupata teknolojia katika misingi ya usawa kupita, kutoa na kuratibu uvumbuzi, kutoa vyeti vya bidhaa gunduliwa, na vyeti vya ugunduzi. Kwa Kiingereza, "*An Act to provide for the Patents Registration so as to make better provisions for the promotion of inventivity and innovation for the facilitation of the acquisition of technology on fair terms through the grant and regulation of patents, utility certificates and innovation certificates.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali inaona vifungu vya sheria hii ambayo tayari inatumika havitoshi, ni vyema ikaileta sheria hii Bungeni ili tuifanyie marekebisho kwani ni wazi kusubiri mpaka mchakato wa maandalizi ya sera na sheria mahususi, unachelewesha uendelezaji wa vipaji vya wabunifu wetu, hasa kwa kuzingatia kuwa Serikali hii imekuwa madarakani kwa miaka zaidi ya 50 na haijawahi kuona umuhimu wa kuwa na sheria hii kwa wakati wote huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia imeshuhudia mikanganyiko na migongano iliyohatarisha amani na utulivu wa nchi kadhaa zilizojaribu kutumia mtambo wa *Bio Metrick Voters Register* katika chaguzi zake mbalimbali. Mifano ya hivi karibuni ni ya nchi za Ghana na Kenya. Mitambo ya aina hii inatumia teknolojia ya juu inayotaka mazingira mazuri yaliyoandaliwa. Katika mazingira ya nchi masikini, yenye kitekinolojia duni na ambayo hata robo ya eneo la nchi haina umeme kama Tanzania, ni jambo linaloshangaza na wala haliingii akilini kuona tunataka kutumia teknolojia hii. Ni lazima tukumbuke msemo usemao, ukiona mwenzio kanyolewa na wewe tia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kujali hali duni ya kiteknolojia inayoikabili nchi yetu, Serikali ya CCM kupitia Tume ya Uchaguzi imeanza mchakato wa kununua mtambo wa *Biometrick Voters Register (BVR)* kwa mabilioni ya fedha za Wahisani. Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na

CHADEMA inaitaka Serikali iache mara moja mpango huo na badala yake ifanye marekebisho kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema haya kwa kuzingatia kuwa, ukiacha ripoti kadhaa zinazoelezea uduni wa maendeleo ya kisayansi na teknolojia nchini, sisi wote humu ni mashahidi kwamba asilimia 80 ya maeneo tunayotoka, hayana umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Sayansi na Teknolojia ina wajibu wa kusimamia na kuratibu tafiti za kisayansi na teknolojia. Pamoja na tafiti nyingi zilizifanywa na wanasayansi mbalimbali nchini, matokeo ya tafiti hizo zimekuwa haziwafikii walengwa. Mathalan tafiti zinazogusa Sekta ya Kilimo, zimeendelea kuishia kwenye vitabu, na kushindwa kuwafikia wakulima vijijini. Hili linatokana na kukosekana kwa uratibu kwa upande wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali ilitenga kiasi cha Sh. 26,476,961,000/=, kwa ajili ya utafiti. Hata hivyo, kiwango hicho cha fedha kimepungua katika bajeti ya mwaka 2013/2014 ambapo Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 16.5 tu kwa ajili ya utafiti. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili ni kwa nini fedha za utafiti zinapungua wakati tunajua kwamba jukumu kubwa la Tume ya Sayansi na Teknolojia ni kufanya utafiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ulazima wa kupandishwa hadhi kwa Taasisi za mafunzo za Sayansi na Teknolojia nchini. Kupandishwa hadhi kwa Taasisi zetu na kuwa Vyuo Vikuu vinavyotoa shahada za ngazi mbalimbali siyo tu itaongeza fursa za kujiendeleza kimasomo kwa wanasayansi wetu nchini, lakini pia itakuza wigo wa maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini na hivyo kuleta maendeleo ya kiuchumi, na kukuza ustawi wa wananchi, ukizingatia kuwa tunahitaji wataalamu wa ndani katika sekta ya sayansi na teknolojia ili kulisaidia Taifa kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia – Mbeya, bado haijapata ithibati ya kudumu toka Tume ya Vyuo Vikuu, ili kuwa Chuo Kikuu kamili. Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali kutamka mbele ya Bunge hili kuwa ni lini Taasisi hiyo itapata ithibati ya kudumu, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na Vyuo vingi vya Sayansi na Teknolojia nchini kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam *(DIT)* ni moja ya Taasisi kongwe nchini. Hata hivyo, pamoja na Taasisi hii kuwepo kwa miaka mingi, kasi ya kukua kwake siyo ya kuridhisha ukilinganisha na umri wake. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuongeza kasi ya ukuaji na kuiwezesha *DIT* kuwa na matawi kila Mkoa, kama zinavyofanya Taasisi nyingine za kitaaluma nchini, hususan Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha, ni Taasisi mpya kiumri. Ili kukuza na kuiendeleza Taasisi hii, Serikali inao wajibu wa kuitengea fedha za kutosha katika bajeti hii ili kuijengea uwezo wa kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo na mafanikio katika Taasisi za taaluma za sayansi na teknolojia nchini zinategemea kwa kiasi kikubwa maandalizi ya wanafunzi yanayopaswa kufanywa katika ngazi za chini za elimu yao. Kwa hali ilivyo sasa, ambapo wanafunzi wa Shule za Msingi wanasoma masomo ya sayansi bila kuwa na maabara wala maktaba, wanasoma somo la *TEHAMA* bila kuwa na kompyuta na asilimia zaidi ya 90 ya Shule za Msingi hazina umeme, ni wazi hawawezi kuwa na uwezo wala motisha ya kupenda kusoma masomo ya sayansi. Hali hiyo pia imetamalaki kwenye Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hali hii ya wanafunzi kutoandaliwa mazingira ya kupenda masomo ya sayansi itaendelea kukua na kukomaa, utafika wakati Taasisi zetu za Sayansi na Teknolojia zitakosa wanafunzi wa Kitanzania wa

kuwadahili, na hivyo Taasisi zetu ama zitakufa, au zitaishia kudahili wanafunzi kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu kuweka mazingira yenye afya kwa ustawi wa masomo ya sayansi ili kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka vivutio kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi kama vile kuwalipia karo wanafunzi wa sayansi ngazi za Sekondari na kuwapa mikopo asilimia mia moja kwa wale watakaoendelea na masomo ya juu katika Taasisi za Sayansi na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za maendeleo ya 2013/2014, Wizara hii imetengewa kiasi cha Sh. 200,000,000/= kwa uanzishaji wa vituo vya jamii vya mawasiliano Vijijini. Lakini kwa mujibu wa idadi, ukubwa na umuhimu wa kazi zilizipongwa katika fungu hili ni wazi kuwa kiasi hicho cha fedha ni kidogo sana na hakiwezi kukidhi malengo yanakusudiwa na Wizara hii.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iongeze pesa kwenye fungu hili ili kuchagiza maendeleo ya mawasiliano ya *Internet* vijijini kwa mustakabali wa mendeleo ya vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda sasa kukishukuru sana Chama changu cha CHADEMA kwa ushirikiano wanaonipa nikiwa ndani na nje ya Bunge. Nikipokee na niwashukuru Viongozi Wakuu wa Chama wakiongozwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe na Dkt. Wilbrod Slaa kwa kuendelea kuniamini na kunipa nafasi ya Waziri Kivuli katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Chama changu na kwa niaba ya Watanzania wote wanaopenda maendeleo ya Kisayansi, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo. Tunaingia katika hatua ya uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Kamishna Dkt. Maua Daftari, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Zungu.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami nataka nichangie mawazo yangu kidogo katika Wizara hii. Kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wizara hii inachangia asilimia 21 ya pato la Taifa. Ni kazi kubwa na kazi nzuri na ni kazi nzuri iliyoanzishwa tuseme na wale ambao wameanza, na tunashukuru wenzetu walioshika nafasi hii sasa wanaendeleza yale ambayo tumeyaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie katika maeneo yafuatayo: Kwanza, nataka nichangie katika maeneo ya tibamtandao *(Telemedicine).* Eneo hili kama tutaliendeleza vizuri, litasaidia sana afya za watu wetu. Napenda niseme hivi kwa sababu wenzetu kule wa Apollo walitufungia mtandao *Telemedicine* pale *Ocean Road Hospital,* lakini mpaka hii leo matumizi yake yako duni sana.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Mheshimiwa Waziri wa Afya kuona kwamba *telemedicine* zinapelekwa katika mahospitali yote ya rufaa na wenzetu wa Apollo walituambia wako tayari kutusadia katika kusomesha wenzetu namna ya matumizi ya *telemedicine.* Kile kituo cha *telemedicine* cha *Ocean Road* naomba sana Mheshimiwa Waziri uwakumbushe wenzetu wanaohusika, najua hakiko kwako, lakini msipotia nyie mguu Wizara ya Afya wao watalegalega vilevile. Naomba mshirikiane kufanikisha hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika suala la ubora wa mawasiliano ambao tunasema *quality of service*. Ubora wa mawasiliano hivi sasa umeshuka sana, watumiaji wengi wanalalamika. Usikivu ni mbaya, kuna kukatikakatika kwa mawasiliano, maongezi huwezi kumaliza kabla simu haijakatika; siku nyingine ukipiga simu unaambiwa

haipatikani wakati yule unayetaka kumpigia naye yupo na simu yake ni nzima, au utaambiwa imefungwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri awalazimishe watu wa *TICRA* kwamba kama mawasiliano ni duni huwa kunatolewa adhabu kwa wale ambao wanatoa mawasiliano. Kwa hiyo, Makampuni hayo ni lazima yawajibishwe walete ubora katika simu zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba nichangie kwenye masuala ya watafiti. Tunazungumza kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya utafiti ni kidogo sana, lakini hata watafiti wenyewe hawaonwi katika mambo yao. Watafiti siku hizi hawasikiki, hatusikii tafiti zao wanazozifanya kusemwa kwenye soko, wengi wao umri wao umeanza kuwa mkubwa na hatuoni kwamba kuna *succession plan* yoyote iliyowekwa kwa ajili ya watafiti wapya. Wakimaliza kazi zao na muda wao watafiti waliopo ina maana watafiti wengine watakuwa hawapo.

Kwa hiyo, naomba nikumbushie kwamba ni vizuri tutoe motisha kwa watafiti na vilevile tuweke mpango maalum kwamba wakiondoka wao wengine wapo wa kuchukua shughuli zao. Fedha iongezwe kama ilivyosemwa kwa ajili ya utafiti na tafiti zifanywe ziingie kwenye soko zisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa tunafanya tafiti tuseme *long grain rice,* halafu zinakwenda kwa walaji zinawasaidia sana namna ya kupata tija katika kilimo na katika mambo mengine. Naomba basi Mheshimiwa Waziri asaidie kwenye masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kuchangia ni hizi Taasisi mbili tulizonazo za teknolojia *DIT* na *MIST*. Tunazungumzia sana juu ya matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuleta *maendeleo*, lakini tunahitaji uwekezaji katika Taasisi hizi za mafunzo za *DIT* na *MIST*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi hizi wanafunzi wanaongezeka kila leo, lakini wakati huo huo fedha

zinazopangwa kuendesha Taasisi hizi zinateremka kila leo. Mwaka 2012/2013 Chuo cha *MIST* kilisajili wanafunzi 3,156 ikilinganishwa na mwaka 2011/2012 wanafunzi 2,591, ongezeko la wanafunzi asilimia 22. Lakini fedha za *OC* zilizotolewa kwa wanafunzi zimeshuka sana kutoka Sh. 1,000,000/= hadi Sh. 300,000/= kwa mwanafunzi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli tunaweza kuleta mabadiliko ya teknolojia kwa fedha hii tunayoitenga? Naomba sana niseme kwamba kiasi cha fedha kilichotolewa hakiwezi kabisa kuendesha Chuo cha *MIST* wala *DIT*. Kwa hiyo, tutasema mawasiliano sayansi na teknolojia, kuleta maendeleo ni ndoto kama hatukipi fedha zinazotosha.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri ulione hilo kwa upeo unaouona, lakini fedha zinazotengwa kwa Vyuo hivi ziongezwe ili ziweze kukidhi mahitaji halisi ya *institution* hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nishukuru kwa sababu sikutaka kusema mengi, mengi tu tunayajua yanafanyiwa kazi. Nikushukuru Mheshimiwa Waziri na timu yako uendelee kutuendeleza. Ahsante sana, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari. Tunakushukuru sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya katika Wizara hii. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu atafuatiwa na Mheshimiwa Leticia Nyerere.

**MHE. MUSSA Z. ZUNGU**: Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwanza nikushukuru, lakini vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri. Mabadiliko yanaonekana polepole, lakini *changes* zipo na *in future* tutapata mabadiliko mengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niipongeze *TCRA*, nawapongeza kwa kazi nzuri, lakini *more can be done.* Sasa hivi wanakusanya *60 billion* katika maduhuli yao. Lakini kwa utaratibu ambao nawajua viongozi wa *TCRA they can*

*do more* wanaweza kwenda mpaka *50 billion Shillings* wakisikiliza ushauri wa watu ambao wana uzoefu na kujua eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza mchango, nilitaka kujua nisije nikasahau na nikakosa muda; mchango wa mchezaji mpira wa timu ya Taifa Jela Mtagwa kutokuwekwa kwenye stempu nchini mwetu kwa miaka zaidi ya 10. Faida gani Serikali ilipata na faida gani mchezaji huyu kapata zaidi ya juzi tu kuambiwa kafanyiwa operesheni ya busha na imetoka kwenye magazeti yote? Mtu ambaye ametumikia Taifa hili na picha yake imetumika kuuza stempu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua, nipate maelezo hayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *future development* ya simu iko kwenye *VAS (Value Added Service). Technology* ya simu inabadilika siku hadi siku, lakini sheria zetu ziko pale pale! Kwa mfano, hakuna *control* ya *import airtime* inayofanywa na *TRA* kujua ni *airtime* gani imekuwa *imported* nchini ili iweze kutozwa kodi? *Airtime* inakuwa *imported* nchini, inakuwa *imported* kama mzigo. Lakini *value* ya ile *airtime* haipo! Kwa hiyo, *TRA* uwezo wao wa kui-*peg* ile 30 *percent* ya *excise duty* na 18 *percent* ya *VAT* inakuwa haiwezekani. Haiwezekani vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria yetu mimi nitakusomea hapa kipengele kidogo tu ambacho *TCRA* wanalalamika, *if these would be changed* tutajikuta tunapata mapato makubwa mno. Hapa wanasema, kutokana na kifungu hiki cha juu ambacho siwezi kukisoma kwa sababu ya muda cha Sheria ya *Finance Act* ya 2009 Na. 14, ukusanyaji wa kodi unalenga tu kwenye huduma ya maongezi *(voice)* na unatokana na *voucher* za simu *(prepaid airtime mobile phone voucher)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaweza kuwa sababu mojawapo kwa Serikali kukosa mapato kutokana na zile

Sheria kutotaja huduma nyingine katika ukusanyaji wa *VAT*. Kama vile kutoa ujumbe mfupi wa maneno *(short message service)*, *internet,* kusafirisha takwimu *(data),* huduma za kifedha na kadhalika.

Sasa kama Sheria zetu hazibadiliki, *technology* inabadilika na Makampuni ya Simu sasa hivi, *voice call* kwao hazina umuhimu sana. Sasa hivi biashara kubwa na pesa ziko kwenye *internet*, *data* na mambo mengine.

Kwa hiyo, mimi niiombe Serikali iwe na *commitment* itueleze lini sasa wanatazamia kubadilisha Sheria kama hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tunalipata ambalo ni kubwa sana, unaponunua *voucher,* tayari umeilipa Serikali asilimia 30 ya *value* ya *voucher*. Kwa mfano, ukinunua *voucher* ya Sh. 10,000/= hela ya Serikali tayari ni Sh. 3,000/=. Hii Sh. 3,000/= haiendi Serikalini *simply* kwa sababu mwenye simu anakusubiri mwenye *voucher* wewe upige maneno ndiyo akate kodi hii.

Sasa kama ukiamua kwa mwaka mzima wewe hupigi simu ya maneno unatuma tu *sms* au unatumia *internet* kodi hii haiendi Serikalini, *simply* kwa sababu Sheria zetu hazi-*spell* kwenye maeneo kama haya. Makampuni haya ya Simu *they are so fast and so knowledgeable,* wanaendelea kubadilisha *technology* na sisi tunakuwa *sensed* na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua mfano nchi ya jirani tu hapo Kenya. Tazama mfano mdogo tu wa *report* ya *Gross Revenue* ya *SafariCom*, Kampuni moja tu ya Kenya na Kenya wana-*operate as one* kwa Makampuni ya Simu. Tanzania tunayo saba, lakini utakuta kila siku wana-*register profit.* Sisi bado Makampuni haya hakuna hata Kampuni moja toka ianze inaonyesha inapata faida. *This is very wrong.*

Kwa hiyo, naomba Serikali sasa itazame umuhimu wa kuzipitia sheria zake na ifanye haraka sana. *Short of that,* tutaendelea kuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wao wanasema unapokata *voucher* yako *only* wakati inakuwa *activated* ndiyo sasa Serikali inaanza kupata mapato. Lakini unaweza ukanunua *voucher, operator* tayari anakusanya ile asilimia 30 wakati wewe ukishanunua *voucher* usitumie ile *voucher* hakuna utaratibu wa *operator* akurudishie ile asilimia yako 30. Kwa hiyo, hapo ndiyo nasema watu wasitizame hizi, watizame maeneo ambayo; kuna maeneo ya *voucher* zinazoagiziwa. Sasa hivi kuna *electronic vouchers*, ambazo *TCRA* na *TRA* wanatakiwa wawe karibu sana kufuatilia mapato yanayopatikana na Makampuni haya. *Financial Statements* za Makampuni haya zinakuwa *declared* na Makampuni haya. Hakuna *forensic audit* ambayo *TRA* wanaweza kufanya kwenye Makampuni haya kwa sababu hawana *capacity* hiyo na wao wana-*admit* kwenye taarifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nipo kwenye Kamati ya Kodi kwa zaidi ya miezi sita, hawana *capacity* hiyo. Kwa hiyo, sasa *it is high time TRA* waweke vijana, wasomee vizuri wabobee kwenye maeneo ambayo *revenue* tunakosa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama muda utanitosha. *Mobile penetration Tanzania,* nafananisha na nchi ndogo tu ya Rwanda. *Mobile penetration* ya Rwanda kwenye kila watu 100, watu 35 wanasimu. *Mobile penetration* Tanzania kwenye kila watu 100 tuko watu 48 wana simu. *Almost 50 percent* ya Watanzania, lakini tazama kodi zinazolipwa na Rwanda. Wanyarwanda sasa hivi wenye simu ni milioni tatu. Sisi tuko milioni 28. Wanyarwanda 2010 Kampuni ya Simu wamelipa 14m *USD*. Nchini kwetu tunalipwa 1.7m *USD.* Yote ni kwa sababu ya nini? Hatuna *mechanism* ya ku-*control* biashara hii ambayo inaweza kuiletea mapato mengi sana Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa ushauri wa mtambo wa *traffic* ambao nashukuru Serikali imeuweka. Lakini vilevile *is not enough*. Rwanda huu mtambo hawana, lakini wanayo *system,* Mamlaka zao zina uwezo wa kuingia katika *National Population Centre* za Makampuni haya ya kufunga *KPI* yake

*(Key Performance Index)* na kujua huyu *operator* ana *earn* Shilingi ngapi? *Which can be done.* Nami najua *TCRA* wana uwezo wa kufanya hiki kitu. Tuliwashauri na ninajua watafanya. Kwa hiyo, *we can earn more*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa *Average Revenue Per User (ARPU).* Unapokwenda kwenye *prom* zako unaingia katika c*ells* za *nock* unapata hizi *information. And this information* zinaweza kuwasaidia *TRA* tukaweza kupata mapato mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano mdogo tu. Makusanyo yanayofanywa na M-PESA *transaction* za Kenya. Kenya kwa mwaka hawana tofauti na sisi. Wanafanya *transaction* ya *over 22 trillion Tanzania Shillings*. Sawasawa na sisi kwa mwaka. Pesa zinazopitishwa kwenye mitandao ya simu inafika Shilingi trilioni 20. Tunaweza tuka-*peg,* tukaweka kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza habari hii na Kiongozi mmoja asubuhi akasema, aah, tutawasumbua wananchi. *No,* siyo suala la kusumbua. Tunaweza tukaweka *five percent* ya *transaction* za M-PESA tukapata *one trillion Shillings* kwa kila mwaka kusaidia matatizo yote haya ya Walimu, Madaktari na Watumishi wengine wa Umma kwa kitu kidogo tu na wao wakajua sisi tunawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *it is very unfortunately,* sijui kama nitamaliza yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, leseni ya *4G*. Nchi zote duniani *4G* inakuwa *auction*. Sasa ni utaratibu wa kuutazama. Kama Kenya wenzetu wali-*auction* Machi mwaka huu 2013 wakapata milioni 500 USD na sisi tutazame njia ya kufanya kama tunaweza kuingia katika utaratibu huo wa kuweza ku-*auction.* Iko katika taarifa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni matangazo ambayo Makampuni ya Simu wanaruhusiwa, ni lazima yawekewe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUSSA Z. ZUNGU**: Ya kwanza hiyo eh! Ya kwanza?

**NAIBU SPIKA:** Ni kengele ya pili.

**MHE. MUSSA Z. ZUNGU**: Ah!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Zungu kwa mchango wako mzuri, inaonyesha umefanya utafiti mzuri wa uhakika, mambo ambayo ndiyo tunapenda Waheshimiwa tujishughulishe nayo. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Leticia Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika Wizara hii ambayo ni Wizara muhimu sana katika teknolojia ya nchi yetu. Naomba nianze kwanza na matumizi mabaya ya mitandao au ya new *technology*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana, Watanzania tumejikita katika matumizi mabaya ya mitandao. Badala ya kutumia mitandao hii katika kuleta maendeleo ya Taifa letu kwa faida ya Watanzania wote. Matumizi mabaya yanaweza yakaleta uchochezi pia. Tumeona kuna watu wanaandika vitu kwenye mitandao ambavyo vinaweza vikaleta uchochezi nchini na hatimaye kukawa na vurugu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa hawa watu wanafanya wengine bila kujua kwamba wanaweza wakakamatwa. Naomba kwanza ku-*declare interest*, wakati nasoma *criminal justice* nilisoma *cyber crime* pia. Kwa hiyo, nataka kuwaeleza Watanzania ambao wamezoea kutumia mitandao vibaya, wanatukana Viongozi, wanatukana watu, wanatukana makundi mengine, uwezekano wa kukamatwa

upo ili mradi ikijulikana *IP address* yako unaweza ukakamatwa na ukaishia jela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iharakishe hiyo Sheria ya *Cyber Crime* ili tuanze kuifanyia kazi kwa sababu Taifa letu limekuwa likidhalilika, Viongozi wetu wamekuwa wakidhalilishwa, wananchi wetu wanadhalilika kwa sababu Watanzania wachache ambao hawana maadili wameamua kutumia mitandao vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa alituachia wosia kwamba tupendane, tushirikiane na tuwe kitu kimoja kama Taifa. Lakini cha kushangaza, leo mitandao ni kutukanana tu. Watanzania tumejikita katika kutukanana. Unapata faida gani unapomtukana mwenzio? Unapata faida gani unapomtukana Mheshimiwa Mbunge? Unapata faida gani? Kwanza, ukikaa sana kwenye mtandao utambue kwamba siyo sahihi kwa afya yako. Ni hatari kwa afya yako, unapokaa sana kwenye mitandao. Wengine wanakesha kwenye mitandao kazi yake ni kutukana tu, kazi yake anabadilisha *ID* tu, yuko *busy* anatukana watu. Hajui kwamba anaweza akapata madhara ya kiafya, hajui kwamba mwisho wa siku anaweza akapata hata *tumor* kwa sababu amekuwa akiji-*expose* kwenye *radiation* kwa masaa mengi kupindukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawasihi Serikali sasa itoe onyo kwa hawa watu ambao wametuchafua mpaka wakati mwingine tunaona aibu, tunashindwa hata kujivunia Utanzania wetu. Sisi Watanzania, jadi yetu na asili yetu ni kupendana. Lakini sasa hivi limekuwa ni Taifa la kutukanana. Yaani wewe unaamka unaanza kutafuta leo nimtukane nani Bungeni, au leo nimtukane nani kati ya Mawaziri. Haitusaidii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ije, Watanzania waelemishwe, waelezwe madhara ya kutumia hata hiyo mitandao. Kuna yale madhara mengine ambayo ni ya kawaida tu na kuna hasara vilevile. Unajua hasara mojawapo ni kupunguza ajira. Kutumia *new technology* ni lazima

tufahamu pia tunajiandaa kupunguza ajira, kwa sababu mtu anayetumia *new technology definitely* atapunguza wafanyakazi kwa sababu hatahitaji utitiri wa wafanyakazi. Kwa hiyo, na hilo Serikali iwaandae Watanzania, iwape elimu ni jinsi gani sasa tuta-*create* ajira kwa vijana wetu bila kuathiri matumizi ya *new technology* ambayo pia tunayatarajia katika kuendeleza Taifa letu*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima pia tuangalie ongezeko hili la makosa ya utumiaji mbaya wa *new technology,* yaani *Cyber Crime*. Tuangalie ni nini ambacho kinasababisha? Kuna watu wanatumia vibaya ama kwa kuiba kwenye Benki au akaunti za watu kwa kutumia hilo *online banking*. Kuna watu pia wanafanya makosa au ya kuiba *ID,* yaani vitambulisho, anajifanya ni Leticia Nyerere ili afanikiwe kile anachotaka kufanikiwa kwenye mtandao, inaitwa *ID theft,* yaani wizi wa utambilisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo kama haya, Taifa letu limeathirika kwa hali ya juu sana na tumekuwa hatuyafuatilii kwa sababu nchi yetu bado inaendelea. Kwa maana hiyo, vilevile hata yale makosa ambayo kwa wenzetu ambayo wenzetu wameshayafanya, yamefanyika nchi zilizoendelea na wakatafuta ufumbuzi na jinsi gani ya kujihami, lakini sisi wala hatufikirii kuanza kuwaelimisha Watanzania ili wachukue tahadhari. Mambo haya ni hatari kwa Taifa na mambo haya ni kikwazo kwa maendeleo ya Taifa letu. Siku nyingine mtakuta mtu anajifanya yeye ndiye Naibu Spika, anasema mambo kwenye mtandao na matokeo yake yanaathiri ile *credibility* ya Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaiomba Serikali, Wizara husika tafadhali mtusaidie ili mambo haya ya *Cyber Crime,* yaelezwe na yaelimishwe kwa Watanzania waogope na wajue kwamba uwezekano wa kukamatwa ni mkubwa. Wengi hawaelewi, anafikiri kwa sababu amejifungia chumbani na kompyuta yake, haamini kwamba anaweza akakamatwa na wengine tena anaanza kuangaza pembeni eti anatafuta kama kuna mtu anayemwona. Siyo hivyo! Makosa ya *Cyber* hayakamatwi kwa njia ya kuonwa na mtu,

yanakamatwa kwa njia ya teknolojia iliyopo *and it is very easy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, kuna baadhi ya watu tena kwa bahati mbaya ni Watanzania wenzetu, waliwahi kukumbwa na mkasa huo kwa sababu ya kutokujali tu, wameamua kumchafua mtu kwenye mtandao na sitamtaja ni nani, lakini aliwashughulikia na hatimaye wote walibambwa na tunavyoongea sasa wengine wako ndani wakisubiri kujibu mashtaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa itenge pia fungu la kushughulikia hili. Kwa sababu nikianza kushinikiza Wizara kwamba waanze kushughulikia uhalifu wa *Cyber Crime* bila pesa itakuwa ni kuwaonea.

Naamini kabisa Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wamefanya kazi kubwa kabisa katika kuelimisha baadhi ya Taasisi kuhusu madhara ya *Cyber Crime* na wamekuwa wakifukuzia kwa hali ya ukaribu kabisa kuhusu hii Sheria ya *Cyber Crime* ili iletwe haraka iwezekanavyo na sisi tuanze kuitumia mara moja. Kwa sababu tumechoka kuwa Taifa la kutukanwa tu. Nyie kutwa mnatukanwa. Unapoteza muda wako unatukana watu! Huo muda ungeutumia kwa ajili ya kujiendeleza, sisi Watanzania tungekuwa mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tatizo watu wanatumia muda mwingi kutukana watu bila faida. Mtukane mtu basi abadilike ndiyo utapata faida! Wewe unatukana kila siku, lakini mwenzio anadunda tu! Wewe umekazana, unatukana, anadunda tu! Sasa maana yake nini na umepata faida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania waelewe waache tabia hii ambayo ni mbovu, ambayo haina faida yoyote, na wataendelea kudidimia kwa umaskini kwa sababu hawatumii vizuri muda wao wa maendeleo. Wangeweza kujiendeleza kielimu, kiuchumi lakini matokeo yake tuko *busy* tu, leo nimtukane nani, unachungulia tu. Wengine wanaangalia kwenye *TV* kwenye Bunge anaanza kusema

nadhani leo nitamchukua Mheshimiwa Sitta. Haisaidii! Haisaidii! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tupendane wote kwa pamoja, Taifa letu ni moja, hatuna sababu ya kutukanana eti kwa sababu ya tofauti ndogo ndogo; tuendeleze Taifa letu ambalo ni changa. Bila sisi kuendeleza Taifa hili, hakika tutaendelea kuogelea kwenye umaskini! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leticia Nyerere, katika siku ambazo umeongea na Taifa ni leo. Mimi mwenyewe shahidi yako, nimetukanwa sana! Lakini naendelea kudunda tu! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Assumpter Mshama, atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, ninayo furaha na heshima kubwa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na mbele za Mungu ili niweze kuchangia katika sekta hii muhimu.

Nitakwenda moja kwa moja, kwanza, nitaomba Wizara hii, kitu cha kwanza kabisa ninachokijua ni kwamba hii Wizara ipo kwa ajili ya kutuelimisha kwa ajili ya kutuunganisha Watanzania na wananchi wa nchi nyingine, kwa ajili ya kuona kwamba *technology* inakua katika Taifa letu, na kitu ambacho napenda niwashukuru kwamba wamefikifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niulize, nitaanza na Jimbo la Nkenge; tumekuwa na matatizo makubwa ya mawasiliano na ninachojua ni kwamba hawa watu wanaokuja kuingia mikataba na nchi au kuingia mikataba na Wizara katika suala la mawasiliano, wanaeleza kabisa kwamba watahakikisha wana-*cover* Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikwambie katika Wilaya yetu ya Misenyi, robo tatu nzima ya Wanamisenyi hawapati mawasiliano na hasa wale waliopo mpakani mwa Uganda wanatumia *network* ya Uganda na matokeo yake uchumi wetu unapotea, pia tunakuwa hatuna uwezo wa kujua nini kinaendelea katika mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ninaloliomba kama Mbunge wa Jimbo la Nkenge, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuwasilisha anieleze lini Misenyi nzima itapata mawasiliano ukizingatia tunaishi katika mpaka wa Tanzania na Uganda, kwa hiyo, tungependa kuwa saa zote kwenye mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimebahatika kidogo kufanya utafiti mdogo kuhusu sekta hii namna gani inaweza kutuongezea mapato katika pato la Tanzania. Kwa mujibu wa *TCRA*, mpaka Julai, 2012 kuna kadi za simu 28,024,611, wote hao wanapiga simu. Kama kweli tungetoza ushuru wa kweli, tungeshughulikia vizuri sekta hii, tungebadilisha *system* au tungeweza kuingiza pato la kutosha kutoka katika pato la simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa *TRA*, mwenendo wanaoutumia katika ukusanyaji wa kodi mwaka huu au 2006 mpaka 2012 sekta hii imechangia 5.2 *percent* mpaka 6.6 *percent* ambayo kwa kweli ni ndogo sana ukilinganisha na kazi zinazofanyika kupitia katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya mapato ya Serikali yanapotea kutokana na utaratibu ambao sio mzuri kama alivyosema msemaji aliyemaliza kusema, Mbunge wa Ilala, alivyoeleza ni namna gani tunapoteza mapato kutokana na kutokata au kutotoza ushuru wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 na mwaka 2012, jumla ya kodi zote zilizolipwa na Makampuni ya Simu, nitanukuu, ni bilioni 366.6, kati ya hizo bilioni 184.8 zinatokana na *VAT* na bilioni 114 zinatokana na ushuru wa bidhaa

ambazo nadhani kama tungekuwa tumetumia utaratibu mzuri, mfano, mtu anapokuwa amenunua kadi, akakwangua akaweka kwenye simu yake, ile kadi ilitakiwa itozwe ushuru pale pale. Lakini utaratibu uliopo, eti mtu mpaka aingize hiyo kadi kwenye simu, aanze kutumia na kama hiyo kadi itakuwa imedondoka au imepotea, yule mwenye kampuni ya simu amepata pesa, lakini Serikali haijapata kodi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama simu utakuwa umetumia elfu tano ikaibiwa na umeweka vocha ya elfu hamsini, ile yote iliyopotea, yule mwenye mtandao amepata pesa yake, lakini Serikali haijapata kodi. Kwa maana hiyo, pale tunakuwa tumepoteza kodi kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali, tuanze kuanzia leo, mtu anaponunua kadi ya elfu tano, ile *thirty percent* ikatwe pale pale ili kusudi tukipoteza, kama sitaitumia, yule mwenye simu atakuwa amepata na Serikali itakuwa imepata. Lakini kitendo cha kuona kwamba, wewe unanunua, muuza kadi amepata pesa, Serikali imebaki bila ushuru, nadhani hilo jambo linapoteza ushuru kwa nchi yetu kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nashangaa, labda ninukuu pale ambapo alikuwa anaongelea Mbunge wa Ilala, Tanzania tukilinganisha na Rwanda, Burundi na Uganda, sisi ndiyo tunatoza kiwango kidogo sana ukilinganisha na wenzetu. Mfano, ukiangalia katika mwaka 2010, Tanzania ilipata dola milioni 1.7; Kenya ilipata dola milioni 79.3; Uganda ikapata dola milioni 29.4 na Rwanda ikapata dola milioni 10.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu linganisha Tanzania na Rwanda upate pato moja! Uangalie ni namna gani tunapoteza pesa nyingi za mapato katika Taifa letu. Hiyo yote ni kwa sababu tunafanya vitu labda bila kuweka umakini wa kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Assumpter, takwimu hizo ni sahihi kweli?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni sahihi kabisa na ninacho kitabu hiki hapa, si za kutoa kichwani. Nina kitabu ambacho nimekifanyia utafiti mzuri kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, yaani sisi dola milioni moja?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nirudie tena.

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninayo miaka ya 2005, 2006, 2007, lakini kwa kukomboa muda niende mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Tanzania tumepata *USD million* 1.7; tukienda Kenya wamepata dola millioni 79.3; tukienda Uganda wamepata dola *million* 31.3 na Rwanda wamepata dola milioni 14, sisi tuna tatizo gani au kuna kirusi gani kinachofanya sisi tushindwe kukusanya kodi kama wenzetu ambao kwa mfano, ukiangalia Rwanda ina watu wachache sana ambao hawawezi kufikisha kadi milioni 28. Sisi Tanzania na Kenya *almost* tunalingana, lakini bado sisi tunawazidi *population*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kitu gani kinasababisha sisi tushindwe kukusanya kodi ya kutosha? Au kuna tatizo katika ukusanyaji kodi au hazifiki kule zinakotakiwa kwenda, labda ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleweshe kwa nini sisi tunazidiwa au tunalingana na Rwanda katika kukusanya kodi inayotokana na mawasiliano. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hapo tutahitaji ufafanuzi kwa kweli wakati wako ukifika. (*Makofi*)

Endelea Mheshimiwa Assumpter!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize ni lini Serikali italeta sheria tuibadilishe, sheria tuliyonayo ya kifungu kidogo 7(4), haitoi ufafanuzi wapi tunaanzia kukata kodi. Kwa hiyo, sheria inachoeleza ni kwamba, utatoza kodi, lakini imetoa vipengele vingine, kama *internet* haielezi, huduma ya miito ya simu haielezi, kutuma pesa haielezi, ina maana sasa hivi watu wanajiingizia *billions of money* kwa sababu wao wanachukulia kwamba sheria haijatuambia chochote. Kwa hiyo, kutokana na sheria kutokusema chochote tunaibiwa hivi hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliongea na *TCRA* wakaniambia, japo tunavyo *technically* vitu vyote vya kutafuta hizo pesa, lakini tunashindwa kuzitoza kwa sababu sheria haijaturuhusu. Ameeleza vitu vingi sana *TCRA* ambayo ni Mamlaka yetu ya Mawasiliano, inasema inavyo vitu vingi vya namna ya kupata *KPI* ambayo inaweza ku-*detect* ni kiwango gani cha mtumiaji wa simu ameweza kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wanacho chombo kingine kinachoweza kupima ni muda gani umetumika katika maongezi na wakagundua ni shilingi ngapi zitabaki kwa Serikali, lakini kwa kuwa sheria haijawaruhusu hawatoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunanenepesha Wazungu au Makampuni wakati watu wetu wanakosa kipato. Nasubiri Waziri atakapokuja aje na tamko la sheria hiyo ataileta lini ili tuibadili kuanzia kwenye kuongea mpaka kwenye kutuma meseji, hebu *imagine* unatuma meseji tangu asubuhi. Pia kingine ambacho wanatudanganya, wanakwambia tuma meseji mia moja wakati ukituma kumi hakuna kitu kinachoendelea, sijui wenzangu mnasemaje, lakini nimeona, wanasema umezawadiwa kuongea bure, *how*! Utaongeaje bure? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tulitamani uendelee kuzungumza Mheshimiwa Nshunju, lakini muda hauko upande wetu. Tunakushukuru sana na natumaini Waziri atapitia na kutuambia kuna tatizo gani katika sheria hiyo. Tupo tayari kuibadili haraka sana.

Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis!

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja katika bajeti hii ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Sub-hanah Wataala* kwa kunipa nguvu kusimama katika Bunge hili. Sayansi ndiyo maisha, tulipokuwa tunasoma sekondari tuliambiwa *science is the study of life and its environment.* Maisha kila siku yanabadilika, ndiyo maana sayansi pia kila siku inabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *speed* ya bajeti ya Wizara hii inayopewa na Serikali, ni *speed* ya yule mdudu kinyonga, maana yule mdudu mwendo wake anakwenda na kurudi, anaweza akatembea kutoka kona moja ya *desk* lako mpaka kona ya pili kwa muda wa siku tano. Kwa hiyo, tuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri kasema katika kitabu chake hapa ukurasa wa 73 kwamba, kuna uhaba mkubwa wa watalaam katika nyanja mbalimbali za sayansi, teknolojia na ubunifu, hali hii inajitokeza kwa kuwepo idadi ndogo ya watalaam. Watalaam wengi wamekuwa wenye umri mkubwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kwenda vizuri na sayansi ni lazima hawa watalaam tuwe nao wa kutosha, lakini ikiwa Wizara inapewa bajeti ambayo haina mshiko, mwaka jana bajeti iliyotengwa katika Wizara hii ilikuwa ni shilingi 71.6 bilioni, lakini mpaka mwezi Machi mwaka huu tunakuja katika Bunge hili ambalo ni Bunge la bajeti ya mwaka unaofuata fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 32.8 ambayo ni asilimia 46 tu. Ikiwa Sayansi ndiyo maisha na bajeti yenyewe ndiyo hii maisha yatawezekana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ni lazima itilie maanani sana jambo hili ili tuweze kuikwamua nchi hii. Mwaka

huu wa bajeti 2013/2014, Wizara imeomba shilingi bilioni 63.1, imepungua kutoka bajeti ya mwaka jana, ndiyo maana nikasema mwendo wake ni wa kinyonga, inakwenda na kurudi nyuma, sasa sijui kama tutavuka lini katika sayansi na teknolojia ya wenzetu waliyonayo ulimwenguni sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inasimamia Vyuo muhimu katika nchi yetu, Chuo cha Nelson Mandela kilichopo kule Arusha, *DIT* Dar es Salaam, *MUST* Mbeya, ambapo Vyuo hivi ndiyo vinategemewa vitoe watalaam wa sayansi na wabunifu watakaoweza kuendeleza sekta mbalimbali katika nchi yetu zitakazoweza kuinua uchumi, lakini fedha hazitolewi kwa ajili ya kuviendeleza vyuo hivi, wanashindwa kusoma, wanashindwa kufanya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Miundombinu ambayo tunaisimamia Wizara hii na ni Mjumbe makini kweli, maana tunafanya ziara kukagua na kuona hali zilivyo, lakini matatizo yaliyopo hayashughulikiwi. Watu wanasoma *theoretically* hawasomi *practically*. Mwanasayansi gani atasoma kwa *theory* tu? Badala yake akimaliza kusoma atakuja kukaa kwenye meza atataka aajiriwe penye mshahara. Wakati yeye anatakiwa avumbue, agundue, awapelekee watu chini ili tuzalishe, lakini bila ya kupewa fedha za kufanya uvumbuzi, fedha za kufanya ugunduzi hatuwezi kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, itifaki ya sayansi ya nchi za *SADC,* inataka asilimia moja ya *GDP* itengwe kwa ajili ya kushughulikia mambo haya ya tafiti, ukitazama asilimia moja ya *GDP* ya nchi yetu ni pesa nyingi kwa kweli, kwa sababu sasa hivi kutokana na takwimu nilizozipata asubuhi ya leo, *GDP* ya nchi yetu ni takribani trilioni 55. Sasa ukitenga asilimia moja ya pesa hizi ni karibu bilioni mia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara nzima ni bilioni 63, wakati inatakiwa itifaki ya *SADC, one percent ya GDP* iwe ni kwa ajili ya utafiti tu ili nchi iweze ku-*move*. Wanasayansi hawa wavumbue, washushe chini uvumbuzi wao, kila mtu kwa sekta yake aufanyie kazi, kwenye kilimo,

kiwanda na mwenye mambo mengine yote ya biashara, afanyie kazi uvumbuzi huo. Lakini ikiwa pesa hazitolewi, ikiwa hii tunasema ni kubwa, basi wapewe angalau 0.25, wapewe shilingi bilioni 110, lakini Wizara nzima bilioni 63 tunacheza na sijui kama tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ni mengi niliyonayo hapa ya kuchangia katika Wizara hii kwa sababu mimi ni mdau mkubwa, lakini nitakwenda kwa kurukaruka ili nipate yale muhimu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu aliyetangulia Mheshimiwa Zungu amesema vizuri sana, sitaki nirudie kule juu ya kuchangia Pato la Taifa kupitia Wizara hii, lakini sina wasiwasi na watalaam waliopo katika Wizara hii, Waziri kajipanga vizuri na Naibu Waziri na timu yake ya watalaam, kule *TCRA* Profesa Nkoma ambaye anaongoza taasisi ile yupo vizuri, lakini wenzangu wameshasema hapa kwamba, fedha nyingi zipo kwenye Makampuni ya Simu, ambapo *transaction* yake ya pesa kwa kila mwaka ni *trillions,* inazidi hata bajeti yetu ya nchi nzima, lakini hatupati chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutapata vipi ikiwa watalaam hatuna, watalaam tutawapataje ikiwa hatutoi pesa za kuwafundisha? Haya ni mambo muhimu ya kuzingatia, Serikali ipo hapa, namwona anayekaimu nafasi ya Kiongozi wa Serikali Bungeni ananitazama vizuri, jambo hili linatakiwa lizingatiwe na lifanyiwe kazi, isiwe tunasema tu wanasikiliza, wanaona, lakini hawayafanyii kazi, tulishaachwa nyuma na tutazidi kuachwa nyuma. Wenzetu wanakwenda kwa *speed* ya ndege, sisi tunakwenda kwa *speed* ya kinyonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yaliyopo katika gharama za mitandao ya simu, tumeambiwa hapa kwamba, gharama zimepungua, upigaji wa simu kutoka 2009 mpaka sasa hivi 2013, lakini bado simu gharama yake ni kubwa. Tunaambiwa simu za nje sasa hivi ni sh. 492 kwa dakika moja, lakini kwa nini wenzetu wana gharama nafuu zaidi kuliko sisi. Isitoshe gharama za kuunganisha simu tumeambiwa

zimepungua kutoka sh. 115 mpaka sh. 35 sasa, lakini bado katika Makampuni ya Simu kuna matatizo mengine makubwa ambayo nataka niyaseme kwa lugha sawa kabisa bila kusitasita, ya wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makampuni haya ya Simu yanawaibia Watanzania maskini fedha zao. Zile ni fedha *cash* wanaingiza *credit* katika simu, wana matangazo mengi, wanatangaza kwamba kuna ofa fulani, ukiweka kifurushi cha ofa ile, fedha zile zimeliwa, hakuna ofa unayopata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwapigia *customer care* wanakuuliza wewe uko wapi? Unawaambia nipo Zanzibar au nipo Pemba au Chakechake, wanasema Mkoa huo hauhusiki na ofa hii, kwa nini wasitangaze mapema kama Mkoa ule hauhusiki na ofa ile? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo simu yangu ya *blackberry,* nikanunua kifurushi cha *blackberry* cha *internet* katika Kampuni ya Simu ya *Zantel*, nikaingiza kifurushi kile, fedha zimeliwa *internet* sikupata. Nikaenda katika ofisi yao, nikawapelekea simu yangu hii, wakaingiza kifurushi kingine pale pale katika kaunta yao na fedha nikalipa. Fedha zimeliwa na *internet* sikupata. Wakasema hii *blackberry* yako haipo katika *list* yetu, alaah! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eti *blackberry* zile wanazouza wao tu ndiyo zimo katika vifurushi vyao, kwa nini wasiseme katika matangazo yao, wanatangaza *blackberry* kifurushi chenu hiki hapa, halafu ukiingiza unaibiwa pesa. Pesa ni pesa iwe elfu kumi na tano au elfu ishirini. Kama Mbunge anaibiwa namna hiyo je, mwananchi wa kijijini kwangu wa Chonga, Tundagua, Kilindi au Pujini hali yake itakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Wizara hii mambo haya yafanyiwe kazi, si mambo ya masihara, watu ni maskini, halafu wanaibiwa na kodi pia haipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mengi, nakuja kwenye analogia na digitali, Serikali hapa ilisema lazima *channel* tano ziwe bure, lakini hazipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunawashukuru sana wachangiaji waliotuchagiza asubuhi hii kuhusiana na shughuli iliyopo mbele yetu tunawashukuru sana.

Ni kweli kufuatana na baadhi ya michango ya Wabunge, bahati mbaya sana Kanuni zetu za Bunge hazituruhusu, Kanuni zetu zinaruhusu Mbunge au hata Kamati ya Bunge kuleta jambo lolote la mabadiliko ya sheria na kadhalika, lakini katika sheria zinazohusu masuala ya fedha, Mbunge au Kamati ya Bunge haiwezi kuleta mabadiliko ya namna hiyo.

Kwa hiyo changamoto za namna hii kwa kweli *purely* ni za Serikali, kwa sababu sasa Wabunge au Kamati hawawezi, kwa kweli *entirely* ni za Serikali na tunamweka Waziri wa Afrika Mashariki mahali pagumu sana inapokuwa kwenye *rating*, kila *rating* Rwanda iko juu, Uganda ipo juu, Kenya ipo juu.

Hii inamfanya Waziri wetu anapokaa kwenye vikao kule anaonekana mwepesi mwepesi hivi. Kwa hiyo, mambo mengine katika *region* lazima tufanane au tuwazidi wenzetu siyo kila kipengele tunakuwa tuna-*lag behind* bila sababu ambazo watu wote tunaweza tukaelewa, kwa nini sisi tuwe nyuma kiasi hicho katika kukusanya mapato kwenye sekta hii.

Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru sana kwa hatua hiyo, jioni ya leo kama muda utaruhusu nitaangalia baadhi ya wachangiaji, lakini atakuwepo Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri tutaendelea. Kama hali itaruhusu naweza nikamfikiria Mheshimiwa Njwayo na Mheshimiwa Amar, muwahi tu, tutaona hali itakavyokuwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapa naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili leo jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, muda wetu ni mdogo sana, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Amar ajiandae na Mheshimiwa Mhita atamalizia.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia kidogo hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja na kwa kweli naunga mkono hoja kwa sababu Serikali imejitahidi sana kuongeza uwezo wa watu kuwasiliana, kwa maneno mafupi ya Kiingereza ile *tele-density,* maana kwa kumbukumbu nilizonazo, mwaka 2000 *tele-density* ya Tanzania ilikuwa asilimia 39, leo hivi tuna karibu asilimia 61, hii ni jitihada kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mkongo wa Taifa unaoendelea kuwekezwa nchini kwetu na utaraboresha sana kwenye eneo hili la mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, naiomba Serikali kwa wapiga kura wangu wa Kata ya Namikupa, Maundo, Mkoreha, Naputa, Mihambwe na Chaume. Watu hawa wamekuwa wakiahidiwa kweli kwa muda mrefu kuwekewa mawasiliano ya uhakika, lakini patupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu wakati wa *Celtel,* waliahidi kule, ikaja *Zain* na sasa kama tujuavyo, Shirika sasa ni Airtel. Maeneo yale kwanza yako mpakani, ni muhimu sana

kuwa na mawasiliano mazuri. Lakini maeneo yale ni ya wazalishaji wakubwa sana wa korosho kule pembeni mwa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata wafanyabiashara wanapopita kule kununua inawawia vigumu sana na wakati mwingine wanakuwa na hela nyingi za kutosha. Lakini wakipata tatizo kidogo inakuwa ngumu sana kuwasiliana na kutafuta ulinzi wa uhakika kwa ajili ya kulinda pesa wanazokuwa nazo. Naiomba Wizara hii kwa kushirikiana na *Operators* hawa pia *UCAF* tusaidiane tuwaboreshee wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa namna moja au nyingine, naona tulikosea kidogo au tulifanya makosa kidogo. Tulipoingia kwenye teknolojia hii ya mawasiliano hatukuzingatia mambo yanayoendana nayo mambo ambayo ni ya msingi sana. Mojawapo ni lile la kuhakikisha kunakuwepo na udhibiti wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EPOCA* na Sheria ya *TCRA* Na. 12 ya mwaka 2003 ziliwekwa kama *Regulatory* tu, hakukuwa na suala la kudhibiti kwa uhakika. Matokeo yake leo kumekuwepo na mitandao mingi ya jamii inayotukana watu, kufanya uchochezi, kwenye mabenki kule *ATM* watu wanalalamika kuibiwa, lakini pia kuingilia kwa mawasiliano ile inayoitwa *Computer hacking.* Watu wamekuwa wakiathirika sana na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata utendaji wenyewe wa *TCRA,* wakati mwingine unatakiwa tujiulize mara mbili mbili, hivi kuna tatizo gani? Kwa mfano, unawaambia watu tusajili simu zetu lakini baada ya muda unakuta watu wasiokuwa *registered* wanapata nafasi ya kuwasiliana na watu wengine na kuwatukana. Hivi *TCRA* inajionaje kama mtu mwenye dhima ya kusimamia Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai hapa kwamba tuanzishe Sheria kama *computer Misuse Act, Data Protection*

*Act* ili kuimarisha udhibiti kama vile wenzetu wa nchi kama Ulaya na Marekani wanavyofanya. Hii itasaidia sana kudhibiti picha za ngono kwa watoto ile inayoitwa *child pornography.* Itasaidia sana watu kupata haki yao ya faragha na usiri kama inavyotakiwa na Katiba yetu, Sheria Mama ile Ibara ya 16(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu spika, sioni kwa nini hatuleti Sheria hizi haraka haraka maana watu waliobobea wapo akina Juma Njwayo wapo hapa wanaojua hii. Wako akina Adam Mambi wanaojua hii, wako akina Mashaka Mfala wako akina Wakili Benadeta Mkandya, kwa kuwataja wachache, tatizo ni nini? Kuwashirikisha tu hawa tukaleta sheria zitakazoweza kudhibiti kwenye eneo hilo. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kupendekeza kufanyiwa mabadiliko ya Sheria zifuatazo iil ziendane na wakati pia ziendane na teknolojia iliyoko sasa. Sheria hiyo ni ile Sheria ya Mikataba, *Law of Contract, Penal Code Cap. 16,* Sheria za Kanuni za Adhabu, *Criminal Procedure* ya mwaka 1966, *Extradition Act* ya mwaka 1965 na *Evidence Act* ya mwaka 1967.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia kuendana na teknolojia ya sasa kama nilivyosema. Kwa sababu unapotaka kufanya haki huku mambo haya yakiwa yamekaa ovyo ovyo na wewe uko *empire,* ni *Judge* au uko Mahakamani haisaidii sana kutenda haki ile inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, suala la *admissibility* ya *evidence* imekuwa ngumu kweli, hakuna *electronically* evidence *admissible* kwa sasa. Nadhani wakati umefika kufanya mabadiliko hayo ili tuendane na wakati ulioko sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba dakika tano, nafikiri nimefikisha ujumbe kwa Serikali. Nakushukuru sana. Mungu akubariki na atubariki Watanzania wote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Juma

Njwayo. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar atafuatiwa na Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita na Mheshimiwa Naibu Waziri ndiye atakayefuata. Mheshimiwa Amar!

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na uwezo wa kusimama tena ndani ya Bunge hili na kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali hii ya CCM kwa kazi nzuri ambayo inaifanya kwa kuwezesha mambo mbalimbali ikiwemo kutawanya mawasiliano katika nchi nzima. Mipango hiyo ni mizuri, nastahiki kuipongeza na kwanza kabisa naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale ni muda mrefu wameahidiwa, leo takriban miaka mitatu, lakini cha ajabu jana nimejaribu kupitia kile kitabu sikuweza kuona angalau Nyang'hwale tunaweza kupangiwa minara mingapi? Baadhi ya maeneo katika Jimbo la Nyang'hwale, Nyang'hwale tuna Kata 12, lakini ni Kata moja ambayo ina mawasiliano na kwa bahati mbaya Kata hiyo iko *centre* na maeneo yaliyozunguka yote hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii likitokea jambo la aina yoyote kule, mawasiliano ni magumu sana kupatikana mpaka waende wakapande kwenye miti, wasafiri maeneo mbalimbali kuweza kutoa taarifa ama kuwasiliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hizo ni Bukwimba, Kafita, Nyugwa, Kakola, Nijundu, Busorwa, Nyang'hwale, Shabaka, Nyabulanda, Izunya na Mwingilo. Maeneo yote hayo hayana mawasiliano. Mawasiliano ya simu hata redio ya Taifa hayasikiki vizuri na kuna maeneo hakuna kabisa taarifa za habari kupitia redio yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naiomba Serikali

hii sikivu, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, nawaomba kwa unyenyekevu angalau basi tuweze kupata hata minara mitatu katika Jimbo hili, kwa sababu nimejaribu kuangalia kwenye kile kitabu jana, kuna baadhi ya Wilaya zimeweka kupata Kata tano au nne, lakini jimbo la Nyang'hwale hatukuweza kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa unyenyekevu, ili tuweze basi angalau kuiboresha Wilaya yetu hiyo mpya kwa sababu mawasiliano ni njia moja ya kuleta maendeleo kwa haraka. Wilaya hiyo ina mambo mengi, ni wakulima wazuri, ni wafanya biashara wazuri na baadhi ya kazi mbalimbali ziko. Kwa hiyo mawasiliano ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nazungumzia mawasiliano ni muhimu, kuna maeneo ya pembezoni kule. Kuna baadhi ya zahanati ziko maeneo yale, lakini hazina madawa. Inapotokea mgonjwa inatakiwa aondoshwe maeneo yale apelekwe kwenye kituo cha afya, mawasiliano hakuna. Matokeo yake inakuwa tatizo kwa mgonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha afya kiko kimoja na maeneo mengine kuna tatizo la Polisi na wenyewe mawasiliano yao hakuna. Lakini kituo cha Polisi kiko sehemu moja, ambapo likitokea jambo la aina yoyote kwenye Kata zile zingine mawasiliano ya haraka labda ya ujambazi au matukio mbalimbali mawasiliano yanakuwa ni matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawaomba wajaribu kuliangalia Jimbo hili kwa huruma, watuhurumie. Ni muda mrefu, mwaka juzi nilizungumza, mwaka jana nimezungumza na mwaka huu nazungumza, angalau tupate minara miwili mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nyang'hwale jiografia yake kama nilivyosema ni kwamba, maeneo mengine kufikiwa kule ni matatizo sana, lakini kuna watu wengi wanafanya biashara za aina mbalimbali kule na penyewe panahitajika minara. Mfano Busolwa, Busolwa ni

eneo la muhimu sana kuna biashara mbalimbali ambazo zinafanyika. Eneo la Shabaka pamoja na Nyang'hwale, naomba maeneo hayo matatu pamoja na Bukwimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi, ninachoomba Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wamesikia kilio change, naomba angalau nipate minara mitatu katika Jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amar kwa mchango wako. Tunakushukru sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita na atafuata Mheshimiwa Naibu Waziri January Makamba. Mheshimiwa Zabein Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa safasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi unaosema, hata bubu aliongea kwa uchungu wa mwanae na alipoongea bubu maneno yalisikika na ndicho ninachotaka kukifanya leo mchana huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kondoa Kaskazini lina Kata 28 na katika Kata 15 Vijiji vyote hakuna mawasiliano ya simu kabisa. Naomba nitoe mfano tu wa hizo Kata haraka haraka, ukianzia Mungulya ambayo ni nje kidogo ya Kondoa; Kata ya Suruke, Serya, Kondomairo, Changaa, Fawi, Kikilo, Sowera, Salanka, Bereko, Kikore, Kisese, Itololo, Masange, Mnenya, Haubi, Busi, Kwadelo, Kinyasi, Itaswi, Kingale na Bumbuta, hakuna mawasiliano kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Kata hakuna minara, mawasiliano ni kutokana na minara ambayo iko Manyara. Sasa pale wananchi wakitaka kuongea, ama

wakapande kwenye majabali au miti, au vichuguu ndipo wapate mawasiliano na mawasiliano hayo siyo muda wote, mtu anaweza akatembea masafa marefu akifika hakuna mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata amani wakati Mheshimiwa Waziri alipotuambia tulete orodha ya vijiji vyote ambavyo havina mawasiliano. Nikazunguka Wilaya nzima kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani na nikawaambia wananchi ufumbuzi unakuja ndugu zangu. Aliyetamka ni mwenyewe Waziri tupeleke idadi na nimepeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa matokeo ya kupeleka orodha ya vijiji ambavyo havina mawasiliano, naomba nitoe sasa matokeo yake. Katika kijitabu hiki ukurasa wa nne Mfuko wa Mawasiliano kwa wote. Awamu ya kwanza, nilipoangalia nikakuta Kondoa Kata saba, nikasema *Alhamdulillah rabil-alamina*, nikashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naangalia sasa Kata zenyewe, katika Kata saba Kata sita si zangu, Kata moja ndiyo ya kwangu. Kata sita ni za Wilaya ya Chemba. Hivi Serikali haijui kwamba Wilaya ya Kondoa na Chemba ni vitu viwili tofauti? Huo sio uchonganishi? Huko siyo kunidhalilisha? Huko ni kunidhalilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaangalia tena ukurasa wa saba awamu ya kwanza (a), nikakuta tena Kondoa Kata tatu. Nikaangalia tena, katika Kata tatu moja ndiyo ya Kondoa, mbili Chemba, kwa maana kwamba, katika Kata 10 zilizoandikwa Kondoa, mbili ndiyo Kondoa na nane ni za Chemba. Nimesikitishwa sana na nimeumia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, wananchi wa Kondoa wakitaka kuwasiliana ni wapande miti, wapande vichuguu, wapande majabali. Naomba nitoe *experience* yangu mimi mwenyewe, maana nikisema watu

wanapanda miti Waheshimiwa Wabunge mnaweza msielewe. Mwaka 2005 nikiwa katika Kijiji cha Bereko nikapata taarifa natafutwa niongee nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wakaniambia mama twende mahali tutakuonesha utakapoweza kuongea. Wapi? Twende, tukaenda mpaka kwenye mti. Nikapanda kwenye mti na kwenye mti huo ni tawi maalum, naambiwa panda tawi hili, siyo mti wowote popote ni tawi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwa uchungu na ninachosema nasema kwa *lillahi*, nilipokwenda katika mti ule taarifa niliyopewa ni kwamba mtoto wangu, mpenzi wangu Najma amefariki. Niko juu ya mti. Najima nisamehe mwanangu, nisamehe nakutaja wakati uko mbele ya haki, nisamehe mwanangu. Nisamehe mama, nisamehe mpenzi wangu. Nikiwa juu ya mti naambiwa mwanangu amefariki. Mwenyezi Mungu akuweke mahali pema. Nasema kwa uchungu, taarifa ya mtoto wangu kufariki nimepata juu ya mti mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo huko Bereko hakuna mawasiliano, nasema kwa uchungu. Haya ninayoyasema ni ya kweli na haya nimewaeleza wakubwa. Tusaidieni mitandao toka 2005 na leo ni 2013, hapa nilipoongea kwenye mti, nikienda tena napanda naongea kwenye mti huo, namkumbuka mtoto wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo maisha ya wananchi wa Jimbo la Kaskazini ambao katika kijitabu hiki wamewekewa Kata 10. Humu ndani kuna Kata 10 Kondoa. Zile Kata mbili ni vijiji vinane. Huko Chemba ambako wameandikiwa Kondoa Kata nane Vijiji 41. Mheshimiwa Waziri ananiambia nini leo, mnawaambia nini watu wa Kondoa leo. Mnawaambia nini waajiri wangu? Mnawaeleza nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo Mheshimiwa Waziri aniambie ana mipango gani ya dharura, mipango gani

ya dhati ya kuokoa watu wa Jimbo la Kondoa Kaskazini ambao wamedhalilika kwa muda mrefu sana. Leo aniambie wananchi wa Kondoa, waajiri wangu sikilizeni majibu ya Mheshimiwa Waziri leo. Halafu mnipigie mimi, nitumieni *SMS* kwa wale ambao wana simu, msipande kwenye miti mtaanguka, msipande katika majabali mtaanguka, wale ambao kuna mtandao wanipigie waniambie nijibu nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka nukta hii naomba radhi, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita na pole sana kwa machungu makubwa.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara inafanya vizuri, wakipewa muda wataendelea kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri Serikali iendelee kusimamia gharama za kupiga simu kwa walaji. Makampuni ya Simu, *Voda, Tigo, Airtel* wana mbinu nyingi za kum-*charge* mlaji. Mara redio, mara miito, mara *promotion* za hela kila aina ambazo zinaongeza gharama kwa mlaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ambayo redio na *TV* zao zinatumia mitandao ya nchi jirani. Mfano, Mkoa wa Kilimanjaro, redio zinazosikika vizuri zaidi ni za Kenya. Nashauri Serikali iangalie maeneo ya mipakani ili wananchi wa maeneo hayo wapate taarifa na *information* kuhusu nchi yao Tanzania. Mfano maeneo ya Kagera mpakani Kilimanjaro, Tanga, Malawi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tanzania ni maskini na *information is power*. Ndio maana Mwalimu Nyerere aliitaka *Matsushita* Kampuni ya Japan watengeneze redio za mkulima ambazo *transmission* yake ilikuwa nzuri popote Tanzania. Wananchi wengi walipata habari kupitia redio hizi. Nashauri Serikali ione uwezekano wa kampuni hii

kuanza tena kutengeneza redio za kuweza kusikika hata vijijini. Siku hizi soko huria ziko redio madukani zina *band* nyingi lakini usikivu wake ni tabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TV* nazo ziwepo *Chanel* za bure ambazo mwananchi wa kawaida pale kijijini anaweza kusikiliza habari. Kuweka kodi ya kulipa kila mwezi wananchi wengi watakosa habari kwa sababu hawana kipato. Vinginevyo, redio hizo zitengenezwe tena ili ziwasaidie wananchi kupata habari. Redio za mkulima zirudi ili wananchi wapate habari vijijini, pia *channel* za bure za *TV* ziwepo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha vyuo vingi vinavyofunza watoto wetu elimu ya TEHAMA. Wakati Afrika ongezeko la idadi ya watu linaendelea kuwa kubwa, Ulaya na Amerika idadi ya watu wanaoweza kufanya kazi inazidi kuwa ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa vijana wetu kupata ajira katika idara za TEHAMA katika bara la Ulaya (mfano, Ujerumani, Uingereza, nchi za Scandinavia) na katika bara la Amerika. Ziko fununu kuwa nchi kama Ujerumani inachukua takribani vijana 400 kila mwaka kufanya kazi katika idara zao zinazohitaji utaalam wa TEHAMA. Hili linaweza pia kufanyika kwa Tanzania na hivyo kuwapatia vijana wetu ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kufuatilia utangazaji nchini. Hata hivyo, ziko redio zinatangaza kwa kutumia lugha tofauti na Kiswahili (kilugha). Hii itaweza kuwa hatari sana kwa Taifa kwa sababu kinachotangazwa wananchi wengi hawataelewa na inaweza kuchochea uvunjifu wa amani. Lugha ya Taifa hili ni Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri matangazo yote ya redio, *TV* yawe kwa Kiswahili au Kiingereza na sio tofauti (Redio Kwizera ya Ngara inatangaza kwa kilugha). Wanaokaidi wanyang’anywe leseni/ wasipewe leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za *M-Pesa*, *Tigo*

*Pesa* na kadhalika zimeongeza kodi (*fee* ya kutuma pesa) tofauti na ulivyoanza mwanzo. Inawezekana kabisa hii ni kutaka ku-*compensate* fedha ambayo Serikali inasema "Gharama za kupiga simu" zimepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali kusimamia kuona kuwa fedha inapelekwa kwa hii mitandao (Biashara hii) inalipa kodi ya Serikali ya kutosha na wakala hao wanalipa kodi, lakini pia kuona kuwa Mtanzania huyu mdogo na maskini haumii na badala yake *M-pesa, Tigo Pesa* na kadhalika iwe ni ya msaada katika biashara/shughuli/maisha ya huyu Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu kuendeleza vipaji ambavyo vimeonyeshwa na vijana wa Kitanzania. Katika maonyesho mbalimbali vijana wengi wameonyesha ubunifu wa kutengeneza vifaa vya ki-*electronic* muhimu Serikali iwafahamu na kuwasaidia vijana wa aina hii ili waendeleze wenzao hasa katika ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inasikitisha sana kutokana na bajeti kidogo sana iliyotengwa ukilinganisha na majukumu makubwa iliyonayo na pamoja na kutengewa bajeti finyu Serikali imekuwa haitoi pesa hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tuna nia ya dhati ya kutaka nchi yetu iende kasi na maendeleo ni vema Wizara hii ingepewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuhama kutoka kwenye mfumo wa Analojia kwenda mfumo wa Dijitali; naipongeza Serikali kwa kuanzisha mfumo huo wa *Digital*, lakini upo upungufu mkubwa sana uliojitokeza katika

uanzishwaji wa mfumo huo. Ningependa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu aweke wazi ili kuwaondolea wasiwasi wananchi.

(a) Gharama kubwa ya Ving'amuzi; kutokana na hali ngumu ya maisha imeonesha gharama hizi wananchi wengi hawatamudu kuwa na ving'amuzi, kwa hiyo, ile dhana ya kuwa kila mwananchi anapata haki ya kupata habari kutotimia.

Hivyo naomba Serikali itueleze imejipanga vipi kuhakikisha kuwa bei ya ving'amuzi angalau inapungua na pia ving'amuzi hivyo vinawafikia wananchi kwa wingi na kwa wakati. Tumeshuhudia wenyewe jinsi baadhi ya mikoa ilivyopata taabu na mateso ya kupanga foleni ili kupata ving'amuzi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); kutokana na kukua kwa matumizi ya mtandao katika shughuli za kijamii na kwa kuwa kumekuwa na uwazi mkubwa sana katika matumizi ya *Internet* hata kufikia wakati mwingine kutumika vibaya sana kama kuonesha picha chafu, kutuma meseji za uchochezi, kuchafuana na hata kutukana viongozi wetu kutumia mitandao na *Face book*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ajibu, Serikali imeweka utaratibu gani wa kufanya udhibiti wa matumizi hayo mabaya kwenye mitandao?

(b) Kumekuwepo na utapeli mkubwa sana unaofanyika kupitia mitandao hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Posta; bado shirika halijapatiwa kipaumbele cha kutosha kuweza kukabiliana na changamoto nyingi zilizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Simbo za Posta *(Postal Code);* mradi huu umekuwa ukitengewa pesa kidogo sana pamoja na kuwa na umuhimu sana hasa wa

kutambua anuani za makazi na Simbo za Posta ambazo ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi kiuchumi, kibiashara, kisiasa na utoaji wa huduma mbalimbali za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea sana Serikali ingekamilisha hili zoezi hata kabla ya kuanza zoezi la vitambulisho vya Taifa, kwa sababu wananchi wengi hawajui anuani zao za makazi katika vitambulisho hivyo wamefanya kukisia tu. Ni vema Serikali ingeweka wazi ni lini hasa zoezi hili litakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufadhili kwa watoto wa kike; somo la Sayansi ni somo ambalo watoto wengi wa kike wamekuwa wakiyaogopa hasa kutokana na mfumo dume ambao ulikuwa umejengeka katika nchi yetu. Je, Serikali imejiwekea mkakati gani wa kuhakikisha watoto wa kike wanasaidiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kusaidia watu wenye ulemavu; Wizara hii inawasaidia vipi, tumeona walikuja hapa Bungeni wakionesha jinsi *Computer* zinavyoweza kuwasaidia kuanza kusoma kuanzia Elimu ya Msingi. Je, katika kuanza TEHAMA katika shule za kawaida hiyo *program* itawasaidia na wenzetu wenye ulemavu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kupeleka mawasiliano katika Kata saba kati ya Kata kumi. Pia katika mpango wa kupeleka mawasiliano (A) imepanga kupeleka mawasiliano katika Kata ya Kiranjeranje katika vijiji sita. Kwa hiyo, kutegemea kupatiwa Kata nane kati ya Kata kumi katika Jimbo la Kilwa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwako ni kumalizia kupeleka katika Kata mbili (2) zilizobaki nazo ni Kata ya Likawage na Kikole. Pia katika vijiji visivyofikiwa na

mtandao katika Kata ya Pande, Vijiji vya Namwedo, Nakimwela/Mikoma, Songomnara. Kata ya Mandawa Vijiji vya Mkondaji, Kiwawa, Maraji na Mchakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia afikirie maombi yangu haya natanguliza shukrani.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na wataalam kwa kazi nzuri waliyoianzisha ya kusimamia maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiyumbishwe na maneno ya watu. Tanzania siyo kisiwa lazima tuzingatie maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kutekeleza Ndoto ya Mwalimu. Ndoto ya kuwa na Kijiji cha Sayansi- *A Science Village*. Mwalimu alikuwa na ndoto ya kuandaa watoto wadogo kuwa *great scientists* wa Taifa letu, alitafuta fedha akamteua Marehemu Profesa Shayo ili aanzishe kijiji hicho cha Sayansi, lakini bahati mbaya haikuwezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tukamuenzi Mwalimu kwa kuanzisha Kijiji hicho kwa kuwa-*identify* wototo wenye vipaji vya Sayansi na kuwa-*develop into Great Scientist.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela hakujibu ndoto ya Mwalimu kwa sababu chuo hicho kinafundisha watu wazima kwa ajili ya Shahada za Sayansi za Uzamili na Uzamivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano hafifu ya simu za mkononi Wilayani Ngara; nimeeleza kwamba Ngara inapakana na Rwanda na Burundi na hali ya usalama Burundi ni tete. Ngara inahitaji kupewa kipaumbele katika kupewa minara ya simu ili tuwe na usikivu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Wizara imefikiria Kata moja tu katika Kata zifuatazo ambazo nimeeleza kwamba hakuna usikivu. Kata za Nyakisasa, Murusagamba, Muganza, Mbuba, Mabawe, Kirushya, Ntobeye, Keza, Mngoma na Bukiriro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru sana iwapo Ngara itapewa kipaumbele kwa sababu za usalama.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu minara ya simu Wilayani Karagwe; kwa niaba ya wananchi wa Karagwe, naomba kwa mara nyingine tena na ya mwisho kuleta kilio cha wananchi wa Kijiji cha Chabuhora, maeneo ya Nono *Secondary* Kata ya Nyakabanga. Ahadi hii ni ya muda mrefu na mnara huu utasaidia kuwapa mawasiliano wananchi wa Vijiji vya Kayungu, Chabuhora, Nyakakika, Kanywamagana, Kandegesho na Kaiho. Wananchi hawa waliahidiwa kuwa mnara wa *Airtel* ungekamilika Aprili, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnara mwingine ninaouomba ni wa Kijiji cha Chamuchuzi na Kijumbura, Kata ya Bweranyange. Hawa wanapakana na nchi ya Rwanda, wanapata mawasiliano ya chini sana toka *MTN* ya Rwanda. Ahadi waliyopewa ni ya muda mrefu sana. Mnara huu utasaidia mawasiliano Vijiji vya Kijumbura, Chamuchuzi, Muguruka na Nyakasozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba mnara kwa Kijiji cha Ruhita na Misha Kata ya Rugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mnara kwa Vijiji vya Rugera, Nyarugando na Omukakajinja Kata ya Rugera.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba mnara kwa Kijiji cha Kibogoizi, Kata ya Ihembe. Kwa ufupi naomba minara mitano tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Mfuko wa Mawasiliano vijijini uje uwanufaishe wananchi wa Vijiji vya Ihembe *One*, Ihembe *two*, Nyaishozi, Nyakayanja na Bisheshe. Umeme ilikuwa ni kikwazo, lakini sasa vijiji vyote hivi vina umeme. Tuleteeni *Tele-centres* vijiji vyote hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara inayobeba majukumu makubwa, lakini ufinyu wa bajeti unapunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu hayo. Napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri na Wataalam wote wanaofanya kazi Wizarani na katika taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Wataalam katika taasisi hizo wanafanya kazi nzuri katika mazingira yasiyoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu nitaanza na matatizo ya kimawasiliano. Kwanza nikiri kuwa sekta ya mawasiliano ni sekta inayokua haraka zaidi kuliko sekta nyingine na imeleta mabadiliko chanya katika uchumi na uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kijamii. Hata hivyo, yapo matatizo na haya nitakayoyaongelea ni baadhi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na tatizo la usalama katika utumiaji wa huduma za fedha kwa mitandao au benki – mtandao. Kumekuwepo na malalamiko mengi kwamba, mtumiaji wa huduma hizi, akikosea kuingiza namba ya mtu anayemtumia fedha na fedha hiyo ikaenda kwa mtu mwingine mwenye namba iliyoingizwa, basi fedha hiyo hupotea (kwa maana kwamba ikichukuliwa na mtu mwenye namba, basi muathirika hana namna yoyote ya kuidai fedha hiyo).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia misingi ya kawaida ya maadili, jambo hili si sawa. Nashauri kuwa Wizara ikae na makampuni ya huduma za benki – mtandao ili uandaliwe utaratibu utakaosahihisha kasoro hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine la hivi karibuni lililowakumba watumiaji wa simu ni lile la mteja kuingiziwa

miito (nyimbo) bila ridhaa yake. Baadhi ya nyimbo ni mbaya na hazifai. Nashauri Wizara ishirikiane na Makampuni husika ili tatizo hili litatuliwe. Uhuru wa mteja unapaswa kulindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine linahusu hitilafu zinazojitokeza mtumiaji wa simu anapopiga simu. Hitilafu hizi hutokea katika mitandao ya *VODA, TIGO* na kadhalika. Baadhi ya hitilafu hizi ni simu kukatika wakati mtu akiongea, sauti kutosikilizika vizuri au mtu akipiga simu kupata ujumbe kwamba "Tunashindwa kutambua namba unayopiga," au "Namba unayopiga haipo," au "Namba unayopiga inatumika," na kadhalika. Makampuni ya huduma za simu yapewe taarifa ili yarekebishe dosari hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kuhusu mawasiliano linahusu minara katika Jimbo langu la Bukombe. Kwanza, nashukuru kwamba maombi ya minara katika Kata za Runzewe, Iyogelo, Butinzya/Ng'anzo (katika Kata ya zamani ya Ushirombo) yamekubaliwa. Naomba sasa michakato iliyobaki ikamilike kwa wakati ili minara hiyo ijengwe ili kuondoa kabisa tatizo la mawasiliano katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, zipo Kata nyingine ambazo bado zina matatizo ya kimawasiliano. Kata hizo ni Bukombe (Vijiji vya Ituga, Nasihukulu, Imalanguzu na Ikalanga), Namonge), Kata hii inapakana na Hifadhi ya Kigosi) na Kata ya Busonzo (Vijiji vya Nakayenze, Nampalahala na Kitongoji cha Kabagole). Kipaumbele hapa kiwe kwa Kata ya Namonge na Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongelea mawasiliano, sasa nitaongea kidogo kuhusu sayansi na teknolojia na nitaongelea mambo machache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, linahusu uhawilishaji wa sayansi na teknolojia. Katika historia ya uhawilishaji, hakuna nchi ambayo imefaulu kuhawilisha teknolojia kwa kutumia lugha ya kukopa. Kwa sababu hii, Wizara inapaswa kuwa na dira sahihi kuhusu suala hili, kwa

kuzidi kupanua matumizi ya Kiswahili katika shughuli zote za uhawilishaji (mafunzo, semina, warsha na kadhalika). *COSTECH* ianze kuandaa vitabu, vijitabu na majarida kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, linahusu athari hasi za maendeleo ya sayansi na teknolojia. Ni ukweli kuwa sayansi na teknolojia hujenga jamii yenye maisha bora. Lakini pia sayansi na teknolojia husababisha uharibifu wa mazingira. Je, *COSTECH* imeanza kuchukua hatua zipi za awali ili kushughulikia athari hasi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja na kuipongeza Wizara kwa kuongeza *Tele-Density* kutoka 39% mwaka 2009 hadi 61% mwaka 2013. Aidha mkongo wa Taifa unaendelea kuimarishwa. Cha msingi ni kuongeza jitihada ili mawasiliano yaimarike zaidi. Hata hivyo, nina mawazo ya kiushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, kwa mujibu wa *TCRA Act No. 12* ya mwaka 2003, ni wajibu wa *TCRA* kusimamia mambo yote yanayohusiana na mawasiliano kuanzia ushindani, ubora na *protection of consumers in Tanzania*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua ni kwa kiasi gani dhima hii inafanywa na *TCRA* kikwelikweli maana malalamiko ya wizi kwa *Operators* kwa watumishi wa simu ni mkubwa kwani ni kawaida maongezi kukatika katikati, ni kawaida kusikia namba unayoipigia haipo wakati jana, juzi na pengine mara kadhaa umeitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimekuwa nalalamikia Kata zangu za Mkohere, Mihambe, Naputa, Kitama, Maundo, Namikupa, Mndumbwe kutokuwa na mawasiliano ya uhakika na hakuna dalili ya kumaliza kadhia hii. Napenda kupata maelezo ya kina kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na

Wizara hii ni lini maeneo haya yatatatuliwa adha baada ya ahadi nyingi kutoka kutotimizwa na kwa kweli ahadi zisizotimizwa husumbua fikira na hivyo kuwa kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 16(1) na (2) inafafanua umuhimu wa kila mtu kuheshimiwa na kulindwa kwa mambo yake ya siri, familia yake, mambo yake ya maisha ya ndoa na mawasiliano binafsi ili mradi havunji sheria. Aidha, maendeleo ya *ICT* nchini hayatoi haki tajwa kwenye ibara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake watumiaji wa mabenki hasa kazi za *ATM* na *E-Banking* wanalalamikia wizi na kudhalilishwa, *Computer Pornography Obscene Sexual images and Fantasies* za *Internet*, kuingilia mawasiliano baina ya watu *(Hacking)* na kadhalika. Kwa nini basi uharaka usiwepo kuanzisha na kupitisha Sheria kama *Computer Misuse Act, Data Protection Act, Computer Fraud, Theft, Privacy et cetera?* Kuwepo kwa sheria hizi kutasaidia kupunguza kiwango cha uhalifu. Pia kuungana na Mataifa mengine duniani ambayo yana sheria hizo na hivyo kutia nguvu msimamo wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, dunia sasa inahitaji ushahidi wa kiteknolojia kupokelewa Mahakamani wakati Sheria yetu ya Ushahidi ya 1967 haitoi nafasi. Ni vyema mazingira wezeshi yawekwe kumudu Mahakama kutenda haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ipo haja ya kuangalia kwa ndani haja ya kifungu 124(1) ya *EPOCA,* 2010 kufanya kazi kama kilivyokusudiwa.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara nyeti ambayo imebeba wasomi (Profesa), tunategemea kupata Madaktari, Watafiti wa kilimo kutoka katika Wizara hii. Cha kushangaza bajeti inayotengewa Wizara hii ni ndogo sana, inashindwa hata kukidhi mahitaji ya vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wanafunzi wanaofaulu masomo ya Sayansi, wanafunzi hawa wanaofaulu masomo ya sayansi wamekuwa wakihangaika na hata wengine kukata tamaa ya kuendelea na masomo ya sayansi kutokana na ahadi za Serikali walizopewa kwa kuwaambia wanafunzi wa sayansi wakifaulu watawasomesha, lakini Serikali inakuwa haitekelezi ahadi zake kwa wakati muafaka. Hii inapelekea wanafunzi kukata tamaa ya kuendelea kusoma masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itahakikisha inatekeleza ahadi zake kwa wakati muafaka kwa wanafunzi wanaofaulu masomo ya sayansi bila kucheleweshewa mahitaji yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nyingi zinazokabili vyuo vikuu vya sayansi. Majengo ni chakavu, ukosefu wa vitendea kazi, hawana maabara ya kutosha na hata Maprofesa wengi wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu. Kwa mfano, Chuo cha Nelson Mandela, Chuo hiki ni kizuri na kina mandhari nzuri. Lakini bado kinakabiliwa na tatizo la miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba chuo hiki kitengewe bajeti ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya chuo hiki kwa sababu chuo hiki ni kikubwa. Nakipongeza Chuo cha Nelson Mandela kwa kusaidia shule za jirani zilizozunguka chuo hiki kwa kuwarahisishia wanafunzi kutoka Teknolojia ya analoji (TEHAMA) kwenda Teknolojia ya Dijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mawasiliano; kuna tatizo la mawasiliano baadhi ya mikoa ya Tanzania bara na Tanzania Zanzibar. Naomba Serikali ifanye utafiti wa kina katika mikoa ya Tanzania bara na Tanzania Zanzibar ili itoe uwiano wa sawa kwa sawa ili kuondoa dhana kwa wananchi, kwa kuona kama kuna mikoa inayopewa kipaumbele na wengine kusahaulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko kutoka kwa Wazanzibar kwani wamekuwa wakichangia kwenye

Makampuni ya Simu, lakini linapotokea suala zima la mawasiliano, Wazanzibari hawapewi kipaumbele (miradi ambayo inasimamiwa na Makampuni ya Simu). Namwomba Mheshimiwa Waziri, mnapogawa miradi hii ya maendeleo Zanzibar na Pemba ikumbukwe kwenye miradi hii ya utafiti na itengewe fedha ya kutosha na vile vile, Wazanzibari wasiwe ni wasindikizaji katika Wizara hii. Hospitali ya Mnazi mmoja na Chake Chake, Pemba ikumbukwe kwenye miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la malalamiko kwenye mitandao ya simu; kuna watu ambao wanawachafua wenzao kwenye mitandao ya simu. Naiomba Serikali wanaobainika kuwachafua wenzao kupitia mitandao ya simu na I*nternet* wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Makampuni ya Simu hayalipi kodi na wamekuwa wakijiingizia kipato kikubwa tofauti na kodi wanayolipa. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kukagua Makampuni ya Simu ili kubaini wale ambao wanakwepa kulipa kodi na kuwachukulia hatua za kisheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi wametoa maeneo yao kwa ajili ya kujenga minara ya simu, wananchi hao wamekuwa wakilalamika, hawalipwi malipo yao kwa wakati muafaka.

**MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri na kubwa yenye ufanisi ambayo kwa kiwango kikubwa inahakikisha nchi yetu inaendana na teknolojia ya kisasa. Aidha, nimpongeze kwa hotuba yake nzuri, lakini mafanikio yote haya bila ya jitihada ya Naibu Waziri Mheshimiwa Makamba *Dotcom Original* yasingekuwa *realized.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Serikali na taasisi walioko chini ya Wizara. Kipekee kabisa nimpongeze *Engineer* Peter Ulanga kwa kazi nzuri anayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, nichukue fursa hii kuwashukuru kwa huduma mnayotupatia sisi wananchi tulioko pembezoni. Tumepokea huduma ya simu katika Kijiji cha Kikunde na mwaka ujao wa fedha katika Kata ya Pagwi, vijiji vinne. Tunasema ahsante, lakini vile vile tuombe eneo ambalo *network* zote hazifiki ni katika Kata zifuatazo:-

(a) Msanja – vijiji vitano;

(b) Kimbe – vijiji vine;

(c) Lwande – vijiji vinne;

(d) Kwekivu – vijiji vitano;

(e) Mkindi – vijiji vitatu;

(f) Kilindi – vijiji vinne;

(g) Masagalu – vijiji vinne; na

(h) Saunyi – vijiji vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa hayo tuliyopata ila na hapa tusaidiwe *(Highlighted a serious problem need to be priority).*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niwapongeze kwa kusimamia vizuri kazi nzuri ya uwekaji wa Anuani za makazi na Misimbo ya Posta, Dar es Salaam na ni imani yangu mtaendelea kwa kasi hadi mikoani. Je, unapoweka majina ya barabara mnawasiliana na nani? Je, wanaopewa majina kwenye barabara wanalipia? Je, wanatoa ombi jina liwekwe kwenye barabara?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niombe kwa

maeneo kama Kilindi, *RTD* inashika kwa shida, mitandao nayo inahitaji umakini? Nifanyeje au nimwone nani niweze kufungua Redio Kilindi? Nitashukuru kwa mwongozo na *support*. Nawapongeza tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kupongeza juhudi na bidii za kazi zinazofanywa na Waziri pamoja na Naibu wake. Yangu ni machache tu.

(i) Serikali ikiendelea na juhudi za kuongeza matumizi ya teknolojia mashuleni, Serikali ijitahidi sana kuweka chujio la matumizi ya mtandao mashuleni na vyuoni. Kwa mfano, tunaweza kuweka mtandao vyuoni, lakini mkachuja matumizi ya *Social Network* ikiwemo *facebook, twitter* na *instagram*. Hii itazuia au kupunguza wimbi la wanafunzi wanaoingia kwenye vitendo vya ukiukaji wa maadili ikiwemo wanafunzi kuendelea kujiuza kutumia mitandao. Kwa mashirikiano na Wizara ya Elimu, ni lazima suala hili lifanyiwe kazi.

(ii) Wizi wa fedha za wananchi zimeendelea kuibiwa kwa kutumia mitandao. Katika wimbi kubwa la wizi lililofanyika, linaihusu Kampuni ya *Airtel* na hili linajulikana. Wizara kupitia *TCRA* imechukua hatua gani dhidi ya Kampuni ya *Airtel*?

Mheshimiwa Naibu Spika, imebainika wafanyakazi wengi wa *Airtel* wamekuwa sio waaminifu na wamekuwa wakishirikiana na majambazi kuwahujumu wananchi wetu. Aidha, *Airtel* imekuwa haitoi mashirikiano na Maafisa wa Polisi wanaofuatilia wafanyakazi hao. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko kwa kampuni zinazoshirikiana na majambazi kuibia fedha za wananchi.

(iii) Mitandao kwa kutumia *Websites* zenye *domain ya blogspot.com* imekuwa ni mingi sana. *Bloggers* wamekuwa ni wengi na wanaendelea kukua siku hadi siku.

Maudhui yamekuwa tofauti kwa kila mojawapo. Imefika hadi, *bloggers* wamekuwa wakidhalilishana au hata kudhalilisha watu katika jamii.

Hivi ni nani anawasimamia hawa *bloggers?* Wizara imekuwa ikielewa hili? *Blogs* nyingi zimekuwa za udhalilishaji kuliko kuelimisha. Kuna picha za utupu za watu wakiwemo wasanii zimekuwa zikionekana kwenye *blogs*. Hii inakubalika kwenye jamii yetu? Hivi tunaweza kusimamia matumizi ya mtandao wa Jamii Forum? Serikali imehujumiwa sana kupitia mtandao huu. Tuna lipi la kuzungumza, naomba tuelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Hotuba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanataka kupata takwimu sahihi kuhusu kodi inayokusanywa kutokana na Makampuni ya Simu kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Kodi inayotokana na upigaji simu.

(ii) Kodi inayotokana na utumaji pesa.

(iii) Kodi inayotokana na miito ya simu.

(iv) Kodi inayotokana na minara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuona inapata kodi kubwa ni ukweli kuwa, bado kuna wizi mkubwa unafanyika wa kukwepa kodi zinazotokana na huduma zitolewazo na kampuni za simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni lini wananchi wa Kata za (i) Uchindile (ii) Masagati (iii)Utengule (iv) Sanje (v) Mkula, Wilaya ya Kilombero zitapata mawasiliano kwani vigezo vinajitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kata hizo nilizoorodhesha hapa juu. Lakini viko vijiji ambapo mawasiliano yanapatikana kwenye Makao Makuu ya Kata tu na vijiji baadhi havina mawasiliano. Je, ni lini Serikali itapeleka minara?

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uwekaji wa anuani za makazi na misimbo ya Posta. Anuani za makazi ni muhimu sana. Ni dhahiri kwamba jambo hili muhimu lilichelewa kuanza, najua zipo juhudi zinaendelea katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa umuhimu wa anuani za makazi unajulikana, naomba Serikali inijibu lini mpango huo utakamilika Dar es Salaam? Vilevile Serikali itufahamishe mpango huu utaanza lini kutekelezwa katika nchi nzima ili kuwa na utambuzi wa sehemu za makazi na sehemu za biashara na shughuli za wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamasisha wanafunzi kusoma *science*. Natambua umuhimu wa kuhimiza watoto wa Kitanzania kusoma masomo ya *science* na natambua zipo juhudi hizo. Hii itasaidia kuwa na wanasayansi mbalimbali lakini pia Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko ya waliohitimu masomo ya *science* mfano waliosoma *Computers Science* na *Engineers* kutopata kazi, wengine hawapati kazi nzuri na kuishia kufundisha *course* fupifupi za *computers* katika vyuo vidogovidogo vya mitaani na kushindwa kutumia ujuzi wao vizuri. Hali hii huwakumba waliosoma *Computers Science*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile *Engineers* huwa *frustrated* kwa kuona walisoma masomo magumu lakini soko la ajira halitambui hilo. Hali hii huwakatisha tamaa vijana kusoma masomo ya *science*. Hivyo nashauri Serikali irekebishe kasoro hizo ndogondogo na iendelee kutoa elimu na kuhamasisha vijana wengi kusoma *science* na uhamasishaji

huo uende sambamba na kuhakikisha shule zote kuanzia za msingi zinakuwa na maabara za kisayansi na za *computer* kwani watakuwa na *base* nzuri wafikapo vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitandao ya simu maeneo ya mpakani. Nchi yetu ni kubwa lakini ni muhimu nchi nzima iwe na mawasiliano ya simu na intaneti. Mawasiliano yanasaidia katika shughuli nzima ya ulinzi na usalama wa nchi na wananchi. Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika vijiji vyake vichache vina mawasiliano ya simu lakini mtandao uliopo wa *Airtel* ni duni sana hivyo wananchi hulazimika kupanda milimani ili waweze kuwasiliana kwa simu na eneo hilo limepakana na Burundi hivyo mawasiliano ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukanda wa Kusini mwa Ziwa Tanganyika vijiji vingi havina mtandao wa simu. Kitabu Wizara ilichotoa kwenye semina kinaonyesha kijiji (kata ya Ilagala tu). Hivyo, nashauri wigo uongezwe ili eneo lote mpaka mpakani na Zambia tupate mawasiliano. Vifo vingi hutokea kwenye usafiri wa boti, kwa ajali, hivyo wakiwa na mawasiliano ya simu itarahisisha kutoa taarifa ili waokolewe itokeapo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, somo la TEHAMA katika shule za msingi na sekondari. Somo hili ni muhimu lakini kutokana na miundombinu mibovu ya shule zetu kutokuwa na umeme, maabara za kompyuta, hali inayolazimisha Walimu kufundisha kwa kuchora *computer* ubaoni. Hii haimsaidii mtoto aliye katika kijiji kisicho na umeme kwani hawezi kuelewa. Naomba Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Elimu ihakikishe miundombinu ya shule zote inarekebishwa ili zipate umeme na maabara za *computer*, ili mpango wa kusomesha somo la TEHAMA ufanikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhama kutoka kwenye analojia kwenda digitali. Baadhi ya Mikoa Tanzania ukiwemo Mkoa wa Kigoma, Televisheni ya Taifa (*TBC)* haipatikani. Nashauri Serikali ifuatilie tatizo hili ili kuondoa kasoro zilizopo ili Watanzania waweze kupata taarifa muhimu zitolewazo na Shirika hilo la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa (ving'amuzi) hasa vya *Star Times*. Watanzania waliambiwa havilipiwi kodi hivyo bei yake itakuwa nafuu, lakini bado bei ni kubwa wengi wanatamani analojia iendelee kwani hawana uwezo wa kununua au kulipia *channels*. Nashauri Serikali iangalie upya suala hili la ving'amuzi, bei ipunguzwe ili wananchi wafaidike na mpango huu mpya wa *digitali*.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja na kuipongeza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kazi nzuri sana ya kuwa na mikakati kabambe ya kuboresha huduma ya mawasiliano nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda pia kuupongeza uongozi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote [*Universal Communication Service Access Fund* (UCSAF)]. Pia kwa dhati kabisa nipongeze Wizara pamoja na mfuko wenyewe kwa namna wanavyofanya kazi, hasa kwa kutoa elimu na uhamasishaji wa hali ya juu wa kuboresha huduma ya mawasiliano na ukuzaji wa sayansi na teknolojia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbogwe ni Wilaya mpya katika Mkoa wa Geita, zipo changamoto nyingi za mawasiliano hasa ya simu katika kata za Mbogwe, Ushirika, Ilolangulu, Bukandwe na Iponya. Naipongeza sana Wizara pamoja na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(UCSAF)* kwa kuyaweka baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Mbogwe hasa Kata za Mbogwe, Bukandwe na Iponya katika mpango wa kujenga minara katika maeneo haya. Ni imani yangu kuwa Serikali itaharakisha mchakato wa ukamilishaji wa ujenzi wa minara hii ili kuboresha huduma za mawasiliano katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la mawasiliano linahusu pia kampuni ya simu ya *TTCL*, lakini ni dhahiri kuwa kampuni hii pamoja na Shirika la Posta, yamekuwa yanakabiliwa na changamoto mbalimbali hasa kutokana mabadiliko ya haraka ya sayansi na teknolojia pamoja na uwepo wa ushindani wa hali ya juu kutoka katika

makampuni mengine yaliyomo katika sekta hii hasa makampuni ya simu za mikononi kama *Airtel, Tigo, Vodacom*. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa mashirika haya yanawezeshwa kiutendaji na kimtaji ili yaweze kuendeshwa kisasa na kuhimili ushindani uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hivi sasa imeingia kwenye mawasiliano ya digitali kutoka analojia. Ni jambo jema kwa sababu dunia inaelekea huko na si vyema kuchelewa. Ziko changamoto nyingi katika kuingia katika mfumo huu lakini changamoto kubwa inayowahusu wananchi moja kwa moja ni ving'amuzi kuwa ghali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoelewa ving'amuzi hivyo vimeondolewa ushuru lakini inavyoonekana kuondoshwa kwa ushuru huko hakujasaidia kuondoa changamoto hiyo. Je, Serikali inasimamia vipi punguzo au msamaha wa ushuru huo ili athari yake iwafikie wananchi itakayowafanya wapate ving'amuzi kwa bei inayoridhisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilisema mkongo wa Taifa utakapokamilika bei au gharama za kupiga simu zitapungua sana. Mkongo wa Taifa umeenea sehemu kubwa na bado gharama ya upigaji simu hapa nchini ni kubwa mno. Serikali inasemaje kuhusu ughali huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi haiwezi kuendelea kwa kasi kubwa katika sayansi na teknlojia bila ya utafiti katika fani hiyo. Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH),* ndio Taasisi inayohusiana na utafiti na kukusanya taarifa zote za utafiti hapa nchini. Changamoto kubwa iliyopo hapa nchini katika utafiti ni fedha ndogo inayotengwa kwa ajili ya utafiti. Inashauriwa fedha inavyotakiwa itumike katika utafiti isipungue asilimia moja (1%) ya bajeti ya Serikali. Hali hiyo sivyo ilivyo. Serikali inaahidi nini katika kuipatia *COSTECH* fedha zinazostahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Wizara, ukurasa 26 aya 43, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeweza kusajili tafiti 430 kutoka nje ya nchi kwa mwaka 2012/2013. Je, ni tafiti ngapi zimesajiliwa kwa tafiti zilizofanywa hapa nchini kwa mwaka 2012/2013 na kwa nini katika Hotuba ya Waziri tafiti hizo hazikutajwa? Ahsante.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru uongozi wa Wizara hususani Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Makame Mnyaa Mbarawa na Naibu wake Mheshimiwa January Makamba kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lushoto, pamoja na shukrani zetu kwa kuongezewa mnara mmoja wa kampuni ya simu ya *Tigo* katika eneo la Kwekango, tunaomba Wizara ihimize kampuni ya *Airtel* wafunge mitambo kwenye mnara huo wa *Tigo* kwa ubia, ili wananchi wengi walio na simu za mtandao wa *Airtel* waweze kupata mawasiliano kwa urahisi kwenye maeneo ya Kwekanga, Mshangai, Mategho na Mziragembei.

Mheshimiwa Naibu Spika, usikivu wa redio usioridhisha. Wilaya ya Lushoto ipo katika milima ya Usambara. Kutokana na miinuko ya milima hiyo, usikivu wa redio ni mbaya sana. Tunaomba Wizara ihimize kampuni za redio hususani *TBC* iweze kuweka mitambo ya kuongeza usikivu wa redio Wilayani Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za simu, tunaipongeza Serikali kwa juhudi za kujenga Mkongo wa Taifa wa mawasiliano. Bado naishauri Serikali ijitahidi kusimamia ushushaji wa gharama za simu nchini kwa kuhakikisha Mkongo wa Taifa wa mawasiliano unafika Wilayani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, TEHAMA shuleni. Kwa umuhimu wa teknolojia shuleni, kuna umuhimu wa kuchukua tahadhari zote ili kulinda utamaduni wa nchi yetu na pia madhara ya teknolojia mbalimbali zinazoletwa na teknolojia mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa digitali, ni jambo jema kupata mfumo wa kisasa wa digitali, lakini mfumo huu una gharama. Tunaomba Serikali ikubali kubeba mzigo wa ving'amuzi. Mfuko wa Mawasiliano usaidie katika kutoa ruzuku ya kulipia ving'amuzi ili vitolewe bure wakati wa kununua *TV* na kufidia wale ambao wamekwishanunua *TV*. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake kwa kazi kubwa wanayofanya kwenye Wizara hii, pamoja na kuandaa Hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati Wizara hii ilifanya semina kwa Wabunge kuhusu kuanza rasmi kwa mfumo wa digitali na kuhama kwenye mfumo wa analojia, walitueleza kwamba bei ya ving'amuzi itakuwa nafuu (*affordable*) ili Watanzania wengi waweze kumudu na kuendelea kupata habari. Ving'amuzi vimepanda kutoka shilingi 38,000/= mwaka 2012 na kufika shilingi 70,000/ = mpaka shilingi 80,000/= mwaka 2013, Watanzania wengi wameshindwa kununua na hivyo kukosa habari. Serikali itoe maelezo hali hii imesababishwa na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa wale walioweza kununua ving'amuzi vyote ni vya viwango vidogo (*low quality*). Hatupati habari kwa uhakika. Taarifa ya habari inakatika zaidi ya mara nne na hivyo kutokupata taarifa kamili. Serikali imejifunza nini kutokana na upungufu wa mfumo huu mpya? Ni hatua gani zinachukuliwa kuondoa tatizo hilo la ving'amuzi kutokuwa *efficiency* na kuleta kero?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza tangu utaratibu wa kusajili simu hapa nchini uanze mwaka 2007 mpaka leo Serikali imeshindwa kuhakikisha zoezi linakamilika na kwa ufanisi. Ni Tanzania pekee ambapo *simcard* zinauzwa kama njugu huko mitaani. Matokeo yake udhibiti wa matumizi ya simu umeshindikana. Simu zinatumiwa kuiba fedha kwenye mabenki na taasisi nyingine za fedha. Simu zinatumika kutoa matusi kwa viongozi na watumiaji

wakitafutwa, wanakuwa wametupa *simcard* mbali hawapatikani. Simu zinatumika kuandaa uharamia, ujambazi na matukio mengi ya uhalifu. Huu ni udhaifu mkubwa sana kwa kuwa na wataalamu kwenye Wizara hii wameshindwa kushughulikia jambo hili, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni ya simu yanafanya wizi na ujambazi mkubwa sana kuiba hela za wateja kwa kutumia mawasiliano ya simu za mikononi kwa kujua hakuna anayefuatilia watu wanahangaika. Tunahitaji majibu ya Serikali kwa haya yafuatayo:-

(i) *Message* zinazotumwa kwenye simu kwamba umeomba wimbo na utakatwa fedha kiasi fulani mfano shilingi 410, shilingi 370, shilingi 210, kwa mwezi wakati hujaomba wimbo na baada ya wiki wakiona umeweka vocha wanatuma tena ujumbe huu.

(ii) Wateja kukatwa pesa nyingi wakati unapiga simu, ikianza tu kuita, hata unayempigia asipopatikana tayari unakatwa pesa wakati huduma hujapata. Huu ni wizi.

(iii) Serikali kusoma hapa Bungeni kwamba gharama za mawasiliano ya simu zimepungua tangu Januari, 2013 wakati sisi tunaona gharama bado ziko juu sana kutokana na makato kuwa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba tozo kuchangia Mfuko wa Mawasiliano *(UCAF)* litaongezeka kutoka 0.3% hadi kufika asilimia 0.15%. Serikali itoe ufafanuzi kuongezeka kwa tozo hizi, hakutaongeza gharama za mawasiliano kwa wananchi? Ikiwa tozo hizo mzigo utapelekwa kwenye makampuni ya simu ni dhahiri kuwa gharama zote zitahamishiwa kwa walaji (wateja) na hivyo gharama za maongezi zitapanda na kuongeza ugumu wa maisha kwa Watanzania kwani mawasiliano ni nyenzo mojawapo ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni ya simu yahakikishe minara wanayoweka kwenye makazi ya watu

iwe inalinda mazingira na kujali jamii wanaoishi maeneo hayo. Minara inaunguruma ni kwa nini wakati ipo minara ambayo haitoi makelele? Makampuni yahakikishe na Serikali ifuatilie hili minara ya simu inufaishe jamii inayozunguka maeneo hayo (wao ndio walinzi) na sio fedha na minara kupewa watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata za Wilaya ya Kaliua ambazo hazina mawasiliano na hazipo kwenye kitabu/ mpango ambazo ni Kata ya kilometa 60, kilometa 34, Uyumbu, Tarafa ya Uliyankuru, Kata za Kanoge, Sasu, Simbo na Uyoa, Tarafa ya Usoke, Kata za Usoke Mlimani, Kiloloni na Uyumbu. Kata ya Usinge – vijiji vya Kombe, Maboha, Shela na Malanga.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii angalau nami niweze kutoa mchango wangu kwa njia hii ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nitoe pongezi kwa watendaji wote wa Wizara hii, nikianza na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote na Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii. Kweli kazi wanayoifanya ni nzuri na matunda yanaonekana. Pamoja na hayo penye maendeleo hapakosi changamoto, hivyo ni vema wakatambua na kuzifanyia kazi kwa faida ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitandao ya simu. Suala la mitandao ya simu limekuwa ni suala muhimu sana hapa nchini, kwani limesaidia kuongeza kasi ya maendeleo. Hivyo natoa shukrani na pongezi kwa mitandao yote kupitia Wizara, kwani mawasiliano yamerahisisha hata wafanyabiashara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo kwa kazi nzuri ya mitandao ya simu Tanzania, bado kuna tatizo kubwa sana kwa suala la kukatwa fedha bila sababu ya msingi. Kwani unalazimishwa kulipia kitu ambacho hukutaka mfano, malipo ya milio au nyimbo hali ukiwa hujaomba.

Ushauri wangu ni kwamba waweke utaratibu wa kununua milio hiyo kama walivyoweka kwenye ununuzi wa salio yaani kuwe na *process* ya mtu kujiridhisha anachotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni yanayoweka mikataba na wasanii kuhusu kazi zao, bado mikataba ile inakiukwa, pia haiko rafiki na msanii na haitekelezeki. Mfano, mkataba unasema kuwa unapopeleka wimbo wako na kuingia mkataba na kampuni hiyo, sharti la kwanza hutakiwi kuingia mkataba na kampuni nyingine kwa wimbo wowote ule hata ukitunga mwingine, kwa kipindi cha miaka kumi (10).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia utaanza kupokea malipo yako baada ya miezi mitatu na kila mwezi utaendelea kupata lakini bado utakuwa hupati fedha yoyote hata kama unasikia wimbo wako uko hewani. Kweli jambo hili ni dhambi na ni dhuluma ya hali ya juu. Hivyo ombi langu, naomba suala hili wakabidhiwe *TCRA* kwa kushirikiana na *COSOTA*, kwani ninaimani na *TCRA* maana wako makini kwa kazi zao na utendaji wao ni wa kiwango cha juu, naamini watatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa Sheria iko wazi kwamba, msanii ambaye wimbo wake utatumika anatakiwa apate asilimia kumi (10%) ya pato la mauzo la wimbo/kazi yake. Naomba hili *TCRA* watakapokabidhiwa wazingatie na ingependeza gawio hili lilipwe moja kwa moja toka kwa *operator* mwenyewe kwenda kwa msanii asipewe kampuni zilizokusanya kazi hizo; kampuni hiyo ipewe chake tu kulingana na makubaliano yao na *operator*. Nasisitiza *TCRA* ijengewe uwezo na iachiwe jukumu hili naamini litatatuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TV*, Radio na vyombo vyote vya utangazaji. Tafadhali naomba sana vyombo hivi vimekuwa vikikwepa kulipa mrahaba wa kazi zote za sanaa wanazotumia ambao hutakiwa walipe *COSOTA* na msanii atapata kule. Cha kusikitisha, hata TV ya Taifa *TBC* hawaonyeshi hata mfano mzuri wa kulipa mrahaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba sana kwa kuwa *TCRA* ndio wanaotoa leseni kwa vyombo hivi,

watusaidie kuvibana na waweke utaratibu utakaowadhibiti. Naamini *TCRA* wakiwezeshwa, watapata tu mitambo ya kisasa itakayosoma moja kwa moja kwamba TV/Radio wametumia kazi zipi na kiasi gani na za msanii yupi. Naomba hilo Mheshimiwa Waziri tusaidie. Naamini atatusaidia kwani utendaji wake wa kazi nimeshauona na ni mtu aliye makini pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli wanastahili pongezi kwani kwa mawasiliano tu, mambo yamekuwa mazuri maana hata babu yangu kule kijijini akitaka kuuza ng'ombe wake, anapiga ili niongee na wateja wake ili wasimdhulumu, pia namtumia fedha bila wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *M-Pesa* zimekuwa ni Bank mbadala kwa matumizi ya muda mfupi na hata mrefu na wanaosafiri siku hizi hawabebi hela kwenye mikoba zote zinakaa kwenye simu hata ukiibiwa simu, bado fedha zako zitakuwa salama, pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila marekebisho kidogo, hebu warekebishe kidogo kwenye utumiaji wa *M-Pesa* hasa pale unapojikuta umekosea namba na hela zikaenda kwa mtu ambaye siye, pale utaona jina tu, namba haitatokea na kwa kuwa utakuwa umekosea namba, hutakumbuka umeandika namba gani, hivyo inakuwa vigumu kumpigia ili umwambie arudishe. Mtu amekosea namba, fedha zikaingia kwako inakuwa vigumu kumpata kwani linaonekana jina tu bila namba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni vema namba na jina vikaambatana. Mfano Mei 24, 2013 saa saba mchana, nilituma shilingi 45,000/= kwa jina la Abdallah Abdallah lakini namba haikusomeka na sikumbuki nilibonyeza namba gani. Nilipogundua kuwa nimekosea, niliwaomba *Voda* wanisaidie irudi, lakini bahati mbaya wakasema, ndani ya dakika tano (5) Abdallah Abdallah akawa ameitumia wakaishia kusema umeibiwa. Sasa, kuna utaratibu gani wa kesi kama hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nitoe

shukrani za dhati kwa *innovative clusters* na hasa kuitambua Singida, Manyoni na kadhalika katika suala la usindikaji wa mafuta ya alizeti na asali pia. Mtakapoendelea zaidi kuhusu kuku, msisite kuja Singida kuna kuku wa kumwaga kule na ni watamu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara hii naunga mkono asilimia mia moja. Sababu za msingi za kuunga mkono Wizara hii, ni kutokana na imani kubwa niliyonayo kwa viongozi wote wa Wizara hii Mheshimiwa Waziri na Naibu wake Mheshimiwa January Makamba. Sababu nyingine ni uwezo wao mkubwa walio nao katika kuiongoza Wizara hii na hata wanavyohangaika kutafuta kila njia ya kuhakikisha suala la mawasiliano linatekelezwa katika maeneo yote nchini, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufafanuliwa ni namna gani Halmshauri za Wilaya zinanufaika na minara ya simu iliyofungwa katika maeneo yao, toa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mtumiaji wa simu asilipwe fidia kutokana na *message* zinazotumwa katika simu zikiwa na matangazo ya kibiashara? Kwani zinasababisha kumaliza *charge* wakati ku-*charge* simu ni gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza kabisa nilikuwa mtu wa kwanza kufika katika ofisi ya Mheshimiwa Waziri kueleza shida ya ukosefu wa mawasiliano katika Jimbo langu. Namshukuru Mheshimiwa Waziri alinijibu vizuri tena kwa maandishi ambayo nilitumia barua hiyo kutuliza wananchi katika mikutano ya hadhara na wananchi walijenga imani kubwa na Serikali. Cha ajabu hadi leo hii vijiji vyangu vimewekwa katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielezwe nini kinasababisha nibakizwe nyuma kiasi hicho pamoja na mawasiliano ya mara kwa mara na viongozi wangu hawa?

Naomba muwaeleze wapiga kura wangu kwa nini? Mimi sieleweki kwani hata kijiji ninachotoka cha Milepa hakuna mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia tena kuorodhesha maeneo yasiyo na mtandao Kata ya Milepa vijiji vya Milepa, Kisa na Msia, Kata ya kaoze vijiji vya Chombe, Tuluhu, Kianda Ogonda na Kapenta, Kata ya Kipeta vijiji vya Kirando, Ilambo, Kilangawane na Mpona, Kata mpya ya Mfinga vijiji vya Mfinga, Msila, Mtapenda na Kasekela.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ni miongoni mwa Wizara ambazo zina uwezo mkubwa wa kuingiza pato la Taifa kupitia sekta ya mawasiliano. Mawasiliano ni maendeleo, mawasiliano ni uchumi na mawasiliano yanaharakisha upatikanaji wa habari ziwe za faraja au za majanga kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inakosa mapato mengi yatokanayo na matumizi ya simu hili linatokana na Serikali pamoja na watendaji kutokuwa makini katika ufuatiliaji wa matumizi ya simu. Ni aibu kwa nchi kama Tanzania kushindwa kuingiza mapato zaidi yatokanayo na mawasiliano ya simu na nchi kama Rwanda na Burundi nchi ambazo wastani wa watu wake si nusu ya watu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala zima la utumiaji wa ving'amuzi toka mfumo analojia na kuingia katika mfumo wa digitali umekuwa kikwazo kwa Watanzania walio wengi kutokana na uwezo wao hivyo ni vyema Serikali ikalianzisha jambo hili kwa kutumia busara ili ufanisi uweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hawana matatizo ya kutumia mfumo mpya wa digitali hata hivyo

wanahitaji kupatiwa elimu na muda wa kutosha kuwatoa kwenye mazoea ya awali wa analojia na kuwapeleka kwenye mfumo mpya wa digitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado siamini kabisa kwamba Wizara hii itaweza kufanya kazi zake kama ilivyokadiriwa kutokana na uhaba wa bajeti iliyopangiwa kwani inavyoelekea kila mwaka bajeti ya Wizara hii inaendelea kushuka. Napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili ni maajabu gani ambayo watayafanya ili waweze kutekeleza maazimio yote waliyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wajibu vilevile kupitia Wizara hii kuangalia namna Posta zetu zinavyofanya kazi hapa nchini. Vilevile tujiulize imesomesha Watanzania wangapi ambao wamepata elimu ya kuelimisha Watanzania wengine ili utumishi wao uwe wa kuigwa na pia kutoa elimu itakayoweza kuwasaidia Watanzania wa sasa na wa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua fika kwamba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ni watu wenye uwezo wa kufuatilia shughuli zao za kazi hata hivyo wasiwasi wangu ni vikwazo vitakavyowakwaza kutokana na utendaji wao walio chini, hivyo Wizara inawajibu wa kuangalia utendaji wa kila mmoja, ili kuwaepusha wale ambao hawastahili lawama kutupiwa maneno yasiyo na msingi.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ni tatizo kubwa katika Wizara hii, miradi mingi ya maendeleo haifikii malengo yake kwani mpaka leo hii mwezi wa Juni tunakaribia kumaliza mwaka wa fedha Wizara imepatiwa asilimia 46 tu. Ushauri wangu fedha zitolewe kwa wakati ili wapate kukamilisha miradi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Mamlaka ya *TCRA* kwa juhudi zao mbalimbali kuendeleza mamlaka hii

lakini kumekuwa na tatizo moja kubwa ambalo watu wengi wanalipigia kelele kuhusu utoaji wa laini za simu (*sim card*) ovyoovyo ambazo zinatumika kwa matumizi yaliyokuwa si mazuri kama kuwatukana watu na mambo mengi yaliokuwa si mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu sehemu nyingi ulimwenguni mtu yeyote anayetaka laini ya simu lazima uoneshe vitambulisho vyake kama yuko halali katika nchi ile halafu baada ya muda akithibitika ndio anapatiwa hiyo '*simcard*'sasa hapa kwetu tofauti zinauzwa njiani tu kama nyugu. Hii ndio sababu kubwa inayosababisha matumizi mabaya ya laini hizo za simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara pamoja na *TCRA* wawe na msimamo madhubuti wa matumizi ya laini za simu. Sasa umefika wakati kwa nchi yetu kuwa na Sheria kali mbalimbali zinazohusu matumizi ya mitandao maana wizi wa mitandao umekuwa mkubwa, matumizi mabaya yanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itimize ahadi yake ya kuipa1% ya pato lake Wizara hii ili tupate kufanyiwa utafiti.Kama unavyojua utafiti ndio chanzo kikubwa cha maendeleo.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi hii, nami niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 2013/2014. Napenda pia kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Bajeti yake nzuri, iliyoandaliwa kwa umakini mkubwa ili kukidhi mahitaji na kukabiliana na changamoto katika Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali katika juhudi zake za kimkakati katika Sera nzuri kwenye uboreshaji wa Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Kufanya hivyo, kumesaidia kuinua Sekta hizo katika kiwango cha kuridhisha ingawa changamoto ni nyingi

ambazo Serikali haina budi kukabiliana nazo. Kuwa na wingi wa matumizi ya simu za mikononi ni sehemu ya maendeleo katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano imekuwa na changamoto nyingi; tumekuwa na makampuni ya huduma za mawasiliano tofauti tofauti na kutoa huduma nchini lakini kumekuwa kuna tatizo la makampuni haya kila baada ya muda kubadilisha majina ya kampuni zao. Naiomba Serikali kupitia Wizara hii, kutueleza sababu za msingi za kupelekea makampuni haya kubadilisha majina kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matatizo tofauti tofauti kwa makampuni haya, mengine gharama zake ziko juu na mengine chini ilhali watumiaji wa huduma za mawasiliano ni wale wale. Hali hiyo hufikia kumwumiza Mwananchi. Ingawa Serikali imekuja na mkakati wa kurekebisha tatizo hilo, lakini naomba marekebisho hayo kwenda kwa haraka ili kumwokoa Mwananchi huyu asiendelee kuumia na hizi gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Sheria katika Sekta ya Mawasiliano lazima zirekebishwe, kwani kuna baadhi ya makampuni yamekuwa yakinufaika zaidi na kuipunja Serikali mapato. Kufanya hivyo kutakuwa kumeisaidia Serikali kuokoa kiasi kikubwa ambacho kilikuwa kinapotea. Wizara kupitia Taasisi zake, waweke utaratibu ambao utakuwa ukifuatilia makampuni haya kubaini pale watakapokuwa wanaenda kinyume cha sheria na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika namna ya kipekee, napenda kuyapongeza Makampuni ya Simu za Mikononi, kwa jitihada zao za kupanua huduma za mawasiliano ya simu hadi vijijini. Makampuni haya yamechangia kuboresha maisha ya Watanzania kwa kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania, kwa ajira ya moja kwa moja au kwa kupitia biashara zinazotokana na huduma za simu, pia kudhamini shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kutokana na umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo ya nchi yetu, katika Jimbo la Kibaha Vijijini tuna matatizo makubwa ya mawasiliano. Kwa mara nyingine nalizungumzia hili kwani nilishaiandikia Wizara barua juu ya jambo hili. Tumekuwa na matatizo ya mawasiliano katika maeneo yafuatayo:-

Kata za Magindu, Lukenge, Miombo, Mkonga, Mzizima, Gwata, Gumba na Kigoda, Soga, Vikuge, Ngoingo, Misufini, Kipangege, Boko, Mnemela, Mpiji, Mkarambati na Kibaoni, Kata ya Ruvu, *Ruvu Station*, Minazi Mikinda, Mnazi Lubungo na Kitomondo, Kata ya Kwala, Dutumi, Madege, Mwembe Ngozi, Msua, Mpera Mumbi na *Kwala Station*.

Matatizo haya yamekuwa ya muda mrefu sana, kwa msingi huo, kama nchi yetu inataka kupiga hatua ya maendeleo kwa haraka, ni lazima mawasiliano yapatikane kwa watu wote, kwa wakati wote na kwa gharama wanayoweza kumudu. Kwa sasa hali haiko hivyo, kwani maeneo mengi nchini hakuna mitandao ya simu za mikononi kama nilivyoeleza hapo awali, bei ya kupiga ni kubwa hasa kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara itafute ufumbuzi wa kukosekana kwa mawasiliano ya uhakika katika Kata hizo Jimbo la Kibaha Vijijini. Vilevile naishauri Serikali kuyashawishi makampuni ya simu kuondoa gharama za kupiga simu kati ya mtandao mmoja na mwingine *(Interconnection Charges).* Kuondoa gharama hizi kutawapunguzia Wananchi kutumia simu zaidi ya moja, pia nayashauri makampuni ya simu kushindana kwa bei zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Vyuo vya Serikali viliyojikita katika kutoa Shahada za Sayansi na Uhandisi hapa nchini ni Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela Arusha. Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo hivi vina Wataalam wengi wenye sifa za kihandisi na wanaweza kubuni vitu

mbalimbali na kufanya tafiti zinazoweza kuwa na manufaa kwa jamii ili kuepuka kutegemea Wataalam na wabunifu kutoka vyuo na taasisi hizi na watumiaji wa utaalam huo katika jamii. Aidha, kwa kuwa Taasisi hizi zinafanya kazi zinazofanana, ziunganishwe kwenye mtandao ili kubadilishana uzoefu na kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza sana, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa juhudi wanazozifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Waheshimiwa Mawaziri hawa, bado kuna changamoto nyingi sana katika maeneo ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate majibu kutoka kwa Serikali katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Jimbo la Mufindi Kaskazini lina Kata 15 na Vijiji 78, lakini zaidi ya Vijiji 24 havina mawasiliano kabisa. Kwa mfano, Kata nzima ya Mpanga Tazara na haimo katika programu za kupata mawasiliano hivi karibuni. Kata ya Ikwaha yenye vijiji vine; Kata ya Mapanda yenye vijiji vitano; Kata ya Ihamu yenye vijiji sita hasa Vijiji vya Isipii na Lulanda; Kata ya Isalavanu Vijiji vya Kikombo na Uguto. Je, lini Serikali itaona kuna umuhimu wa kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo?

Pili, kuna malalamiko yapo kati ya Wilaya ya Mufindi na Wilaya ya Mbarali kuhusu mnara uliojengwa Kijiji cha Igomaa kuwa upo Wilaya ya Mbarali Mkoa wa Mbeya wakati upo Mufindi Mkoa wa Iringa na mapato yanayotokana na mnara huo yanalipwa Mbarali. Tunataka tamko la Serikali kwa sababu kumekuwa na mgogoro mkubwa ambao unaendelea kukua siku hadi siku.

Tatu, ni vyema Serikali ikatoa mwongozo kuhusu mapato yanayopatikana kutokana na ujenzi wa minara, kueleza Vijiji na Halmashauri wapate asilimia ngapi.

Nne, Makampuni ya Mawasiliano yanapata mapato makubwa sana kutokana na huduma wanazozitoa kwenye mawasiliano na *transactions* zingine za kibiashara kama *MPESA, TIGOPESA* na kadhalika. Ni vyema Serikali ikazibana kampuni hizi zisaidie kuboresha huduma kuliko zilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja ya bajeti hii ili wapate pesa wakasaidie kupeleka mawasiliano katika maeneo tunayoyalalamikia.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza safu yote ya Uongozi wa Kisiasa na Kitaalam Wizarani na kwenye Taasisi zilizo chini ya Wizara hii; ni Uongozi mahiri, makini, usiokuwa wa kubabaisha wala kubahatisha. Naifahamu safu kwa kuwa nimefanya nayo kazi nilipokuwa Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu; hongereni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nyuma Waheshimiwa Wabunge, tuliagizwa kuorodhesha maeneo yote katika Majimbo yetu yenye matatizo ama yasiyokuwa na mitandao ya simu. Niliorodhesha katika Jimbo langu la Magu, Tarafa nzima ya Ndagalu, yenye Kata nne za Ng'haya, Nkunghulu, Jinjimili na Shishani, hakuna hata mnara mmoja. Mnara pekee uliopo wa *VODACOM* uko kwenye mpaka wa Kata ya Ng'haya na Kata ya Kasoli (Wilaya ya Bariadi), katika Kijiji cha Salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza, katika mpango wa mawasiliano kwa wote, unaofadhiliwa na *World Bank* na ule unaotekelezwa kwa fedha za Serikali (1A na 1B), Tarafa ya Ndagalu, kwa maana ya Kata nilizozitaja hapo juu, haimo. Kwa nini Tarafa hii imeachwa wakati kiukweli ni Tarafa yenye wakazi wengi sana, ina uchumi ulio juu, minada miwili mikubwa katika vijiji vya Mahaha na Kabila; na Tarafa hii huchangia (inaongoza) kiasi kikubwa sana cha mapato ya Serikali Wilayani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Tarafa hii nayo iingizwe kwenye orodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DAVID Z. KAFULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuona Kata za Sunuka, Sigunga na Ikagala, zimeingizwa kwenye mipango na ratiba ya Wizara yako. Naomba kusisitiza utekelezaji uwe wa ufanisi na uendane na ratiba, kwani Kata hizi zipo mpakani Ukanda wa Ziwa ambao upo wazi na kuna tatizo kubwa la kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kalya na Kata ya Mtego hazipo kwenye mpango wowote kwa kadiri nilivyosoma kitabu kilichotolewa kwenye semina jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusisitiza hasa kuhusu Kata ya Kalya, kwani hii ndiyo Kata inayopakana na DRC na hapa kuna *cases* nyingi za kukamatwa silaha zinazoingizwa kiharamia kutoka DRC. Nashauri sana hata kwa dharura, Kata hii ipatiwe mawasiliano, kwani Polisi wanapata shida sana kuhakikisha ulinzi eneo hili. Hata kikosi cha Jeshi (JWTZ), waliopo eneo hili wanalalamika sana kuhusu simu eneo hili, kwani mpaka ni mrefu na upo wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mtego imezungukwa na Kata zenye simu isipokuwa yenyewe tu. Naomba sana kwani wateja ni wengi, ni Kata ya miaka mingi na ina idadi ya watu inayofikia 15,000 na kuna shughuli nyingi za biashara na kilimo cha Tumbaku na wote wana fedha kumudu gharama za simu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara na Mawaziri wake, kwa jitihada kubwa wanazofanya katika utekelezaji wa majukumu yao pamoja na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la maeneo mengi hasa eneo la Kilwa Kaskazini; nachukua nafasi

hii, kuishukuru Serikali kwa ahadi ya kujenga minara katika Jimbo la Kilwa Kaskazini kama Mitole, Chumo, Kandawale, Kipatimu. Naiomba na kuisisitiza Serikali kuharakisha mchakato kwa utekelezaji wa miradi hii hasa kwa kuzingatia ni ahadi ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kuhusu mitandao ya simu kuzidisha makato kwa watumiaji wake. Serikali iharakishe ufungaji wa mtambo wa kuifuatilia mitambo ya simu. Hii itasaidia pia kudhibiti mapato yanayodhaniwa kukwepwa kulipwa na wamiliki wa kampuni za simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu *COSTECH* wamekuwa wakifanya tafiti nyingi ambazo hazitumiwi ipasavyo. Licha ya hayo, bado naishauri Serikali kuendelea kuijengea uwezo na kuipa kasma ya kutosha ili iongeze ufanisi kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ni pamoja na kuhakikisha kwamba, vyombo vya mawasiliano ikiwemo simu za mkononi, vinatumika vizuri. Kwa masikitiko makubwa, imeonekana kwamba, *TCRA* imeshindwa kutimiza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inajidhihirisha kutokana na *sms* zinazotumwa na baadhi ya watu nchini, zikiwa na *element* za uchochezi na kuzidisha migogoro ya kidini na uhalifu nchini. *Sms* hizi ambazo waanzilishi wake wanajulikana vizuri sana na *TCRA*, zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku huku watumiaji wa *sms* hizi wakitoa ushawishi kwa wenzao wanaowatumia kwamba nao watume kwa watu kumi au mia moja.

Kwa utaratibu huu wa kusambaza ujumbe wa namna hii, matokeo yake kila mtu huhamasisha chuki kwa watu kumi au mia moja ambao hao huhamasisha kumi au mia moja kila mmoja na huo mlolongo huendelea kukua kila kukicha; mwisho wa siku maelfu ya watu huingia katika zoezi hili ambalo ni baya kabisa katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizi si mpya kwa *TCRA* maana wengi wamekuwa wakitoa taarifa huko, lakini mpaka sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kuhusu tabia hii chafu. Kwa nini *TCRA* imekuwa ikizembea tatizo hili? Je, tuamini kwamba *TCRA* nao ni sehemu ya mpango huu ovu unaoligawa Taifa letu? Naitaka Serikali itoe tamko kali kwa *TCRA* pamoja na kwa wale wanaohatarisha amani na kuleta uchochezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kupiga simu na *internet* bado ziko juu sana.  Pamoja na Serikali kujirudi kwamba, zimepungua kwa kiasi kikubwa, Tanzania bado ni nchi ambayo gharama za kupiga simu ziko juu kupita nchi zingine za Afrika Mashariki. Gharama za *internet* pia bado ziko juu sana na kuwafanya Wananchi walio wengi kushindwa kumudu kuzitumia. Ni wakati mwafaka sasa kwa Serikali kutoa tamko la kiutendaji na si la kisiasa, kwa makampuni ya simu ili kushusha gharama zake na hatimaye Wananchi waweze kufaidika nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuboresha upatikanaji wa habari na kujiondoa kutoka katika kutumia analojia na kuanza kutumia dijitali, mpango huu bado ni wa kinyonyaji kwani Wananchi wengi wanashindwa kununua ving'amuzi hivi kutokana na bei zake kuwa kubwa na huku zikitofautiana kati ya kampuni na kampuni. Wananchi wangependa kupata habari mbalimbali kwa bei nafuu hasa wanaponunua *airtime* kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei hizi ni kubwa kwa Mwananchi wa kawaida hasa ukizingatia ukweli kwamba, wengi hutegemea umeme wa Gridi ya Taifa na umeme huu hukatika mara kwa mara na hivyo kumfanya Mwananchi

kutonufaika na pesa aliyonunulia *airtime* akitegemea kupata habari kwa muda wa mwezi mzima. Hali haiwi hivyo maana kwa mwezi anaweza kuangalia *TV* kwa wiki mara mbili tu na zingine zinapotea kutokana na kukatika kwa umeme. Ni wajibu wa Serikali kuwa *fair* katika kuwanufaisha Wananchi wake pamoja na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. HAJI HUSSEIN MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ninasikitishwa na mwendelezo wa kutenga bajeti finyu kwa Wizara, hivyo kuifanya kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)*, bado haujafanikisha malengo yake ya kuzifikia sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara ya mawasiliano, licha ya umri mkubwa uliokuwa nao (takribani miaka minane). Sababu kubwa kwa hili ni kukosekana kwa utayari wa wadau, watoa huduma, ambao wengi ni makampuni binafsi ya kibiashara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ruzuku iliyotengwa katika Kata 152 zikiwemo Kata za Iragua, Itete, Sofi, Ngoheranga na Kilosa Mpepo Wilayani Ulanga, lakini bado makampuni haya binafsi wanashindwa kupeleka huduma za mawasiliano katika Kata hizo kwa kisingizio cha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kwamba, pamoja na karoti (ruzuku) walizotoa kwa makampuni haya ili yashawishike kufikia Kata hizi 152, lakini pia watumie mbinu zingine kama vile kutoa masharti ya leseni katika biashara za mawasiliano ili kuwabana watoa huduma wasambaze huduma zao katika sehemu za vijijini na hasa zile zisizokuwa na mvuto wa kibiashara, yaani Serikali kwa changamoto hii watumie mfumo wa *Carrot and Stick,* kwani hii ni nchi yetu, tusiwaachie wafanyabiashara peke yao kuendesha biashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa madhumuni ya kufanyika kwa tafiti ni kwa ajili ya kuboresha na kuendeleza maendeleo ya kisayansi, ambayo yanasaidia sana katika kuongeza ujuzi na utaalam kwa nchi yetu. Je, ni tafiti ngapi zimefanywa chini ya Wizara hii na ni ngapi zimefanyiwa *application* na kutumiwa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu; na je, kuna utaratibu gani wa kuzi-*expose* tafiti hizo na kuzitangaza kwa watumiaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Watanzania hapa nchini, wanaofanya tafiti mbalimbali kwa kujigharamia wao binafsi. Tafiti nyingine za kisayansi zipo zilizofanikiwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha watafiti binafsi wanaofanya tafiti mbalimbali kwa kujigharamia wao wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalifu wa mtandao umeendelea kutumika na kukua kwa kiwango kikubwa. Wapo Wananchi wasiojali, wametumia *internet* kufanya uhalifu bila kujali huku wakijua hawatachukuliwa hatua zozote. Serikali iweke sheria ya kudhibiti matumizi mabaya ya *internet* ili wale wote watakaogundullika kufanya uhalifu kwa njia ya mtandao, waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa simu za viganjani zimetumika kuhamisha fedha na kutuma fedha na kulipia malipo mbalimbali kama vile kununua umeme, kulipia bili za maji na kadhalika. Hata hivyo, biashara hiyo inayofanywa na makampumi ya simu kwa faida kubwa sana, Serikali haipati chochote kwani hakuna ushahidi kwamba makampuni hayo yanalipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wamekuwa wakilipa kodi kubwa sana *(PAYE)* huku wafanyakazi wa kampuni za simu wakiachwa kufanya huduma za kibenki kwa kutumia simu za viganjani bila kulipa kodi, huku ikijulikana wazi kwamba ni kuinyonya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke utaratibu wa haraka kwa kuwatumia Wataalam wetu wa Kodi ili kuelekeza ni kwa namna gani kodi itakusanywa kutokana na huduma za kibenki zinazofanywa na *M-PESA, TIGO-PESA, AIRTEL MONEY, Z-PESA* na kadhalika. Hiyo itasaidia sana katika kuboresha na kuendeleza mipango mbalimbali ya maendeleo kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa namna wanavyofanya kazi na jinsi wanavyoonesha *commitment* katika utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Sayansi na Teknolojia ndiyo chombo pekee ambacho kitaivusha nchi yetu kutoka mifumo ya uchumi wa Kitanzania na kuingia katika uchumi wa kisasa ambao ni uchumi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF),* una malengo mazuri na ni matarajio ya Wananchi walio wengi kuweza kupata mawasiliano kwa ukaribu na urahisi kupitia Mfuko huu. Kwa kuwa Mfuko huu ni wa Kitaifa, namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie ufafanuzi ni kwa nini Mfuko huu unafaidisha zaidi upande mmoja wa Muungano tu, yaani Tanzania Bara na hatuoni hatua zozote ambazo zinachukuliwa na Mfuko huu kwa ajili ya Vijiji vya Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri awe mkweli na atupatie ufafanuzi wa kina; Mfuko umeanzisha mfumo wa matibabu kwa Teknolojia (*Telemedicine*), kwa mujibu wa maelezo ya Wataalam na Mheshimiwa Waziri, mfumo huu utaanza kwa Hospitali za Bara tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kisiwa cha Pemba tayari kimeshaunganishwa na Mkongo wa Taifa,

namwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ni kwa sababu zipi mfumo huu usiweze vilevile kutumika katika Hospitali za Chakechake, Wete na Mkoani ili angalau mfumo huu uonekane unatumika upande wa pili wa Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni vyema *UCAF* ikapeleka fedha zake kwa *TTCL* ili *TTCL* iweze kujenga minara ya mawasiliano hapa nchini badala ya makampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara, kwa kusikia kilio cha Wabunge wa Pemba cha kudai kupatiwa Ofisi ya *TTCL* Pemba. Ujenzi umeanza na mategemeo yetu ni kwamba, ujenzi wa jengo hilo utakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la *TTCL* bado linasuasua, ninaiomba Serikali iliangalie upya Shirika hili kwa kuliongezea mtaji ili liweze kuingia katika ushindani wa kibiashara na makampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itilie maanani ya kwamba, eneo la mawasiliano ni eneo nyeti kwa usalama wa nchi yetu, siyo vyema kuachia moja kwa moja makampuni binafsi kuhodhi kwa asilimia kubwa mwenendo mzima wa mawasiliano nchini.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie Hotuba hii kwa kujikita kuhusiana na kero ya mawasiliano ya simu vijijini. Katika Jimbo langu la Mvomero, kuna maeneo mengi hayana mawasiliano ya simu. Mwaka 2011 niliuliza kupata maelezo Serikali itapeleka lini mawasiliano ya simu Kata ya Kanga, Pemba, Kinda, Maskati na Vijiji vya Matale, Kibogoji na Diburuma katika Kata ya Kibati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuhoji, Waziri - Mheshimiwa Prof. Mbalawa, alijibu vijiji tajwa vipo katika mpango huo wa kupatiwa mawasiliano. Aidha, mwaka 2012 Wizara na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote walitoa orodha

ya Vijiji vya Matale, Kinda, Ndole, Dibago, Masimba, Kata ya Kanga na Pemba, vimo kwenye orodha ya vijiji vya kupatiwa mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kupitia semina ya Wabunge na Kitabu cha Mpango wa Mawasiliano kwa Wote, wametoa orodha ya vijiji vitakavyopatiwa mawasiliano kwa awamu na katika orodha na awamu zote Wilaya ya Mvomero haimo katika orodha kabisa. Naomba maelezo wakati wa kujibu hoja za Wabunge, Mfuko wa Mawasiliano utapeleka mawasiliano lini na kwa awamu ipi Kata za Kanga, Pemba, Maskati na Kinda pia Vijiji vya Matale, Kibogoji, Msolokelo, Ng'ungulu, Misengele na Yowe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kupata majibu ya maombi yangu kushughulikiwa. Naunga mkono hoja.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu, kwa kunipa nguvu na afya. Nianze moja kwa moja kuchangia kwa suala la mabadiliko ya Teknolojia ya Utangazaji kutoka anolojia kwenda dijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*, ina dhamira nzuri sana, lakini suala hili linatakiwa kuangaliwa upya juu ya gharama za ununuzi na gharama kwa matumizi hasa kwa Wananchi, kulingana na kipato duni kwa Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama kwa miezi ya malipo zinatofautiana kulingana na uhitaji wa *channel.* Kwa nini Serikali isiamue angalau kupunguza gharama na kama malipo yataendelea kuwa juu kwa nini Serikali isiendelee kupinga kulipia huduma kwa kuchangia *channel?*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bado Wananchi wanahitaji kupata elimu juu ya teknolojia ya dijitali na kama Serikali imepoteza pesa nyingi kwa kuhama kutoka anolojia

na kuingia kwenye ulimwengu wa digitali, basi yatupasa kuwahakikishia Wananchi huduma ya uhakika na siyo matangazo ya kukatika katika kama ambavyo Wananchi wanalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikihamia kwenye suala la Kampuni ya Simu *(TTCL),* katika Mwaka wa Fedha wa 2011/ 2012, Serikali ililipa Sh. 1,774,800,000 kama deni la Serikali kwa Kampuni hiyo ya Simu. Kampuni hii imekuwa nyuma kutoa huduma kwa jamii ukilinganisha na kampuni nyingine za mitandao kama *Tigo, Vodacom, Airtel* na *Zantel*. Huduma za *TTCL* hazijasogezwa kwa jamii na hatujui tatizo ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara chini ya Waziri mwenye dhamana kuwa, Kampuni hii ya *TTCL* sasa iuze simu na huduma nyingine, kama mitandao mingine ilivyo. Pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa jitihada zinazofanyika za kuhakikisha Mkongo wa Taifa unasambaa kwa kasi japo kuna changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna minara ya simu inayojengwa karibu na makazi ya watu. Je, minara hiyo ina madhara gani kwa watu? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akihitimisha, anijibu kwa faida ya Wananchi waliojengewa minara hiyo ya Kampuni za Simu katika makazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la Mawasiliano; tunafahamu kuwa mawasiliano ni Sekta inayokua kwa kasi hapa nchini na Duniani kote na imekuwa ikichangia ukuaji Uchumi wa Taifa na Mataifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta hii ni Sekta Mama kwa sasa kwa kuwa imekuwa ikisaidia Sekta nyingine zote kukua kiuchumi na kurahisisha shughuli. Pia kuna maeneo mengine ambayo yanashindwa kuendelea kwa kukosa mawasiliano; kwa mfano, Wilaya ya Mpanda, Mkoani Katavi, kuna maeneo kama Kasekese, Sibwesa na Kata ya Katuma.

Hivyo, tujitahidi na kuiomba Serikali kuhakikisha

maeneo yote ambayo hayana mawasiliano yapewe kipaumbele ili kukuza maendeleo kwa haraka. Je, nini kinachosababisha maeneo kama haya niliyoyataja yasifikiwe na huduma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na kuunga mkono hoja ili Waziri apate hela akaendelee na kazi nzuri ya kutuletea maendeleo katika Sekta hii ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja, Mkoa wa Geita ni miongoni mwa Mikoa mipya iliyoanzishwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ni muhimu sana katika Mikoa hii mipya ili kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa huu wa Geita umesahaulika kabisa; sijui kwa nini kwenye orodha ya Mheshimiwa Waziri aliyotupatia jana Mkoa wa Geita pamoja na Wilaya zake za Nyang'hwale, Bukombe, Chato, Mbongwe na Geita, hazina kabisa mawasiliano na wala kwenye mpango wa kupatiwa mawasiliano hatumo kwenye orodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja za Wabunge; anieleze ni lini sasa Wananchi wa Mkoa wa Geita na Wilaya zake watapata Mawasiliano hasa ikizingatiwa kuna maeneo kama Nyang'hwale watu wakitaka kupiga simu huwalazimu kwenda umbali mrefu sana kama kilometa kumi au kupanda kwenye miti ya miembe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini Waziri aniahidi ni lini atawapa mawasiliano Wananchi wangu wa Mkoa wa Geita.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na

Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya. Naomba pia kumpongeza Mtendaji Mkuu wa *TCRA* kwa kazi kubwa anayoifanyia nchi yetu. Nawaomba wote hawa waongeze bidii ili twende kwa kasi zaidi, maana uwezo wanao.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wabunifu wametambuliwa, lakini naamini tunao wabunifu/wagunduzi wengi hasa vijijini, hawa tumeweka utaratibu gani wa kuwafahamu? Napendekeza tuweke utaratibu kupitia Halmashauri za Wilaya kwa kuwa na mijadala toka ngazi ya Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hili, ni lile la kuwatia moyo vijana toka Shule za Awali, pengine mashindano huko vijijini yanaweza kusaidia kutia moyo kukuza na kuendeleza vipaji hivyo. Kupitia mashindano hayo, tunaweza kutambua Wasanii, Wanasayansi au Wanasiasa.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa imefanywa katika Mawasiliano ya simu, lakini bado ipo kazi zaidi. Jimbo la Mbinga Mashariki kwa mfano, Kkata ya Ukita na vijiji vyake vyote hawana mawasiliano kabisa ya simu. Nitashukuru sana kupata msaada wa haraka/lakini kwa *program* ya mfuko huu ni hivi vijiji vyote vitafikiriwa, pengine Makampuni ya Simu yenye wajibu wa msingi kufika huko yangeshirikishwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa postikadi na Simbo za *PDG,* huu ni mradi mzuri na utasaidia Serikali kukusanya kodi, kwani ni mwanzo wa kurasimisha.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, itakuwa vyema kama Mbinga inaweza kushirikishwa katika mradi huu. Nawakaribisha sana, nawatakia mafanikio.

**MHE. SAID SULEIMAN SAID:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi zake nzuri inazozifanya chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kupata taarifa kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambao tayari umeshafika Pemba. Je,

umeshaanza kutumika? Kama umeshaanza kutumika: Je, ni Taasisi zipi ambazo zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano zilizoko Pemba?

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote kwa kupitia mradi wake wa *Telemedicine,* miongoni mwa mipango yake ni kuunganishia mtandao wa Mawasiliano kwa hospitali zote za Serikali ili kuwepo na ushirikiano wa kitabibu kwa njia ya mtandao na kuondoa tatizo sugu la uhaba wa Madaktari bingwa katika hospitali zetu hapa nchini. Je, Wizara iko tayari kuiunganisha na mtandao wa mawasiliano hospitali ya Chakechake ambayo inakabiliwa na upungufu mkubwa wa Madaktari Bingwa? Vilevile hospitali hii ya Chakechake iliyoko Pemba inatoa mafunzo ya Udaktari ikishirikiana na Chuo cha Afya cha Mbweni, Zanzibar chini ya usimamizi na msaada wa Madaktari kutoka *Cuba*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda nami kuchukua fursa hii kuchangia katika hotuba ya Wizara hii maalum katika mustakabali wa Mawasiliano na Sayansi.

Mheshimiwa Spika, nataka kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri juu ya mkonga wa Mawasiliano wa Taifa ambao tayari umekamilika kwa asilimia mia moja katika Kisiwa cha Pemba. Je, ni kwanini matumizi ya mkonga huu hayajaanza kutumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda kujua hili, sababu kuna mradi wa *Telemedicine* ambao miongoni mwa mipango ya mradi huo ni kuunganisha mtandao wa mawasiliano katika hospitali zote za Serikali ili kuwepo na ushirikiano wa kitabibu kwa njia za mtandao, kuondoa tatizo sugu la uhaba wa Madaktari Bingwa katika hospitali zisizo na Madaktari Bingwa.

Mheshimiwa Spika, mradi huu katika Zanzibar

haujawekwa katika mpango wa utekelezaji. Hii inatokana na kutokujengwa kwa mkongo wa Taifa katika Kisiwa cha Unguja, hivyo kuifanya hospitali ya Rufaa ya Mnazi mmoja kutokuwekwa katika orodha ya hospitali za awali zitakazofaidika na mradi huu. Swali langu ni kwamba Zanzibar ni mchanganyiko wa Visiwa viwili, na Pemba tayari Mkonga huu umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini mpaka sasa Pemba haikuingizwa katika mradi huu wa *Telemedicine* ambao ungeziwezesha hospitali za Chakechake Mkoani, Wete na Micheweni zikaunganishwa na mpango huu wa *Telemedicine,* hasa ukichukulia uhaba au kukosekana kabisa Madaktari Bingwa katika hospitali hizo? Tunaiomba Serikali itupatie majibu muafaka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie upya Makampuni ilizowapa mikataba/leseni ya kuingiza na kuuza ving'amuzi hapa nchini, kwani kumekuwa na malalamiko makubwa kwa wananchi kuhusu ubora wa *decoder* hizo, na kupelekea nyingine kutopatikana kwa *TV* zote za hapa nchini kinyume cha masharti yao ya kupatiwa leseni za kuingiza/ kusambaza.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, ni lini Serikali itafunga kifaa kitakachoratibu na kuweka rekodi za matumizi ya simu zinazofanywa na Makampuni ya Simu ili kuiwezesha Serikali kupata mapato yake halali ya kodi yatokanayo na biashara kubwa inayofanywa na Makampuni ya Simu?

Mheshimiwa Spika, Serikali kuendelea kuahidi tu na kuacha kuchukua hatua za haraka kutekeleza jambo hili ni kuendelea kuifanya Serikali iendelee kupoteza mamilioni ya fedha ambazo Serikali na Taifa tunazihitaji kwa maendeleo ya watu wetu. Naiomba Serikali itueleze, ni lini jambo hili litakamilika?

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo kuhusu minara ya simu. Kumekuwa na mkanganyiko kwa baadhi ya wananchi kuhusu hii minara

ya simu inayojengwa katika makazi ya watu. Je, hakuna madhara yoyote ya kiafya yapatikanayo kutokana na minara hiyo? Kwani kumekuwa na hofu juu ya minara hii ambayo imewekwa katika makazi ya watu, na hofu kubwa ni mionzi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na wataalam kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara isimamie na isimike haraka vifaa vya kudhibiti matumizi ya simu za mkononi na kuhakikisha kuwa mapato ya Kampuni za Simu zinalipiwa kodi stahili. Pia udhibiti ukazwe ili kukomesha matumizi mabaya.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mfuko wa *UCSAF* utumike kupeleka mawasiliano katika maeneo ya nchi ambayo hakuna mawasiliano. Pia soko halipeleki mitambo kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu na uhaba wa watu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ikazane kuweka mtambo wa mawasiliano katika Tarafa ya Makami Wilayani Kiteto. Tarafa nzima haina Mawasiliano na kumekuwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM kwa zaidi ya miaka mitano sasa.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, suala la mabadiliko la mfumo wa utangazaji kutoka analojia kwenda dijitali, bado ni changamoto katika maeneo ambao tayari mfumo umeshaanza kutumika. Changamoto hizi ni pamoja na bei ya ving'amuzi, matangazo kunatanata *(stuck) chanel* nyingine na hasa *local chanel* hazionekani maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kuna haja sasa ya kuangalia uwezekano wa kukabiliana na hizi changamoto kabla ya zoezi kumalizika nchi nzima. Kuna manung'uniko mengi sana kutoka kwa wateja. Naomba hili Serikali iliangalie na kulitatua mapema, vilevile ili iweze kwenda na kasi, ni vizuri Serikali

kupitia Wizara, iunde kikosi kazi. Kikozi kazi kitajikita kufanya utafiti ili kujua awamu hii ya kwanza utekelezaji wake ukoje na una mafanikio gani.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana sasa hivi la kuibuka kwa wizi mkubwa kwa njia ya mtandao. Wananchi wengi wamepoteza mabilioni ya pesa kutoka kwenye Taasisi na hasa mabenki nchini, *ATM machine* na miamala mingine ambayo inatumia *computer.*

Mheshimiwa Spika, kama nchi ya Tanzania, tunafanyaje ili kunusuru pesa za wananchi hawa? Naomba Serikali inisaidie kama kuna Sheria ambayo inathibiti uhalifu mitandaoni nijue. Kama hakuna, basi hata mkakati tu wa Serikali ukoje juu ya hili suala?

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na Makampuni mengi sana ya simu nchini, lakini kadri siku zinavyokwenda, "huduma kwa mteja" ni kero. Kwanza, haipatikani kwa urahisi na Makampuni mengine yanakata Sh. 100/= mara opareta anapopokea simu yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuepuka usumbufu, naomba au niishauri Serikali kupitia Wizara hii na Makampuni yote yatumie namba moja tu na isiwe na mlolongo wowote. Unapomhitaji mtoa huduma hata kama yuko *busy,* basi iwe ni mpigo wa mara moja, na siyo mara bonyeza mbili, sijui tatu, ni usumbufu mkubwa!

Mheshimiwa Spika, *sevirce levy* zinazotolewa kwenye Halmashauri zimekaaje? Naomba kujua, kuna *fixed rate* kwa Halmashauri zote au kila Halmashauri inapata kulingana na minara iliyonayo? Naomba ufafanuzi kwa hili?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia ya wateja kununua simu mpya bila kuisajili na matokeo yake vibaka wameongezeka kwa sababu akiiba simu anaweza kuuza na mnunuzi kuitumia bila wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali isimamie

hili suala kuhakikisha Makampuni ya Simu yanatoa elimu kwa wateja wao. Mara mteja anaponunua simu mpya, basi akaisajili ili vibaka wa simu wapungue jamani!

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna baadhi ya watumishi kwenye Makampuni ya Simu wanatoa siri za wateja wao kwa watu wengine aidha, kwa malipo makubwa au kwa utashi wao tu. Serikali iangalie upya maadili hata ya watumishi hawa wanaoajiriwa ili wasitoe mawasiliano yoyote bila ruhusa ya mteja. Vinginevyo, sheria kali itengenezwe kwa watumishi ambao sio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezekaji minara ya simu, ningeomba kupata taarifa za uhakika juu ya maeneo niliyoomba ya kuweka minara ili kuwapo na usikivu wa simu ambazo hazipo kabisa. Maeneo haya niliyoomba ni:-

(1) Kata ya Izazi – Kijiji cha Izazi;
(2) Kata ya Mahuninga – Kijiji cha Mahuninga;
(3) Kata ya Malengamakali – Kijiji cha Mkulula; na
(4) Kata ya Nyang'oro na Usolanga – Kijiji cha Mangawe.

Mheshimiwa Spika, naomba leo nipate majibu ya maandishi, ni lini na wapi minara ya simu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, mawasiliano ni muhimu sana katika uchumi wa nchi, pia kuunganisha wananchi kutoka sehemu moja na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mawasiliano ndiyo njia pekee katika kuinua hali ya uchumi hasa vijijini, ipo haja kubwa ya kuimarisha miundombinu katika vijiji vyote vya

Tanzania. Kuna vijiji vingine havina hata barabara inayounganisha Kijiji na Mjini kwa mfano Kijiji cha Idete kilichopo Kata ya Idunda, na Kijiji cha Kwatwanga kilichopo Kata ya Ihowanza.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Regema na Udenyimembe, hata hivi havina mawasiliano. Vijiji vyote vipo katika Jimbo la Mufindi Kusini Wilaya ya Mufindi. Naiomba Serikali kupeleka minara katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanalalamika kuhusu Makampuni ya Simu kuwachaji gharama ya nyimbo katika simu kwa kupokea mlio wa kupigiwa au kupiga bila ridhaa ya mwenye simu. Pia matangazo katika simu yamezidi na yanasababisha usumbufu kwa watumiaji wa simu.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la simu ni kupeleka ujumbe au kupokea ujumbe na mmiliki wa simu, siyo kusumbuliwa na ujumbe wa Kampuni ya simu. Kampuni zinatakiwa kulipa gharama kwa mtumiaji wa simu.

Mheshimiwa Spika, pia ving'amuzi bado havifanyi kazi kama vilivyokusudiwa. *TV* zetu bado zinaonesha chenga. Kwa hiyo, Watanzania tunashindwa kupata habari iliyo safi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu yote ya Wizara hii kwa juhudi kubwa wanazofanya ili Watanzania wote waweze kuwa na mawasiliano (mawasiliano kwa wote).

Mheshimiwa Spika, hakuna asiyejua umuhimu wa mawasiliano. Mawasiliano ya simu yanapatikana kwa urahisi mijini, lakini vijijini na hasa maeneo ya mipakani, mawasiliano ni nadra na pengine hakuna kabisa. Mkoa wa Rukwa maeneo ya mipakani kama vile Mambwe Kenya, Mambwe, Nkoswe (Kalembe) Legeza Mwendo, Katete, Sopa, Kisumbu (Wilaya mpya ya Kalambo).

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya hapo Sumbawanga Vijijini ni maeneo yasiyo na mitandao ya *Voda, Tigo, Airtel* pia hupatikana kwa shida sana kwa sababu minara ya *Airtel* iliyoko huko haina nguvu, kwani mara zote ukifika kwenye maeneo niliyotaja hapo juu, *sms* za *Hellow welcome to Zambia Airtel* hapo mawasiliano Tanzania hutoweka.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwamba *operators* waliangalie hili ili wananchi wa maeneo ya mipakani wawe katika mawasiliano saa 24, na mawasiliano yasiwe na mwingiliano.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo yote ya mipakani Redio Tanzania na Redio nyingine zote hazisikiki. Hii nipamoja na Kata ya Mkali. Hivyo suala la kuboresha masafa lingeangaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, wana-Rukwa Vijijini japo hawana umeme wa *solar*, lakini wanatamani kununua na kutumia Runinga lakini ni tatizo la masafa hayapatikani Vijijini. Hivyo basi, wana-Rukwa nao kama wananchi wengine nchini wanayo haki ya kutoa na kupata habari na kujua mambo yanayoendelea ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ni muda amuafaka sasa kwamba Seikali katika mambo yote na katika shughuli za Wizira zote itupie jicho lake la umakini na huruma mkoa wa Rukwa kwa maendeleo ya haraka ya wananchi wa Rukwa.

*Otherwise*, naunga mkono hoja kwa 100% ili fedha itakapotoka, basi Rukwa iwe ya kwanza kuhudumiwa. Ahsante, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. AMINA ABDALLA AMOUR:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kuwa wachapa kazi na juhudi zao tunaziona, lakini kuna tatizo, Serikali haijaipa umuhimu Wizara hii kwa kutoa bajeti ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kujenga uwezo wa watafiti ni muhimu sana, lakini inasikitisha, bajeti ya Wizara hii ni ndogo. Je, Wizara ina mikakati ya kukubaliana na tatizo hili? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho anijibu suala langu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii iwe makini katika mipango ya maendeleo hasa kwa kuwa suala la maendeleo huwa tunategemea Wafadhili, lakini mara nyingi Wafadhili hao huwa hawatimizi ahadi zao au huwa fedha zinachelewa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iliwezeshe Shirika la Posta ili liweze kutoa huduma nzuri na bora zaidi. Mikoa mingi na vijiji vingi havina Ofisi za Posta na nyingine zimechakaa, ziko katika hali mbaya sana. Naomba Serikali ilione na ilipatie ufumbuzi wa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TTCL* ni Shirika la kwanza lilianza kutoa huduma za simu, lakini hivi sasa ni Shirika la mwisho linalotoa huduma nzuri. Naiomba Serikali kulikwamua Shirika hili la *TTCL* kifedha na kiutendaji na pamoja Serikali kusimamia madeni yote inayodai hili Shirika la Simu, yalipwe haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunakosa mapato kwenye huduma za simu za mkono, naiomba Serikali ifanye mabadiliko ya Sheria ili iwe na uwezo wa kutoza kodi simu za mkononi. Naiomba Serikali kuweka mfumo mzuri wa kukusanya mapato kwenye mtandao wa simu katika huduma za kupiga simu na kupokea na pia katika huduma za M'Pesa.

Mheshimiwa Spika, udahili wa wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi uende sambamba na huduma zinazohitajika kama vile maktaba yawe na vitabu, maabara na vifaa vyake vinavyohitajika. Naiomba Serikali ione umuhimu wa jambo hili na ilipatie ufumbuzi ili watoto wetu waweze kuwa wahitimu wazuri.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, usambazaji

wa minara ulianza kwa kasi mwanzoni mwa miaka ya 2000 kwa ushindani mkubwa kati ya *Vodacom, Celtel* na *Tigo*. Wananchi walihamasika sana kuchangamkia simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Jimbo la Manyoni Magharibi, minara ilisimikwa Kata ya Itigi *(Vodacom na Celtel na Tigo)* na kuendelea, Kata za Mitunda *(Vodacom* na *Celtel)* na baadaye Kata ya Rungwe *(Vodacom).*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ni kwamba katika ushindani huo wa kusambaza minara, Kata moja muhimu sana ilirukwa. Kata hiyo ni Mwamagembe ambako *Celtel (Aritel)* walifanya utafiti na kubaini kuwa wateja walikuwa wengi kiasi cha kuona umuhimu wa kuweka mnara pale Mwambagembe kutokana na uchumi mzuri wa zao la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, lakini tokea watoe ahadi hiyo mwaka 2009/20010 hadi leo bado hawajaweka mnara eneo hilo muhimu sana. Hii imewatenga wananchi wa eneo hilo katika mawasiliano. Mwamagembe iko kati ya Kata ya Mitundu na Kata ya Rungwa ambazo zina minara. Naiomba Serikali iingilie kati ili Makampuni ya Simu yapeleke mnara haraka Kata ya Mwamagembe.

Aidha, naomba pia minara kwa Kata zifuatazo ili kuimalisha mawasiliano:-

(1) Kata ya Idodyandole;
(2) Kata ya Ipande;
(3) Kata ya Kitaraka;
(4) Kata ya Sanjaranda;
(5) Kata ya Aghondi; na
(6) Kata ya Mgandu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kuona kuna mipango ya kuweka minara Kata ya Idodyandole, na Kata ya Mgandu kwenye *phase* hii ya pili ya kusambaza minara. Aidha,

nasisitiza sana Kata ya Mwamagembe iigizwe kwenye *phase II* kwa fedha za ndani maana katika mpango wa fedha za Benki ya Dunia, Kata ya Mwamagembe imesahaulika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwaasilisha.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Ushirikiano wanaonipa katika kutatua shida za kimaendeleo za Jimbo langu zinazohusiana na Wizara yao. Kwa maana hiyo, naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kuwa wananchi wa Kata za Kashishi (ambayo inajumuisha Selele na Sasu) Usinge, Igagola na Kazaroho ambayo inajumuisha na Kata ya Igunsi ambazo zilifanikiwa kuingizwa katika mzunguko wa kwanza wa fedha za minara katika mpango unaosimamiwa na Mpango wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)* sasa wananchi wake wanasubiri utekelezaji wake kwa shauku kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kuwa kutokana na jiografia ya Jimbo langu na shida za kijamii hususan afya na usalama, mawasiliano ya simu za mkononi, ni suala muhimu sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri anipe unafuu wa maisha kwa wananchi wa maeneo haya kwa kuhakikisha utekelezaji unakwenda haraka.

Mheshimiwa Spika, wakati inatangazwa, zipo Kata zilionekana hazivutii kabisa kutokana na umbali *(distance).* Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kuwa Kata hizo zinastahili haki ya huduma hii kama Kata zile za hapo juu. Hii inatokana na ukweli kwamba zina watu wengi sana na uzalishaji mali wa hali ya juu sana kupitia mazao yetu makuu ya biashara ya Tumbaku, Asali na Ng'ombe, bila kusahau mchango wetu katika kuzalisha na kuuza mazao makuu ya chakula kama Mahindi na Mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kata hizi zinazalisha Pamba kwa wingi kwa maeneo hayo. Namwomba Mheshimiwa Waziri katika utekelezajia wa tenda wa awamu inayofuata (ya pili), naomba sana Kata za Kaliua, Mwangozo, Silambo, Ugunga, Nzugi, Khemba, nazo ziwemo katika utekelezaji wa usambazaji wa minara.

Naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA S. NKAMIA**: Mheshimiwa Spika, pasipo na shaka yoyote, naomba kwanza kuunga mkono haja.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Maafisa wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha nchi yetu inakuwa na mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba kazi ya kujenga minara ya simu katika Kata za Mpendo, Sanzawa, Odada, Lalta, Makorongo na Paranga ufanyike kama Serikali ilivyoahidi na kuifanya Wilaya ya Chemba nayo iwe na mawasilianao ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iziweke Kata za Tandala na Msaada nazo zipewe kipaumbele katika awamu nyingine ya kupatiwa minara ya simu kwasababu Kata hizi zina idadi kubwa ya watu na kuna shughuli nyingi za kibiashara na kilimo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nachukua tena nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na wasitetereke na msimamo wao ubaki huo huo kwamba hakuna sababu ya kubadilisha mchanganuo huo kama ilivyoonesha katika vitabu kwenye semina ya jana. *Thanks.*

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono haoja hii iliyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Serikali na Wizara yake hii ya Mawasiliano chini ya Waziri wake, Mheshimiwa Mbarawa na Naibu Waziri, Mheshimiwa January Makamba kwa juhudi zao katika kuhakikisha maeneo mengi ya nchi yetu kufikiwa na huduma ya simu za mikononi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua hatma ya kilio cha wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale na Wilaya mpya ya Nyang'hwale cha muda mrefu sana kuhusu huduma ya simu za mikononi. Jimbo hilo lina Kata 12. Ni Kata moja tu ndiyo ina huduma hii ya simu au mnara, ambayo ni Kata ya Khalumwa na ndipo Makao Makuu ya Wilaya yalipo sasa. Napenda kuuliza maswali yafuatayo:-

(1) Je, bajeti hii ya mwaka 2013/2014 Jimbo la Nyang'hwale limepangiwa mipango gani kuhusu kufungiwa minara?

(2) Je, ni Kata ngapi ambazo zitafungiwa minara kati ya Kata 11 ambazo ni Kata ya Bukwimba, Nyungwa, Kafita, Izunya, Kakora, Nyijundu, Busorwa, Nyang'hwale, Shabaka, Nyaburanda na Mwingiro?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Waziri na Naibu wa Wizara hii Mwenyezi Mungu awape Afya njema na umri mrefu ili mwendelee kulitumikia Taifa hili. Nawaomba mniangalie Jimboni kwangu angalau Kata chache ili kunipunguzia kero za wananchi wangu kuniuliza maswali kila mara. Nitashukuru sana Mawaziri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Napenda kusikia katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri kuhusu Kata za Kilolambwani, Rutamba, Kiwawa na Mipingo kuwemo katika mpango wa mawasiliano ya simu katika bajeti ya mwaka huu ya *UCAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani.

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Januari Makamba, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Karibu, dakika 30 nadhani.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kuchangia na ni fursa ngumu hasa baada ya mchango wa Mheshimiwa Zabein Mhita. Mchango ambao umetuumiza sote, kama binadamu na mchango ambao umemkumbusha uchungu wa kuondokewa na mwanaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu pamoja na kwamba, Serikali haijengi minara na Serikali haina uwezo wa kusema upelekwe mnara mahali, lakini nataka nimwahidi na niwaahidi wananchi wa Jimbo lake kwamba, tutafanya kadiri tutakavyoweza, kuhakikisha kwamba, tunamsaidia Mheshimiwa Mhita na watu wake, ili wapate mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yetu kwamba, pamoja na kwamba, kwa kupeleka mawasiliano hayo hakutamwondolea uchungu wa kuondokewa na mwanaye, lakini angalau kutapunguza machungu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema na baraka zake kwa kutuwezesha kufika leo na kuhitimisha mjadala huu wa Bajeti ya Wizara yetu. Napenda vilevile nitambue uwepo wa mke wangu, Mama Jasmin, yuko pale juu. Ahsante kwa kuja kuniunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kwa kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Profesa Makame Mbarawa, kwa ushirikiano na Mwongozo tunaopeana katika kutimiza majukumu yetu ya Wizara. Nawashukuru pia Watendaji wa Wizara Dkt. Florence Turuka, Katibu Mkuu; Profesa Patrick Makungu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya

Wizara yetu, kwa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha uwasilishaji wa Hotuba hii, lakini na majukumu ya Wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Nawashukuru kwa urafiki na udugu wenu ambao mmekuwa mnauonesha kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia maeneo kadhaa na mengine atayachangia Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu ya kuokoa muda, Mheshimiwa Waziri atawataja wote katika ujumla wao wale ambao wamechangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu nianze kwa kuweka sawa jambo moja lililojitokeza kwenye Hotuba ya wenzetu wa Kambi ya Upinzani. Kwamba, yapo baadhi ya mambo ambayo waliyapendekeza katika hotuba yao ya mwaka jana na wameyataja kuanzia ukurasa wa tatu mpaka wa nne na baadaye wakasema kwamba, Kambi hiyo inaitaka Serikali, kutoa Taarifa, *Progressive Report* ya utekelezaji wa hoja za Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niwakumbushe tu wenzetu kwamba, sisi hatuwajibiki kutoa *Progress Report* kwao na kwamba, hii hotuba ni maoni na mchango ambao tunautolea majibu. Sisi ambacho tunapaswa kuripoti ni Ilani yetu, ambayo ndio inatuelekeza Dira na Malengo ya Taifa ya 2025 pamoja na Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu kuelewa, ili wenzetu msiwe *disappointed* kwa sababu, sisi sio wajibu wetu kutoa ripoti ya utekelezaji wa fikra zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumzia suala la *TTCL.* Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea kuhusu uhai na ustawi wa Shirika hili muhimu kwa Taifa letu; Shirika la kwanza kabisa la mawasiliano hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi kumekuwa na matatizo ya aina tatu, kwanza ni *Management.* Kulikuwa na *management* mbovu huko nyuma, kulikuwa na wizi na

ubadhirifu unaoendelea pale, tuhuma, lakini vile vile kulikuwa na jambo lingine ambalo ni ndoa kati ya Shirika hili na Kampuni ya *Airtel,* ambapo sisi tuna 65% na *Airtel* wana 35%.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la mtaji, kwamba Kampuni hii imekuwa na mtaji mdogo kiasi cha kutoweza kujiendesha na kuendesha mambo yake na kufanya mambo mapya na muhimu na kuendana na teknolojia hii ya mawasiliano, ambayo inabadilika haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeyafanya mambo yote haya matatu, kama Serikali, kukabiliana nayo. Kwanza, binafsi nilikwenda pale kuzungumza na wafanyakazi wengi tukafanya fujo pale na kufanikisha Bodi kuchukua uamuzi wa kuwasimamisha baadhi ya Watumishi Viongozi kwenye *Management,* waliokuwa wanatuhumiwa kwa ubadhirifu na tukaomba *CAG* aende pale akakague.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile binafsi, mimi kama raia, niliandika barua kwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU pamoja na vielelezo, ili ubadhirifu ule uliokuwa unatuhumiwa ufanyiwe uchunguzi na kama wahusika watabainika kwamba, wamehusika na vile vitendo, basi Sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumefanya jitihada za kusafisha *Management* na sasa tunaye *CEO* mpya. Kwa muda mrefu, Kampuni ile ilikuwa na Kiongozi ambaye anakaimu, kwa hiyo, sasa hivi tumepata *CEO* mpya, kijana, mwenye uwezo mkubwa, mwenye uzoefu na shirika hili. Tunaamini kwamba, tukimsaidia na Bodi ikimsaidia ataweza kulibadilisha Shirika hili, ili liweze kuwa na hadhi ambayo inastahili na liweze kushindana na Makampuni binafsi ya Simu na liweze kuipatia Serikali, fedha, gawio.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kama nilivyosema ni ndoa kati ya Shirika letu hili na *Airtel.* Kwa muda mrefu tulishafanya uamuzi kwamba, tutengane ili Serikali iweze kumiliki Shirika hili kwa 100%. Faida ya kumiliki Shirika hili kwa 100% ni kwamba, tutaweza kufanya maamuzi yetu

wenyewe kwa maslahi ya Taifa, lakini vile vile tutaweza kuwekeza au kudhamini upatikanaji wa mtaji. Tumezungumza na wenzetu, tumekubaliana kimsingi kwamba, tutengane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishafanya tathmini ya 35% zile za *Airtel* na hivi tunavyozungumza mazungumzo yameanza na itakapofika mwisho wa Juni, tutakuwa tumemaliza mazungumzo na tutakuwa kwenye hatua inayofuata ya kutafuta fedha za kuwalipa wenzetu hawa, ili kununua 35%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yetu kwamba, kama itakubalika kwamba, Hazina ndio ilipie, basi wenzetu watakuwa tayari kufanya hivyo, ili tuweze kulimiliki Shirika hilo 100%. Kama fikra nyingine kwamba, maana na sisi tuna 40% kwenye *Airtel,* kama tunaweza kuuza 1%, 2% au mpaka 5% ambazo zitatusaidia kununua 35%, basi tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulimiliki Shirika hili kwa 100% ndio tutafika mahali sasa ambapo tunaweza kuweka mtaji au kudhamini shirika hili ili lipate mtaji, lakini katika kipindi hiki kifupi ambacho uongozi mpya umeingia, kumetokea matumaini; mwamko wa wafanyakazi na ari imeongezeka, bado yako matatizo kadhaa ambayo inabidi yashughulikiwe na tunaamini kwamba, Bodi chini ya Uenyekiti wa Dkt. Bukuku, watafika mahali ambapo watatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia, ni suala la udhibiti wa matumizi mabaya ya simu, ukiwemo uhalifu, wizi na uchochezi na Waheshimiwa Wabunge kadhaa wamechangia kwenye hili. Sasa yapo mambo kadhaa ambayo wananchi wanayalalamikia na Waheshimiwa Wabunge, wameyalalamikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni suala la *promotions* ambazo zinasumbua wananchi. Kwamba, wakati

wowote iwe saa tisa usiku unapigiwa simu na vile vile wenzetu wa Kambi ya Upinzani wamelizungumza na kwamba, mwaka jana vile vile walilizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni uhalifu unaotokana na kutumia simu kwamba, simu yako ghafla inakuwa haifanyi kazi, lakini mtu mwingine amesha-*swap* anatumia ile kuiba pesa kwenye akaunti yako ya benki au fedha ambazo umeziweka kwenye salio lako, aidha ni la *tiGO Pesa* au *M-Pesa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni uchochezi na matusi, kwamba, simu hizi zinatumika kutuma ujumbe mbalimbali ambao unawagawa Watanzania kwa misingi ya Dini, Kabila, Kanda na matukio yanapotokea, lakini nalo vile vile lina propaganda za kisiasa ambazo hazina msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, tulianzisha sisi utaratibu wa kuandikisha simu hizi miaka kadhaa iliyopita. Nakumbuka kulikuwa na vita kubwa sana iliyoongozwa na Makampuni ya Simu kwamba, suala hili sio la lazima, kwamba, hatuko tayari na kwamba, ni usumbufu na ni gharama. Lakini tulifanya zoezi lile kwa makusudi kabisa tukiamini kwamba, litasaidia kudhibiti vitendo hivi vya uhalifu na vitendo vya matumizi mabaya ya zile simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya haikusaidia sana kwa sababu, tulivyofanya wakati ule tulitoa ruhusa ya siku 30 ya kutosajili. Kwamba, unaweza kununua *sim card,* ukapewa saa hiyo hiyo ukaanza kuitumia saa hiyo hiyo. Sasa baadhi ya watu walikuwa wanatumia kipindi hiki cha siku 30 kufanya uhalifu kwa kutumia hii mitandao. Vile vile kutokana na kutokuwepo na mfumo mzuri wa *identity (ID),* watu wengi wamekuwa wanatumia majina ambayo sio yao kusajili hizi simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ambacho tumefanya kuanzia Juni 1, kwanza tumeondoa zile siku 30. Kwa maana hiyo, ukinunua *sim card* huwezi kuitumia saa hiyo hiyo, kuanzia

terehe 1 Juni, itakuchukua muda; lazima uende ukajiandikishe jina lako, lijulikane na uonekane *physically,* ndio utaweza kutumia ile *sim card.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, simu zote ambazo zinatumika sasa na ambazo hazijasajiliwa na ambazo zinatumika katika maovu na zenyewe tumezizima rasmi kuanzia tarehe moja. Sasa tunaamini kwamba, hii itasaidia angalau kupunguza, lakini suluhisho la kudumu ni pale tutakapopata Vitambulisho vya Taifa vya kudumu, ambapo inaweza kutulazimu kuhakiki tena taarifa na *identity* za wenye wenye simu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu masuala ya *promotion,* yako matatizo ya aina mbili; kwanza kuna Taarifa zisizo sahihi unapoletewa ule ujumbe. Lakini vile vile kuna taarifa ambazo zimefichwa, wanasema *terms and conditions applied,* lakini zile *terms and conditions* huzijui, kwa hiyo, unajikuta umebonyeza mahali ambapo panakugharimu fedha. Sasa kwa hiyo, unajikuta unapokea *message* kila siku, milio kila siku, simu kila siku, lakini kumbe kwa namna moja au nyingine umekubaliana na hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ambacho tunaongea Wizarani, mambo mawili; kwanza, tuangalie namna ya kutengeneza kanuni, kuimarisha Kanuni, ambazo zitatoa fursa kwamba, ili upate ujumbe au upate simu ya *promotion* lazima uwe umekubali kwanza wewe mwenyewe. Wenzetu, Makampuni ya Simu, wameelekezwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwamba, waweke mfumo ambapo mtu unaweza ku-*unsubscribe* kwamba, ukipata *message* ile unaweza kubonyeza mahali kwamba, siitaki tena milele. Wamesema kwamba, wanahitaji muda kutekeleza hiyo *technology,* lakini ndipo tunapoelekea kwamba, uwe na ruhusa ya kusema sitaki kupokea tena *promotion* na iwe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini njia nzuri ambayo tunadhani baadhi yetu ni kwamba, wananchi waruhusiwe kutumia namba fulani, unapeleka namba yako kule, inakuwa

kwenye *register* ya simu ambazo hazitaki kupokea *promotions.* Ili siku unapopata *promotion* ya *message* au ya mlio au ya simu, unaweza kwenda kuonesha na kulalamika kwamba, namba yangu niliiorodhesha, lakini bado napata *promotion,* kwa hiyo, inakuwa ni rahisi zaidi kuyaadhibu Makampuni ya Simu pale yanapokuwa yamekiuka matakwa ya mteja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchochezi na uhalifu na matusi, kama walivyoongea baadhi ya Wabunge kwamba, simu hizi zinatumika vibaya sana. Saa nyingine katika siasa ya nchi yetu hapa tulipo *message* za uchochezi, *message* za migawanyiko zinatembea haraka sana na zinachochea hamasa ya watu kuchukiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa imekuwa ni vigumu huko nyuma kwa sababu, *message* hizi zinatembea kwa wingi na wakati mmoja, kupata chanzo. Lakini Serikali, imeamua kwa dhati kabisa kuwekeza kwenye *facilities* zitakazotuwezesha kujua chanzo hasa cha *message* hizi ni nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuwaonya wale ndugu zangu ambao wanapenda kukaa na kujifungia na kutunga *message* za uchochezi kwamba, tutawafahamu na tuitakapowafahamu tutawachukulia hatua kali. Hii teknolojia ambayo inapaswa kutumika kwa ajili ya ukuaji wa uchumi, kwa ajili ya shughuli za kijamii, tunaitumia vibaya kwa ajili ya kuwagawa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wameongelea kuhusu bei ya huduma za mawasiliano kwamba, bado ziko juu na bado ni gharama kubwa. Sisi ambao tuko kwenye Sekta hii na ambao tumekuwa tunafuatilia mwenendo wa Sekta hii, tunafarijika kwamba, bei pamoja na kwamba, inawezekana bado ziko juu, lakini zimekuwa zinashuka kwa kasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua mwaka 2009, gharama ya kupiga simu kwa dakika kwenye mtandao

mmoja ilikuwa ni 147/= kwa dakika. Ukipiga kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine, unajumlisha 115/=. Kwa hiyo, mwaka 2009 kupiga simu kwa dakika, ilikuwa ni 262/= kwa dakika. Sasa mwaka huu wastani wa kupiga simu kwa dakika kwenda kwenye mtandao mmoja ni 60/=, kutoka 147/= na tumeshusha gharama za muunganiko, ile *inter-connection fee* kutoka 115/= mpaka 35/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira yetu ni kwamba, twende taratibu mpaka hizi gharama zisiwepo kabisa, za *inter-connection fee.* Kwa hiyo, ukichukua tangu mwaka 2001, ukachora chati ya gharama za mawasiliano, chati ile inaonesha kwamba, gharama za mawasiliano zinashuka kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kujua, linganisha tu na bidhaa nyingine; bei za mkate, sukari, mafuta, umeme, kila kitu zinakwenda juu, bei pekee zinazoshuka ni bei za mawasiliano. Kila kitu kinapanda kuanzia ada za shule na vitu vingine, lakini bei za mawasiliano zinashuka, kwanza kwa sababu ya Sera ambazo tumeziweka sisi kwenye Serikali, za kuwezesha ushindani na kuwezesha bei hizi kushuka, lakini pamoja na uwekezaji mkubwa kwenye Mkongo wa Taifa, ambao umewezesha kupunguza gharama za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile sio tu gharama za kupiga simu hata gharama za *internet.* Mwaka 2009, *GB* moja, kifurushi kile cha *GB, Giga Bite* moja, kilikuwa ni sh. 36,000/=, mwaka huu ni 9,000/=. Unaweza ukanunua hadi kifurushi cha 500/= cha *internet,* kwa hiyo, tunaamini kwamba, kuendelea kushuka kwa gharama hizi kutawawezesha wananchi wengi kuweza kushiriki katika mapinduzi haya makubwa ya sekta ya mawasiliano ambayo yanaendelea sasa nchini na duniani kwa ujumla. Tunaamini kwamba, kwa kadiri mazingira ya ushindani yanavyoongezeka, basi bei zitaendelea kushuka na wananchi wengi zaidi watanufaika na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia, ni suala hili la mawasiliano vijijini.

Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza na ningependa tu Watanzania wanaonisikia kote niwaambie kwamba, kokote ambako hamna mawasiliano Wabunge wenu wanawasemea sana na wanatusumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishaamua huko nyuma kwamba tunaingia kwenye soko huria na kwamba sekta ya mawasiliano, kampuni za simu ni sekta binafsi, kwa hiyo makampuni yanaamua yapeleke mawasiliano wapi. Ni uamuzi wa msingi ambao tuliufanya huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaja tukagundua kwamba, kwanza si vema kuwaacha Watanzania wenzetu kutonufaika na haya mapinduzi makubwa ya mawasiliano kwa sababu Waheshimiwa Wabunge katika miaka hamsini iliyopita hamna mapinduzi makubwa kwenye teknolojia ambayo yamekuwa *inclusive* yamewajumuisha watu wote kuanzia wamachinga, mama ntilie, wakulima, wafugaji kama simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokana na mazingira na jiografia ya nchi yetu tumebaini kwamba wako Watanzania wenzetu wengi ambao hawanufaiki na haya mapinduzi. Kwa hiyo Bunge hili likaamua na Serikali ikaamua kuleta Sheria hapa na Bunge likaipitisha ili tuanzishe Mfuko wa kuweza kutoa ruzuku kwa makampuni haya binafsi kupeleka mawasiliano kule ambapo makampuni haya yameona hakuna mvuto wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Muko huu umechelewa sana kuanza kazi, vyanzo vya Mfuko huu viko viwili; kwanza, ni tozo kutoka kwa Makampuni ya Simu 0.3% ya pato ghafi la Makampuni yote ya Simu na vile vile tulipata mkopo Benki ya Dunia wa dola milioni 30. Hizi pesa za tozo ni kidogo 0.3% na hazitatuwezesha na zisingetuwezesha kutoa ruzuku ya kutosha kupeleka mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi ambazo tumekuwa tunazifanyia kazi katika miaka miwili au mitatu iliyopita ni fedha za benki ya dunia na wakati tunasaini

mkataba wa mkopo ni fedha za mkopo, kulikuwa na masharti magumu sana na mengi sana ya matumizi ya hizi fedha. Kwa hiyo baadhi ya ucheleweshaji Waheshimiwa Wabunge mnaouna na unaoendelea sasa hivi unatokana na masharti magumu ya hizi fedha. Ukitaka kununua karatasi lazima upate *no objection,* ukitaka kufanya kitu chochote lazima upate *no objection*. Mtakumbuka Miradi ya Maji ilivyochelewa na ilivyokuwa na matatizo, vile vile ni katika mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeingilia kati na kujaribu kuzungumza na wenzetu wa Benki ya Dunia kuhusu umuhimu wa kutuachia kidogo uhuru na sisi kuamua hizi fedha tunazitumiaje kwa sababu ni fedha za mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka tuliwaambia wenzetu wa *UCAF* kwamba wapeleke mawasiliano kwenye maeneo ya mipaka kwa sababu yapo maeneo mengi ya mipaka ya nchi yetu kwenye ukanda wa Ziwa Tanganyika, ukanda wa Ziwa Nyasa kule kwenye mbuga kwa mzee wangu Telele na mzee wangu Laizer, kule milimani Rombo, Manyovu kwa mzee Ntukamazina, pia kule Ludewa na maeneo yote ya mipakani, kwa sababu kwenye vituo vingi vya mipaka ambako kuna Askari wetu wa Jeshi pamoja na Polisi hakuna mawasiliano, kwa hiyo, usalama wa wananchi wetu upo hatarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukasema kwa sababu tunayo fursa hapa ya hizi fedha za ruzuku, basi ikiwezekana tutoe ruzuku ya 100% ili tujenge minara kwenye maeneo hayo, lakini wenzetu wakasema hapana hamjafuata vigezo. Kwa hiyo, tukagombana kidogo na baadhi yetu tukakasirika kwa sababu tunaona tumekosa ule uhuru wa kuamua mambo gani ya msingi kwa maendeleo ya nchi yetu na tuyafanye kwa manufaa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukasema sasa tutumie fedha zetu kwa ajili ya maeneo ambayo tunadhani ni muhimu na ambayo hatukwazwi na vigezo vya benki ya dunia na mpaka sasa kilichofanyika ni kwamba, viko vijiji 316 ambavyo tayari makampuni yamepatikana na

tumewekeana mkataba, mawasiliano yatakwenda. Pia viko vijiji vingine 968 ambavyo wakati wowote kuanzia sasa tutatangaza tenda ili makampuni yajitokeze na ku-*bid* na kupeleka mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini viko vijiji vingine tena 489 ambavyo tutatumia fedha yetu wenyewe kwa ajili ya kupeleka mawasiliano. Sasa katika kipindi cha mwaka huu peke yake, tutaweza kupeleka mawasiliano katika vijiji zaidi ya 1,700, jambo ambalo halijapata kutokea huko nyuma. Kwa hiyo, pamoja na kwamba Waheshimiwa Wabunge kuna malalamiko, lakini jitihada zinafanyika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi yetu hili jambo linatusumbua kwa sababu tunafahamu ahadi tuliyoitoa sisi kama Chama cha Mapinduzi na kama Serikali kwamba, nchi hii lazima kote kuwe na mawasiliano itakapofika mwaka 2015 na tumedhamiria kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa njia ya Mfuko ni njia moja, ambacho nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, hatutabaki na njia hii hii Bungeni hapa kila siku mtu anakuja anasema kijiji changu, kijiji changu tunaangalia njia nyingine mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tu ni kwamba, kesho naondoka hapa saa kumi alfajiri kwa sababu nawahi mkutano saa tatu Dar es Salaam wa kukutana na wenzetu wengine watakaotusaidia kwenye mambo haya ya *UCAF,* lakini lazima nikutane nao kesho kwa sababu wanaondoka na kwa sababu hatujafikia makubaliano isingekuwa vyema kutangaza hapa, lakini kuna matumaini makubwa sana tukapata namna ambayo tunaweza tukalifanya jambo hili kwa haraka na kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Mhita na Waheshimiwa Wabunge wengine na Mheshimiwa Ameir pale kama

itawafariji niwaambie tu kwamba na Bumbuli na yenyewe tuna Kata 16 na Kata nane hazina mawasiliano na ukiangalia kwenye awamu ya kwanza na awamu ya pili, simo.

Mheshimiwa Naibu Spika, name napata shida zaidi kwa sababu wapiga kura wangu wananiambia kila tunapokuona Bungeni unaahidi mawasiliano kwa watu wengine, wakati hapa uliposimama hebu toa simu yako mfukoni hakuna mawasiliano. Kwa hiyo mnaye mwenzenu ambaye tatizo hili ni la kwake, kwa hiyo nami nina-*interest* ya kumaliza hili tatizo haraka iwezekenavyo ili tuweze kupata mawasiliano katika nchi hii ili Watanzania wote waweze kunufaika na haya mapinduzi ya mawasiliano na naamini kwamba tutaweza na tutafanya na hilo sina shaka nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kuongelea Chuo cha Sayansi na Teknolojia, Mbeya. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamechangia pamoja na wenzetu wa Kambi ya Upinzani; kwanza; kuhusu ithibati, kwamba Chuo kile kina ithibati ya muda na ningependa kuwaambia kwamba, ni utaratibu, lazima upate ithibati ya muda kwanza kabla hujapata ya kudumu. Kwa hiyo, tuko mbioni kwa sababu wamekidhi vigezo vyote ya kupata ithibati ya kudumu na ithibiti ya kudumu itatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu ya Chuo, ni kweli kwamba Chuo kile kilianza kama Chuo cha Ufundi, Mbeya *Tech,* ikawa taasisi *MIST,* baadaye ikawa *MUST* Mbeya *University,* lakini ni dhahiri kwamba na nilikwenda pale mwezi wa 12 na ukiangalia miundombinu ya pale bado haijakidhi kuitwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyokuwa pale baada ya kuona mazingira na baada ya kuongea na uongozi wa Chuo nilimpigia simu Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye alikuwa likizo Mpanda, nilimsumbua kumwomba atusaidie haraka ili tuweze kurekebisha miundombinu ya pale. Bahati nzuri na yeye akasaidia na Chuo hiki kimeingizwa kwenye mchakato wa kupata karibu shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kukiimarisha kuweka miundombinu ili kiwe na hadhi ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao uzoefu wa kufanya hivyo, kwa sababu Chuo cha Nelson Mandela pale Arusha tulifanya vile vile, tulitafuta fedha nyingi na za kutosha na tukakiinua hadhi, ukienda pale unapata fahari ya kuwa Mtanzania na hivyo hivyo ndiyo tutakavyofanya kwenye Chuo Kikuu Cha Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazungumzo yanaendelea vizuri na mambo yakienda vizuri, basi itakapofika mwisho wa mwaka huu tutaweza kutoa taarifa nzuri kuhusu miundombinu ya kile chuo na nchi yetu itakuwa katika safari ya kutengeneza wataalam na wanasayansi na wavumbuzi na wagunduzi ili watusaidie kuleta mapinduzi ya sayansi na teknolojia ambayo sote tunayataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa January Makamba. Sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Mbarawa.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele yenu na kutoa mchango wangu katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wa Bunge kwa uwezo na umahiri mkubwa mnaoonyesha katika kuliendesha Bunge letu. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa umakini wake wa kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyowasilisha leo asubuhi

hapa Bungeni, kwa michango yao mizuri na ya kina yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa Wizara yangu. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingi zimetolewa na hii ni dalili ya dhati ya uwepo mkubwa kwa upande wa kuendeleza maeneo ya mawasiliano, sayansi na teknolojia na ubunifu kwa umma wa Tanzania ili tuweze kupiga hatua zaidi katika maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika michango hiyo, imedhihirisha wazi juu ya mahitaji makubwa ya mawasiliano ya simu kama ilivyo huduma ya usafiri wa reli, barabara na bandari kwamba, ni nyenzo muhimu za maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile imeonekana dhahiri kuwa masuala ya kuendeleza shughuli za utafiti yana umuhimu mkubwa katika kutekeleza programu mbalimbali za kiuchumi na za kijamii. Aidha, uendelezaji wa vyuo vya sayansi, teknolojia utawezesha Taifa kuongeza wataalam wa fani hizo wenye ujuzi na weledi unaohitajika katika kuleta maendeleo ya nyanja za uzalishaji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Mbunge mmoja aliyechangia katika sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja mbalimbali kuhusu sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imechangiwa na wachangiaji wengi, wachangiaji tisa wamechangia kwa kuzungumza na wachangiaji 46 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge wote ilikuwa mizuri sana na inaonysha

mapendekezo na ushauri hasa namna bora ya kuendeleza sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia ili iweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu na Watanzania kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, siyo rahisi kujibu hoja zote Waheshimiwa Wabunge kwa kina na kutosheleza kwa muda huu mfupi, lakini naahidi kwamba, hoja zote tutazijibu kwa maandishi na tutawapatia Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu imezingatiwa, vilevile maoni na ushauri kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani utazingatiwa. Hata hivyo, ningependa nitumie muda mfupi nilionao kutoa ufafanuzi wa dhati wa baadhi ya hoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu suala la Mheshimiwa Mhita limetugusa sana kama Wizara na tunamhakikishia tutafanya kila tunaloweza ili kuhakikisha na yeye ataweza kupata mawasiliano katika Kata zake. Tunaomba awe mvumilivu kidogo, lakini tutafanya kila tunaloweza kuhakikisha kwamba mawasiliano yanafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nijielekeze kwenye hoja kwanza za Kamati ya Kudumu ya Miundombinu. Kamati ya Kudumu kwanza ni Kamati muhimu kwetu, ndiyo *think tank* ya Wizara yetu na tunaisikiliza vizuri na inatushauri vizuri na tunaamini kuwa tunavyofanya kazi kwa pamoja tutaweza kupiga hatua kubwa kwenye sekta hii ya mawasiliano, sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yao ya kwanza ilikuwa fedha za bajeti ya Wizara zimepungua kwa ujumla, fedha kwa ajili ya utafiti na maendeleo zimepungua kwa kiasi kutoka shilingi bilioni 21 hadi bilioni 16, je, ipo dhamira ya kweli ya Serikali ya kuongeza pesa hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali kweli tuna dhamira ya kweli ya kufanya hiyo shughuli ya kuongeza fedha, lakini mchango wenyewe utategemea sana na pesa ambazo zinatokana na makusanyo ya kodi. Kama tunavyoelewa tengeo la utafiti mara nyingi linagawika kwenye mafungu matatu; fungu la kwanza, linapelekwa kwenye Serikali na fungu la pili linapelekwa kwenye taasisi nyingine kama vile taasisi ya kilimo au Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo ama Wizara ya Afya. Vile vile kuna tengeo lingine ambalo linatoka kwenye sekta binafsi na mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali kama inlivyosema safari hii kwenye bajeti yetu, sisi tumeweka shilingi bilioni 16 kwa ajili ya utafiti. Tunaamini kwamba kwenye Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Afya kuna pesa vile vile zimewekwa kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yao ya pili ilikuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge zitolewe kama zilivyoidhinishwa. Ni kweli mpaka sasa hivi zimeanza kuletwa na mpaka sasa hivi kwenye Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia tumepokea shilingi bilioni 25 ambazo ni sawa na 64% na tunaamini kabla ya mwisho wa mwezi huu tutaendelea kupata hiyo 36% ili tuendelee na mipango yetu ambayo tumejipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja inayohusu kwamba, Serikali isimamie kikamilifu utoaji wa taarifa wakati wa usajili wa laini za simu. Mheshimiwa Naibu Waziri amelizungumza hili kwa dhati na ni suala muhimu na sisi Serikali tumejipanga vizuri, nachukua nafasi hii kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge vile vile na Watanzania kwa ujumla kwamba ukitoa habari za uongo wakati unapojisajili hilo ni kosa na hatua kali zitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niliposimama nina *copy* ya gazeti la Mtanzania inayoonesha kuna Mtanzania

mmoja amefungwa mwaka mmoja kwa kutoa vielelezo vya uongo kuhusu usajili wake wa simu. Kwa hiyo, Sheria tutaisimamia na tutakuwa wakali na tutahakikisha kwamba watu wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ambazo nitaruka kidogo, Serikali iunde kikosi kazi kitakachohusisha wadau wote muhimu wa mawasiliano ili kufanya tathmini ya mafanikio na athari kutokana na uhamiaji wa mfumo wa utangazaji wa digitali. Hili tumelipokea na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojua sasa hivi tunatayarisha kikosi hicho na wadau wote tutahakikisha kwamba wanashiriki kwenye kikosi hicho kwa sababu ni muhimu kila mtu atoe maoni yake ili wakati tutakapokwenda kwenye awamu ya pili iwe tuna hakika kwamba changamoto zote zilizojitokeza kwenye awamu ya kwanza zimefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna maoni yanayosema kwamba, wasambazaji wa *signal* wasimamiwe kuhakikisha kuwa *channel* tano za Kitaifa zinazotakiwa kutolewa zitolewe bila gharama. Hili tumelichukua na sisi tunaifanya hiyo kazi, tunahakikisha kwamba *channel* zote tano *TBC, ITV, Channel Ten, EATV* na *Star* zote zinapatikana bure bila gharama yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ambayo inazungumzia Kitengo cha Taifa cha *Computer Emergency Respond Team* kiimarishwe kwa kupatiwa mafunzo. Hili tunalijua na tumeanza kulifanyia kazi na tunaamini kwamba kikosi hicho kitafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja inayozungumza kwamba, Serikali iharakishe kuleta Sheria ya *Cyber* ya Usalama katika mtandao. Kazi hii imeanza kufanyika kama nilivyosema asubuhi kwenye hotuba yangu. Ninaamini kwamba, itakapofika mwisho wa mwezi Desemba mwaka huu, tutakuwa na Sheria hizo na mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wakati ukifika muweze kuzipitisha sheria hizo.

Vilevile ipo hoja inayozungumzia kuhusu Mkongo, Serikali iongeze kasi ya utoaji wa Fedha kwa ajili ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Hoja hii tumeipokea na Serikali kama nilivyosema kwenye Hotuba yangu leo asubuhi kwamba, tumesaini Mkataba na Serikali ya Watu wa China na tumeweka Dola za Kimarekani milioni mia kwa ajili ya kujenga awamu ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi, lakini sitaenda kwenye hoja zote. Serikali kupitia *COSTECH* iongeze juhuzi za kuhamasisha ugunduzi na ubunifu hasa kwa vijana na kuhakikisha kuwa, bidhaa na huduma zinazozalishwa zinapelekwa sokoni. Kazi hii inafanywa na *COSTECH* na kama nilivyosema, *COSTECH* ilishatenga karibu shilingi bilioni 3.2 na hivi sasa kuna Mfuko ambao unaanzishwa, ambao tunauita *Innovation Fund*, kazi yake kubwa ni kusimamia wagunduzi na wabunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja za Kambi ya Upinzani, sitaweza kwenda kwenye hoja zote lakini nitachagua tu baadhi ya hoja hizo.

Hoja ya kwanza, inazungumzia Sayansi na Teknolojia kutoa kipaumbele katika uvumbuzi wa kielektroniki. Kama ninavyosema, Serikali inaendelea kutoa kipaumbele katika ufumbuzi wa kielektroniki kwa kuanzisha atamizi maalum pale Dar es salaam, ambayo tunaiita *Dar es Salaam TEKNOHAMA Business Incubator (DTBI),* ambayo mpaka sasa vijana kama mia moja na ishirini na tano wameunda makumpuni kwa kutumia atamizi ile.

Pia, kuna makupuni ambayo yanajulikana leo hapa Tanzania; kwa mfano, *Maxcom* ambayo ina mtandao wake unaitwa *Max-malipo,* ambao kila Mtanzania anaujua na mtandao huu unafanya kazi kule Rwanda na Sudani ya Kusini. Vilevile kuna programu ambayo imetengenezwa pale ambayo tunaita *Dewan Softcom Program* kwa ajili ya kukusanyia mapato, inafanya kazi vizuri na imeonesha usanifu mkubwa kule katika Wilaya za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine inayosema kwamba, *TCRA* itoe bei elekezi kwa Kampuni za Mawasiliano ya Simu. Kulingana na Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Mwaka 2003, inaitaka Mamlaka hiyo idhibiti bei za jumla *(whole sale)*. Kwa kuzingatia hilo, Mamlaka ya Mawasiliano imekuwa ikitoa bei elekezi kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, bei ya sasa hivi kwa ajili ya mwingiliano *(Interconnection Fee)* ni shilingi 34.92 kwa dakika na itaendelea kushuka mpaka kufikia shilingi 27 kwa dakika mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja inayozungumzia kwamba, kuhama kutoka mfumo wa analojia kwenda dijitali kumewanyima raia wengi haki ya kupata habari. Hadi kufika tarehe 30 mwaka 2013, teknolojia ya zamani ya analojia ilikuwa imesitisha rasmi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Mwanza, Moshi, Arusha na Mbeya. Hatua hii ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mabadiliko ya hapa nchini, hivi sasa Serikali kupitia Kamati ya Ufundi inayoshirikisha, inaangalia jinsi gani changamoto ambazo ziliathiri katika hatua hii ya mwanzo. Baada ya kuziangalia changamoto hizo na kuona Watanzania wangapi hawakuweza kuingia kwenye mfumo huu, tuone tutaweza kuwasaidiaje ili kuhakikisha kwamba, Watanzania wengi wanafaidika na teknolojia hii.

Kuna hoja nyingine kama nilivyosema, kuhakikisha kuwa *TBC, ITV, STAR TV, CHANNEL TEN* na *EAST AFRICA,* vinarusha matangazo bure kwa nchi nzima. Kama tunavyojua, hii inasimamiwa na tutahakikisha kwamba

tunaisimamia kuhakikisha kwamba, *signal distributor* wanarusha matangazo hayo kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nijielekeze kwenye hoja ambazo zimetolewa na Mbunge mmoja mmoja. Kwanza, kuna hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mussa Azzan, Mheshimiwa Assumpter Mshama na Mheshimiwa Rebecca Mngodo.

Kwanza, nikianza na Mheshimiwa Mussa Azzan, tunakushuru sana, hoja zako tunazipokea vizuri. Wewe ndiyo mtu wa mwanzo uliyetushauri kuhusu kufunga huko mtambo wa *TCRA* na mtambo huo sasa unaanza kufanya kazi na tunaamini utakapofika mwisho wa mwezi wa saba, utakuwa unafanya kazi. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, makampuni yote ya simu yanalipa kodi kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika tunamshukuru kwa kuunda kamati ya taarifa ya mapendekezo ya matumizi ya Serikali na moja kati ya sekta iliyokuwa imeangaliwa kwa makini ni Sekta ya Mawasiliano.

Hayo mapendekezo yatakapotoka, bado hayajatoka lakini yakitoka rasmi, tukiletewa Serikali, bila shaka tutayaangalia na tutafanyia kazi. Kulikuwa na malalamiko kwamba, Kampuni za Simu Tanzania hazilipi kodi inavyotakiwa ukilinganisha na Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina *data* ambazo zinaonesha malipo ya kodi ya Tanzania na malipo ya kodi ya Rwanda. Mwaka 2010 Kampuni za Simu Tanzania zililipa Dola za Kimarekani 173.84 milioni, wakati kampuni za Rwanda zililipa dola 42.95 milioni. Mwaka 2011 Kampuni za Tanzania zililipa Dola za Kimarekani 197 milioni, wakati Kampuni za Rwanda zililipa dola 48 milioni. Mwaka 2010 Kampuni za Tanzania zililipa dola 232 milioni wakati Kampuni za Rwanda zililipa Dola milioni 60 za Kimarekani. Sasa unaona kwamba, Kampuni za Tanzania zinalipa pesa nyingi ukilinganisha na Kampuni za Rwanda. Ukichukua mfano tu, *Vodacom*

yenyewe mwaka 2012 ililipa karibuni Dola za Marekani 97 milioni. Hii ni kubwa kuliko kampuni zote za Rwanda.

Mheshimiwa Mussa Azzan, vilevile ulikuja na hoja kwamba, *Safaricom* inafanya vizuri; ni kweli tunakubaliana kwamba, Kampuni ya *Safaricom* ya Kenya inafanya vizuri; mwaka huu imevunja *record* kubwa. Kitu cha muhimu cha kuangalia ni kwa nini *Safaricom* inafanya vizuri, ni kwa sababu matumizi ya watu wa Kenya, *Telecom Revenue per user*, kwa Mkenya wa kawaida, *average* hiyo ni shilingi 10,000, wakati *Tanzania Telecom Revenue per user* ni shilingi 4,000, kwa hiyo ni lazima Kampuni ya *Safaricom* itafanya vizuri zaidi kuliko kampuni zetu za hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo yako ni mazuri, Waheshimiwa wote waliochangia, mawazo yenu ni mazuri na tutaendelea kuyafanyia kazi na ndiyo sababu tukaweka ule mtambo pale *TCRA* kuhakikisha kwamba, Watanzania hawaibiwi tena pesa zao za malipo ya kodi ya Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Mussa Azzan, ulikuwa na hoja nyingine ambayo inataka kufahamu ni kwa nini sasa na sisi tusiende ku-*auction* hizi *frequency* za *4G or LTE*. Tunakuhakikishia kwamba, ushauri tumeuchukua na sisi kabla hatujaenda kufanya hiyo *auction* au kuzitoa hizi *frequency* za *LTE,* tutahakikisha kwamba, tumefanya *study* ya kutosha na kuhakikisha njia ipi ni nzuri ya kuziuza *either* kwa kutumia *auction* au utaratibu wa kawaida. Tutahakikisha kwamba, tunafanya na ushauri wa Wabunge wote utachukuliwa kwenye suala hili.

Mpaka sasa hivi kuna *frequency* ambazo tumezitoa, *frequency* hizo zilikuwa ni za *WiMAX,* lakini wana uwezo wa kutumia kwa *LTE* na ndiyo kama unavyoona, kampuni kama ya *smile communication* imeanza kufanya hiyo kazi ya *LTE,* lakini hawatumii zile *frequency* ambazo sisi tunazo, ambazo ni *700 megahertz (MHz),* wanatumia *frequency* za *WiMAX*. Waheshimiwa Wabunge, mawazo yenu tunayachukua na tutayafanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja za Mheshimiwa Maua Daftari, anasema kwamba; fedha kwa ajili ya vyuo vyetu zimepungua sana. Tunakibaliana na yeye, kama Serikali, tutafanya linalowezekana kuongeza fedha hizo ili kuhakikisha kwamba, vyuo vyetu vinafanya vizuri na vinaendana na teknolojia ya kisasa.

Amezungumzia pia suala la matibabu mtandao pale *Ocean Road Hospital*, kwa kweli hiyo sasa hivi tunafanya, ile *centre* iliyoko pale imeunganishwa na Hospitali za India na zinatumika katika kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa *masters* walioko pale. Vilevile kama Serikali, tumeshaanza utaratibu wa kuziunganisha hospitali zetu za pale Dar es Salaam kwenye matibabu mtandao kuhakikisha kwamba, teknolojia ile inawasaidia Watanzania wengi.

Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, kuna hoja ambayo unaizungumzia, Serikali ina wajibu wa kusimamia utendaji wa Shirika la Posta; je, ni utaratibu gani mzuri wa kutoa mafunzo? Maelezo kuhusu hoja hii, Shirika la Posta limejipanga vizuri kiutendaji na linawajibika kutoa taarifa za watendaji Wizarani kila robo mwaka.

Kuhusu mafunzo, Shirika letu lina utaratibu wa kutoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wake ili kuwapa uwezo wa kutoa huduma bora kwa Watanzania. Pia, Shirika linapata misaada ya kiufundi kutoka Umoja wa Posta Duniani katika maeneo ya kimafunzo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mussa Azzan, nimeshazungumzia hiyo, kuna suala vilevile la picha ya mchezaji Jellah Mtangwa, kuwekwa kwenye stempu. Ni kweli kuwa, picha ya mchezaji mahiri wa mpira wa miguu iliwekwa kwenye stempu. Kanuni na taratibu za kuchapisha Stempu za Posta zinaruhusu kuchapisha picha za matukio muhimu Kitaifa na Kimataifa na watu maarufu, bila Serikali au Posta kulipa *royalty* yoyote. Picha ya Mheshimiwa Jella Mtangwa, ilichapishwa kwenye stempu kama njia ya kumuenzi na kumtangaza mchezaji huyo.

Mheshimiwa Ritta Kabati amekuja na hoja kwamba, Shirika la Posta lipatiwe kipaumbele ili kuweza kukabiliana na changamoto zinazohusiana na utekelezaji wa mafunzo muhimu ya anwani za makazi na posta. Serikali kupitia Msajili wa Hazina, inatekeleza mpango wa kusafisha mizani ya Shirika la Posta na kuweka utaratibu wa kuliwezesha Shirika la Posta kukopa ili liweze kutekeleza mipango yake ya kujiendesha kibiashara. Pia, utekelezaji wa Mradi wa Mawasiliano ya Makazi na Simbo za Posta, unaratibiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Vilevile Shirika la Posta wanapewa mafunzo ili kuweza kuendana na mpango huu.

Mheshimiwa Horoub Muhammed Shamis, amezungumzia kwamba, *Channel* zinazotoa hazionekani kwenye *Zuku* na *DSTV.* Kwanza, naomba ifahamike kwamba, katika ubadilishaji wa kutoka analojia kwenda dijitali, *ZUKU* na *DSTV* hazimo kwa sababu *ZUKU* na *DSTV* ziko dijitali kwa muda mrefu. Kama kuna matatizo kama hayo, tutalichukua kwenye *DSTV* na *ZUKU* kuhakikisha kwamba, wanatoa hizo *channel* ambazo zinatakiwa, lakini wao hawatoi bure kwa sababu hii *Pay TV.*

Mheshimiwa Rajab Mbarouk Muhammed, ana hoja mbili za *TTCL;* ya kwanza kuhusu *UCAF* na ya pili kuhusu ujenzi wa Ofisi ya *TTCL* pale Pemba. Tukianza na suala la ujenzi wa *TTCL* pale Pemba, ujenzi umeanza na unaendelea. Ujenzi ulichelewa kwa sababu mbili za msingi. Sababu ya kwanza, kile kiwanja cha pale kilikuwa ni kiwanja cha Posta na *TTCL,* kwa vile kwanza ilitakiwa kigawiwe kile kiwanja na tumefanya hiyo kazi na sasa hivi ujenzi unaanza.

Suala la pili, ilitakiwa kwanza, ifanyike *soil analysis* pale, kwa sababu kwenye kiwanja kile ilikuwa sehemu ambayo imewekwa wakati wanatengeneza ile barabara ya Madungu. Kazi imefanyika na majibu yametoka na hivyo shughuli hii inaendelea vizuri.

Suala lingine Mheshimiwa Mbarouk aliuliza hili hata kwenye semina yetu jana, ambalo *UCAF* kama anavyosema, ina mpango wa kwenda Zanzibar, lakini kwa Zanzibar

tunaangalia hasa kupeleka mambo ya *Telemedicine* na *telecentres*, kwa sababu Zanzibar hakuna changamoto sana za mambo ya minara. Kama nilivyokwambia jana kwamba, kuna Kampuni zipo tayari kupeleka minara Zanzibar, lakini tunapata matatizo huko Zanzibar. Tunaamini kwamba, tutakaa pamoja na Zanzibar na hayo matatizo tutayatatua. Nafikiri Mheshimiwa Mbarouk, nimekujibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala nafikiri ni la Mheshimiwa Rebecca Mngodo, nimeshalijibu kuhusu kodi za makampuni ya simu. Yapo masuala mengi hapa, lakini nitachagua. Kuna suala kuhusu *Cyber Security* la Mheshimiwa Leticia Nyerere kwa kweli umetusaidia sana, mchango wako umekuwa mzuri, tutahakikisha kwamba maoni yako tutayachukua na wakati ukifika wa kutoa maoni ya wadau, tutakukaribisha uje ufanye kazi hiyo, kwa sababu hili ni jambo muhimu na tunashukuru wewe umelijua. Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuelimishana ili Wananchi wetu wasitumie teknolojia hii nzuri kwa mambo mabaya.

Vilevile suala hili limechangiwa na Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Rachel Mashishanga, Mheshimiwa Ritta Kabati amechangia, Mheshimiwa Juma Abdallah na Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha. Maoni yenu tumeyasikiliza na wakati ukifika wa kutoa maoni tutawakaribisha ili tuifanye kazi hii kwa pamoja. Hili ni jambo letu, ni lazima tushirikiane kuhakikisha kwamba, mambo yanaenda vizuri.

Pia, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Betty Machangu na Mheshimiwa Mendrad Kigola, wanazungumzia kuhusu haki za wasanii. Nafikiri hili suala kama nilivyolieleza awali; Sekta ya Mawasiliano imewezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi, ikiwa ni pamoja kuwasaidia wasanii mbalimbali. Mapato ya Sekta ya sanaa hupatikana kwa kiasi kikubwa kupitia miito ya simu, yaani *ring back tones*.

Malipo ya wasanii yanapolipwa kutokana na nyimbo zao zilizofanya miito ni makubaliano ya biashara kati ya wasanii na makampuni yanayojishughulisha na uchakataji

wa nyimbo hizo, yaani *content service provider*. Aidha, kufuatia kuwepo kwa upungufu ulioripotiwa kuhusiana na haki za malipo hususan kwenye upande wa Sekta za Sanaa; Wizara ilifanya vikao vitatu na wadau pamoja na mamlaka zinazohusika za Sekta ya Mawasiliano na Sanaa, ikiwemo *BASATA*, *COSOTA*, *TCRA* pamoja na mashirikiano ya wasanii mbalimbali, ambayo Mheshimiwa Martha Mlata alikuwa kiongozi na alisimamia jambo hili vizuri na maamuzi yalipatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, maamuzi muhimu yaliyokwisha tekelezwa katika kikao kile, *TCRA* kuweka utaratibu kwa kushirikiana na *BASATA* na *COSATA,* katika kushughulikia maombi ya leseni za makupuni yanayojishughulisha na mauzo ya sanaa za muziki kupitia teknolojia za habari na mawasiliano.

Pia, wadau kwa pamoja walijadili na kukubaliana kuwa ni vyema utekelezaji wa malipo ya kiwango kisichopungua asilimia kumi kwa msanii kutokana na mapato yanayoingia moja kwa moja kwa mwuzaji au makampuni ya simu kama kinavyotajwa kwenye Sheria ya *COSOTA,* ukajadiliwa upya kwa kushirikiana na wadau wote. Utaratibu uliopo hivi sasa ambapo msanii hulipwa asilimia hiyo kutoka kwa *Content Service Provider* ambaye hivi sasa ndiyo anayeingia mkataba na msanii na *Content Service Provider* anaingia mkataba na Makapuni ya Simu. Kwa hiyo, hili tunalijua na tunalifanyia kazi na wale wasanii wote ambao wanasimamia jambo hili, tutawaalika kwenye kikao cha pamoja tena ili kuhakikisha kwamba, jambo hili tumelisimamia vizuri.

Yapo masuala mengine ambayo Mheshimiwa Anna MaryStella Mallac na Mheshimiwa Betty Machangu, wamezungumzia, yanayohusu mabadiliko ya teknolojia kutoka analojia kwenda dijitali na uenezaji wa matangazo katika maeneo ya mipakani ili Wananchi wasipokee matangazo kutoka vyombo vya habari vya nje.

Kama mnavyoelewa, hadi kufikia Tarehe 30 Aprili, 2013, teknolojia ya zamani ya analojia ilikuwa imesitishwa rasmi kwenye Miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Mwanza, Moshi, Arusha na Mbeya. Pia hatua hii ni utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mabadiliko ya utekelezaji huo. Hivi sasa Miji ya Kigoma na Morogoro ipo katika majaribio ya urushaji wa matangazo ya dijitali ambayo usimamiaji wa mitambo yake ulitekelezwa wakati wa awamu ya kwanza.

Awamu ya pili ya usimikaji wa mitambo ya dijitali itaendelea katika Miji ya Musoma, Bukoba, Tabora, Singida, Kahama, Iringa, Lindi, Shinyanga na Songea. Mitambo ya analojia katika miji tajwa, itazimwa miezi mitatu baada ya kuwashwa mitambo ya dijitali. Mitambo ya dijitali katika Miji tajwa inatarajiwa kuwashwa mwezi Septemba na tunaamini katika maeneo yote ya mipakani sasa watakuwa wanapokea matangazo ya *Television* za Tanzania kupitia mtandao huu wa dijitali.

Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Anna MaryStella Mallac, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Ritta Kabati tena hapa wanazugumzia juu ya gharama za ving'amuzi kuwa ni kubwa sana. Serikali tunalifahamu hilo na Serikali imesamehe ushuru wa kodi ya ving'amuzi kwa Makampuni yote ili kuwezesha bei ya ving'amuzi, Watanzania wengi waweze kupata huduma hii. Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kutumia njia mbalimbali kuhakikisha kuwa, bei ya ving'amuzi inaendana na masilahi ya hali halisi ya Watanzania walio wengi.

Kuna suala lingine la usikivu wa *TBC*, matangazo ya *Television* kule Rukwa siyo mazuri. Wizara ya Mawasiliano tumelipokea hili na kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, tutaona tutafanya nini ili kuhakikisha kwamba, maeneo haya yanaweza kufikiwa vizuri na *channels* zote tano ambazo zinapatikana kwenye *Digital Television.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri nimekwenda karibu kwenye hoja zote, hoja nyingine zinajirudia rudia tu,

Mheshimiwa Naibu Waziri ameshajibu zote kwa mfano hoja za *UCAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Katibu, hatua inayofuata!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMITI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

Kif. 1001- *Administration and HR Management* ... ... ... .... .... .... .... .... Sh. 1,543,797,000

**MWENYEKITI:** Sasa Katibu nisaidieni kuandika kwanza. Waheshimiwa Wabunge, simameni hapo mlipo, lakini hapo ni mshahara wa Waziri. Orodha yenu ninayo, msiwe na wasiwasi.

Naomba kuwatoa tu wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, naona hamsikilizi; baada ya Jaji Warioba kutoa yale maneno yake, naona watu wamechanganyikiwa changanyikiwa! Napenda kuwahakikishia msiwe na wasiwasi, tusikilizane tutafika safari yetu. *(Kicheko)*

Orodha ninayo, msiwe na wasiwasi, kwa sababu hapa ni kwenye mshahara wa Waziri. Utaratibu wetu ule wa Kikanuni, ninayo yale majina yetu tayari. Sasa tuanze na Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zungu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya awali. Nataka kujua ni lini Sera ya Wizara hii katika suala zima la masafa, yaani *speed*

*spectrum*; nauliza suala hili kwa sababu kumekuwa na tatizo kubwa sana la masafa hapa nchini; wawekezaji wengi wakitaka kuwekeza katika Sekta ya Mawasiliano wanaambiwa hakuna masafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile natambua kwamba, kuna baadhi ya watu ambao wameshikilia masafa hayo bila kuyaendeleza; na wote tunajua kwamba, masafa haya ndiyo roho ya mawasiliano. Hatuwezi kuwa na Redio wala *Television* bila kuwa na masafa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie; nini Sera ya Ugawaji wa Masafa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na suala hilo, nataka kujua kwamba, lengo muhimu lililotupeleka kwenye dijitali ni pamoja na suala zima la kuokoa masafa yetu. Nipende pia Mheshimiwa Waziri atuambie, baada sasa ya kuingia kwenye dijitali kutoka kwenye analojia; ni kiasi gani tumeweza kuokoa masafa ili tuweze kuelewa sasa nchi yetu inaelekea wapi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo, ameulizia swali la kwanza la Sera kuhusu masafa na kwamba, watu wengi wanayo masafa, lakini hawatumii kwa muda mrefu.

Kwanza, Sera kuhusu masafa; ipo Sera ya Mawasiliano ya Mwaka 2003, ambayo inasimamia na inaelekeza *TCRA* jinsi ya kugawa masafa.

La pili, kweli kuna watu wana masafa ambayo hawayatumii, lakini kuna utaratibu wa kuyapata masafa hayo; ni lazima tufuate ule utaratibu na tumeanza kuufuata kwa ajili ya kuyapata hayo masafa ambayo hayatumiki.

Suala la pili, anauliza madhumuni makubwa ya kwenda kwenye mfumo wa dijitali ni kupata baadhi ya masafa baada ya kuhamia kwenye mfumo wa dijitali; kweli

tumeanza hiyo safari, lakini kwa sasa hatuwezi kuyatoa hayo masafa mpaka tumalize mchakato wote wa kuhamia kwenye dijitali. Baada ya hapo kutafanyika *study* kuangalia hayo masafa na baada ya hapo masafa hayo yataweza kutolewa. Hatujajua tutatoa kwa mfumo gani; kwa mfumo wa kawaida au mfumo wa *auction* kama alivyouliza Mheshimiwa Zungu leo, lakini Wananchi na Kampuni zote za Simu zitaarifiwa rasmi wakati utakapofika na njia gani ambayo itatumika kutoa masafa hayo.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi nina nia ya kutoa shilingi kwenye hoja na ninaitangaza kabisa nia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo kamili ya Serikali kwenye masuala ya Makampuni ya Simu, wanapoingia mikataba kati ya makampuni ya hapa na ya nje kwenye *management fee* na hasa kwenye *transfer pricing*.

**MWENYEKITI**: Sogeza kidogo *microphone*.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na hasa kwenye *transfer pricing*, kuna mchezo mkubwa sana wa kusafirisha fedha kutoka nchini kupeleka nje kwa kupewa huduma ambazo zinaweza zikafanyika hapa. *(Makofi)*

Serikali ipo *very silent* kwenye kitu kama hiki na wengine hawa wanachajiana *up to three percent.* Sasa nataka kujua na ukitazama kwa mfano kwenye *customer services*, unaambiwa *your call is not reachable*, hazungumzi Mtanzania. Hii ni *computerized message* ya kutoka nchi za nje, ambayo tunailipia sisi, lakini *this could have been done here!* Sasa nataka kujua ni taratibu gani zitatumika kuhakikisha vitu kama hivi kwenye *transfer pricing* na *management fee* vinaondoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, nataka kuondoa shilingi katika hili suala mpaka nipate majibu ya kuridhisha kwa *benefit* ya Taifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lipo tatizo kubwa sana, labda tu kwa maelezo mafupi ni kwamba, asilimia 60 ya thamani ya biashara ya kimataifa siyo kati ya nchi na nchi, siyo kati ya makampuni na nchi, siyo kati ya makampuni na makampuni, ni kati ya Makampuni Mama.

Kwa hiyo, ni kweli anachosema Mheshimiwa kwamba, lipo tatizo kubwa na siyo Tanzania tu na Duniani kwamba, una kampuni hapa; kwa mfano, kampuni labda ya *Vodacom*, ina Kampuni Mama na kampuni inanunua bidhaa kwa Kampuni nyingine Mama. Kwa hiyo, bidhaa inazonunua inauziwa kwa bei ya juu, lakini bidhaa inazouza kwa Kampuni nyingine Mama ambayo iko nchi nyingine, inaziuza kwa bei ya chini.

Siku zote gharama za kampuni zitakuwa kubwa, mapato yatakuwa madogo, kwa hiyo, mtakuwa hamlipwi kodi. Ipo kila Sekta, siyo Mawasiliano tu. Sasa kuna vitu wanaita *transfer pricing rules*, ambavyo wenzetu kwenye Wizara ya Fedha wanavifahamu na watu wa *TRA* wanavifahamu, kujaribu kuweka taratibu ambazo wanaita *Arms Length Rules,* ambazo makampuni ambayo hayana mahusiano hayawezi kufanya biashara ili biashara kati ya makampuni mama ambazo nyingi zina udanganyifu inakuwa haifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili ni suala zaidi la mapato na kodi, ni suala zaidi la Wizara ya Fedha, ni suala zaidi la *TRA*. Nataka niwahakikishie tu kwamba, nalifahamu kwa sababu tunalizungumza Serikalini, namna ya kukabiliana na namna ya kuimarisha hizi *transfer pricing rules* ili tusiwe na tatizo kama hili na tumeshalizungumza na wenzetu kwenye makampuni ya simu, kuhusu tatizo lililopo.

Naomba niwahakikishie kwamba, kwa kuwepo mtambo, kwa sababu kama nilivyosema, mapato ni kitu kimoja, lakini gharama za uwekezaji ni kitu kingine. Kwa hiyo, kama kodi inatozwa kati ya mapato na gharama za uwekezaji na kama huna uwezo wa kujua gharama za

uwekezaji, siku zote watu watakuwa hawalipi kodi. Kwa hiyo, ni suala la kujenga uwezo kwa mamlaka yetu ya kodi, kuweza kujua haya makampuni yanatumia gharama gani za uwekezaji na kwa sababu *TRA* iko moja na sekta ziko nyingi, Madini, Mawasiliano, Gesi, ambapo *TRA* inapaswa kujua hizi gharama, kwa hiyo, *capacity* ya *TRA* ni muhimu zaidi kwenye mambo haya.

Hili jambo ni kubwa zaidi kuliko letu, lakini kwa sababu tunalizungumza Serikalini na wanafahamu, namwomba Mheshimiwa Zungu asiondoe shilingi, kwa sababu Serikali inalifahamu na inalishughulikia. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokutana na *COSTECH*, alitoa ahadi kwamba, kuanzia kipindi hiki tutatumia siyo chini ya asilimia moja hadi tano kwenye kuisaidia *COSTECH* ifanye kazi zake za kiutafiti. Mheshimiwa Waziri, ameliainisha pia hili kwenye Hotuba ya Bajeti yake.

Sasa nataka kujua, pamoja na hili kuwa limezungumzwa, utekelezaji wake ukoje; kwa sababu mwaka jana ilikuwa hiyo na mwaka huu imerudia hivyo hivyo, fedha bado hazitoshi na hatuwezi kuendelea bila kuwa na utafiti wa kutosha kwenye kilimo na kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hili halitaniridhisha, nitatoa shilingi mbili, siyo moja. Ahsante.

**MWENYEKITI**: Kanuni hairuhusu hayo unayoyataka. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi!

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakubaliana na Mheshimiwa Mangungu, ni kweli Bajeti ya *COSTECH* imeendelea kushuka, lakini kama tunavyofahamu kwamba, fedha za utafiti zinapelekwa kwenye sehemu mbalimbali. *COSTECH* ni sehemu moja, lakini wakati huo huo fedha za

utafiti zinakwenda kwenye Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Afya.

Kwa upande mwingine, *COSTECH* vilevile ina mkakati maalum ambao unapata fedha kutoka sehemu nyingine, kama nilivyosema kwenye Hotuba yangu leo; *COSTECH* sasa hivi ina mpango ambao itapata *Euro* milioni 30 kutoka Uingereza kwa ajili ya kufanya utafiti.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu, nilielezea wizi wanaofanyiwa Watanzania katika mitandao ya simu, wanavyoibiwa fedha zao wanapoingiza *credit.* Nilitoa mfano hapa wa kwamba, zinatolewa *offer*, kifurushi cha shilingi 500 au 2000, ukiingiza kifurushi kile, *then* zile fedha zinaliwa zote bila kupata ile huduma, unaambiwa wewe Mkoa uliko huduma haifiki wakati kwenye matangazo yale haikuainishwa kama *offer* ile ni kwa Mikao fulani tu. *(Makofi)*

Nikatoa pia mfano wa *internet* niliyojiunga mimi mwenyewe, kifurushi cha shilingi 15,000 katika simu ya *Blackberry,* halafu wakajibu kwamba ,*Blackberry* hii haihusiki na *offer* hii, wakati hawajatangaza jambo lile katika matangazo yao, walisema simu zote za *Blackberry*. Je, Serikali inalishughulikiaje suala hili katika kuondosha wizi huu wanaofanyiwa Wananchi wetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi kuhusu Sera za wizi.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Haroub, ni kweli hiyo inaweza kutokea, hatuwezi kubisha na hili suala sisi tutalichukua na tutalifanyia kazi. Napenda kusema kuwa, kama ulivyoambiwa kwamba *Blackberry* yako haipo kwenye programu hii, ninavyofikiria mimi, baadhi ya Makampuni ya Simu yanakuwa na *contract* na makampuni yanayotengeneza simu.

Kwa mfano, *Samsung* inakuwa na *contract* na *Airtel*, ukienda pale anakwambia kutokana na *contract* hii utalipa

fedha hizi, utapata *service* hii na hii. Sasa hili itabidi tulifuatilie tujue likoje.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nashukuru kwamba, Mheshimiwa Waziri amejitahidi kutoa majibu, lakini bado napenda atuthibitishie, kwa sababu Serikali yetu imeweka mazingira mazuri sana kwa ajili ya wasanii kujipatia kipato, kwa sababu nayo ni ajira. Baadhi ya makampuni ambayo yanaingia mikataba na wasanii ambayo ni feki, lakini bado hata ulipaji wake unakuwa ni wa kitapeli. Kampuni moja tu labda *Push Mobile* ambao wamejitahidi kwa sasa hivi ambao wao wanapoingia mkataba na msanii wanalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kwa haya makampuni mengine ambayo bado yamekuwa ya kitapeli wasanii, nikasema kwamba, *TCRA* wakabidhiwe shughuli hii, kwa sababu wao wanaweza wakaweka mitambo ya kuweza kuwanasa, kwa sababu wao wanatoa leseni.

Mheshimiwa Waziri, umeeleza kwamba tulikaa kikao, ni kweli yale makubaliano ambayo tumekubaliana; je, yataanza kutekelezwa lini, kwa sababu yale ya mezani ni ya mezani, lakini utekelezaji wake ni jambo lingine? Kwa hiyo, naomba ufafanuzi zaidi ili na wasanii waweze kusikia. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka nimpongeze Mheshimiwa Mlata, kwa kufuatilia hili jambo kwa muda mrefu. Niseme tu kwamba, hili ni jambo mtambuka, linahusu watu wengi, Taasisi nyingi; linahusu *COSOTA*, Wizara ya Viwanda na Biashara, BASATA, Makampuni ya Simu, *TCRA, TRA* na Polisi.

Kwa hiyo, makubaliano na maamuzi na utekelezaji ambao unahusu Taasisi nyingi, unachukua muda, kwa sababu lazima wote mkubaliane na kila mmoja uwezo wake na *interest* zake zizingatiwe.

Kitu ambacho tunaweza kufanya kwa haraka ni kuweka uwazi kwenye hii biashara kwamba, ijulikane kwa sababu saa nyingine wasanii wanaingia mikataba isiyofaa, kwa kuwa hawajui *potential* ya kipato. Kwa hiyo, tutakapoweka *Rules* za uwazi na Mheshimiwa hapa yuko tayari kuandika *Regulations* za kuweka uwazi kwenye biashara ya milio ya simu ili makampuni yaone aibu kuingia mkataba wa ovyo wakati kipato kinajulikana kwa biashara hiyo.

Kwa hiyo, hicho ndicho kitu cha haraka ambacho tunaweza kukifanya sisi, lakini mambo ya *enforcement* na masuala mengine, yanahitaji tukubaliane pande zote. Vilevile ni muhimu kufahamu kwamba, *TCRA* ina majukumu yake kisheria ya udhibiti. Kwa hiyo, tungependa kuwa waangalifu kuiongezea majukumu ambayo hayahusiani kabisa na *core responsibilities* zake, lakini kwa ushirikiano wako na wasanii kwa ujumla na ni muhimu wasanii nao wakaungana, kwa sababu wasanii wenyewe wanagombana, wana makundi, kwa hiyo, ni vigumu kutafuta haki yao kwa pamoja.

Naomba uwashauri na tuwashauri kwamba, waungane kwa pamoja ili tunapoitisha vikao, kwanza wawe wanakuja, wawe wanatoa taarifa na vilevile wapate washauri na Mameneja ambao watawasaidia kuingia mikataba ambayo ni sahihi. Sisi Serikali tuna nia thabiti kabisa ya kuwasaidia kuhakikisha kwamba, mnapata mnachostahili, kwa sababu sisi tunafaidi kipaji chenu zaidi kuliko kitu kingine. Ahsante.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naondoa shilingi kwa kutoridhika na maelezo hasa ambayo Mheshimiwa Waziri aliyatoa kwa kulinganisha Rwanda na Tanzania.

Sisi tunaongelea *corporate tax* na ukiangalia kwenye *chart* aliyonipa yeye mwenyewe, utaona kuna shirika kama *Vodacom* haikulipa kabisa, *Celtel* haikulipa kabisa na *Zantel* haijalipa kabisa. Ukiangalia tena katika *chart* niliyompa ni ya utafiti wa ukweli ambao tuliufanya, labda muda hautoshi,

aseme ukweli labda atoe muda aje alete hizi takwimu ambazo nimempa mimi, aangalie ukweli uko wapi. Kwa sababu hapa naona kaijibu tu haraka haraka. Ukiangalia miaka tuliyotoa au mwaka niliompa, Tanzania ukilinganisha na Rwanda, ukweli ni kwamba malipo yetu yapo chini sana.

Mimi nataka anieleze ukweli hizi *data* kwa nini zinatofautiana na kama zinatofautiana anieleze kwa nini *Vodacom, Celtel* na kwa *Zantel* hawajalipa *corporate tax* na hapo tunapoteza mapato?

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi pia naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba; suala la mawasiliano kwa upande wa Pemba na Zanzibar hata kwenye Jimbo lako unakotoka, mawasiliano siyo mazuri. Kwa mfano, ukiwa Kandani Wete, mawasiliano siyo mazuri na Wazanzibari kwenye suala hili la mitandao ya simu na sisi tunachangia.

Nataka utufahamishe tutapata lini mawasiliano mazuri Pemba na Zanzibar? Hilo ndiyo swali langu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu kwanza swali la Mheshimiwa Mshama kwamba, katika karatasi niliyompatia, anaangalia mwaka 2012 *corporate tax, Vodacom* wamelipa *36.5 billion,* yaani mwaka jana wameanzia Aprili mpaka Machi mwaka 2013.

Tigo wamelipa *12.3 billion* na hiyo karatasi nafikiri Mheshimiwa anayo na Shirika letu ambalo siyo changa lakini uwezo wake ni mgumu, *TTCL* limelipa *84 million corporate tax*, kwa vile makampuni yanalipa na *total corporate tax* ya mwaka 2012 ni *48.9 billion*.

Swali la pili ni la Mheshimiwa Maryam Msabaha; kwanza, ni kweli Mfuko wa *UCAF* unatakiwa upeleke mawasiliano Zanzibar, lakini kuna vitu viwili vya kuangalia; nikianzia na Jimbo la Mkanyageni ninakotoka mimi, suala la

mawasiliano siyo tatizo, umejengwa mnara mmoja juzi juzi na *Zantel.*

Swali la pili, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Mbarouk, suala la Zanzibar kupeleka minara ya mawasiliano kidogo lina changamoto, kwa sababu hivi ninavyoongea na wewe, kuna Kampuni ya *Hellows Tower,* ambayo kazi yake ni kujenga minara, inataka kujenga kama minara saba Zanzibar, lakini wameshindwa kupata kibali kutoka Zanzibar.

Sasa kosa sijui lipo wapi, lakini bado kama Serikali tunalifanyia kazi na tunaamini tutapata ufumbuzi kwa masilahi ya watu wetu.

**MWENYEKITI:** Tumemaliza *round one,* kabla ya kuvuka hapo sasa wale walioonesha *doubts* endapo majibu yao yako sawasawa, tukianza na Mheshimiwa Zungu, ni wawili tu; Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Assumpter Mshama. Mheshimiwa Zungu umeridhika?

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Majibu mengi yametolewa na Mheshimiwa Waziri, *with due respect,* hayana usahihi na sitaki kurudia hoja ya Mheshimiwa Mshama hainihusu, *we know that this report* haipo sahihi, lakini sitaki kwenda huko.

Mimi nina mkataba wa kampuni moja ya simu ambayo sitaki kuitaja, hiyo kampuni inasema *the company* ambayo ndiyo *Tanzania requires to render certain management and technical services to its firm but not limited to accounting finance,* hii najaribu kuonesha tu namna wanavyoingia mikataba hii. *Then* kampuni mama hiyo ya nje na sitaki kuitaja hiyo nchi, *has agreed to provide such management and techno service to Tanzania,* yaani *Tanzania has agreed to accept and pay for those service subject to and in accordance with agreement.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni hii; wanasema sasa; *the company* ambayo ndiyo ya *Tanzania shall pay service to* kampuni hiyo ya nje *at the rate of three percent.*

*Three percent of gross revenue per month* au ukichukua *per month* na ukichukua *per year* vilevile. Hii inakuja wanasema, *during the term of this agreement in respect of the provision of the services specified in schedule one or such other amount that may mutually agreed between the parties provided that such agreed amount is not contrary to the applicable laws of Tanzania;* hatuna chombo kinachodhibiti hizi *transfer* za fedha, ndiyo hoja yangu mimi.

Ninachokitaka ni *commitment* kwamba, sasa mmeliona hili na ukichukua mfano; *gross revenue* ya *400 billion* ni *12 billion* kwa mwaka. Tunawalipa watu, tuna-*transfer job,* tuna *export* kazi za Watanzania tunawapa watu *wa* nje, *simply because of* maandishi tu. Kwa hiyo, nataka *commitment* ya Serikali iniambie hiki kitu na sisi tumekiona, ukiniambia ni suala la Kimataifa, mimi *I don't know the Kimataifa, I know about this Taifa* tu basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka *commitment* waniambie tu bwana tumeliona na sisi tutalifuatilia *and then* tupate *commitment*. Baada ya kusema hivyo, mimi sina sababu ya kuzuia mishahara ya watu, nataka nafasi nichangie mara ya pili ili na wao wajue sisi tunachokijua, *we have this statement.*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri umepewa na maneno ya kusema. Ufafanuzi!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kama nilivyosema mwanzo kwamba, Serikali inalifahamu, kwa sababu nakumbuka nilisema hivyo na tunalishughulikia. Niseme tu kwamba, siyo kwenye mawasiliano; kwa mfano, watu wengi hawafahamu kwamba, Kampuni ya Bia kwa mfano ile *brand* sitaki kuitaja ambayo ni *local* mnaijua, ile *brand* peke yake imekuwa *registered* Netherlands na moja ya gharama za Kampuni ya Bia ni kwamba, wanalipia fedha nyingi ya *royalty* ya *brand* ambayo ni jina la Kiswahili. Jina la Kiswahili lakini limekuwa *registered* Netherlands na kila mwaka

wanalipia *royalty* na hiyo *royalty* inawekwa kama ni sehemu ya gharama, kwa hiyo, haitozwi kodi.

Mheshimiwa Zungu ni jambo ambalo tunalifahamu, kwa sababu mimi binafsi nimekaa vikao na watu wa *TRA* tangu mwaka jana kuhusu mambo haya haya; kwa hiyo, tunayafahamu na tutayashughulikia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zungu, *commitment* imetoka. Mheshimiwa Assumpter Mshama!

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo, nataka ...

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo, naona Waziri wa Fedha amesimama.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Ooh, samahani!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote, sheria hizi tunazipitia upya ili zikidhi mahitaji yetu.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, Mheshimiwa Assumpter Mshama!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naona tunapotofautiana na nilichoongea asubuhi na ninarudia, ni ulinganifu wa makusanyo ya kodi ya mapato katika nchi za Afrika kuhusu mambo ya simu. Yeye anaongelea kuhusu *corporate tax,* mimi ninaongelea makusanyo kwa kuyalinganisha na ilikuwa siyo *big deal,* ni kuonesha namna gani tunakusanya kidogo, ambapo ningemwomba Waziri akubali kwamba tunakusanya kidogo ukilinganisha na watu tulionao na malipo yanavyolipa simu. Tukienda kwenye *details* ataona tu kwamba, ni kweli Tanzania tunakusanya kidogo. Ninaomba akubali hilo halafu tuendelee.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana na Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mshama umekubaliana na sentensi hiyo tu basi?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana na ninarejesha shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Matumaini yangu ni kwamba, mwakani hatutakuja hapa na Waziri wa Fedha atatuambia tunakusanya kidogo Afrika Mashariki nzima. Kwa hiyo, siyo kukubali tu ili kuondoa jamvi mahali pa kuzungumzia, lakini ni kazi ya kufanya kwamba mwakani tukirudi hapa, siyo vizuri tuje na aibu hii ya kuwa tunakusanya kidogo kuliko Kanda nzima ya Afrika Mashariki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ...... ... ... ... ... ... Sh. 274,526,000
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ...... ... ... ... ... ... ... Sh. 476,414,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mmesimama au mnatembea? Mheshimiwa Vita Kawawa, peke yake. Naomba wakati huu msitembee tembee mjizuie kwani mnaniletea mkanganyiko kidogo.

**MHE. VIRA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu Kidogo 1003 - Sera na Mipango, *Item 220200 – Utilities Supplies And Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka kujua Idara hii kama ipo ndani ya jengo hili la Wizara? Pili, nataka kufahamu imeongezeka ...

**MWENYEKITI:** Ni swali moja tu!

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Hoja ni kwamba, imeongezeka mara tatu ya gharama ya mwaka jana. Pia nataka kujua kama lipo ndani ya Jengo la Wizara kwa sababu Idara zote hakuna kifungu cha *utilities and services* lakini Idara hii peke yake ina kifungu hicho.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara hii ipo kwenye Jengo la Wizara, yaani Jengo la Serikali.

**MWENYEKITI:** Ndiyo anauliza sasa kwa kuwa Idara nyingine zote hazina *utilities and services* ana-*assume* zipo kwenye *administration somewhere*; kwa nini Idara hii peke yake ya *Policy* inakuwa na *utilities and services?*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa *centralised* kila kitu kwenye Idara hii.

**MWENYEKITI:** Nadhani swali lakehalijaeleweka, hebu fafanua vizuri Mheshimiwa Vita!

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwenye utawala ipo shilingi milioni 50 ya *utilities and services,* ambayo nadhani ina-*combine* Idara zote. Sasa Idara hii peke yake; ndiyo maana niliuliza kwamba ipo katika jengo hilo hilo au lipo katika jengo lingine? Kwa nini imewekewa kifungu hiki cha *utilities and services* wakati *administration* kuna shilingi milioni 50 ya *utilities and administration,* kifungu 1001?

**MWENYEKITI:** Nami ndivyo nilivyokuelewa Mheshimiwa Mbunge, natumaini Mheshimiwa Waziri umempata sasa?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kweli kwamba Idara hii ipo jengo hilo hilo moja na Idara nyingine. Kifungu hiki pesa yake imeongezeka, kwa sababu baadhi ya fedha ambayo

itakuwa iko kule kwa ajili ya kuangalia Wizara hii, inahamishiwa katika kifungu hiki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 138,843,000
Kif. 1005 - *Legal Unit* ... ... ..... .... ... ... ... ... ..... Sh. 45,191,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Government Communication Unit* ... ... Sh. 88,207,000

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nataka maelekezo kidogo.

Kifungu 1006, Kifungu Kidogo 230400 - *Routine Maintenance and Repair of Vehicles and Transportation Equipment.* Mwaka jana kilikuwa na sifuri na mwaka huu ni sifuri. Hivi sehemu hii haina gari hata la kufanya *service?*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Idara hii haina gari isipokuwa inatumia magari ya Utawala tu *(Administration).*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 - *Procurement Management Unit* .... ... Sh. 152,585,000
Kif. 1008 - *Management Information System* ... ... Sh. 98,902,000
Kif. 2001 - *Communication Division* ... ... ... ... ... ... Sh. 392,397,000
Kif. 2002 - *Information, Communication and Technology* ... ... ..... ...... ........ ....... .... Sh. 413,641,000
Kif. 3003 - *Science and Technology* ... . ... ... ... Sh. 23,593,861,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 100,000,000
Kif. 2001 - *Communication Division* ... .... ... ... ... Sh. 3,495,482,000
Kif. 2002 - *Information, Communication and Technology* ... ... .... ..... ..... ..... ..... ...... Sh. 1,100,000,000
Kif. 3003 - *Science and Technology* ...... .... Sh. 31,233,753,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono na kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wengine wote wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi

na Teknolojia. Matumaini yetu ni kwamba, tutakaporudi mwakani, Waheshimiwa Wabunge hawatarudi tena kuzungumzia mengi yaliyozungumzwa mwaka huu, hali ya mawasiliano na usikivu wake itakuwa imeboreka zaidi. Ninatumaini kabisa ya kwamba, dada yangu Mheshimiwa Zabein Mhita, mwakani atasimama hapa kutoa hotuba ya shukurani, lakini vilevile Kongwa msisahau maana mimi sijalia tu hapa lakini hali ni tete. *(Kicheko)*

Tunawashukuru sana, kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya; tunasema ahsante sana na tunawatakia kila la kheri.

Baada ya hatua hiyo, sasa tunaingia katika kipengele cha maelezo binafsi ya Mheshimiwa Mbunge na naomba nimwite Mheshimiwa Mfutakamba pale alipo atupitishe kwa dakika chache sana.

## MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

### Magonjwa ya Mazao ya Mahindi, Muhogo, Ndizi na Mengineyo Pamoja na Athari Zake kwa Wananchi, Wanyama na Uchumi kwa Ujumla

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(11) na (12) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kutoa maelezo binafsi kama ifuatavyo:-

Katika kipindi cha karibuni, nchi yetu imekuwa katika janga kubwa sana la magonjwa ya mazao mbalimbali, ambayo kwa kiwango kikubwa yameathiri sana ustawi wa Wananchi wetu na nchi yetu kwa ujumla katika ukuzaji wa kipato na upatikanaji wa chakula. Siyo Tanzania pekee iliyokumbwa na janga la magonjwa ya mazao, bali hata majirani zetu wa Uganda, Kenya, Msumbiji na DRC Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu, maeneo yaliyopata athari kubwa ni pamoja na Kanda ya Ziwa. Kwa Mikoa ya Kagera, Wilaya za Ngara, Kyerwa na Karagwe, Zao

la Ndizi limeathirika sana. Zao la Mahindi limeathirika katika Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita na Mkoa wa Shinyanga Wilaya ya Meatu. Kanda ya Kaskazini Mikoa ya Arusha hususan kata za Singisi, Seela, Akeri na Kikwe.

Mkoa wa Manyara, Wilaya za Babati na Kiteto ndizo zimeathirika kwa mahindi. Mkoa wa Kilimanjaro mahindi yameathirika Wilaya za Hai na Siha. Kwa Zao la Mihogo na Miwa katika Ukanda wa Mashariki, Mkoa wa Morogoro Zao la Muhogo limeathirika katika Wilaya ya Kilosa kwa asilimia 80. Muhogo unalisha watu milioni 500 Afrika. Zao hili lipo pia Mikoa mingine ni Pwani, Tanga, Lindi na Mtwara pamoja na Kanda za Kati na Magharibi mwa nchi yetu; Singida, Tabora na Kigoma. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini itazamwe katika maradhi ya chai na kahawa. Kwa Mikoa ya Pwani, Tanga, Lindi na Mtwara, Kanda ya Kati, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi mwa nchi yetu, kiujumla maeneo mengi ndani ya nchi yetu yamepata athari kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia Zao la Kahawa likinyauka na kufa kwa ugonjwa unaosababishwa na *Fangas Hemileite Vartatrix*, Mihogo ikishambuliwa na magonjwa ya *Cassava Musaic Desease (CMD)* na *Cassava Brown Streak Desease (CBSD)*, migomba ikishambuliwa na *Aphids (Musa Balbisuah or Musa Acumunata),* Korosho ikisumbuliwa na *Ubwili Unga,* Chai ikiathiriwa na *mbu wa chai (Tea Mosquito)* na magonjwa mengine yakishambulia mazao mbalimbali kama vile Mahindi, Mpunga, Nyanya, Viazi, Karafuu, Karanga na kadhalika.

KWA KUWA magonjwa ya mazao yamekuwa yakizidi kushambulia mazao hayo na kusababisha uhaba wa chakula na upungufu wa kipato kwa Wananchi wetu katika maeneo mengi ya nchi yetu;

NA KWA KUWA hakuna taarifa mahususi ya magonjwa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Serikali mpaka sasa inayotoa tathmini ya maambukizo ya magonjwa mbalimbali ya mimea;

NA KWA KUWA Gonjwa la Ndizi *(Banana Bacterial Wilt Disease - BBW)* limesambaa kutoka Ethiopia kwenda Uganda, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Rwanda na kuingia Tanzania katika Mkoa wa Kagera;

NA KWA KUWA mpaka sasa Bunge lako halijapewa taarifa jinsi gani Serikali imekuwa ikidhibiti maambukizi ya magonjwa kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine;

NA KWA KUWA Mazao ya Ndizi na Mahindi yana soko la ndani na la nje kwa nchi za Rwanda, Burundi, Uganda na Sudan Kusini na kutuingizia fedha za kigeni; pia Zao la Muhogo lina soko la Ufaransa, Italia, Uholanzi, Ubelgiji na Uingereza, kama malighafi ya kuzalisha wanga na chakula cha mifugo nyakati za baridi *(winter)* hasa kwa ng'ombe na tuna Balozi zetu zenye Maafisa wa Biashara;

NA KWA KUWA sumu kuvu *(aflotoxin)* inayotokana na mahindi yaliyoathirika na wadudu *Aphids* na *Thrips* yakisagwa unga bila kukobolewa (dona), huweza kusababisha saratani ya koo na mfumo wa chakula kwa binadamu na pumba kwa kuku na wanyama, pia kwa binadamu iwapo itatumiwa kutengenezea pombe kama Kangara na vitu vingine;

NA KWA KUWA hakuna taarifa ya tathmini iliyofanywa ya athari ya magonjwa haya yanavyoweza kuathiri viumbe wengine hasa binadamu na mifugo;

NA KWA KUWA linapotokea tatizo linalohusu jamii, Bunge lako Tukufu lina wajibu wa kulinda masilahi ya jamii kwa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa masilahi mapana ya umma;

HIVYO BASI, naomba Bunge lako liazimie kwa kuiagiza Serikali yafuatayo:-

(a) Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pia ikishirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Afya na Ustawi Wa Jamii ili kubaini na kutambua kama Wananchi na mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na kadhalika, hawajaathirika na magonjwa yanayosababishwa na wadudu aina ya *Aphids* na *Thrips* katika maeneo ya ufugaji na kilimo.

(b) Waziri wa Kilimo atoe maelezo Bungeni kuhusu kuibuka kwa magonjwa ya mazao mbalimbali ya chakula na biashara ikiambatana na tathmini ya athari kwa uhakika wa chakula na uchumi kwa jamii.

(c) Waziri wa Kilimo atoe maelezo ya hatua zipi za haraka zimechukuliwa kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati, na mrefu, kukabiliana na magonjwa ya mazao na athari zake.

(d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (Idara ya *Economic Diplomacy*) na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko (*External Trade*), waeleze Bunge ni jitihada na mikakati gani wameichukua kupata wanunuzi wa nje wa mazao ya muhogo na ndizi ili ziada hata sisi Wanaigalula na kwingineko nchini, tusafirishe na kuuza nchi za Ulaya kwa bei ya juu na kuongeza Pato la Taifa kwa fedha za kigeni na kupunguza uwiano usio sawa baina yetu na nchi jirani na za nje *(Trade Imbalance).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hayo ni maelezo binafsi ya Mheshimiwa Mbunge, ambayo Serikali itatazama na kuyapatia majibu katika wakati mwafaka na kwa mawasiliano na Meza, tutaweza kupata ufafanuzi wa jambo hilo muhimu kuhusu magonjwa yanayoathiri sehemu kubwa ya mazao ambayo ni tegemeo letu kwa chakula hapa nchini.

Waheshimiwa Wabunge, orodha ya shughuli za leo imekamilika, shughuli zote zimefanyiwa kazi vizuri. Ninawashukuru tena kwa ushirikiano wenu.

Naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.07 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 4 Juni, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*